

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Nne - Tarehe 22 Aprili, 2016

(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI: Hati za Kuwasilisha Mezani.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU):

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Ulemavu) kwa mwaka wa fedha 2015/2016, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

NAIBU SPIKA: Samahani Mheshimiwa, wewe ndio Mwenyekiti wa Kamati ya masuala ya UKIMWI? Bado ya kwako?

MBUNGE FULANI: Bado.

MHE. - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MASUALA YA UKIMWI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya masuala ya UKIMWI, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Madawa ya Kulevya na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania) kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO (K.n.y. MSEMaji MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA WAZIRI MKUU):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

NAIBU SPIKA: Katibu!

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI: Maswali!

NAIBU SPIKA: Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mbunge wa Mtambwe, sasa aulize swali lake.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 31

Tatizo la Dawa za Kulevya Nchini

MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA aliuliza:-

Dawa za kulevya nchini zimekuwa na athari kubwa sana kwa wananchi wetu hususan kundi la vijana ambao ndio nguvu kazi ya Taifa:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kwa kutumia vyombo vyake inaweza kubaini watumiaji, wauzaji mpaka vigogo wanaoingiza na kusambaza dawa nchini?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa dhati wa kuwaweka waathirika wa dawa za kulevya katika makambi maalum ya kuwatibu na hatimaye kurudi katika hali yao ya kawaida?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU - MHE. DKT. ABDALLAH S. POSSI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mbunge wa Mtambwe lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali siku zote hutumia vyombo vyake kuwabaini, kuwakamata na kuwachukulia hatua za kisheria wafanyabiashara wadogo na wakubwa wa dawa za kulevya nchini kwa kushirikiana na wananchi wakiwemo watumiaji wa dawa za kulevya. Juhudi hizi zimefanikisha kuwakamata wauzaji wadogo na wakubwa na kuwafikisha kwenye vyombo vya kisheria. Baadhi ya watuhumiwa wakubwa wa biashara hiyo waliokamatwa ni Ali Khatibu Haji (maarufu kwa jina la Shkuba), Mohammed Mwarami (maarufu kwa jina la Chonji na Mwanaidi Mfundo maarufu kwa jina la Mama Leila).

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia inaendelea na progamu maalum ya kutoa huduma za upataji nafuu katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Serikali imetoa mwongozo wa uendeshaji wa huduma hizo na inaendelea na ujenzi wa kituo kikubwa cha huduma za matibabu na utengemano katika eneo la Itega, Mjini Dodoma na inaratibu ujenzi wa kituo kama hicho Mjini Tanga.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, swali la nyongeza!

MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majawabu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Hoja ilikuwa ni kwa namna gani vyombo vya Kiserikali vinaweza kusaidia au kushirikiana na hawa watumiaji wa uraibu huu ili kuweza kuzifikia zile *channel* za waagizaji, wasambazaji na watumiaji. Je, kuna mlinganisho gani wa wale waliokamatwa pamoja na watumiaji wenyewe ambao wako mitaani? Serikali inaweza kutupa ulinganisho kwa sababu mitaani wako wengi lakini ambao wanakamatwa ni wachache?

(b) Ni kweli kuna baadhi ya watumiaji wako katika maeneo ambayo wanapatiwa huduma za kupata nafuu. Vijana hawa na watu wengine kwa jumla wanatumia dawa hizi na wakati mwingine kwa vishawishi lakini na wakati mwingine kwa kukata tamaa tu za maisha. Sasa mara baada ya kwisha kuwapa dawa hizi au nafuu hii wakitoka mitaani tumewaandalia mambo gani

ambayo yanaweza kuwasaidia katika kujenga maisha yao huko mitaani?
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU - MHE. DKT. ABDALLAH S. POSSI): Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena.

(a) Serikali inatumia vyombo vyake na wakati mwingine nalazimika kupata taarifa kutoka kwa waraibu wa dawa hizi ili kuwakamata wafanyabiashara wakubwa na wadogo wa dawa hizi. Ndiyo maana tumefanikiwa sasa kukamata baadhi ya watu wenye majina makubwa katika biashara hii na ninavyozungumza wako vizuizini na kesi zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, limeulizwa swali kuhusu mlishanganisho; kuna mlinganisho gani kati ya wale wanaokamatwa na wale wanaotumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima niseme kweli, hakuna *statistics* lakini lazima tuweke wazi kwamba biashara hii tofauti na biashara ya nyanya au vitunguu ni biashara inayofanyika kwa kificho sana. Kwa hiyo, kusema kwamba utapata *proper statistics* itakuwa ni kudanganya watu. Wapo watu maofisini na katika maeneo mbalimbali wanatumia dawa hizo na huwezi ukajua moja kwa moja.

(b) Huduma za kupata nafuu. Kwanza naomba nirekebishe kitu kimoja ambacho kinaweza kikaonekana kama *over generalization*. Siyo kila mtumia dawa za kulevya anafanya hivyo kutokana na kukata tamaa ya maisha. Mifano ipo ndani na nje ya nchi. Akina Michael Jackson na wengine siyo kama walikuwa wamekata tamaa ya maisha. Vishawishi *is fine!*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba juhudi za Serikali zinazochukuliwa za kukuza uchumi na kadhalika zina lengo la kuondoa ugumu wa maisha unaowaingiza vijana katika kutumia dawa za kulevya, kwa sababu sote tunafahamu kwamba vijana ndio nguvu kazi ya Taifa hili na nchi yeyote yenye nia thabiti ya kuendelea, ni lazima ichukue hatua madhubuti ya kuwalinda raia wake kutokana na kutumia dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, niongezee tu kwamba juhudi za kuondoa watu kwenye vishawishi vya kutumia dawa za kulevya, siyo

za Serikali peke yake, hili ni tatizo la kila mtu. Kwa hiyo, kila mtu awe ni kiongozi wa kisiasa, kiongozi wa familia na raia wote, wana jukumu la kuhakikisha kwamba wananchi wanaondokana na vishawishi vya kutumia dawa za kulevya mara baada ya kumaliza tiba inayohusika. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Salma Mohamed Mwassa, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 32

Kuzifanyia Marekebisho Sheria Ndogo Katika Halmashauri Zetu Nchini

MHE. SALMA M. MWASSA aliuliza:-

Miongoni mwa changamoto zinazokwamisha kuleta tija katika ukusanyaji wa kodi kwenye Halmashauri zetu ni pamoja na ubutu wa Sheria Ndogo Ndogo (By laws):-

Je, ni lini sheria hizo zitarekebishwa ili zilete tija katika ukusanyaji kodi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salma Mohamed Mwassa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria Ndogo katika Halmashauri zinatungwa chini ya Sura Namba 290 ya Sheria za Fedha za Serikali za Mitaa ambayo imewekwa sharti la faini isiyozidi shilingi 50,000/= na kifungo kisichozidi miezi mitatu au miezi sita au vyote kwa pamoja kutegemea na aina ya kosa ambalo mtu amefanya. Hivyo, kukosa umadhubuti kwa sheria ndogo hizi ni kutokana na masharti yaliyomo katika Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa inayotumika kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) imeandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura Namba 290 ambayo yatawasilishwa hapa Bungeni ili Bunge lako liweze kujadili na kuridhia. Lengo letu siyo kuwaumiza wananchi, bali kuongeza umadhubuti wa Sheria za Serikali za Mitaa na hatimaye kuzipa makali Sheria Ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kukuza mapato ya Halmashauri.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwassa, swali la nyongeza!

MHE. SALMA M. MWASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mazoea ya kuchelewa kurekebishwa kwa sheria hizi ndogo ndogo na Serikali Kuu na badala yake kwa zile Halmashauri ambazo zinajitahidi zenyewe hasa zikiwemo za mijini, zinakuwa zinanyang'anywa mamlaka yake na Serikali Kuu. Kwa mfano, Kodi ya Majengo (*Property Tax*) kupelekwa TRA na tume-prove kwa miaka miwili ya nyuma TRA ilishindwa kabisa kukusanywa kodi hii; na sasa tunaambiwa kodi hii inaenda tena TRA. Je, ni lini hasa Serikali Kuu itaacha kuingilia mamlaka au kunyang'anya mamlaka ya Serikali za Mitaa ili ziweze kujitegemea? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wakati mwingine Marekebisho ya Sheria yanachelewa lakini mara nyingi sana yanafanyika mara baada ya mahitaji mahususi yanapotokea. Kwa sababu tuelewe kwanza katika suala zima la Serikali za Mitaa kuna maeneo matatu; kuna Sura Namba 287, 288 na 290. Sura ya 290 ndiyo inalenga hasa katika ukusanywaji wa kodi na ushuru mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajenda ya kusema kwamba ni lini sasa Serikali itaanza kuzuia suala zima la kunyang'anya mamlaka ya Serikali za Mitaa, kutoa kodi kwa mfano katika kodi ya majengo; Serikali sasa hivi tuko katika Serikali ya Awamu ya Tano, naamini Bunge hili ndiyo Bunge ambalo mara ya kwanza tunajadili bajeti yetu katika kipindi hiki cha Awamu ya Tano na ninaamini kwamba mjadala huu wa bajeti utakapofika katika suala zima la Wizara ya Fedha, mwisho katika Wizara ya Fedha kuna ile Sheria ya Fedha ya mwisho pale ndio tutapata way *forward* tunapokwenda ni wapi. Lengo kubwa la Serikali ni kuhakikisha mapato yanakusanywa katika Serikali yake ili mradi mambo yaweze kuendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwahiyo, nina imani tutakapofika katika suala zima la Sheria ya Kodi ambayo mwisho wa siku Waziri wa Fedha ata-*table* hapa mezani, tutakuwa tumefika mahali muafaka na kupewa maelekezo ya kutosha nini tunataka tufanye. Lengo kubwa ni kwamba Serikali iweze kukusanya kodi ya kutosha na miradi ya maendeleo iweze kufanikiwa.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba record kwanza iwekwe sawa. Mimi ni Mbunge wa Mkoa wa Rukwa na siyo Arumeru Magharibi kama ilivyoandikwa hapa.

Na. 33

Madai ya Walimu Nchini

MHE. AIDA J. KHENANI aliuliza:-

Suala la madai ya walimu nchini limekuwa ni tatizo sugu hususan kwa walimu wa shule za msingi na sekondari. Je, Serikali imechukua hatua gani ili kumaliza tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kulipa madeni yasiyo ya mishahara na mishahara kwa walimu walioko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kila yanapojitokeza na kuhakikiwa. Aidha, mwezi Oktoba, 2015 Serikali ililipa madeni ya walimu yanayofikia shilingi bilioni 20.125 na mwezi Februari, 2016 imelipa jumla ya shilingi bilioni 1.17 ya madeni ya walimu nchini. Katika fedha za madai ya walimu zilizolipwa Oktoba, 2015 Mkoa wa Arusha ulipelekewa jumla ya shilingi milioni 504.6 ambapo kati ya hizo Halmashauri ya Wilaya ya Meru ilipokea jumla ya shilingi milioni 27.6 ambazo zilitumika kuwalipa walimu 716.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea kukusanya madeni mapya ya walimu ambapo hadi tarehe 19 Aprili, 2016 madeni yasiyo ya mishahara yanafikia kiasi cha shilingi bilioni 17.5 kwa shule za msingi na sekondari wakati madeni ya mishahara yakifikia shilingi bilioni 49.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni haya yatafanyiwa uhakiki na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kisha kuwasilishwa Hazina ili yalipwe. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, swali la nyongeza.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, lakini ni aibu kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Majibu hayo ni ya Arumeru na siyo ya Mkoa wa Rukwa. Halafu mnajiita Serikali ya kazi tu, hapa! Swali hili sijaleta jana, lakini kwa sababu madai ya walimu yako nchi nzima, nitauliza maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Serikali ina mkakati gani wa kuwalipa madeni kwa wakati walimu ambao wamekuwa wakilia kila siku na ni malalamiko ya kila siku!

Swali la pili, mpaka sasa walimu wanadai fedha walizosahihisha mitihani ya mwaka 2015 ya kidato cha nne, ni lini Serikali itawalipa walimu hawa na kuwatendea haki kama wafanyakazi wengine wa nchi hii? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niweke wazi, katika mchakato wa madeni ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI pale ina maswali zaidi ya takriban 15 ambayo yote moja kwa moja yanalenga katika suala zima la madai ya walimu na yote yanafanana fanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwahiyo, kwa *concern* ya Mheshimiwa Mbunge siyo kwamba Serikali haiko makini, isipokuwa jambo hili limekuwa ni kilio karibuni kwa Wabunge wote. Kwa hiyo, suala la msingi ni jinsi gani tutafanya kutatua tatizo hili tuweze kulimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati uliopo, nilisema Serikali kwa awamu ya kwanza ilishalipa haya madeni, lakini naomba niwambie, katika madeni haya katika sehemu nyingine ni *fake*. Tunafahamu sasa hivi hata katika suala zima la mishahara hewa, mmeona jinsi ambavyo kuna matatizo makubwa, wengine wanaingiza ilimradi waweze kupata pesa. Kwa hiyo, Serikali imejipanga na ndiyo maana uhakiki umefanyika. Katika jibu langu la msingi nimesema kwamba kuna madeni yameshaanza kulipwa na ndiyo maana tulichokifanya ni kuelekeza Halmashauri zote zifanye uhakiki kwa haraka ilimradi walimu waweze kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tukiri kwamba madeni haya hata tukilipa lazima yataendelea kwasababu kila siku walimu wanahama na kila siku walimu wanaenda likizo. Jambo la msingi ni kwamba madeni yanapojitokeza, inapaswa sasa watu waweze kulipwa haki zao wanazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la Walimu, ni kweli, katika mitihani ya *form two* na *form four* mwaka 2015, tulipata takriban shilingi bilioni 14. Katika mapato hayo, maana yake tulikuwa na *deficit* ya shilingi bilioni 6.6, lakini kilichofanyika ni nini? Zoezi lilipokwenda ikaonesha kwamba kuna tofauti na tumeomba sasa hivi Hazina watupatie hizo pesa, lakini kulikuwa na *requirements* kufanya uhakiki wa yale matumizi ya mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeelekeza Mikoa yote ihakikishe kwamba wanahakiki suala zima la pesa za mwanzo zilizotumika kwasababu mara nyingi fedha hizi zinapokwenda, kuna wengine wanaingiza katika mikono yao, haziwafikii walimu. Kwa hiyo, *requirements* ni kwamba Mikoa yote tumeielekeza ilete takwimu hizo haraka na tuliweka *deadline* tarehe 15 mwezi huu wa Aprili. Kwa bahati mbaya sasa hivi naomba nitaje Mikoa ambayo mpaka leo hii imeshawasilisha suala zima la mitihani ya walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mkoa wa Mbeya, Mara, Tanga, Arusha, Iringa, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi na Mtwara. Ina maana tuna Mikoa mingi bado haijaleta. Naomba nitoe agizo hili hapa, hakikisheni mikoa yote ambayo mpaka jana tumepokea mikoa tisa kati ya mikoa 29. Tunataka tukifika Jumatatu tuhakikishe mikoa yote, yale madeni ya walimu ambayo hawakulipwa katika kipindi cha mitihani, yawe yamefika Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tupeleke Hazina. Lengo letu ni kwamba walimu waweze kupata haki zao za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba Serikali hairidhiki kuona watumishi wetu ambao wanafanya kazi kubwa wanadai madeni yao mbalimbali. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chegeni!

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, tunatambua kwamba Serikali ina mzigo mkubwa sana kuhusiana na masuala ya madai ya walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuuliza kwamba kuna zaidi ya 3,000 ambao wamestaafu mwaka 2014 na mwaka 2015, mpaka sasa hivi hawajalipwa mafao yao. Je, ni lini Serikali angalau mafao ya watu ambao wameshastaafu tayari wanahitaji walipwe warudi majumbani kwao watalipwa pesa hizi? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna Walimu wamestaafu, nami naomba nikiri kwamba hata katika Ofisi yangu kuna baadhi ya walimu walifika pale moja kwa moja kuleta madai yao. Kwa mfano, kuna mwalimu mmoja alikuwa akifundisha pale Bahi. Walimu wengi waliokuwa na changamoto, walikuwa katika Mfuko wa PSPF.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Serikali imetoa maelekezo katika Mfuko wa PSPF kwamba haraka iwezekanavyo walimu wote waliokuwa wanadai, wahakikishe stahili zao zimelipwa, kwa sababu Serikali imefanya mchakato mkubwa sana kuiwezesha PSPF katika madeni iliyokuwa inadai kwamba iweze kupata mafungu ya kutosha ilimradi PSPF iendelee kulipa madeni na Serikali imetimiza hilo.

Sasa naomba nitoe agizo kwamba Mamlaka zinazohusika katika hii mifuko zihakikishe kwamba Walimu wote ambao waliokuwa wanadai waweze kupata stahili yao. Siyo jambo jema kutokuwalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano, mwalimu mmoja kutoka pale Morogoro alizimia kabisa kwa kudondoka kwasababu hakupata mafao yake. Ndiyo maana tumetoa maelekezo mazito na ni imani yangu kwamba Mfuko wa PSPF kwa sababu umeshaanza kupata mafungu yale yaliyokuwa yanadai Serikalini, iwalipe walimu wetu ilimradi waendelee kuishi maisha mazuri. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Wizara ya Nishati na Madini. Mheshimiwa Oran Manase Njenza, Mbunge wa Mbeya vijijini sasa aulize swali lake.

Na.34

Utekelezaji wa Mradi wa REA II - Mbeya Vijijini

Halmashauri ya Mbeya ina vijiji vingi ambavyo havijapata umeme katika Mpango wa REA na pia utekelezaji wa REA II uko nyuma sana:-

(a) Je, ni vijiji vingapi vya Halmashauri ya Mbeya vimo kwenye REA II na mradi utakamilika lini?

(b) Je, Kwa nini mradi wa REA II haujalenga kupeleka umeme kwenye huduma za kijamii kama vile Shule, Zahanati, Nyumba za ibada na vyuo?

(c) Je, ni lini sasa vijiji vilivyobaki vitapewa umeme wa REA?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vya Halmashauri ya Mbeya vilivyomo kwenye REA Awamu ya Pili ni 27, vikiwemo vijiji vya Chang'ombe, Hatwelo, Haporoto, Idimi, Kasele, pamoja kijiji cha Wambishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi unaotekelezwa katika Awamu ya Pili , unafanywa na Mkandarasi *SINOTEC* ambao umefikia asilimia 54.33 na mradi huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2016/2017.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi yote inayotekelezwa na Serikali kupitia Mfuko wa REA Vijijini, kipaumbele kimewekwa kwenye huduma za kijamii kama vile shule, zahanati, vituo vya afya, nyumba za ibada na mashine za kusukuma maji. Katika Mpango wa Awamu ya Pili ya umeme vijijini maeneo ya huduma za jamii ambayo yatafikishwa huduma ya umeme katika Halmashauri ya Mbeya Vijijini ni pamoja na shule za msingi 23, shule za sekondari tano, zahanati 10, kituo cha afya kimoja, pamoja na nyumba za ibada 42.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vingine vya Mbeya Vijijini ambavyo havikupata umeme kwenye Mpango wa REA kabambe Awamu ya Pili, vimewekwa kwenye Awamu ya Tatu unayotarajiwa kutekelezwa mara baada ya bajeti hii ya mwaka 2016 kupitishwa na Waheshimiwa Wabunge. Jumla ya vijiji 111 katika kata 30 za Mbeya Vijijini vimejumuishwa katika REA Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kupeleka umeme kwenye maeneo yanayojumuisha ujenzi wa shule za umeme pamoja na zahanati, inafanyika kwa ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 480; ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 530, ufungaji wa transfoma 137 za ukubwa mbalimbali pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 7,465. Gharama ya kazi hii inakadiriwa kufikia shilingi bilioni 51.52

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Oran Manase Njeza, swali la nyongeza!

MHE. ORAN M. NJENZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, kwanza napenda kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na vilevile kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri inayoifanya kwa kusambaza umeme karibu vijiji vyote vya Tanzania hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuwapongeza Mainjini wa TANESCO waliopo pale Mbeya akiwemo *Engineer Maze* na *Engineer Kiduko* pamoja na *Engineer Mbalamwezi*. Pamoja na hayo, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Wizara ina mpango gani wa kusambaza umeme pamoja na hii REA kwenye vitongoji vilivyobaki katika vijiji hivyo vilivyotajwa? *(Makofi)*

Swali la pili, kutokana na ongezeko la usambazaji wa umeme vijijini, inaelekea *capacity* ya watumishi wa TANESCO ikiwemo vifaa, haitoshelezi tena.

Je, Wizara ina mkakati wa kuhakikisha kuwa inaongeza *capacity* ya watumishi ili iendane pamoja na usambazaji wa umeme vijijini? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Mheshimiwa Mbunge, ni kweli kabisa, pamoja na mradi huu kabambe wa REA kuendelea kufanya kazi yake, lakini bado kuna miradi mingine itaendelea kwa ajili ya kukamilisha shughuli zinazoachwa na REA. Baadhi ya kazi zinazoendelea hapa sambamba na miradi ya REA ni pamoja na mradi wa *Underline*. Mradi wa *Underline* unaendelea kupita kukamilisha maeneo ambayo yanaachwa na TANESCO pamoja na REA.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusiana na uwezo na *capacity* pamoja na *management*, ni kweli kabisa, kama mnavyojua, TANESCO ni shirika la zamani, lakini tuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge pamoja Serikali ya Awamu ya Tano, ni kwamba tunapata uwezo wa kuongezewa nguvu. Kwa sasa hivi tunaongezewa nguvu Shirika letu la TANESCO kwa maana ya kulinunulia vifaa vya kutosha kama transfoma pamoja na *generators* ambako tunatumia mafuta. Kwahiyo, Mheshimiwa Mbunge nimhakikishie kwamba Shirika la TANESCO pamoja na REA pamoja na miradi mingine, itaendelea kuimarishwa ili ifanye kazi zake vizuri. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Mikumi.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Suala hili la Mbeya Vijijini linafanana sana na tatizo sugu la umeme katika Jimbo letu la Mikumi.

Swali langu ni kwamba, je, ni lini Serikali itapeleka umeme huu wa REA kwenye Kata za Tindiga, Mabwerebwere, Ulaya, Zombo, Muhenda, Uleling'ombe na Vidunda? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa hapa tulipofika REA Awamu ya Pili tunatarajia ikamilike mwezi Juni mwaka huu. Vijiji vyote ambavyo vitakuwa vimesalia bila ya kuwa na umeme pamoja na vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge vya kwenye Wilaya pamoja na Jimbo la Mikumi, vyote tunatarajia tuvifikishie umeme kwenye REA Awamu ya Tatu. Kwahiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba vijiji vyake vyote vitapata umeme wa REA Awamu ya Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge, kama tutakavyoleta bajeti yetu, tuna matumaini makubwa kwamba bajeti yetu ya kupeleka umeme vijijini itapitishwa na Waheshimiwa Wabunge na ikishapitishwa, kama tunavyosema siku zote, kwa sababu suala la umeme ni la kufa na kupona, dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kupeleka umeme kwenye vijiji vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kwenye Awamu ya Tano ifikapo 2025 vijiji ambavyo vitakuwa havina umeme vitakuwa ni vya kutafuta. Kwahiyo, vijiji vyote vitapata umeme wa REA Awamu ya Tatu. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nkamia!

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niulize swali moja dogo la nyongeza. Katika usambazaji wa umeme kwenye hii REA Phase II, Makao Makuu ya Wilaya ya Chemba, umeme ule umepelekwa kwenye nyumba ya Mkuu wa Wilaya tu. Pia katika vijiji vya Gwandi, Farko na Kwamtoro ambavyo vilikuwepo kwenye programu hii havijapelekwa hata nguzo. Mheshimiwa Waziri naomba anihakikishie hapa kwamba je, mpaka kufika Juni miradi hii itakuwa imekamilika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa baadhi ya maeneo ambayo yamepelekewa umeme tumepeleka kwenye vituo vikubwa hatujaanza kusambaza kwenye vijiji, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Nkamia kwamba ni kweli vijiji ambavyo vimesalia kwenye ile awamu ya pili sasa hivi kazi inayofanyika ni kuvihakiki ili tubaini ni vituo gani na vijiji gani havijapata umeme kwenye REA Awamu ya Pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, azma yetu ya kwanza ni kuhakikisha kwamba vijiji vyote vilivyokuwa kwenye scope ya REA Awamu ya Pili kwanza vinakamilika ifikapo Juni mwaka huu, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kama itaoneka kwa dosari za kibinadamu vijiji vitasalia, vyote vitakavyokuwa vimebaki vitaingia kwenye REA Awamu ya Tatu pamoja na vijiji vya Mheshimiwa Nkamia.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea. Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi; Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, sasa aulize swali lake.

Na. 35

Utaratibu wa Wahitimu wa Stashahada Kujiunga Vyuvo Vikuu

MHE. BONIPHACE M. GETERE aliuliza:-

Wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita na kupata fursa ya kujiunga na vyuo mara tu wamalizapo masomo yao, huruhusiwa kutumia *National Examination Results Slip* kwa ajili ya taratibu za kujiunga na chuo.

Je, kwa nini wanafunzi wanaomaliza stashahada katika vyuo mbalimbali na kutaka kujiunga na elimu ya juu wasiruhusiwe kutumia *academic transcripts* badala ya kutakiwa kuwasilisha vyeti halisi ambavyo huchukua muda mrefu kutolewa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kiujiibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua kuwa vyeti vya kuhitimu stashahada huchelewa kutolewa, wanafunzi wanaomaliza stashahada katika vyuo mbalimbali na kutaka kujiunga na elimu ya juu wanaruhusiwa kutumia hati ya matokeo yaani *academic transcripts* ili kupata usajili wa muda yaani *provisional registration* mpaka hapo wanapopata vyeti vyao ili kupatiwa usajili kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa udahili wa wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya elimu ya juu hufanyika kupitia mfumo wa udahili wa pamoja yaani *central admission system*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu unaratibiwa kwa pamoja kati ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Tume ya Vyuo Vikuu na hutumia matokeo ya mitihani ya ngazi ya stashahada yaliyohifadhiwa kwenye *Hazina data* ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi. Hivyo, waombaji udahili hawatumii vyeti kuomba udahili kwa kuwa baadhi ya taasisi zinazotoa mafunzo ya Stashahada huchukua muda mrefu kutoa vyeti hivyo katika jitihada za kudhibiti udanganyifu wa vyeti.

Kwa hiyo, wanafunzi hawa wanapo-report vyuoni hupewa usajili wa muda na baada ya kupata cheti ndipo huwasilisha taarifa hizo na kupata usajili kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa wito kwa wanafunzi wanaopata tatizo la kutumia hati ya matokeo kusajiliwa vyuoni watoe taarifa ili Wizara yangu iweze kufanyia kazi ipasavyo suala hili. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza!

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante, tatizo la watoto au wanachuo wanaohitimu elimu ya diploma au stashahada ni kubwa mno. Haya mambo hayakuanza leo, toka mwaka 2007 wanafunzi wa Vyuo Vikuu kwa Taasisi ya *TAHLISO* wanadai hili suala halipo vizuri sana.

Kwanza vyuo vyenyewe vinapomaliza muda wake, muda wa kuhitimu masomo unakwepana na muda wa kusajili. Wanafunzi wanapopata ile wanaita *supplimentary*, kiswahili sijui; lakini na hawa wanachelewa kufanya mitihani yao kujiunga nao chuo. Sasa kama kweli majibu haya yako sahihi, kwanini bado wanapata matatizo haya?

Swali la pili, tatizo hili la kudahili wanafunzi wa diploma, wanapata shida sana kupata mikopo yao kwa maana vyuo vyao vinachelewa sana kupata vile

vyeti na wao watu wa Bodi ya Mikopo hawapokei *transcript* ya mwanafunzi wa diploma. Sasa tunauliza, kwa kutumia hii Taasisi ya Elimu na kwa umaarufu wa Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Ndalichako na kwa kutumia ma-engineer...

NAIBU SPIKA: Naomba ulize swali Mheshimiwa.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Naam!

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la msingi ni kwamba naomba wanafunzi wanaomaliza stahahada wapewe nafasi ya kupata mikopo ya elimu ya juu, nalo ni tatizo. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani una swali moja hapo la nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ni kweli kwa siku za nyuma kulikuwa na usumbufu kidogo ambao ulikuwa unajitokeza hususan kwa hawa wanafunzi ambao wanamaliza stahahada. Tatizo ambalo lilikuwa likijitokeza ni kwamba kwa upande wa wale ambao ni wanafunzi kwa mfano *form six*, wao matokeo yao yanakuwa moja kwa moja yanapitia Baraza la Mitihani ambalo ni moja, lakini kwa upande wa vyuo kumekuwa na utaratibu kati ya chuo na chuo kiasi kwamba baadhi ya vyuo vikuu vimekuwa haviamini kwa uharaka kwamba matokeo tunayoletewa ni sahihi. Kwa hiyo, walikuwa wanatafuta namna ya kufuatilia zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukaa pamoja na kuelezana uhalisia na kwa sababu matokeo hayo ya vyuo vilevile yanaenda kuhifadhiwa katika *Hazina data za NACTE*, kwa misingi hiyo hakuna huo usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hiyo, napenda nitoe agizo kwa vyuo vyote kwamba hakuna sababu ya kufanya usumbufu kwa wanafunzi hao ikizingatiwa kwamba matokeo yao yapo na yanaongea moja kwa moja na *system* ambayo inafanya shughuli ya udahili.

Kwa upande wa suala la udahili wa Stahahada kusababisha wanafunzi kushindwa kuingia katika nafasi za mikopo, kwasababu suala hili linalohusiana na mfumo, ni vyema tulichukue tuendeleo kulifanyia kazi na hivyo tutashirikaiana na wewe mwenyewe Mheshimiwa Mbunge kupitia Kamati. Ahsante.

NAIBU WAZIRI: Mheshimiwa Waziri wa Elimu!

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu wangu wa Elimu, ningependa kuchangia kidogo tu katika suala hili.

Kwanza napenda kutoa ufafanuzi kwamba mwanafunzi ambaye ana *supplementary* bado hajamaliza chuo. Mwanafunzi anakuwa amemaliza chuo pale ambapo anakuwa ame-clear mitihani yake. Kwa hiyo, mwanafunzi ambaye ana *supplementary* hawezi akadahiliwa kwenda katika chuo kwa sababu bado hajakamilisha masharti ya kumaliza elimu yake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia kuhusiana na mikopo kwa wanafunzi wenye stahahada ya ualimu. Mwanafunzi anapata mkopo kulingana na vigezo vinavyowekwa na hivyo basi, kama mwanafunzi wa stahahada amekidhi matakwa ya kujiunga na elimu ya juu na anakidhi matakwa ya mikopo, hakuna usumbufu wowote unaotokea katika upatikanaji wa mkopo. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Tunaendelea. Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 36

Tatizo la Upatikanaji Pembejeo kwa Wakati

MHE. NEEMA W. MGAYA aliuliza:-

Lini Serikali itatatua kero ya pembejeo za kilimo kutofika kwa wakati katika Kata za Kipengele, Wangama, Igima, Ulemwe na Makoga?

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ucheleweshaji wa pembejeo kwa wakulima unasababishwa na baadhi ya mambo kama haya yafuatayo:-

La kwanza, ni mawakala kutokulipwa kwa wakati kutokana na uhaba wa fedha na hivyo kuwapunguzia uwezo wa kutoa huduma hiyo kwa wakati.

Pili, utaratibu au mchakato mzima unaofanya mpaka mkulima apate vocha au pembejeo ni mrefu na hivyo huchukua muda mwingi na kuchangia kuchelewa kwa pembejeo. Serikali inaangalia jinsi ya kurahisisha utaratibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika msimu wa mwaka 2015/2016 imetumia makampuni ya pembejeo za kilimo kuteua mawakala wa kusambaza pembejeo kwa wakulima. Kupitia utaratibu huu, mawakala waliteuliwa na makampuni badala ya Kamati za Pembejeo za Wilaya ili kuokoa muda wa pembejeo kuwafikia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wanufaika wa vocha za pembejeo, Wizara ilikabidhi vocha za pembejeo kwa Mkoa wa Njombe tarehe 4/11/2015 na kwamba Mkoa ulikabidhi Wilaya ya Wanging'ombe tarehe 6/11/2015 na Kata ya Igima ilipokea vocha tarehe 9/11/2015. Kata ya Kipengele, Wangama, Ulembwe, Kidugalo, Imalinyi, Igosi na Makoga zilipokea vocha za pembejeo tarehe 10/11/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia tarehe 20/11/2015 huduma ya usambazaji wa pembejeo ilianza kutolewa na mawakala walioteuliwa na Makampuni ya Pembejeo ili kuwahi msimu wa kilimo ambao huanza kati ya mwezi Oktoba na Novemba.

Wizara ya Kilimo na Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Mikoa na Halmashauri za Wilaya tunaendelea kuhamasisha Makampuni na mawakala wa pembejeo kufikisha pembejeo kwa wakulima kwa wakati kabla ya msimu haujaanza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Neema William Mgaya, swali la nyongeza!

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini zile pembejeo hazifiki kwa wakati. Kwa hiyo, lengo lililokusudiwa haliwanufaishi wakulima. Nataka kujua, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba wakulima wananufaika na pembejeo hizo ikiwa ni kufika kwa wakati? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Neema Mgaya kwa swali lake zuri na kwa jinsi anavyofuatilia jambo hili la pembejeo ikizingatiwa kwamba Mkoa wa Njombe ni

Mkoa wa kilimo na hivyo waliomchagua hawakufanya kosa kumrejsha Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu mfumo huu wa pembejeo umekuwa na upungufu mwingi na Serikali imejitahidi mara kwa mara kuangalia mifumo mipya ili kuhakikisha kwamba kusudi lililokusudiwa linakuwa na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, nakiri kwamba pembejeo zinapochelewa kusudi la Serikali linakuwa halijafikiwa. Kwa hiyo, kwa sasa hivi tunachoangalia kwenye pembejeo, katika mfumo mpya tunalenga mambo mawili; kwanza ni kuhakikisha kwamba pembejeo zinafika kwa wakati; na pili, tunaangalia namna bora ambayo itafanya pembejeo ziwafikie wakulima wengi kuliko hivi sasa ambavyo tunachukua wachache.

Kwa hiyo, utaratibu ambao tunapanga kama Mheshimiwa Mbunge alivyopendekeza ni kuangalia mfumo ambao utawezesha pembejeo hizi zipatikane madukani kama zinavyopatikana nyingine zile ambazo hazitolewi kwa ruzuku ili wakulima wengi waweze kujinunulia pembejeo zikiwa madukani na zikiwa na bei nafuu. Tunaangalia pembejeo hizi ziweze kupatikana kama coca cola inavyopatikana dukani kwa maskini na tajiri na kila eneo anaipata kwa wakati pale pale anapotaka kuichukua. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Tuendeleo. Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki Kikanda na Kimataifa. Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, sasa aulize swali lake.

Na. 37

Watanzania Walio Ughaibuni

MHE. HAFIDH ALI TAHIR aliuliza:-

Baadhi ya Watanzania wanajitafutia maisha katika nchi mbalimbali duniani na wamepata maendeleo katika sekta mbalimbali:-

(a) Je, ni Watanzania wangapi wanajulikana rasmi kuwa wako ughaibuni, wanachangiaje maendeleo ya nchi yao na kwa kiasi gani?

(b) Je, ni Watanzania wangapi wakiwemo kutoka Tanzania Zanzibar ambao hawakufuata taratibu walipoondoka lakini Balozi zetu zina taarifa ya uwepo wao kwenye nchi hizo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania waishio nje ya nchi wanakadiriwa kuwa zaidi ya milioni moja kote duniani. Makadirio hayo yanatokana na takwimu tunazokusanya kupitia Balozi zetu ambazo zinashirikiana kwa karibu na Jumuiya za Watanzania katika maeneo yao ya uwakilishi. Hata hivyo, idadi hiyo inaweza kuwa ndogo kwa kuwa bado hatujaweza kukamilisha uwezo wa kuwafikia Watanzania wote ughaibuni kwa ajili ya kuwatambua na kuwahesabu. Mipango ya kutekeleza azma hiyo inaendelea na hivyo tunatarajia siku za usoni tutaweza kuwa na takwimu bora kabisa za wenzetu walioko ughaibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea na juhudi za kuhamasisha Watanzania waishio ughaibuni kuona umuhimu wa kuchangia maendeleo ya nchi yao. Tumeweza kupata mafanikio kadhaa yanayopatikana kutoka kwenye mwitikio wa baadhi ya Watanzania hao. Taasisi zetu za fedha hazijaweza kukusanya takwimu zote za fedha zinazotoka ughaibuni kwa Watanzania kama kama *remittance*, kwasababu ya changamoto mbalimbali ikiwemo gharama kubwa za utumaji wa fedha nyumbani. Changamoto hizo zinawalazimisha kutumia njia mbadala kama hawala. Hata hivyo, imeweza kuthibitika kuwa kaya nyingi zinapata misaada ya fedha kutoka kwa ndugu zao na jamaa zao waishio ughaibuni. Mathalani, asilimia 12 ya kaya za Zanzibar zinaishi kwa kusaidiwa na ndugu zao hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania hao wameendelea kuratibu na kuleta misaada hapa nchini hususan katika sekta ya afya na elimu. Mifano michache, mwezi Februari, 2015 Watanzania waishio Marekani walifanikisha upatikanaji wa mashine ya kupimia saratani ya matiti yenye thamani ya dola za Marekani 200,000 iliyotolewa katika Hospitali Kuu ya Jeshi ya Lugalo.

Aidha, mwezi Julai 2015 Watanzania wengine kutoka huko huko Marekani, waliratibu ziara ya kitabibu ya Madaktari wa Marekani kuja kutoa huduma za tiba bure za magonjwa kama ya moyo, meno na saratani ya kizazi na matiti katika hospitali ya Mwananyamala, Dar es Salaam pamoja na Hospitali ya Mnazi Mmoja kule Zanzibar. Vilevile walitoa msaada wa vifaa tiba vyenye thamani ya dola za Marekani 300,000 katika hospitali hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo rahisi kubaini idadi ya Watanzania walioondoka bila taratibu zilizopo hapa nchini. Watu wanaondoka kwa sababu tofauti na wakifika huko siyo rahisi kufahamu yanayotokea. Hata hivyo wale wanaojiandikisha katika Balozi zetu, mara nyingi taarifa za muhimu zaidi ni kuthibitisha Utanzania wao. Madhumuni yetu ni kuwatambua kama Watanzania wenzetu, kuwapa huduma wanapohitaji na kuwahamasisha kusaidia ndugu zao walikotoka na kuchangia maendeleo ya nchi.

Aidha, kupitia Balozi zetu, tumekuwa tukiwasisitiza Watanzania waishio ughaibuni kuheshimu sheria na taratibu za nchi wenyeji ili kuendelea kulinda heshima na sifa nzuri ya nchi yetu. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hafidh, swali la nyongeza!

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Naibu Waziri kwa jawabu zake. Kabla sijauliza masuala mawili muhimu ya nyongeza naomba ninukuu kidogo katika majibu yake pale aliposema kwamba; "madhumuni yetu ni kuwatambua kama Watanzania wenzetu, kuwapa huduma wanazo stahiki."

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania hivi sasa kupitia Wizara hii ya Mambo ya Nchi za Nje, kuna deni ambalo linadaiwa na Hospitali ya *London Bridge* ambayo ni pounds za Kiingereza 79,567 ambazo zimetokana na Ubalizi wa Uingereza kwa Tanzania kuchukua dhamana ya matibabu ya mmoja kati ya Watanzania anayelitwa Nassoro Moyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ndugu Nassoro Moyo aliondoka Zanzibar kama Mtanzania wa kawaida, alipofika London...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hafidh, naomba ufupishe kidogo swali lako tafadhali.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Naibu Spika, nafupisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, alipofika pale, Ubalizi ukachukua dhamana ya kumpatia matibabu na bahati mbaya akafa. Hospitali inadai kiwango hicho cha pesa nilichokitaja, lakini Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanapeleka barua Zanzibar kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kulilipa deni hili kwa barua ya tarehe 17/08/2007 na barua nyingine ni ile ya tarehe 21 Januari, 2016. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tahir, hilo ni swali la nyongeza, naomba ulifupishe tafadhali.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Swali. Hivi SMZ kama hawakulipa kiwango hicho cha pesa kama walivyotakiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje watachukua hatua gani? La kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo inatambulikana nje ya Tanzania, je, Mheshimiwa Waziri ataondoa vipi aibu hii ya pesa ambazo zinadaiwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Mtanzania aliyechukuliwa dhamana na Jamhuri? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, nia ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kutumia Balozi zetu zote zilizoko nje ni kuhakikisha usalama, haki za wananchi wetu walioko nje ya nchi zinalindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamana ambayo Ubalozi wa Uingereza uliochukua ni kuhakikisha tu kwamba mwananchi yule wa Tanzania ambaye yeye mwenyewe amekiri kwamba alikuwa ni Mtanzania, ni kuhakikisha kwanza usalama wake na analindwa kwa kipindi kile. Kwa vile tu Mtanzania huyu alifariki, lakini Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haikuombea hayo ila ilikuwa inajitahidi kulinda haki za Mtanzania yule.

Kuhusu suala la kwamba deni lile limeletwa kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikikataa kulipa deni lile Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itafanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua uwepo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na inafanya kazi kwa karibu, inaheshimu taratibu na sheria. Jambo hili litaisha kwa usalama kabisa, nahikikisha hilo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Tuendeleo. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 38

Ujenzi wa Barabara ya Mtwara Mjini Hadi Masasi

MHE. TUNZA I. MALAPO aliuliza:-

Serikali inatambua umuhimu wa barabara; na barabara inayounganisha Mtwara Mjini, Nanyamba, Tandahimba, Newala hadi Masasi haipitiki vizuri wakati wote na hivyo kuwafanya wananchi waone kama wametengwa na Serikali yao.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara (TANROADS) ilisaini mkataba na Mkandarasi Mshauri *Multi Tech Consult (pty) Ltd.* kutoka Botswana akishirikiana na *Unitec Civil Consultants Ltd* ya hapa nchini tarehe 15 Mei, 2014 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mtwara Mjini – Nanyamba – Tandahimba – Newala na hadi Masasi yenye urefu wa kilometa 210 kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami kwa gharama ya shilingi milioni 1,280,832. Usanifu wa kina wa barabara hii ulikamilika mwezi Aprili, 2015.

Taratibu za kumpata Mkandarasi wa kujenga kwa kiwango cha lami sehemu ya Mtwara hadi Mnivata ambapo ni kilometa 50, zipo katika hatua za mwisho ambapo ujenzi utaanza mara baada ya mkataba kusainiwa. Aidha, ujenzi wa sehemu iliyobaki kati ya Mnivata na Masasi, utafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha na kwa kuzingatia kwamba barabara hii imeahidiwa katika ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 hadi 2020 na wakati huo huo iliahidiwa na Mheshimiwa Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Nne na wa Awamu ya Tano. Kwahiyo, tutaijenga.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, tunaomba utusomee tena hicho kiasi ulichosoma kwenye majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, ni shilingi 1,280.832 au shilingi bilioni 1.280.832.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Malapo, swali la nyongeza!

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba Mheshimiwa Waziri aniambie ni lini ujenzi huo utanza? Kwa sababu barabara hii imekuwa ikizungumzwa kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Swali la pili; *issue* hapo ni ku-sign mkataba ama ni pesa? Kwasababu tumekaa kwenye kikao cha RCC ingawa Meneja wa TANROADS Mkoa alishindwa kusema wazi, lakini kinachoonekana pesa hakuna. Kwahiyo, *issue* ya msingi naomba kujua; ni kwamba mkataba haujasainiwa ama pesa zinazofanya mkataba usainiwe hazipo? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, Tunza Issa Malapo, kwa niaba ya Wabunge wote wa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu walikuwa na kikao cha RCC na walikataa kujadili barabara hii wakataka ije ijadiliwe hapa Bungeni. Naomba nikuhakikishie, hamna sababu ya kujadili hapa Bungeni. Barabara hii imetengewa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017 barabara hii imetengewa fedha tutakayohakikisha hizo kilometa 50 zinajengwa. Tunachosubiri ni taratibu za mkandarasi ku-sign mkataba kukamilishwa. Fedha zimetengwa! *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Tuendeleo. Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, swali lake liitaulizwa na Mheshimiwa Rashid Chuachua.

Na. 39

Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano

MHE. RASHID M. CHUACHUA (K.n.y. MHE. JEROME D. BWANAUSI) aliuliza:-

Kulikuwa na ahadi ya Serikali ya kujenga minara ya mawasiliano katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji.

(a) Je, ni lini wananchi wa Kata ya Mchauro, Mkundi na Sindano watajengewa minara ili kurahisisha mawasiliano?

(b) Je, ni utaratibu gani unaotumika ili waliotoa maeneo yao na kijiji husika wapate ushuru kutoka kwenye Kampuni iliyojenga mnara?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Rivango kutoka katika Kata ya Mchauro, pamoja na Kijiji cha Luatala kutoka katika Kata ya Sindano na Vijiji vya Chipango, Mkoropola, Nakachindu na Kijiji cha Nakalola kutoka katika Kata ya Mikundi vimeshapata huduma ya mawasiliano kupitia utekelezaji wa Awamu ya kwanza ya mradi wa Kampuni ya Simu ya Viettel.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vya Lichehe, Sindano kutoka katika Kata ya Sindano na vijiji vya Maparawe, Mkowo Mwitika na Nangomwa kutoka katika Kata ya Mchauro vipo katika orodha ya miradi ya Viettel inayotegemewa kutekelezwa katika Awamu ya Pili na ya Tatu iliyoanza Novemba, 2015 na kutarajiwa kukamilika Novemba, 2017. *(Kicheko/Makofi)*

Aidha, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imevijumuisha Vijiji vya Mchauro, Mhata, Mirewe na Namwombe katika orodha ya miradi ya siku za usoni itakayotekelezwa na mfuko katika mwaka wa fedha 2016/2017 kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Kicheko/Makofi)*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kiutaratibu kampuni inayotaka kujenga mnara huingia mkataba na mwananchi mwenye eneo husika na hukubaliana kiasi cha malipo kwa mwezi kwa muda wa mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama kuna wananchi walitoa maeneo yao kwa makubaliano ya kulipwa, basi wafatilie utekelezaji wa mkataba wao na kampuni husika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chuachua, swali la nyongeza!

MHE. MOHAMED R. CHUACHUA: Ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali yafuatayo ya nyongeza:-

Swali la kwanza, je, Serikali sasa haioni haja ya kuingilia kati na kutoa mwongozo kwa makampuni haya ambayo ni wawekezaji ili waweze kuwalipa wananchi hawa wanaotoa maeneo yao kwa kiwango kinachostahili, kwa sababu wengi wao hawajui thamani ya uwekezaji huo?

Swali la pili, katika eneo la Mji wa Masasi au Jimbo la Masasi, maeneo ya pembezoni karibu yote hayana mawasiliano, je, ni lini Serikali itajenga minara katika Kata za Marika, Mombaka, Temeke, Matawale, Surulu, Mwenge Mtapika pamoja na Chanika Nguo? Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, labda nitumie fursa hii kutoa wito kwa wananchi wote wanapofanya mikataba na wawekezaji mbalimbali wapate huduma ya ushauri kutoka kwa Wanasheria pamoja na wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mkataba umesainiwa kati ya kijiji na wananchi hata kama haukufata ushauri na pengine siyo mzuri kwa wale wanakijiji, ni ngumu kuwalazimisha upande mmoja katika mkataba kurekebisha, kwa sababu ni kinyume cha misingi ya mkataba.

Kwa hiyo, tutachunguza mkataba uliopo wa kijiji hiki kuona kama tunaweza wao wawili waliokubaliana wanaweza kukubali wakarekebisha ili waboreshe kile ambacho wananchi watakipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali la pili, amenipa orodha ndefu. Kama Serikali naomba tupewe nafasi, hiyo orodha tuiwasilishe kwenye makampuni mbalimbali ambayo yanatoa hiyo huduma tuone kampuni ipi itakuwa tayari kujenga minara katika maeneo hayo au kupitia mfuko wetu wa Mawasiliano kwa Wote halafu tutamjulisha kwa maandishi.

NAIBU SPIKA: Tuendeleo na swali la mwisho, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 40

Ujenzi wa Barabara ya Kidahwe - Kasulu - Nyakanazi

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya Kidahwe – Kasulu – Nyakanazi itakamilika kwa lami?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Kigoma - Kidahwe - Kasulu hadi Nyakanazi yenye urefu wa kilometa 330 unafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha ambapo sehemu ya barabara hii kutoka Kigoma hadi Kidahwe yenye urefu wa kilometa 28.2 imejengwa kwa kiwango cha lami na kukamilika, sehemu ya Kidahwe - Kasulu yenye urefu wa kilometa 50 na sehemu Kibondo - Kakonko mpaka Nyakanazi yenye urefu wa kilometa 50 zinaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami.

Aidha, kazi ya kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu zilizobaki kati ya Nyakanazi na Kasulu, pamoja na barabara ya Kasulu hadi Manyovu zenye jumla ya kilometa 250 inatarajiwa kuanza Aprili, 2016 kwa kutumia fedha za NEPAD kupitia Benki ya maendeleo ya Afrika chini ya utaratibu wa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara hii inatarajiwa kuanza baada ya kukamilika kwa mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Genzabuke, swali la nyongeza!

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya barabara hii, lakini hazipelekwi. Mara tatu mfululizo imekuwa ikitenga fedha hazipelekwi; mara ya kwanza shilingi bilioni nne; mara ya pili mwaka 2015/2016 zilitengwa shilingi bilioni 10 hazikwenda.

Je Serikali inaweza kulihakikishia Bunge hili na wananchi wa Mkoa wa Kigoma kuwa fedha zitatengwa sasa na kupelekwa Kigoma ili barabara hii iweze kukamilika? *(Makofi)*

Swali langu la pili, Kidahwe – Kasulu kuna mkandarasi ambaye yupo pale lakini amesimama kwa sababu hajaweza kulipwa fedha zake. Je, ni lini mkandarasi huyo atalipwa ili aweze kuendelea na kazi ya ujenzi wa barabara hiyo? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sehemu ya swali lake la kwanza naomba kuthibitisha kwamba ndivyo itakavyokuwa.

Kwa swali lake la pili, naomba kumhakikishia kwamba wakandarasi wote Tanzania nzima tumeshaanza kuwalipa madai yao ikiwa ni pamoja na huyo mkandarasi. Kwa hiyo, muda siyo mrefu huyu mkandarasi atarudi *site* na kuanza kukamilisha hiyo kazi.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mwongozo wa Spika!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa naomba ukae. Kuna matangazo kidogo hapa. Tangazo la kwanza linahusu wageni.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni hawa wafuatao; wageni 68 kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu ambao ni Wakuu wa Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Ofisi hiyo pamoja na Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi na Watumishi wengine wakiongozwa na Ndugu Uledi Musa, Katibu Mkuu, Waziri Mkuu na Bunge.

Mwingine ni Dkt. Hamis Mwinyimvua, Katibu Mkuu, Sera na Uratibu; mwingine ni Ndugu Erick Shitindi, Katibu Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu; mwingine ni Jaji Francis Mutungi, Msajili wa Vyama vya Siasa; mwingine ni Dkt. Fatma Mrisho, Mwenyekiti Mtendaji - TACAIDS. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia kuna mgeni wa Mheshimiwa Suzan Masele, Mbunge wa Viti Maalum Mkao wa Mwanza, anaitwa Ndugu Baraka Ekigo.

Wageni wa Mheshimiwa Kunti Majala, Mbunge wa Viti Maalum ambao ni Madiwani wa Halmashauri ya Chemba; kuna Mheshimiwa Stumai Bakari, Mheshimiwa Athuman Kidunda, Mheshimiwa Idd Kibonge, Mheshimiwa Siraji Bakari na Mheshimiwa Fatma Issa.

Mgeni mwingine ni wa Mheshimiwa Yosepher F. Komba, Mbunge wa Viti Maalum Tanga na mgeni wake anaitwa Jaffary Ndege ambaye ni Mratibu wa CHASO Morogoro.

Wageni wengine ni wanafunzi 45 na walimu watano kutoka shule ya msingi Feza ya Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni viongozi 57 kutoka umoja wa Serikali za Wanafunzi kutoka Vyuo vya Elimu ya Juu Tanzania, yaani *TAHLISO*, karibuni sana.

Pia tunao wanafunzi 87 na Walimu wao 13 kutoka shule ya msingi Ebenezer. Japo siwaoni, naona tangazo lao liko hapa. *(Makofi)*

Tangazo lingine, Ofisi ya Katibu wa Bunge inawajulisha Waheshimiwa Wabunge wote ambao hawajachukua hati zao za kusafiria (*passport*) kufika Idara ya Uhusiano wa Kimataifa na Itifaki kwa ajili ya kuzichukua. Kwahiyo, waende wakachukue.

Tangazo lingine, hili siyo tangazo ni maagizo kwa Naibu Waziri wa TAMISEMI; kulikuwa na tatizo kwenye Swali Na. 33, Mbunge aliyekuwa anauliza hili swali hatoki Arumeru, anatoka Rukwa. Kwa majibu yale yaliyokuwa yametolewa hapa yana takwimu za Mkoa wa Arusha. Kwa hiyo, hili swali litarudiwa tena, naomba utatayarisha hayo majibu Sekretarieti watalipanga. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, sasa anakuja kunipokea Mheshimiwa Spika ili tuendelee na hoja za Serikali.

MBUNGE FULANI: Mwongozo.

NAIBU SPIKA: Spika akiwa amesimama huwezi kusema Mwongozo.

Hapa Spika (Mheshimiwa Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

SPIKA: Katibu!

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI: Hoja za Serikali kwamba Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, Mwongozo!

SPIKA: Naomba nimkaribishe Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Amegoma!

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI zilizochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2016/2017.

Vile vile naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, huu ni Mkutano wa Bunge wa kujadili Bajeti ya Serikali baada ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba, 2015. Hivyo, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Watanzania kwa kuendelea kuwa na imani na Chama cha Mapinduzi na hivyo kukiwezesha kushinda na kukipa tena ridhaa ya kuunda Serikali na kuiongoza nchi yetu. *(Makofi)*

Aidha, kwa njia ya pekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuongoza Serikali ya Awamu ya Tano. Pia nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Vile vile nampongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Aidha, nampongeza Balozzi Seif Ally Idd kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, nawapongeza pia Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa kushika nyadhifa zao hizo muhimu. Nawahakikishia wananchi wote kwamba Serikali ya Awamu ya Tano itawatumikia kwa nguvu zake zote bila kujali itikadi zao za kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba kutumia fursa hii pia kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa kuniteua mimi kuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na uteuzi huo kuungwa mkono na

Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa asilimia 73. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi wote kwamba sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, Mbunge, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika.

Pia nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kila mmoja kwenye Jimbo lake kuwa wawakilishi wa wananchi katika Bunge hili. Jukumu lililo mbele yetu sote ni kuwatumikia wananchi waliotuchagua ili kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 nchi yetu imekumbwa na majanga mbalimbali yaliyosababisha vifo na uharibifu wa mali. Nitumie fursa hii kumwomba Mwenyezi Mungu awajalie wale walioumia kupona haraka na kurejea katika shughuli za ujenzi wa Taifa. Ninawapa pole wote waliofiwa na ndugu, jamaa na marafiki. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kupitia kwa kina Makadirio ya Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kipekee nitumie nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi inayoongozwa na Mheshimiwa Hasna Sudi Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini na Kamati ya bajeti inayoongozwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini. *(Makofi)*

Kamati hizo zimetoa mchango mkubwa wakati wa maandalizi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu. Pia naomba niwapongeze Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi kubwa ya kupitia makadirio ya sekta zote. Maoni na ushauri wao umesaidia sana katika kuboresha makadirio ya bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makadirio ya bajeti ninayowasilisha leo ni mwendelezo wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015. Ilani hiyo imeainisha ahadi ambazo Serikali ya Chama cha Mapinduzi itazitekeleza katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Aidha, makadirio ya bajeti yamezingatia ahadi za Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania alizozitoa wakati wa kampeni na katika uzinduzi wa Bunge la Kumi na Moja tarehe 20 Novemba, 2015. Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kujenga Taifa imara lenye uchumi na maendeleo ya watu katika Kanda ya Afrika Mashariki na Barani Afrika kwa ujumla. *(Makofi)*

Mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano, kabla ya kuwasilisha mapitio ya kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na mwelekeo kwa mwaka 2016/2017, niruhusu kupitia Bunge lako Tukufu niwakumbushe Watanzania wote kuhusu dhima ya Serikali ya Awamu ya Tano yenye falsafa ya Hapa Kazi Tu. Sote tunatambua kwamba ili Tanzania ifikie nchi yenye uchumi wa kipato cha kati, ifikapo mwaka 2025 ni sharti kila mmoja wetu afanye kazi kwa bidii, maarifa na ubunifu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, ili yawepo mapinduzi ya kweli ya kuelekea kwenye uchumi wa kati tunaodhamiria, ni lazima tuimarisha uwajibikaji wa maadili kwa viongozi, watendaji kwa kila Mtanzania. Sote tumeshuhudia hatua zilizochokuliwa na Serikali dhidi ya watumishi wasio waadilifu wanaotumia fedha za umma au madaraka yao vibaya na kukwamisha utekelezaji wa mipango ya maendeleo tuliyojiwekea. Hatutaweza kufikia uchumi wa kati unaoendeshwa kwa viwanda kama tutaendelea kulea uzembe, ubadhirifu, uvivu na kukwepa wajibu wetu. Ndiyo maana tumeanza kwa nguvu kuimarisha nidhamu, uwajibikaji na matumizi sahihi ya fedha za umma ili zielekezwe kwenye shughuli za manufaa kwa Watanzania walio wengi na siyo vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuimarisha ufanisi na tija ndani ya utumishi wa umma tumebaini kuwa changamoto ya utamaduni usioridhisha wa ufanyaji kazi upo katika sekta zote za umma na binafsi; wizi, uzembe, udhuru kwa kila siku na huduma mbaya kwa wateja ni baadhi ya malalamiko ya wawekezaji hapa nchini. Tabia hizi ni lazima zikemewe kama tunataka nguvukazi yetu ipate ajira katika zama hizi tunazohamasisha mapinduzi ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, ni wajibu wa kila mmoja wetu katika jamii kusimamia maadili na makuzi ya vijana ili nguvukazi iweze kutumika ipasavyo katika kuchangia ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, imani yetu ni kwamba tumeanza vizuri kwenye suala la kuongeza uwajibikaji na maadili ndani ya Serikali. Serikali itaendelea kuwawajibisha wale wote ambao hawataendana na falsafa na mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano. Jambo la msingi ni kwamba tutachukua hatua kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie Watanzania kwamba hakuna mtumishi au mwananchi atakayeonewa au kunyanyaswa katika zoezi hili. Wale wote ambao wako safi waendeleo kufimiza wajibu wao bila uwoga. Kazi zifanyike kwa weledi na kwa kasi bila urasimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua hatua za kuongeza mapato na kuziba mianya ya ukwepaji kodi ambazo zimeonesha manufaa makubwa. Mathalani hatua tulizochukua za kubana mianya ya ukwepaji kodi zimeimarisha makusanyo na mapato ya ndani kutoka wastani wa shilingi bilioni 870 mwezi Novemba, 2015 na kufikia shilingi trilioni 1.3 mwezi Machi, 2016. Tunaendelea na kuimarisha ukusanyaji mapato kwa njia za kielektroniki, kuziba mianya ya ukwepaji kodi na kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kila anayetakiwa kulipa kodi alipe na fedha hizo zitumike kutekeleza mipango ya maendeleo.

Vilevile Serikali itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kusimamia matumizi sahihi ya rasilimali. Fedha zinazopatikana zitaelekezwa kwenye miradi ya kipaumbele yenye kuleta maendeleo ya haraka kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa viwanda utajengwa na sekta binafsi. Kazi ya Serikali ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na mazingira rafiki kwa sekta hiyo kuwekeza. Hivyo Serikali itaendelea kubuni na kutekeleza miradi itakayoweza sekta binafsi kuwekeza bila vikwazo. Miradi hiyo ni pamoja na miundombinu muhimu ya uchukuzi, usafirishaji, umeme, mawasiliano na maji kwa ajili ya uzalishaji na biashara.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwahakikishia wawekezaji wote nchini na wengine wanaokusudia kuja kuwekeza kwamba Serikali imedhamiria kushirikiana kwa karibu na sekta binafsi, hatua zote zinazochukuliwa sasa ni za kuhakikisha kwamba sekta binafsi inawekewa mazingira wezeshi na yenye ushindani wa haki ili iweze kuimarika.

Mheshimiwa Spika, mtangamano wa kisiasa ni nguzo muhimu sana katika kujenga nchi yenye maendeleo makubwa na ya uhakika. Mtangamano wa kisiasa unajumuisha siasa safi za kiustaarabu na zinazoheshimu mawazo ya kila mmoja wetu. Siasa za aina hii ndiyo chimbuko la mustakabali wa amani na utulivu wa Taifa letu tangu tujipatie uhuru.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la faraja na la kufurahisha kwamba pamoja na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 kujaa ushindani mkubwa, Taifa letu limeendelea kuwa na amani, utulivu na mshikamano mkubwa kitaifa kiasi cha

kupigiwa mfano Barani Afrika na duniani kwa ujumla. Hali hii inaonesha kukua na kuimarika kwa demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini ambapo hadi sasa vipo vyama 22 vyenye usajili wa kudumu na Vyama vitatu vyenye usajili wa muda na vingine sita vimewasilisha maombi ya kupata usajili wa muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 umesaidia sana kupima namna demokrasia inavyozidi kukua na kupanuka, kwani kwa mara ya kwanza kulikuwa na mwitikio mkubwa wa kujitokeza kwa wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi na wananchi wengi kujiandikisha kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, vyama vinane vilisimamisha wagombea wa nafasi ya Urais na vyama 22 vilisimamisha Ubunge na Udiwani. Idadi ya wapigakura waliojiandikisha kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilikuwa ni 23,161,440 sawa na 96.9% ya makadirio. Idadi ya watu waliopiga kura ilikuwa ni milioni 15,596,110 sawa na 67.3% ya waliojiandikisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni iadai kubwa ya wapigakura ikilinganishwa na chaguzi zote zilizopita. Hivyo, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Tume ya Uchaguzi ya Taifa kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya kuanzia katika uboreshaji wa daftari la wapigakura, ugawaji wa Majimbo mapya ya uchaguzi, kutoa elimu kwa umma, uandikishaji wa wapigakura na kuusimamia kwa umakini mkubwa uchaguzi wenyewe na kutangaza matokeo. Tume ilifanya kazi yake kwa uhuru na kwa weledi mkubwa. Nawapongeza viongozi na wananchi wote walioshiriki uchaguzi huo kwa amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Tume ya Uchaguzi na wananchi kuitikia wito wa kujiandikisha na kupiga kura, bado kulikuwa na idadi kubwa ya waliojiandikisha, lakini hawakupiga kura. Naiagiza Tume ya Uchaguzi kufanya tathmini ya kina kubaini sababu zilizowafanya wapigakura zaidi ya 7,000,000 waliojiandikisha kupiga kura kutoitumia haki yao ya Kikatiba. Hii itasaidia kuboresha chaguzi zijazo, kwani wananchi wana wajibu wa kutumia haki yao ya msingi kuchagua viongozi wanaowataka. *(Makofi)*

Aidha, tathmini itasaidia sana kubaini iwapo kuna vikwazo vinavyowazuia baadhi ya watu kupiga kura ili kwa pamoja tuweze kuviondoa. Ndani ya Bunge hili tupo Wabunge wa vyama mbalimbali, lakini kwa lengo moja tu la kuwawakilisha wananchi wetu na kuishauri Serikali ili ipange mipango mizuri itakayoharakisha maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba Uchaguzi Mkuu umekwisha na Serikali zetu zipo madarakani kwa mujibu wa Katiba. Hivyo, tuienzi falsafa ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania ya Hapa Kazi Tu kwa kuchapa kazi na tusitoe nafasi kwa tofauti zetu za kisiasa na kiitikadi kuwa kisingizio cha kukwamisha shughuli za maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano, ni kuendeleza kukuza demokrasia ili kuwezesha ushiriki mpana wa wananchi katika kufanya maamuzi ya maendeleo yao katika Taifa letu chini ya mfumo wa vyama vingi vya siasa. Hivyo, Serikali inaandaa Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya Mwaka 1992 na Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya Mwaka 2010 kwa lengo la kuondoa changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wake na kuzifanya ziendane na hali halisi ya siasa nchini na kwa mtazamo wa baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malengo yetu ya kufikia nchi ya kipato cha kati na kufanyika mapinduzi makubwa ya viwanda, yanategemea sana utulivu wa uchumi. Kwa ujumla ukuaji wa uchumi umekuwa wa kuridhisha kwani mwaka 2015 uchumi ulikuwa kwa 7.1% ikilinganishwa na ukuaji wa 7% kwa mwaka 2014. Sekta zilizochangia katika ukuaji huo ni pamoja na ujenzi, mawasiliano, fedha, uchukuzi na nishati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukuaji huu mzuri wa ujumla, Sekta ya Kilimo inayoajiri zaidi ya 66.3% ya Watanzania wote wanaofanya kazi ilikua kwa 3.4% tu kwa mwaka 2014. Ukuaji huo ni mdogo, unamaanisha kwamba juhudi za ziada na kubwa zinahitajika ili sekta hii muhimu iweze kutoa mchango mkubwa zaidi wakati tunapotekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo. Historia ya maendeleo ya uchumi inatuambia kwamba, sekta ya kilimo ina mchango mkubwa na muhimu wenye mapinduzi ya viwanda. Hivyo, hatuna uchaguzi mwingine bali, kulekeza nguvu zaidi kwenye sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla tutahitajika kuongeza ufanisi na tija katika sekta zote za uzalishaji na utoaji huduma ili malengo yetu ya ukuaji uchumi yaweze kufikiwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Katika kufikia azma hii, tutaelekeza sera madhubuti za fedha na kodi zitakazowezesha mfumuko wa bei kuendelea kushuka na kubaki katika tarakimu moja kama ilivyo sasa. Mathalani mfumuko wa bei mwaka 2015 ulifikia wastani wa 5.6% ikilinganishwa na wastani wa 6.1% kwa mwaka 2014. Mwelekeo huu wa utulivu wa uchumi utavutia mitaji mingi kutoka sekta binafsi kuwekeza kwenye sekta za kipaumbele kuwezesha ongezeko la ajira na kupanua wigo wa ulipaji kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali nilidokeza kwamba uwekezaji kwenye viwanda na sekta nyingine za kiuchumi utafanywa na sekta binafsi na jukumu la msingi la Serikali ni kuweka mazingira wezeshi. Kwa msingi huo, Serikali ya awamu ya tano

itachukua hatua madhubuti na za haraka kupunguza muda, gharama na idadi ya taratibu za kiutawala ambazo wafanyabiashara na wawekezaji hulazimika kuzifuata ili kufanya biashara hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, taratibu zinapokuwa ngumu ndefu husababisha ongezeko la gharama za kufanya biashara na hivyo kuwakatisha tamaa wawekezaji wetu. Taarifa ya wepesi wa kufanya biashara duniani inayotolewa na Benki ya Dunia iliyochapishwa mwezi Novemba, 2015 inaonesha kwamba katika mwaka wa 2016 Tanzania imeshika nafasi ya 139 kati ya nchi 189 duniani. Hali hii haikubaliki kabisa, hivyo eneo hili ni lazima lifanyiwe kazi kwa haraka ili kuharakisha mapinduzi ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali itaimarisha utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini. Utekelezaji huo utazingatia maelekeo aliyoyatoa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa Mkutano na Wafanyabiashara uliofanyika mwezi Disemba, 2015.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huo pamoja na mambo mengine Mheshimiwa Rais aliwataka Watendaji kupunguza urasimu usio wa lazima kwa wafanyabiashara na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwataka Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuyatumia Mabaraza ya Biashara ya Mikoa na Wilaya ili kuhakikisha juhudi shirikishi za uboreshaji wa mazingira ya biashara zinatekelezwa hadi ngazi ya chini. Pia nawataka watumishi wa umma kuepuka kuwachelewesha kwa uzembe au makusudi wawekezaji wenye nia njema ya kuwekeza nchini ili kuleta maendeleo endelevu kwa wakati. Mtumishi yeyote wa umma atakayeendeleza urasimu usio wa lazima, hatavumiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, azma ya kuwawezesha Watanzania kushiriki kikamilifu kwenye uchumi wa viwanda ni jambo la msingi. Hivyo basi, Serikali itaendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kuwadhamini wajasiriamali wenye miradi itakayokidhi vigezo kwenye taasisi za fedha ili wapate mikopo yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo, mpango maalum wa ushiriki wa Watanzania katika miradi mikubwa ya uwekezaji ulioandaliwa utatekelezwa sasa. Mpango huo unalenga kuhakikisha kwamba Watanzania wananufaika zaidi na rasilimali za nchi yao kwa njia ya ubia kwenye miradi ya uwekezaji, ajira na kandarasi mbalimbali zitakazotolewa na kampuni kubwa kwa wazawa.

Mheshimiwa Spika, wananchi pia, wataendelea kuwezesha kupitia mikopo yenye masharti nafuu kwa vikundi mbalimbali vya kiuchumi vya wakulima, wafugaji, wavuvi, wafanyabiashara na wachimbaji wadogo wa madini inayotolewa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Serikali imeruhusu mifuko hiyo kutoa mikopo nafuu kwa wanachama wa vikundi vinavyojiunga na mifuko, kunufaika na Mafao ya Afya na Pensheni yanayotolewa na mifuko husika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali imehamasisha uanzishaji na usajili wa vikundi vya kiuchumi kama vile Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa (SACCOS) na Benki za Jamii Vijijini (VICOBA). Serikali pia imesimamia uanzishwaji wa taasisi mwamvuli ya kusimamia VICOBA inayoitwa VICOBAFETA. Takwimu zilizotolewa mwezi Februari, 2016 Na taasisi hiyo zilionesha kuwa kuna vikundi 100,000 vya VICOBA vyenye wanachama milioni 2.2 na mtaji wa shilingi trilioni 1.2. Ni jambo la kujivunia kwamba 79% ya wanachama wa VICOBA ni wanawake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, moja ya ahadi muhimu iliyopo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 ni kutenga Shilingi milioni 50 kwa kila kijiji nchini zitakazotumika kwa utaratibu wa mzunguko (Revolving Fund). Lengo ni kuwawezesha wananchi kuanzisha na kuendeleza shughuli za uzalishaji kupitia ushirika wa kuweka na kukopa na vikundi vingine vya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, uhakiki wa Vyama vya Ushirika wa Kuweka na Kukopa uliofanywa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika unaonesha kwamba idadi ya SACCOS zinazokidhi vigezo vya usajili nchini imepungua kutoa 5,559 mwaka 2013 hadi 3,856 mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, kati ya hizo SACCOS 2,125 sawa na 55% zipo vijijini na SACCOS 1,740 ziko mijini. Ni dhahiri kwamba mpango wa Shilingi milioni 50 kwa kila kijiji unahitaji maandalizi mazuri ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uanzishaji wa usajili wa SACCOS na vikundi vya kiuchumi vinavyokidhi vigezo ili kuhakikisha kwamba fedha zinzotolewa zinawafikia walengwa na zinatumiwa kwa shughuli zilizokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ninaziagiza Halmashauri zote nchini ziweke orodha sahihi za Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa vilivyosajiliwa kwa kila kijiji na kuchukua hatua za kuwezesha uanzishaji wa usajili wa SACCOS zinazokidhi vigezo kulingana shughuli za uzalishaji katika Halmashauri husika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba maandalizi ya utekelezaji wa mpango huo yanaendelea vizuri katika kila Halmashauri. Tutatumia uzoefu uliopatikana kwenye utekelezaji wa mifuko

mingine ukiwemo Mfuko wa Kuwawezesha Wananchi wa Kuongeza Fursa za Ajira, maarufu kama Mabilioni ya JK ili changamoto zilizokuwa zimejitokeza zitusaidie kuboresha mpango huu mpya.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuziwezesha kaya maskini ili ziweze kupata mahitaji yao ya msingi na kuongeza kipato kupitia Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii – TASAF. Tangu utekelezaji wa mpango huu uanze, kaya maskini 1,099,289 zimepokea kiasi cha shilingi bilioni 164.8 kama ruzuku katika Halmashauri 159 za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Aidha, kupitia mpango wa ajira wa muda wa kaya maskini, iliandaliwa miradi 1,880 yenye thamani ya shilingi bilioni 42.6 kutoka Halmashauri 40 za Tanzania Bara na Zanzibar. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali itaendelea kufanya utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini katika maeneo ambayo hayakufikiwa.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 imeweka umuhimu katika kupanua fursa za ajira kwa kutumia rasilimali zilizopo nchini ili kila mwenye uwezo wa kufanya kazi achangie kwenye uchumi na kupata kipato halali. Msisitizo huo huo wa Ilani ya Uchaguzi unatokana na ukweli kwamba utafiti wa hali ya ajira nchini wa mwaka 2014 umeonesha kuwa kiwango cha ukosefu wa ajira kimepungua kutoka 11.7% mwaka 2006 hadi 10.3% mwaka 2014. Aidha, ukosefu wa ajira kwa vijana umepungua kutoka 14.2% mwaka 2006 hadi 11.7% mwaka 2014. Kiwango hicho bado ni kikubwa na tunaweza kufanya vizuri zaidi. Jitihada za Serikali za kuvutia uwekezaji kwenye sekta mbalimbali na urasimishaji wa sekta hiyo isiyo rasmi, zitaendelezwa ili kupunguza zaidi kiwango cha ukosefu wa ajira nchini.

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto zinazosababisha ukosefu wa ajira ni vijana wetu kutojengewa maarifa na ujuzi wa kuajiriwa na kuajirika. Hivyo, Serikali itaendelea kutekeleza programu ya miaka mitano ya kukuza ujuzi nchini kwa mwaka 2015/2016 hadi mwaka 2019/2020. Programu hiyo inayolenga kuongeza idadi ya watu wenye kiwango cha juu cha ujuzi kutoka 3% ya sasa hadi 12% inayotakiwa kuendesha uchumi wa viwanda. Vilevile kupunguza idadi ya watu wenye kiwango cha ujuzi wa chini kutoka 75% ya sasa hadi 54%. Utekelezaji wa programu hiyo, utasaidia sana kupunguza pengo la mahitaji ya rasilimali watu nchini ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya haraka ya uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, Serikali itahakikisha kuwa suala la ukuzaji ajira linazingatiwa katika mipango yote ya uwekezaji pamoja na mipango ya maendeleo ya kissekta katika ngazi zote. Hivyo, naziielekeza Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi za Umma, Mikoa na Mamlaka ya

Serikali za Mitaa kuhakikisha ukuzaji wa ajira unakuwa ni ajenda ya msingi ya kudumu katika utekelezaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo. Tayari Mheshimiwa Rais amewaagiza Wakuu wa Mikoa kuhakikisha kwamba vijana ambao ndio nguvu kazi ya Taifa wanatumia fursa inayopatikana kutokana na shilingi milioni 50 zitakazotolewa kwa kila kijiji kuanzisha miradi ya maendeleo ya kujipatia kipato chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana ni hazina na rasilimali watu muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 inaonesha kuwa idadi ya vijana wenye umri kati ya miaka 15 na 35 ni takribani milioni 16.2 sawa na asilimia 35.1 ya Watanzania wote. Aidha, utafiti wa nguvu kazi wa mwaka 2014 unaonesha kuwa vijana ni asilimia 59 ya nguvukazi ya Taifa. Matokeo ya tafiti hizo yanathibitisha kuwa kuna umuhimu wa kuzingatia mahitaji ya vijana na ushirikishwaji wao katika mipango ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 hadi 2015/2016 Serikali imewawezesha vijana kiuchumi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.6 imetolewa na mfuko huo kwa vikundi kwa vijana 284 na mafunzo yametolewa kwa viongozi wa vikundi 2,552 kutoka Halmashauri 59. Vilevile Serikali imetenga maeneo maalum ya shughuli za kiuchumi na huduma kwa vijana katika Halmashauri 30 nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha dhana ya ushiriki na ushirikishwaji wa vijana katika shughuli za maendeleo, Bunge la Kumi lilitunga Sheria Na.12 ya Baraza la Taifa la Vijana ya mwaka 2015. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba sasa kanuni za utekelezaji wa sheria hiyo zimekamilika na hivyo katika mwaka wa 2016/2017 Serikali itaendelea kuratibu uanzishwaji wa Baraza la Vijana la Taifa na kuhimiza uanzishaji na uimarishaji wa SACCOS za vijana katika Halmashauri zote nchini na kuziwezesha kupitia Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Vijana na Taasisi za Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maadili na makuzi ya vijana ni suala linalopewa kipaumbele na Serikali ya Awamu ya Tano. Hatuwezi kujenga uchumi imara wa viwanda, kuongeza fursa za ajira na kuwa na matumizi sahihi ya rasilimali za Umma kama Jamii yetu hasa vijana hawajajitambua na kuwa waadilifu, wazalendo na wachapakazi. Serikali itaendelea kuratibu utekelezaji wa programu ya Stadi za Maisha za Programu ya kujitolea kwa vijana ili kukuza maadili, uzalendo na kujenga utamaduni wa kuchapa kazi kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inathamini mchango mkubwa wa watu wenye ulemavu katika maendeleo na kwamba wana haki sawa ya kutumikia nchi hii

na kutumia fursa mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Katika kuzingatia azima hiyo, Serikali inatekeleza sheria ya watu wenye ulemavu namba tisa ya mwaka 2010 ambayo imewezesha kuundwa kwa Baraza la Kitaifa la Ushauri la Watu Wenye Ulemavu ili kuongeza ushiriki wa watu wenye ulemavu katika maamuzi na mambo mengine.

Aidha, Kamati ya kushughulikia masuala ya watu wenye ulemavu zimeundwa katika ngazi za Mikoza, Halmashauri, Kata, Mitaa na Vijiji kwa ajili ya kuratibu masuala muhimu ya watu wenye ulemavu katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali kuwalinda na kuwapatia fursa, kumekuwepo na matukio ya vitendo vya ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu hususan wenye ualibino. Ukatili huo umesababisha watu wenye ualibino kupoteza maisha na wengine kupata aina nyingine ya ulemavu wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo haikubaliki na haivumiliki katika jamii ya Watanzania. Serikali inafanya jitihada kubwa kukomesha vitendo hivyo ikiwa ni pamoja na kuwakamata wote wanaojihusisha na vitendo hivyo na kuwafikisha katika vyombo vya sheria. Aidha, tutaendelea kutoa elimu kwa jamii ili kubadili mitazamo na imani potofu kuhusu watu wenye ualibino na ulemavu kwa ujumla. Napenda kusisitiza kwamba watu wenye ulemavu wana haki ya kuthaminiwa utu wao na kulindwa dhidi ya ukatili wa aina yoyote ya ubaguzi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali itaviboresha Vyuvo vya Ufundi na Maendeleo (*Vocational and Rehabilitation Training Centers*) vya watu wenye ulemavu nchini ili kutoa ujuzi unaoendana na mahitaji yao katika soko la ajira. Serikali pia itaandaa walimu wa elimu maalum na kutoa vifaa visaidizi kwa walimu na wanafunzi wenye ulemavu mashuleni. Kwa sasa Serikali imeanzisha utaratibu wa kuwahabarisha watu wenye usikifu hafifu kwa kuanzisha tafsiri za matangazo kwa njia za alama. Hivyo, wamiliki wote wenye *television* wametakiwa kujiri wakalimani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa sheria na viwango vya kazi kwa kufanya kaguzi ili kuhakikisha kwamba waajiri wanazingatia mikataba ya ajira na wanazingatia pia masaa ya kazi, likizo na ujira kwa lengo la kupunguza migogora na kuongeza tija.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2016 jumla ya kaguzi za kazi 1,305 zilifanyika na migomo 23 katika sekta za usafirishaji, viwanda, ujenzi na kwenye migodi ilisuluhishwa na kupatiwa ufumbuzi. Aidha, kaguzi za kawaida

4,670 na kaguzi maalum 17,005 zilizojumuishia kaguzi za umeme, mitambo, vipimo vya mazingira ili kuhakikisha wafanyakazi wanakuwa na afya njema na usalama mahali pa kazi zilifanyika pia.

Mheshimiwa Spika, Sheria za Kuratibu Ajira ya Wageni Na.1 ya mwaka 2015 ilitungwa na kumpa Kamishna wa Kazi mamlaka ya kutoa vibali vya kazi nchini ili kukuza fursa za ajira kwa Watanzania. Tangu sheria hiyo ianze kutumika rasmi tarehe 15 Septemba, 2015 hadi mwezi Machi, 2016 mapato yaliyopatikana kutokana na vibali vya kazi vilivyotolewa nchini ni shilingi bilioni 21.1, sawa na asilimia 356 ya lengo la makadirio ya shilingi bilioni 7.5 kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imefanya kaguzi katika makampuni na taasisi 400 zenye jumla ya wageni 3,939 na kubaini wageni 779 kuwa hawana vibali vya kuishi na kufanya kazi nchini. Kati ya hao, wageni 29 waliondolewa nchini, wageni 317 walipewa hati maalum (*special pass*), 77 walifikishwa mahakamani na 356 walielekezwa kukamilisha taratibu za ukaazi wao kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Sheria ya Uhamiaji. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali itafanya kaguzi za kazi 56,200 katika maeneo mbalimbali ya kazi nchini na itaanzisha Bodi mbili za kupanga kima cha chini cha mishahara kwa sekta ya umma na binafsi.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Hifadhi ya Jamii ina mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi yetu. Kwa kutambua hilo, Serikali imeifanyia tathmini mifuko sita ambayo ni *GEPF, LAPF, NHIF, NSSF, PPF* na *PSPF* kwa lengo la kupima uendelevu wake. Tathmini hiyo imebainisha kuwa mifuko hiyo bado ni endelevu na rasilimali zake zimefikia shilingi trilioni 8.8. Aidha, mamlaka ya usimamizi na uthibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii, imetoa miongozo ya kupunguza gharama za uendeshaji wa mifuko hiyo itakayoanza kutumika Julai, 2016. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha uhakiki wa madeni ya *PSPF* yaliyokiwepo kabla ya kuanzishwa kwa mfuko huo kwa mwaka 1999 yenye thamani ya shilingi trilioni 2.9. Hadi sasa Serikali imelipa sehemu ya deni la *PSPF* kiasi cha shilingi bilioni 180 ili kuhakikisha kwamba mafao ya wastaafu wa mfuko huo yanalipwa kwa wakati. Serikali pia itaendelea kulipa deni la shilingi bilioni 840.4 linalotokana na miradi ya Serikali inayogharamiwa na mifuko ya *GEPF, LAPF, NHIF, NSSF* na *PPF*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hadi sasa asilimia 6.5 ya Watanzania wote ndio wanaofikiwa na huduma ya hifadhi ya jamii. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali itaendelea kutekeleza Programu ya Maboresho ya Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa kuongeza wigo wa wanaofikiwa na huduma hiyo. Hii ni pamoja na

kujumuisha makundi mengine katika jamii kama vile wazee na watu wenye ulemavu ambapo rasimu ya andiko la mpango wa pensheni wa makundi hayo imeshakamilika.

Mheshimiwa Spika, hatua inayoendelea hivi sasa ni ushirikishwaji wa wadau na taasisi zinazohusika katika kutekeleza mpango huo. Aidha, Serikali itaendelea kuhamasiha uchangiaji wa hiari na kusimamia uendeshaji wa mifuko ya hifadhi jamii na kuhakikisha inaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kuchangia zaidi katika ukuzaji wa uchumi bila kuathiri mifuko yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee sekta ya uzalishaji mali, na hasa uzalishaji wa mazao ya akiba ya chakula. Sekta ya kilimo inayojumuisha uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na mazao ya misitu ndiyo tegemeo la maisha ya Watanzania walio wengi. Hata hivyo ukuaji wa sekta hiyo umekuwa siyo wa kuridhisha kutokana na matumizi ya teknolojia isiyoendana na wakati na pia kutegemea majaliwa ya Mwenyenzi Mungu ya hali ya hewa. Pamoja na changamoto hizo, hali ya upatikanaji wa chakula imeendelea kuwa ya kuridhisha katika maeneo mengi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa mwaka wa fedha 2014/2015 wakulima walizalisha tani milioni 15.5 za mazao ya chakula. Kutokana na uzalishaji huo, nchi imejisheheneza kwa chakula kwa asilimia 120 kwani mahitaji ya chakula kwa mwaka 2015/2016 ni tani milioni 12.95. Hali hii pia imetuwezesha katika msimu huu kutoa chakula cha msaada na cha bei nafuu katika maeneo yaliyopata upungufu wa chakula.

Aidha, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) iliiza jumla ya tani laki 239,322 ya akiba yake kwa wafanyabiashara nchini ili kukabiliana na mfumuko wa bei za vyakula hususan unga wa Sembe katika masoko ya mijini.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili mwaka 2016 NFRA ilikuwa na akiba ya tani 67,895 za chakula, katika mwaka wa 2016/2017 Serikali itanunua tani la 100,000 kwa ajili ya hifadhi ya chakula.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuleta mapinduzi katika sekta ya kilimo kwa kupanua na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji ili kuzalisha zaidi kwa ajili ya usalama wa chakula chetu, kuuza ziada nje na kupata malighafi za viwandani. Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2015 inalenga kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 461,326 za sasa hadi hekta 1,000,000 ifikapo mwaka 2020. Ili kufikia lengo hilo, Serikali itashirikiana na sekta binafsi katika kujenga, kukarabati na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji maji nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ongezeko la tija katika uzalishaji wa mazao unategemea sana kwa kiasi kikubwa matumizi ya pembejeo zikiwemo mbole na mbegu bora zenye ukinzani na ustahimilifu wa magonjwa na ukame, zenye uwezo mkubwa wa kutoa mavuno.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa mwaka 2015/2016 Serikali imetoa vocha milioni tatu za pembeje za kilimo zikiwemo tani 10,271 za mbegu bora za mahindi na mpunga na tani 99,923 za mbolea ambazo zimesambazwa katika Mikoa 24 ya Tanzania Bara na kunufaisha kaya 99,926. Ninawaagiza Wakuu wa Mikoa hiyo kuhakikisha kuwa pembejeo hizo zinawafikia walengwa kwa wakati na zinatumika kama ilivyotarajiwa na kuwachukulia hatua wale wote waliohujumu mpango huu na ambao pia watakaohujumu mpango huu.

Mheshimiwa Spika, mwezi Agosti, mwaka 2015 Serikali ilizindua Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili kuwawezesha wakulima kupata mikopo yenye riba nafuu. Benki hiyo inatoa mikopo ya muda mrefu, muda mfupi, lakini pia kwa riba nafuu kati ya 7% na 12% na imeanza na mtaji wa shilingi bilioni 60. Mikopo inayotolewa na Benki hiyo inalenga inasaidia kugharamia uandaaji wa mashamba, ununuzi wa pembejeo za kilimo, usindikaji wa mazao pamoja na hifadhi ya mazao.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuiongezea mtaji Benki hiyo ili ikopesheke na iweze kukopesha wakulima wengi zaidi hasa kupitia vikundi vya wanawake na vijana vinavyojihusisha na kilimo. Benki hiyo itasimamia kiasi cha Dola za Marekani milioni 25 kwa ajili ya kudhamini mabanki ya biashara ili yaongeze ukopeshaji kwenye mitaji, miradi, miundombinu ya masoko na kuendeleza ubunifu kwenye miradi ya maendeleo vijijini chini ya programu ya miundombinu ya masoko, uongezaji wa thamani, huduma za kifedha vijijini, vilevile benki hiyo itakuwa Wakala wa Serikali wa kusimamia fedha za ruzuku ya pembejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaimarisha utekelezaji wa Programu ya Miundombinu ya Masoko, uongezaji wa thamani na huduma za kifedha vijijini inayotekelezwa katika Mikoa yote Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Programu hiyo inasaidia sana kuboresha miundombinu ya masoko zikiwemo barabara na maghala ya kuhifadhia mazao, kuwawezesha wananchi waishio vijijini, kuongeza thamani ya mazao yao ya kilimo lakini pia kuwajengea uwezo wananchi, wa kuyafikia masoko na kupanua wigo wa huduma za kifedha vijijini.

Mheshimiwa Spika, chini ya programu hiyo, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Serikali imekarabari barabara vijijini zenye ulifu wa kilometa 180 kwa

kiwango cha changarawe, zikiwemo kilomita 63.6 za Zanzibar. Aidha, imejenga maghala matano yenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 za mazao kila moja na kuvijengea uwezo wa kufika masoko vikundi mia 780 vikiwemo vikundi 101 vya Tanzania Zanzibar. Vilevile imezijengea uwezo asasi ndogo za kifedha zikowemo SACCOS 291 na Benki tisa za wananchi ili ziweze kutoa huduma endelevu za kifedha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali itaendelea na uboreshaji wa miundombinu ya masoko, katika Halmashauri 38 za Tanzania Bara na Wilaya 10 za Zanzibar. Aidha, itaendelea kuwajengea wazalishaji wadogo uwezo wa kuhifadhi na kusindika mazao, mbinu za kufikia masoko na mfumo wa stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Spika, tunayo fursa ya kufanya mageuzi makubwa kwenye sekta ya mifugo kama tutawekeza kwenye viwanda vya kusindika nyama ili kuongeza thamani na kuzalisha bidhaa za aina mbalimbali kutokana na mifugo iliyopo nchini. Hali iliyoko sasa siyo nzuri kwani tunauza mifugo mingi nje ya nchi ikilinganishwa na nyama. Mathalan katika mwaka wa 2015/2016 hadi kufikia mwezi Machi, 2016 ng'ombe milioni 1.5, mbuzi milioni 1.2 na kondoo 235,243 wenye thamani ya shilingi bilioni 976.5 waliuzwa nje ya nchi. Hii ina maana kuwa mazao kama ngozi, kwato na damu za wanyama hao ambazo zingeweza kutumika kuzalisha bidhaa nyingine za viwandani yamekwenda nje badala ya kutumika hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaweza kabisa kugeuza hali hii haraka kwa kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani na mifugo. Nashauri wawekezaji binafsi kwenye sekta ya mifugo kuchangamkia fursa ya kufufua viwanda vya nyama vilivyopo na kujenga vingine vipya ili kuongeza thamani ya mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuanze kubadili fikra za wafugaji ili ufugaji uwe wa tija kwa kuwa idadi ndogo ya mifugo yenye ubora wa kisasa na inayoendana na uwezo wa eneo la malisho. Serikali itaweka msisitizo wa kipekee katika kuboresha sekta za mifugo ili kuzalisha mifugo yenye tija kwa kusambaza ng'ombe bora kwa ajili ya uzalishaji wa mazao, maziwa na nyama kutoka katika mashamba ya kuzalisha mifugo na kuimarisha uwekezaji katika viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo. Vilevile juhudi za kudhibiti magonjwa ya mifugo yasiyokuwa na mipaka na yenye athari kubwa katika uchumi wa Taifa zitaongezwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kufanya tathimini ya uendeshaji wa ranchi za Taifa, zilizobinafsishwa ili kuhakikisha kwamba wale waliopewa vitalu

vya mifugo wanavitumia kwa mujibu wa mikataba ya mauzo au vinginevyo tutawanyang'anya na kuwapa wengine wenye uwezo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuweka nguvu kubwa katika sekta ya viwanda ili kufikia lengo la kuwa na nchi ya uchumi wa viwanda. Azma hiyo imesisitizwa sana na Mheshimiwa Rais John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati wa Kampeni ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015. Ili kufikia uchumi wa viwanda, kuanzia mwaka 2016/2017 jitihada kubwa itawekwa katika kutenga na kuendeleza maeneo maalum ya viwanda, kuweka miundombinu muhimu ya nishati, usafirishaji, maji na maghala.

Aidha, tutaweka utaratibu endelevu wa upatikanaji wa mitaji na teknolojia ikiwemo kuanzisha dirisha maalum katika Benki za *TIB Corporate* na *TIB Development* na Benki ya Maendeleo ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia itapitia mifumo ya kodi, tozo na taratibu mbalimbali kwa lengo la kuzipunguza na kuondoa urasimu ili kupunguza gharama za uzalishaji wa ndani na kuwezesha bidhaa zetu kushindana katika soko la ndani na Kimataifa pia. Aidha, Serikali itaifanyia mapitio Sera ya Uwekezaji ya mwaka 1996 na Sheria yake ya mwaka 1997 ili kuendana na wakati.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa masoko ya uhakika unategemea mambo makuu manne; ubora wa bidhaa au mauzo, uhakika wa kupatikana kwa mazao au bidhaa wakati wote, unafuu wa bei dhidi ya washindani wengine katika soko na ufungashaji wa ujenzi wa jina la bidhaa (*brand*), hivyo ni lazima mlolongo wote wa uzalishaji, uongezaji thamani na usafirishaji uwe mzuri kwa ajili ya kuwezesha uwepo wa soko la uhakika. Mtiririko huo, katika mnyororo wa thamani wa bidhaa zenye uhakika wa soko, ndiyo msisitizo wa Serikali ya Awamu ya Tano na msingi wa kuhamasisha mapinduzi ya viwanda kwa lengo la kuongeza thamani bidhaa zetu kabla ya kuuzwa.

Mheshimiwa Spika, msukumo mkubwa utawekwa katika uendelezaji wa upatikanaji wa soko la ndani na nje kwa bidhaa zinazozalishwa nchini, hususan katika masoko ya upendeleo ya Jumuiya ya Afrika mashariki na masoko mengine ya kimkakati ya kikanda na Kimataifa, hivyo hivyo, uondoaji wa vikwazo vya kibiashara, pamoja na kusimamia viwango vya ubora wa bidhaa za ndani na nje ya nchi nao pia utaendelezwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2015/2016, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwemo Tanzania, zimekamilisha mkataba mwingine wa kutumia soko la Marekani, bila ushuru chini ya mpango wa AGOA.

Kwa kipindi kingine cha miaka kumi, kuanzia tarehe 30 Septemba, 2015 hadi tarehe 30 Septemba, 2025 ni muhimu sana kutumia fursa hii mpya ya AGOA kufanya biashara na Marekani katika kipindi cha miaka kumi ijayo. Vyama vya wafanyabiashara ni lazima viwaandae wanachama wao, kupata taarifa kamili kuhusu bidhaa zinazohitajika na ubora unaotakiwa. Aidha, Serikali itasimamia sana uanzishwaji wa bidhaa bora, kulingana na ubora unaotakiwa na masoko yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa uchimbaji madini mdogo, kama kichocheo cha kuongeza ajira na kukuza kipato cha wachimbaji wadogo wa madini, na wananchi wanaozunguka maeneo husika ya madini.

Aidha, uchimbaji mdogo wa madini unachangia kukuza ajira na uchumi kwa ujumla na kuondoa umaskini. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kuwatengea maeneo, kuwapatia ruzuku na kutoa mafunzo ya kuwawezesha kutekeleza kazi zao kwa ufanisi na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Serikali ilitenga hekta 7,731 kwa ajili ya uchimbaji wa madini mdogo katika maeneo ya Nyamongo Tarime na Muhitiri Singida. Aidha, Serikali kupitia Benki ya Maendeleo (TIB) imetoa mikopo ya masharti nafuu, yenye thamani ya shilingi bilioni 7.2 kwa ajili ya kukuza mtaji wa wachimbaji wadogo.

Pia mikopo hiyo inaweza kutolewa pia na Benki ya TIB Corporate ambayo nayo huwa inatoa mikopo ya masharti nafuu. Pia mafunzo yametolewa kwa wachimbaji wadogo 1,520. Katika mwaka wa 2016/2017 Serikali itatenga zaidi ya maeneo tengefu, kwa ajili ya uchimbaji wa madini mdogo na kuongeza kiasi cha ruzuku inayotolewa kwa wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga shilingi milioni 900 kwa ajili ya ruzuku na Benki ya Dunia imeridhia kutoa Dola za Marekani 3,000,000 kuchangia kwenye ruzuku hiyo.

Aidha, Serikali itaimarisha usimamizi katika biashara ya madini ya *Tanzanite* na kutoa mwongozo mpya wa namna ya kuendesha uchimbaji wa madini mdogo kwa tija. Mafunzo kuhusu namna ya kufanya utafiti wa awali na

madini na uchenjuaji bora wa madini yataendelezwa ili kazi ya wachimbaji wa madini wadogo, zifanyike kwa ufanisi na tija ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, sekta ya utalii ni moja ya sekta muhimu ambapo fursa zilizopo zikitumika vizuri, zitasaidia sana kukuza ajira na kupunguza umaskini.

Juhudi kubwa ambazo zimefanywa na sekta katika kuboresha huduma na miundombinu ya kitalii, pamoja na kutangaza vivutio vya utalii zimeuwezesha sekta ya utalii kuchangia 17% ya pato la Taifa na zaidi ya 25% ya mapato yanayotokana na mauzo ya nje mwaka 2015. Aidha, mwezi Julai, 2015 Serikali ilizindua kampeni maalum ya kukuza utalii wa ndani ili kuhamasisha Wananchi kutembelea vivutio vilivyopo katika hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, *campaign* hiyo imeongeza idadi ya watalii wa ndani kutoka watalii 115,913 mwezi Septemba 2014, hadi 148,406 mwezi Septemba, 2015. Mafanikio hayo yanadhihirisha kwamba sekta ya utalii ikiboreshwa zaidi ina fursa nyingi za kuchangia pato la Taifa na kuongeza ajira na kipato cha wananchi. Hata hivyo, unahitajika uwekezaji mkubwa kwenye miundombinu ya utalii, ikiwemo hoteli, usafirishaji na rasilimali watu imara na yenye weledi katika kuwahudumia watalii wa ndani na ya nje.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji kufanya vizuri zaidi kwa kupanua vyanzo vya utalii na kuhakikisha fedha nyingi wanazozitumia watalii kuja Tanzania, zinalipwa hapa nchini badala ya utaratibu wa sasa wa malipo hayo kufanyika nje ya nchi, kwenye nchi wanazotoka watalii. Tunahitaji pia kupanua na kuvutia utalii wa kihistoria na mali kale kama vile Mji Mkongwe wa Kilwa, mikindani, Bagamoyo na Mji Mkongwe Zanzibar na vivutio vingine visivyo na mfano Barani Afrika, kuliko kuegemea tu utalii wa wanyamapori na maliasili nyingine.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017 Serikali itaandaa mkakati wa Kitaifa, wa kuendeleza utalii nchini, pamoja na kutangaza utalii wetu hasa vivutio maarufu, kama vile mbuga ya Serengeti, Mlima Kilimanjaro, Mapango ya *Olduvai Gorge* yaliyoko nchini Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inakabiliwa na tatizo la ujangili hasa wa tembo, faru na biashara haramu ya nyara za Serikali. Katika kukabiliana na tatizo hili, Serikali ilizindua mkakati wa kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara za Serikali ulioanza kutekelezwa mwaka 2015, kwa kuchukua hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hatua hizo ni pamoja na kutumia vifaa vya teknolojia ya kisasa kama vile *Geographical Information System (GIS)* na *Global*

Positioning System (GPS), kuimaimarisha mfumo wa mawasiliano ya redio kutoka mfumo wa analogia kwenda digitali na kuanza kutekeleza mpango wa kikanda wa kukusanya taarifa za kiintelijensia, zinazoongoza doria katika kukamata watuhumiwa na wahalifu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaimarisha utekelezaji wa mkakati huo, hususan kwa kuzingatia ukubwa wa changamoto ya vitendo vya uwindaji haramu vinavyofanywa na majangili kwa kushirikiana na baadhi ya watumishi wa Idara ya Wanyamapori wasio waaminifu, na baadhi ya wananchi wanaoishi maeneo yanayozunguka mapori.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano itahakikisha kwamba ujangili huu unakomeshwa haraka, lakini pia hatua kali zitachukuliwa. Nachukua fursa hii kuziomba jamii zinazozunguka hifadhi zetu, kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Serikali katika vita hii kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huduma za kiuchumi, nikianza na sekta ya ardh. Ili azma yetu ya kufanya mapinduzi ya viwanda ifanikiwe, inahitajika ardhi iliyopimwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda. Changamoto tuliyonayo hivi sasa ni kwamba sehemu kubwa ya ardhi yetu, haijapimwa na kupatiwa hati miliki. Hivyo, tumeanza kuchukua hatua za haraka zitakazowawezesha kupatikana kwa ardhi ya kutosha kwa ajili ya ujenzi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Mikoa na Wakurugenzi wa mamlaka ya Serikali za Mitaa, walishaagizwa kutenga maeneo ya viwanja na biashara katika Mipango Miji. Napenda kutumia fursa hii kuitaka Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makaazi, kutopitisha maombi yoyote ya Mipango Miji yasiyokuwa na maeneo ya viwanda na biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefarijika pia kuona kwamba chini ya mpango wa maeneo huru ya biashara, baadhi ya Mikoa imeshatenga ardhi ambayo itaweza kuanza kutumika mara moja kutekeleza mpango huu kwa kuwekewa miundombinu muhimu na kukamilisha upimaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, zishirikiane kufanya uhakiki wa haraka wa maeneo hayo ili wawekezaji watakaonesha nia ya kuwekeza kwenye viwanda, wapatiwe maeneo yenye hati miliki kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba kuna migogoro ya ardhi katika baadhi ya maeneo nchini, Migogoro hiyo wakati mwingine ilisababisha uhalibifu wa mali, majeruhi na mauaji ya binadamu na mifugo. Njia muafaka ya

kudhibiti migogoro hiyo, ni kupima kila kipande cha ardhi, kukimilikisha kwa mtumiaji kwa kumpatia hati miliki na kusimamia matumizi yake. Kwa kutambua hilo, mwezi Februari, 2016, Serikali ilizindua Programu ya Kuwezesha Umilikaji Ardhi, ambayo imeanza kutekelezwa na majaribio katika Wilaya za Ulanga, Kilombero na Malinyi Mkoani Morogoro.

Mheshimiwa Spika, programu hiyo imelenga kuongeza kasi ya kupima ardhi na kutoa hati miliki za kimila, ambazo zinaweza kutumika kama dhamana kwa wakulima na wafugaji kupata mikopo, lakini pia kupunguza na kuondoa migogoro ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi hiyo na kuhifadhi kumbukumbu za ardhi kwa matumizi sahihi ya rasilimali hiyo.

Mheshimiwa Spika, programu hiyo itatekelezwa kwa muda wa miaka mitatu, kwa gharama za Dola za Marekani milioni 15.2. Baada ya majaribio hayo na mafanikio kuonekana katika Wilaya hizo, programu itatekelezwa katika Wilaya zote nchini. Ninawaagiza viongozi wa Mikoa, Mkoa wa Morogoro na Wilaya zinazohusika, kusimamia kwa karibu utekelezaji wa programu hiyo, kwani matokeo yake ni ya muhimu sana kwenye mustakabali wa upimaji matukio na matumizi endelevu ya ardhi yetu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2015 Serikali iliwaomba Waheshimiwa Wabunge, kuainisha na kuwasilisha Serikalini migogoro ya ardhi iliyopo kwenye Majimbo yao. Napenda kutumia fursa hii, kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge walioitikia wito huo. Mchango wao katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 umewezesha jumla migogoro 1,130 ya ardhi kupokelewa Serikalini kutoka katika Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa migogoro hiyo unaendelea ambapo taarifa za awali, zinaonesha kwamba migogoro mingi iliyopo ni kati ya wakulima na wafugaji, uvamizi wa mashamba, viwanja; migogoro kati ya Mamlaka za Hifadhi ya Taifa na wananchi; na kati ya wawekezaji na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, tayari Serikali imechukua hatua kali dhidi ya Maafisa Ardhi waliokiuka sheria na taratibu za usimamizi wa ardhi nchini. Hii ni pamoja na kuwasimamisha kazi ili kupisha uchunguzi. Kwa mfano, hatua kali zimechukuliwa katika Halmashauri ya Majiji ya Mwanza na Arusha, Manispaa za Bukoba na Kahama na kutengua madaraka kwa Maafisa Ardhi Teule wa Manispaa ya Temeke.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kushirikiana na Halmashauri zao, hususan Maafisa Ardhi na kutumia dawati

maalum la kuratibu migogoro ya ardhi, lilianzishwa katika kila Halmashauri nchini ili kuendelea kubaini migogoro iliyopo na kuitafutia ufumbuzi wake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017 Serikali itaifanyia mapitio Sera ya Taifa ya ardhi ya mwaka 1995 ili kuweka vipengele muhimu vya kudhibiti migogoro baina ya watumiaji wa ardhi na kuzipa nguvu zaidi Ofisi za Ardhi za Kanda zitakazosaidia Mamlaka ya Serikali za Mitaa kupima na kupanga matumizi ya ardhi na kutoa hati karibu zaidi na wananchi. Aidha, Serikali itapitia upya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1969 ili kuzifanyia marekebisho muhimu kuendana na wakati.

Mheshimiwa Spika, miundombinu imara ni msingi muhimu wa maendeleo ya sekta nyingine zote, ikiwemo sekta ya viwanda na biashara.

Katika miaka ya hivi karibuni, tumeshuhudia uwekezaji mkubwa katika ujenzi wa barabara nchini. Mathalan katika mwaka 2015/2016, Serikali ililenga kujenga kilometa 523 za barabara kuu kwa kiwango cha lami. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016, jumla ya kilometa 4014.3 za barabara zilikuwa zimekamilishwa kwa kiwango cha lami, sawa na 79% ya lengo, tulilokuwa tumejiwekea. (Makofi)

Aidha, jumla ya kilometa 82.4 za barabara kuu zilizokarabatiwa kwa kiwango cha lami, ikiwa ni sawa na 73% ya lengo la kilometa 113. Kwa upande wa barabara za Mikoani, jumla ya kilometa 52.19 zilizojengwa kwa kiwango cha lami, sawa na 68% ya lengo la kilometa 77; na jumla ya kilometa 676 za barabara za Mikoa zilizofanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe, sawa na 54% ya lengo la kilometa 1,252. Ujenzi wa madaraja makubwa 11 uliendelea, ambapo daraja la Kigamboni tayari limekamilika na limefunguliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mradi wa uboreshaji wa miundombinu na huduma za reli ya kati, lengo ikiwa ni kuboresha reli hii iliyopo kwa kutandika reli mpya ya uzito zaidi; kuimarisha matuta, mifereji na tabaka la kokoto. Aidha, tutaendelea na utekelezaji wa makubaliano baina ya Serikali yetu na Serikali ya Rwanda na Burundi, kuhusu ujenzi wa reli ya Dar es Salaam, Isaka, Keza, Kigali yenye urefu wa kilometa 1,464 na Keza Msongati yenye urefu wa kilometa 197 kwa kiwango cha *standard gauge*.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa ndani ni wa kujenga kiwango hicho hicho cha *standard gauge*, Dar es Salaam - Kigoma, zenye matawi ya Kaliua, Mpanda mpaka Kalimie; pia Tabora - Mwanza, huku pia tukiwa na miradi ya

Mtwara, Songea Mbambabay na kuimarisha reli ya Pugu iendayo Tanga, Moshi mpaka Arusha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Serikali imeanza kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha ufanisi wa bandari zetu kwa kuanzia na Bandari ya Dar es Salaam ambayo ni lango kuu la biashara katika Afrika Mashariki na kati na kufuatiwa na Bandari za Mtwara na Tanga. Tumeanza kwa kuwaondoa watumishi wote wasio waaminifu ambao wanachangia kupoteza mapato ya Serikali yanayohitajika sana katika kutoa huduma muhimu kwa wananchi wetu. (Makofi)

Vile vile tumefanya kazi kubwa ya kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato kwa kuhakikisha kwamba malipo yote yanayofanyika benki na kuoanisha mifumo ya Mamlaka ya Bandari, pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie wananchi na wafanyabiashara kuwa, Serikali itaendelea na kuboresha huduma katika bandari zetu na hususan Bandari ya Dar es Salaam, kwa kupunguza idadi ya siku za kutoa mizigo bandarini ili tufikie siku mbili au chini ya siku hizo. Aidha, tutaziondoa kero zote zilizoainishwa na Mawakala wa Forodha, nilipokutana nao mimi mwenyewe tarehe 21 Machi, 2016 Jijini Dar es Salaam. Vile vile Serikali itaziba mianya yote ya upotevu wa mapato Bandarini na wale wote watakaobainika kushiriki kwenye wizi wa aina yoyote ile, wataondolewa na kuchukuliwa hatua za kisheria. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kukamilisha mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa, wa mawasiliano nchini, ikiwemo na ujenzi wa kituo mahiri cha kutunzia kumbukumbu katika Jiji la Dar es Salaam.

Aidha, Serikali inaendela na ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano vijijini, ambapo hadi sasa tumefanikisha ujenzi wa kilometa 18,000 kati ya kilometa 20,000 za miundombinu ya mkongo katika Wilaya zote nchini.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zinazoendelea kwa sasa ni ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano katika vijiji 4,000 visivyokuwa na mawasiliano, kuunganisha Ofisi zote za Wakuu wa Wilaya, Hospitali za Wilaya, Mahakama, Vituo vya Polisi vya Wilaya, Ofisi za Posta na kuziwezesha shule 431 kupata huduma za *internet* bila malipo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imedhamilia kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika, unaokidhi mahitaji na wenye gharama

nafuu ili kusukuma mapinduzi ya viwanda kwa kasi zaidi. Ili kutekeleza azma hiyo, Serikali mwaka 2015/2016, Serikali imeongeza uwezo wa mitambo ya kufua umeme, kutoka megawati 1,226.24 mwaka 2015 hadi kufikia 1,516.24 mwezi Januari, 2016, sawa na ongezeko la 24%.

Mheshimiwa Spika, ongezeko hilo limetokana na uamuzi sahihi wa Serikali wa kutekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa bomba la gesi, pamoja na mradi wa kufufua umeme wa *Kinyerezi I*, wenye uwezo wa kuzalisha Megawata 150 na mradi huo baadaye utapanuliwa na kuweza kufikia megawati 333 ifikapo mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hiyo, tarehe 16 Machi, 2016 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa kituo kingine cha *Kinyerezi II* cha kufua umeme, kutokana na gesi asilia, ambapo utakapokamilika, uzalishaji wa megawati 240 utakuwa umeanza.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali katika kipindi cha miaka mitano ijayo, ni kuongeza uwezo wa uzalishaji umeme hadi kufikia megawati 4,915 na hivyo kuwezesha 60% ya Watanzania kupata umeme wa uhakika ifikapo mwaka 2020 na kutekeleza ipasavyo azma ya kuongeza uwekezaji mkubwa kwenye Sekta ya Viwanda.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha fedha cha mwaka wa fedha 2015/2016 Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) umeendelea kusambaza na kuunganisha umeme kwa wananchi waishio vijijini. Katika kipindi hicho, idadi ya wananchi waliopata umeme kupitia mradi wa *REA* awamu ya pili ni 71,724 katika vijiji 1,669. Aidha, hadi mwezi Januari, 2016 Serikali imekamilisha ujenzi wa kilometa 12,193 za njia za msongo wa kati na kilometa 1,830 za msongo mdogo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa awamu ya pili ya usambazaji wa umeme vijijini. Vilevile umeme umefikishwa kwenye Makao Makuu ya Wilaya mpya 12 za Buhigwe, Busega, Chemba, Kitilima, Kakonko, Kalambo, Kyerwa, Mkalama, Mlele, Nyasa, Nanyumbu na Uvinza. Utekelezaji wa miradi hiyo umeongeza kiwango cha wananchi wanaopata huduma za umeme kufikia 40%. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali itaendelea kutekeleza mradi wa *Kinyerezi II* pamoja na kuimarisha na kujenga njia ya usafirishaji umeme katika *grid* ya Taifa za msongo mkubwa wa *Kilovolt 400* kutoka Iringa kupitia Dodoma na Singida hadi Shinyanga na kutoka Dar es Salaam kupitia Chalinze na Tanga hadi Arusha; pamoja na mradi wa *Kilovolt 220* kutoka Makambako hadi Songea. Aidha, Serikali itakamilisha awamu ya pili

ya mradi wa usambazaji wa umeme vijijini na kuanza utekelezaji wa awamu ya tatu ya mradi wa REA.

Mheshimiwa Spika, baada ya ugunduzi mkubwa wa gesi asilia nchini, mikakati ya Serikali inayoendelea ni kubuni miradi mbalimbali hasa ile itakayoendeshwa na wafanyabiashara wazawa ili rasilimali hiyo iweze kuwanufaisha Watanzania na kuwawezesha kumiliki uchumi wa Taifa lao. Serikali imetenga eneo la ardhi huko Likongo Mkoani Lindi kwa ajili ya kujenga miundo mbinu ya kuchakata gesi asilia ikiwa ni sehemu ya kutekeleza azma hiyo ya kuwawezesha wazawa. Serikali itaanza kutekeleza mradi huo katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba nchi inakuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta kwa ushindani na gharama nafuu; Serikali imenzisha Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa pamoja, yaani *Petroleum Bulk Procurement Agency* ulioanza kazi rasmi mwezi Januari, 2016. Utaratibu huo utaiwezesha Serikali kuimamia vizuri kabisa udhibiti wa uagizaji wa mafuta nchini na kuwawezesha wananchi kuwa na uhakika wa kupata mafuta bora yenye viwango vinavyokubalika Kimataifa na kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo na kijamii.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa elimu kama nyenzo imara ya maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii, Serikali ya awamu ya tano imeanza kuchukua hatua madhubuti ya kuboresha na kuimarisha Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Ufundi na Elimu ya Juu. Hatua zinazochukuliwa zinalenga kuhakikisha kwamba elimu ya Tanzania ni ya viwango vya ubora wa hali ya juu ili kuwawezesha vijana wetu kukabiliana na changamoto za maisha kwa kujijiri wenyewe na kumudu ushindani katika soko la ajira la ndani kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, hatua hizo zitatuwezesha kuwa na rasilimali watu yenye weledi wa kutosha kujenga uchumi wa viwanda nchini. Moja ya hatua kubwa iliyochukuliwa na Serikali ni utekelezaji wa ahadi ya utoaji wa elimu bila malipo kuanzia Elimu ya Awali hadi Kidato cha Nne kwa shule za Umma kuanzia mwezi Januari, 2016. Ahadi hiyo iliyotolewa na Mgombea Urais kupitia CCM wakati wa kampeni ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba mwaka 2015 ambaye kwa sasa ndio Rais wa Jamhuri Ya Muungano wa Tanzania.

Vilevile matakwa ya kifungu cha 52 kifungu kidogo cha (a) cha Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 ambacho kinasisitiza kwamba Serikali itaandaa mfumo, muundo na taratibu nyumbufu za kutoa Elimu ya Awali na

Elimu ya Msingi bila malipo ili kila Mtanzania apate fursa sawa ya kupata elimu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kuwa hatua hiyo nzuri iliyochukuliwa na Serikali ya awamu ya tano itawapunguzia wazazi na walezi hasa wananchi maskini mzigo wa kugharamia elimu ya vijana wao. Kupitia Waraka wa Elimu Na. 5 wa mwaka 2015 Serikali imefuta michango ya maji, umeme, ulinzi, mitihani na ada iliyokuwa inachangishwa shuleni kwa idhini ya Kamati na Bodi za Shule.

Hata hivyo, yapo majukumu yanayohusu mahitaji ya msingi ya mtoto ambayo yataendelea kutekelezwa na wazazi wenyewe na walezi kama ilivyokuwa inafanyika awali. Majukumu hayo ni pamoja na kumnunulia mtoto sare za shule na michezo, madaftari, kalamu na chakula kwa wanafunzi wa shule za kutwa kwa utaratibu utakaowekwa na wazazi na walezi wenyewe. Maeneo mengine ni kulipia nauli ya kwenda na kurudi shule wanafunzi na mahitaji mengine kama vile kununua godoro, shuka na vifaa vya usafi binafsi. Vilevile mzazi au mlezi anao wajibu wa kugharamia matibabu ya mtoto wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuanza kwa utekelezaji wa mpango wa elimu bila malipo kumejitokeza changamoto kadhaa. Baadhi ya changamoto hizo ni uelewa wa jamii juu ya umuhimu wa kuweka utaratibu muafaka wa kutoa chakula cha mchana kwa wanafunzi wa kutwa na uendeshwaji wa mabweni ambayo wazazi na walezi au jamii walikuwa wanachangia fedha za chakula. (Makofi)

Mheshimiwa spika, changamoto nyingine ni pamoja na upungufu wa miundombinu kama madarasa, mabweni, maabara, nyumba za Walimu na vyoo. Napenda pia kuwahakikishia wananchi kwamba Serikali itaendelea kuzifanyia kazi changamoto hizo na jitihada kubwa zimewekwa katika kuelimisha jamii na wadau mbalimbali kuhusu mpango mzima wa utoaji elimu bila malipo.

Mheshimiwa Spika, tunayo changamoto ya upungufu mkubwa wa madawati baada ya kuanza kuandikisha watoto shule bila malipo. Hili ni jambo kubwa na tulishatoa agizo kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi kuhakikisha kwamba kila Halmashauri inatumia rasilimali zake kutengeneza madawati kwa kila shule.

Natumia nafasi hii kuwashukuru wadau walioanza kuchangia madawati katika maeneo mbalimbali na ninawasihi wengine waendeleo kuunga mkono jitihada hizi za Serikali. Kuanzia leo hii nawaagiza Wakuu wa Wilaya na

Wakurugenzi waliokamata mbaao ndani ya Halmashauri zao, mbaao hizo zitumike kutengenezea madawati.

Narudia tena, kuanzia leo hii nawaagiza Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi waliokamata mbaao ndani ya Halmashauri zao, kuzitumia mbaao hizo kutengenezea madawati na siyo kuzipiga mnada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi huu kukushukuru wewe na Watendaji wa Bunge kwa mkakati wa kubana matumizi uliowezesha kupata Shilingi bilioni sita zitakazotumika kutengenezea madawati na madawati hayo kusambazwa nchi nzima. Suma JKT na Magereza wameanza kazi ya kutengeneza madawati hayo na tunatarajia kupata madawati 80,000 ambayo tutawagawia Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo yote nchini na kwa wastani kila Jimbo linaweza kupata madawati yasiyopungua 300 au zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote tushirikiane katika jitihada za kuunga mkono uamuzi wa Serikali kuhusu elimu bila malipo. Aidha, nawaomba wote kwa ujumla wetu kushirikiana katika kuwaelimisha wananchi kuhusu mpango huu na wajibu wa kila mmoja wetu katika kuhakikisha kwamba watoto wetu wanapata fursa za kupata elimu bora. Tukifanya hivyo, tutaweza kufikia lengo letu la kuwa nchi yenye kipato cha kati kwa haraka zaidi kwa Watanzania wote kuwa na elimu ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ni nguzo muhimu ya kuwapatia ujuzi na kuwajengea uwezo na uzoefu wanafunzi wanaomaliza Elimu ya Msingi na Sekondari. Uzoefu wa nchi za Asia zilizowekeza katika Elimu ya Ufundi na Ufundi Stadi unaonesha kwamba maendeleo ya haraka waliyoyapata na hususan kufikia uchumi wa kati na wa viwanda umechangiwa sana na elimu ya ufundi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu huo, Serikali itaelekeza nguvu zake katika kujenga na kuimairisha miundombinu ya Elimu ya Ufundi na kuboresha mitaala ili iendane na mahitaji ya sasa ya uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia, Serikali imeridhia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kuhamishiwa Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi na kufanyiwa ukarabati kwa ushirikiano na sekta binafsi ili viweze kutoa mafunzo ya ufundi. Hatua hiyo itaharakisha kufikiwa kwa lengo la Serikali kuwa na Chuo cha Ufundi kwa kila wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, udahili katika Vyuo vya Elimu ya Juu umeongezeka sana kutoka wanafunzi 214,722 mwaka 2014 hadi kufikia wanafunzi 220,531 mwaka 2015. Aidha, hadi kufikia Februari, 2016 idadi ya wanafunzi walipewa mikopo ya Elimu ya Juu ilifikia 122,886 na kiasi cha fedha cha mikopo kilichotolewa kwa wanafunzi hao ni Shilingi bilioni 207. Hata hivyo, hali ya urejeshwaji mikopo iliyotolewa hairidhishi, hivyo naiagiza Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kufuatilia urejeshaji wa mikopo hiyo ili fedha hizo zitumike kuwakopesha wanafunzi wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uimarishaji wa huduma za afya nchini kwa maana ya kinga na tiba ni muhimu sana. Nguvu kazi yenye afya njema hutoa mchango mkubwa kwenye uchumi ikilinganishwa na nguvu kazi dhaifu kiafya. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma za kinga, uchunguzi na upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali ya Rufaa ya Kanda, Hospitali Maalum, Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imetoa maelekezo kwa Bohari Kuu ya dawa (MSD) kufungua na kuendesha maduka ya dawa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali za Rufaa za Mikoa na Hospitali za Wilaya ili kuhakikisha kwamba dawa za kutosha zinapatikana wakati wote na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Bohari Kuu ya Dawa imefungua na inaendesha maduka ya dawa yanayouza bidhaa zake kwa bei nafuu ndani ya maeneo ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali ya Sekou Toure (Mwanza), Mawenzi (Kilimanjaro) na Mount Meru (Arusha), Pamoja na juhudi hizo za Serikali za kuimarisha huduma za afya nchini, milango iko wazi kwa sekta binafsi ya ndani na nje ya nchi kuwekeza katika Sekta ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha wananchi kujiunga na huduma za Bima ya Afya ili kuongeza na kuimarisha upatikanaji wa huduma ya afya kwa watu wote. Idadi ya wanufaika wa Bima ya Afya tangu kuanzishwa kwake ni 11,729,281 sawa na 27% ya Watanzania wote kulingana na sensa ya mwaka 2012. Kati ya hao, wanufaika milioni 8,390,550 wapo katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na 3,339,755 ni wanachama wa Mfuko wa Afya ya Hamii CHF.

Hata hivyo, idadi ya wanufaika wa mfuko bado ni ndogo. Hivyo, naagiza viongozi wa mifuko hiyo kushirikiana pamoja, kutoa elimu na kuhamasisha wananchi wengi zaidi kujiunga na mifuko hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuangalia uwezekano wa Hospitali za Rufaa za Mikoa kuwa chini ya Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Wazee na Watoto ili Katibu Tawala wa Mkoa aendeleo kuratibu maendeleo ya hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati zilizoko kwenye Halmashauri za Wilaya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza Program ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa malengo ya kuwapatia wananchi huduma ya maji safi, salama na ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Desemba, 2015 Serikali imefikisha huduma ya maji safi na salama kwa asilimia 72 katika maeneo ya vijiji, asilimia 86 Miji Mikuu ya Mikoa na asilimia 60 katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji midogo. Mafanikio haya yametokana na utekelezaji wa miradi ya maji 1,143...

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, naona muda hauko upande wetu, basi tupate kama dakika kumi hivi umalizie hotuba yako. Endelea.

WAZIRI MKUU: Nakushukuru sana.

Aidha, huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Bagamoyo na Kibaha, imeongezeka kwa kufikia asilimia 68, lengo ikiwa kufikia asilimia 95, ifikapo mwaka 2025. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali inatekeleza awamu ya pili ya Program ya Maendeleo ya Sekta ya Maji pamoja na kukamilisha miradi 712 ambayo haikutekelwa katika awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa wananchi wote kutunza vyanzo vya maji pamoja na miundombinu yake ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji vijijini na mijini.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kwamba maji ni moja ya vigezo muhimu katika kuanzisha na kuendeleza viwanda, hivyo hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha upatikanaji wa huduma mjini nchini. Pamoja na kuongeza huduma ya maji safi na taka, ina lengo la kuongeza mchango wa Sekta ya Maji, katika Sekta ya Viwanda, mathalan ongezeko la maji kutokana utekelezaji wa miradi ya kuboresha miundombinu ya maji ya Ruvu Juu na Ruvu Chini; umesaidia kupunguza tatizo la maji katika jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Serikali itahakikisha kuwa, maeneo yenye viwanda na yanayotegemewa kuwa na viwanda, yanaunganishwa na miradi mikubwa ya maji ili kuongeza kasi ya uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vyombo vya ulinzi na usalama vimeendelea na jukumu la kulinda mipaka, raia na mali zao. Kwa ujumla hali ya ulinzi na usalama na nchi yetu ipo shwari. Napenda kutumia rufsa hii kuvipongeza vyombo vyote vya ulinzi na usalama kwa kazi yao nzuri, weledi na wazalendo wa hali ya juu katika kuhakikisha kwamba Taifa letu lina usalama wa kutosha, pia kuchangia usalama wa Mataifa mengine duniani, yenye migogoro ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, mambo yote haya yanatokana na ukweli kwamba Serikali imekuwa ikiviwezesha vyombo vyetu vya ulinzi na usalama na kuwa na uwezo wa kulinda mipaka yote ya nchi, raia na mali zao katika kujenga utayari wa majeshi wakati wote.

Mheshimiwa Spika, Askari wetu wameshiriki kwa ufanisi katika majukumu ya Kimataifa na kulinda amani katika nchi yenye migogoro duniani hususan Darfur, Sudan, Lebanon na Mashariki ya Mji wa Demokrasia ya Kongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2015/2016 jumla ya vijana 27,463, walipatiwa mafunzo ya kujenga uzalendo, ukakamavu, maadili mema, Utaifa pamoja na *study* za kazi za kuimarisha kazi.

Kati yao vijana ni 7,517 ni wa kujitolea na 19,976 ni kwa mujibu wa sheria na nijambo la kutia moyo kwamba vijana 5,453 waliopitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa wamenufaika na utaratibu wa kuajiriwa na vyombo vya ulinzi na usalama. Kati ya hao, vijana 3,521 wameajiriwa na JWTZ, Polisi 1,185, Usalama wa Taifa 106, TAKUKURU vijana 24 na Jeshi la Zimamoto vijana 617. *(Makofi)*

Aidha, Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kuishi kwa watumishi wa vyombo vya ulinzi na usalama ambapo nyumba 4,774 za makazi zimekamilishwa, kati ya nyumba 6,064 za awamu ya kwanza kwenye mradi wa nyumba 10,000 zinazotarajiwa kujengwa nchini. Serikali itaimarisha Jeshi letu kwa kulipatia mafunzo, zana bora za kisasa zaidi, kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na maslahi.

Aidha, itaimarisha uwezo wa Jeshi katika utafiti wa kuendeleza teknolojia kwa madhumuni ya kuongeza ubunifu katika uzalishaji wa bidhaa bora zaidi na huduma kwa ajili ya matumizi ya Jeshi na raia ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limeendelea kulinda usalama wa raia na mali zao na kudumisha amani na utulivu nchini kwa kipindi cha Januari hadi Desemba 2015. Jumla ya makosa makubwa ya jinai 68,814 yaliripotiwa katika Vituo vya Polisi kote nchini ikilinganishwa na makosa 70,153 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2014, sawa na upungufu wa 1.9%.

Upungufu huo wa makosa umetokana na kuongezeka kwa ushirikishwaji wa wananchi katika vita dhidi ya ualifu na kuongezeka kwa taaarifa za kiintelijensia. Aidha, Jeshi limeimarisha doria za nchi kavu, majini pamoja na kufanya misako ya oparesheni maalum kwa ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya, Tarafa, Kata na Shehia katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Jeshi la Polisi litaendelea kutoa elimu ya ulinzi shirikishi kwa wananchi ili waweze kuongeza ushirikiano na Jeshi la Polisi katika utekelezaji wa majukumu ya kupambana na uhalifu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, yale yote ambayo sitayapitia lakini yote yaingie kwenye *Hansard* kadri ambavyo nimewasilisha mezani.

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze suala muhimu la vita dhidi ya rushwa. Serikali inaendelea kupambana na rushwa na kuchunguza tuhuma za rushwa na kuwafikisha watuhumiwa mbele ya vyombo vya sheria. Katika mwaka 2015/2016 Serikali imeshughulikia tuhuma 3,911 ambapo uchunguzi wa tuhuma 324 ulikamilika. Kati ya tuhuma hizo majalada 252 yaliyooombewa kibali na Mkurugenzi wa Mashtaka, ambapo majalada 156 yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani.

Aidha, majalada 329 yaliyotokana na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali yalichunguzwa. Majalada 19 yalikamilika na kuomba kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka, ambapo majalada 12 yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani. Vilevile majalada nane yaliyohusu tuhuma za rushwa kubwa yalifikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashitaka. Kati ya hayo majalada mawili yamepata kibali na watuhumiwa wamefikishwa mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuchunguza tuhuma 3,444 zilizopo na mpya zitakazojitokeza na kukamilisha uchunguzi wa tuhuma kumi za rushwa kubwa. Aidha, itawajengea uelewa wa masuala ya rushwa makundi mbalimbali katika jamii hususan asasi za kiraia, madhehebu ya dini na wanahabari ili washiriki kikamilifu kuwaelimisha wananchi kuhusu kudhibiti rushwa na kuendelea kufungua na kuimarisha klabu za wapinga rushwa katika

shule za msingi, sekondari na vyuo ili kuendelea kujenga jamii inayochukia rushwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza suala la maafa, ikiwa ni jukumu la kuwalinda na kuwasaidia wananchi dhidi ya maafa yaletwayo na matukio mbalimbali ya kiasili. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na Serikali kutoa tani 31,134 za chakula kwa Halmashauri 69 zilizokumbwa na upungufu wa chakula. Katika mwaka 2015/2016 kati ya hizo tani 7,727 zilitolewa bure kwa kaya zisizo na uwezo na tani 23,457 zilitolewa kwa bei nafuu ya shilingi 50 kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa misaada mbalimbali ya kibinadamu yenye thamani ya shilingi milioni 42.5 na kiasi cha shilingi milioni 143.5 kwa ajili ya ununuzi wa mbegu za mihogo na mtama kwa waathirika wa maafa ya mafuriko, mvua ya mawe na upepo mkali. Mikoa iliyopata misaada hiyo ni Mtwara, Mara, Dodoma, Shinyanga, Iringa, Tanga, Pwani, Lindi na Tabora. Pia shilingi milioni 516 zilitolewa kwa fidia kwa watu waliotakiwa kupisha ujenzi wa upanuzi wa mtaro katika eneo la Buguruni - Mnyamani.

Serikali imeimarisha mfumo wa upatikanaji wa taarifa za tahadhari na majanga kwa haraka na kujenga vituo 16 vya upimaji wa hali ya hewa na kuweka vifaa vya kupima wingi na kiasi cha maji kutoka vituo 10 vilivyopo katika mabonde ya Mto Pangani na Mto Ruvuma. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha Kamati za Maafa za Mikoa, Wilaya na kuendelea kuimarisha mfumuko wa taarifa za tahadhari za awali.

Mheshimiwa Spika, kwenye taarifa yangu liko eneo la dawa za kulevya, lakini pia ustawishaji wa Makao Makuu ya Dodoma, ushirikiano wa kimataifa, lakini na uratibu wa shughuli za Serikali ambao sasa unaendelea.

Mheshimiwa Spika, mwisho; nimetumia muda mrefu sana kueleza baadhi ya shughuli ambazo Serikali ya Awamu ya Tano inazipatia kipaumbele. Kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, napenda kusesitiza masuala yafuatayo; moja, tunayo changamoto kubwa ya kutumia rasilimali fedha kidogo tuliyonayo kukidhi mahitaji makubwa ya kutoa huduma bora kwa wananchi. Uko upotevu wa mapato kwa kushindwa kudhibiti na kusimamia mapato na matumizi ya fedha za umma. Serikali ya Awamu ya Tano itasimamia na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato na kuhakikisha kwamba fedha za umma zinatumiwa kulingana na sheria na kanuni za matumizi ya fedha za Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mbili; tumedhamiria kufanya mapinduzi ya viwanda ili kujenga uchumi imara na kwa faida ya wananchi. Mpango wetu wa miaka

mitano umeeleza vizuri juu ya mpango wa viwanda. Tatu; tunahitaji kuboresha sekta za kilimo, mifugo uvuvi na bidhaa za masoko kama njia ya kujenga muunganisho wa sekta hizi na viwanda, na Wizara itakuja kuleta mpango imara wa maeneo haya. Pia tunalo jukumu kubwa la kuboresha huduma za jamii, ikiwemo elimu, afya, upatikanaji wa maji safi na salama na miundombinu ya umeme, hasa vijijini. Bado tuna matatizo kubwa la biashara na matumizi ya dawa za kulevya, na hili bado vita yake inaendelea. Nataka niwatahadharishe wale wote wanaojishughulisha na eneo hili kuachana na biashara hiyo ya dawa za kulevya, Serikali inaimarisha miundombinu, utaratibu na utaalum wa kudhibiti hali hii.

Mheshimiwa Spika, pia tunayo changamoto ya ukuaji wa uchumi ambayo huenda sambamba na kasi ya upatikanaji wa ajira, ambayo pia itafafanuliwa kwenye bajeti yetu. Katika hili tuendeleo kuunga mkono falsafa ya Mheshimiwa Rais ya Hapa Kazi Tu na ile ambayo inasema asiweifanya kazi na asile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawaomba Watanzania wote kuendelea kuishi kwa amani na utulivu, tunayo nchi nzuri na Watanzania wote ni watu wenye upendo, tudumishe amani, umoja na mshikamano kwa kuwaunga mkono viongozi wetu wote ili tuongeze kasi ya kuleta maendeleo katika nchi yetu, na kwa maana ya umoja ni nguvu, sekta binafsi ambayo ndiyo injini ya ukuzaji na uchumi wa Taifa letu isiwe na tashwishi hata kidogo, Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kuienzi na kuisaidia sekta binafsi katika kuchangia maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ninawashukuru Mawaziri, Watendaji Wakuu kwenye Wizara, Kamati ambazo pia zimeshiriki kikamilifu katika kuandaa bajeti yetu, na Watendaji wote ndani ya ofisi ya Waziri Mkuu ambao wameshiriki kikamilifu katika hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2016/2017. Kwa Mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 236,759,874,760; Kati ya fedha hizo shilingi 71,564,293,773 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi 165,195,580,933 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimia Spika, naafiki.

**HOTUBA YA WAZIRI MKUU, MHE. KASSIM M. MAJALIWA (MB), KUHUSU
MAPITIO NA MWELEKEO WA KAZI ZA SERIKALI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA 2016/2017 KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI zilizochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2015/2016 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2016/2017. Vilevile, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka 2016/2017.

2. Mheshimiwa Spika, huu ni Mkutano wa Bunge wa kujadili Bajeti ya Serikali baada ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba, 2015. Hivyo naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Watanzania kwa kuendelea kuwa na imani na Chama Cha Mapinduzi na hivyo kukiwezesha kushinda na kukipa tena ridhaa ya kuunda Serikali na kuiongoza Nchi yetu. Aidha, kwa njia ya pekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuongoza Serikali ya Awamu ya Tano. Pia, nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa kushika nyadhifa hizo muhimu. Nawahakikishia wananchi wote kwamba Serikali ya Awamu ya Tano itawatumikia kwa nguvu zake zote bila kujali itikadi zao za kisiasa.

3. Mheshimiwa Spika, kipekee naomba kutumia fursa hii kumshukuru kwa dhafi Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na uteuzi huo kuungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge kwa asilimia 73. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi kwamba sitawaangusha.

4. Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.), kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Pia, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kuwa Wawakilishi wa Wananchi katika Bunge hili. Jukumu lililo mbele yetu sote ni kuwatumikia wananchi waliotuchagua ili kuwaletea maendeleo.

5. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Nchi yetu imekumbwa na majanga mbalimbali yaliyosababisha vifo na uharibifu wa mali. Nitumie fursa hii kumuomba Mwenyezi Mungu awajalie wale walioumia kupona haraka na kurejea katika shughuli za ujenzi wa Taifa. Ninawapa pole wote waliofiwa na ndugu, jamaa na marafiki. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. **Amina!**

6. Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kupitia kwa kina Makadirio ya Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kipekee, nitumie nafasi hii, kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI inayoongozwa na Mheshimiwa Hasna Sudi Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini na Kamati ya Bajeti inayoongozwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini. Kamati hizo zimetoa mchango mkubwa wakati wa maandalizi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu. Pia, naomba niwapongeze Wenyeviti na Makamu wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi kubwa ya kupitia makadirio ya sekta zote. Maoni na ushauri wao umesaidia sana katika kuboresha Makadirio ya bajeti ya Serikali.

7. Mheshimiwa Spika, makadirio ya bajeti ninayowasilisha leo ni mwendelezo wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015. Ilani hiyo, imeainisha ahadi ambazo Serikali ya Chama Cha Mapinduzi itazitekeleza katika miaka mitano ijayo. Aidha, makadirio ya Bajeti yamezingatia ahadi za Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizotoa wakati wa Kampeni na katika uzinduzi wa Bunge la Kumi na Moja, tarehe 20 Novemba 2015. Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kujenga Taifa imara kiuchumi na maendeleo ya watu katika Kanda ya Afrika Mashariki na Barani Afrika kwa ujumla.

MWELEKEO WA SERIKALI YA AWAMU YA TANO

8. Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha mapitio ya kazi za Serikali kwa mwaka 2015/2016 na mwelekeo kwa mwaka 2016/2017, niruhusu kupitia Bunge lako Tukufu niwakumbushe Watanzania wote kuhusu dhima ya Serikali ya Awamu ya Tano yenye falsafa ya "Hapa Kazi Tu". Sote tunatambua kwamba ili Tanzania ifikie Nchi yenye Uchumi wa Kipato cha Kati ifikapo mwaka 2025 ni sharti kila mmoja wetu afanye kazi kwa bidii, maarifa na ubunifu wa hali ya juu.

9. Mheshimiwa Spika, ili yawepo mapinduzi ya kweli ya kuelekea kwenye uchumi wa kati tunaodhamiria ni lazima tuimarisha uwajibikaji na maadili kwa Viongozi, Watendaji na kwa kila Mtanzania. Sote tumeshuhudia hatua zinazochukuliwa na Serikali dhidi ya Watumishi wasio waadilifu wanaotumia fedha za umma au madaraka yao vibaya na kukwamisha utekelezaji wa mipango ya maendeleo tunayojiwekea. Hatutaweza kufikia uchumi wa kati unaoendeshwa kwa viwanda kama tutaendelea kulea uzembe, ubadhirifu, uvivu na kukwepa wajibu wetu. Ndiyo maana, tumeanza kwa nguvu kuimarisha nidhamu, uwajibikaji na matumizi sahihi ya fedha za umma ili zielekezwe kwenye shughuli zenye manufaa kwa Watanzania walio wengi na siyo vinginevyo.

10. Mheshimiwa Spika, pamoja na kuimarisha ufanisi na tija ndani ya utumishi wa umma, tumebaini kuwa changamoto ya utamaduni usioridhisha wa ufanyaji kazi upo katika sekta zote, za umma na binafsi. Wizi, uzembe, udhuru wa kila siku na huduma mbaya kwa wateja ni baadhi ya malalamiko ya wawekezaji hapa nchini. Tabia hizi ni lazima zikemewe kama tunataka nguvu kazi yetu ipate ajira katika zama hizi tunazohamasisha mapinduzi ya viwanda. Hivyo, ni wajibu wa kila mmoja wetu katika jamii kusimamia maadili na makuzi ya vijana ili nguvu kazi hii iweze kutumika ipasavyo kuchangia ukuaji wa uchumi.

11. Mheshimiwa Spika, imani yetu ni kwamba tumeanza vizuri kwenye suala la kuongeza uwajibikaji na maadili ndani ya Serikali. Serikali itaendelea kuwawajibisha wale wote ambao hawataendana na Falsafa na Mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano. Jambo la msingi ni kwamba tutachukua hatua kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma. Niwahakikishie Watanzania kwamba hakuna mtumishi au mwananchi atakayeonewa au kunyanyaswa katika zoezi hili. Hivyo, wale wote ambao wako safi waendeleo kutimiza wajibu wao bila woga. Kazi zifanyike kwa weledi na kwa kasi bila urasimu.

12. Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua hatua za kuongeza mapato na kuziba mianya ya ukwepaji kodi ambazo zimeonesha manufaa makubwa. Mathalan, hatua tulizochukua za kubana mianya ya ukwepaji kodi zimeimarisha makusanyo ya mapato ya ndani kutoka wastani wa Shilingi Bilioni 870 mwezi Novemba, 2015 na kufikia Shilingi trilioni 1.3 mwezi Machi, 2016. Tunaendelea kuimarisha ukusanyaji mapato kwa njia za kielektroniki, kuziba mianya ya ukwepaji kodi na kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kila anayetakiwa kulipa kodi alipe na fedha hizo zitumike kutekeleza mipango ya maendeleo. Vilevile, Serikali itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kusimamia matumizi sahihi ya rasilimali. Fedha zinazopatikana zitaelekezwa kwenye miradi ya kipaumbele yenye kuleta maendeleo ya haraka kwa wananchi.

13. Mheshimiwa Spika, uchumi wa viwanda utajengwa na Sekta Binafsi. Kazi ya Serikali ni kuhakikisha kunakuwa na mazingira rafiki kwa sekta hiyo kuwekeza. Hivyo, Serikali itaendelea kubuni na kutekeleza miradi itakayoweza sekta binafsi kuwekeza bila vikwazo. Miradi hiyo ni pamoja na miundombinu muhimu ya uchukuzi na usafirishaji, umeme, mawasiliano na maji kwa ajili ya uzalishaji na biashara. Napenda kutumia fursa hii kuwahakikishia wawekezaji wote nchini na wengine wanaokusudia kuwekeza kwamba Serikali imedhamiria kushirikiana kwa karibu na sekta binafsi. Hatua zote zinazochukuliwa sasa ni za kuhakikisha kwamba sekta binafsi inawekewa mazingira wezeshi na yenye ushindani wa haki ili iweze kuimarika.

SIASA

14. Mheshimiwa Spika, mtangamano wa kisiasa ni nguzo muhimu katika kujenga Nchi yenye maendeleo makubwa na ya uhakika. Mtangamano wa kisiasa unajumuisha siasa safi, za kiustaarabu na zinazoheshimu mawazo ya kila mmoja wetu. Siasa za aina hii ndiyo chimbuko la mustakabali wa amani na utulivu wa Taifa letu tangu tujipatie uhuru. Ni jambo la faraja na kufurahisha kwamba, pamoja na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 kujaa tashwishwi na ushindani mkubwa, Taifa letu limeendelea kuwa na amani, utulivu na mshikamano mkubwa Kitaifa kiasi cha kupigiwa mfano Barani Afrika na dunia kwa ujumla. Hali hii inaonesha kukua na kuimarika kwa demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini ambapo hadi sasa vipo vyama 22 vyenye usajili wa kudumu na vyama vitatu vyenye usajili wa muda na vingine sita vimewasilisha maombi ya usajili wa muda.

15. Mheshimiwa Spika, Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 umesaidia kupima namna demokrasia inavyozidi kukua na kupanuka kwani kwa mara ya kwanza kulikuwa na mwitikio mkubwa wa kujitokeza kwa wagombea wa nafasi

mbalimbali za uongozi na wananchi wengi kujiandikisha kupiga kura. Vyama nane vilisimamisha wagombea wa nafasi ya Urais na vyama 22 Ubunge na Udiwani. Idadi ya wapiga kura walioandikishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilikuwa 23,161,440, sawa na asilimia 96.9 ya makadirio. Idadi ya watu waliopiga kura ilikuwa ni 15,596,110, sawa na asilimia 67.3 ya waliojiandikisha. Hii ni idadi kubwa ya wapiga kura ikilinganishwa na chaguzi zote zilizopita. Hivyo, naomba nichukue fursa hii kuipongeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya kuanzia katika uboreshaji wa Daftari la Wapiga Kura, ugawaji wa majimbo mapya ya uchaguzi, kutoa elimu kwa umma, uandikishaji wa wapiga kura na kuusimamia kwa umakini mkubwa uchaguzi wenyewe na kutangaza matokeo. Tume ilifanya kazi yake kwa uhuru na kwa weledi mkubwa. Niwapongeze viongozi na wananchi wote walio Shiriki uchaguzi huo kwa amani na utulivu.

16. Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Tume na wananchi kuitikia wito wa kujiandikisha na kupiga kura, bado kulikuwa na idadi kubwa ya waliojiandikisha lakini hawakupiga kura. Naiagiza Tume ya Uchaguzi kufanya tathmini ya kina kubaini sababu zilizofanya wapiga kura zaidi ya Milioni saba waliojiandikisha kupiga kura kutoitumia haki yao ya Kikatiba. Hii itasaidia kuboresha chaguzi zijazo kwani wananchi wana wajibu wa kutumia haki yao ya msingi kuchagua viongozi wanaowataka. Aidha, tathmini itasaidia kubaini iwapo kuna vikwazo vinavyowazuia baadhi ya watu kupiga kura ili kwa pamoja tuviondoe. Ndani ya Bunge hili tupo wabunge wa Vyama mbalimbali lakini kwa lengo moja tu la kuwawakilisha wananchi wetu na kuishauri Serikali ili ipange mipango mizuri itakayoharakisha maendeleo yao. Niseme tu kwamba sasa Uchaguzi Mkuu umekwisha na Serikali zetu zipo madarakani kwa mujibu wa Katiba. Hivyo, tuienzi falsafa ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya "Hapa Kazi Tu!" kwa kuchapa kazi na tusitoe nafasi kwa tofauti zetu za kisiasa na kiitikadi kuwa kisingizio cha kukwamisha shughuli za maendeleo ya Nchi yetu.

17. Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuendelea kukuza Demokrasia ili kuwezesha ushiriki mpana wa wananchi katika kufanya maamuzi ya maendeleo yao katika Taifa letu chini ya mfumo wa vyama vingi vya siasa. Hivyo, Serikali inaandaa mapendekezo ya marekebisha ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 na Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya Mwaka 2010 kwa lengo la kuondoa changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wake na kuzifanya ziendane na hali halisi ya siasa nchini na kwa mtazamo wa baadaye.

UCHUMI

Ukuaji wa Uchumi

18. Mheshimiwa Spika, malengo yetu ya kufikia Nchi ya kipato cha kati na kufanyika mapinduzi makubwa ya viwanda yanategemea sana utulivu wa uchumi. Kwa ujumla, ukuaji wa uchumi umekuwa wa kuridhisha kwani mwaka 2015, uchumi ulikua kwa asilimia 7.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2014. Sekta zilizochangia katika ukuaji huo ni pamoja na Ujenzi, Mawasiliano, Fedha, Uchukuzi na Nishati. Pamoja na ukuaji huu mzuri wa ujumla, Sekta ya Kilimo inayoajiri zaidi ya asilimia 66.3 ya Watanzania wote wanaofanya kazi ilikua kwa asilimia 3.4 tu mwaka 2014. Ukuaji huo mdogo unamaanisha kwamba juhudi za ziada na kubwa zinahitajika ili sekta hii muhimu iweze kutoa mchango mkubwa zaidi wakati tunapotekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo. Historia ya maendeleo ya uchumi inatuambia kwamba, Sekta ya Kilimo ina mchango mkubwa na muhimu kwenye mapinduzi ya viwanda. Hivyo hatuna uchaguzi mwingine bali kuelekeza nguvu zaidi kwenye sekta hii ya kilimo.

19. Mheshimiwa Spika, kwa ujumla tutahitajika kuongeza ufanisi na tija katika sekta zote za uzalishaji na utoaji huduma ili malengo yetu ya ukuaji uchumi yafikiwe katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Katika kufikia azma hiyo, tutatekeleza sera madhubuti za fedha na kodi zitakazoweza mfumuko wa bei kuendelea kushuka na kubaki katika tarakimu moja kama ilivyo sasa. Mathalan, mfumuko wa bei mwaka 2015 ulifikia wastani wa asilimia 5.6 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.1 kwa mwaka 2014. Mwelekeo huu wa utulivu wa uchumi utavutia mitaji mingi kutoka Sekta Binafsi kuwekeza kwenye sekta za kipaumbele, kuwezesha ongezeko la ajira na kupanua wigo wa ulipaji kodi.

Mazingira Wezeshi ya Uwekezaji

20. Mheshimiwa Spika, awali nilidokeza kwamba, uwekezaji kwenye viwanda na sekta nyingine za kiuchumi utafanywa na sekta binafsi na jukumu la msingi la Serikali ni kuweka mazingira wezeshi. Kwa msingi huo, Serikali ya Awamu ya Tano itachukua hatua madhubuti na za haraka kupunguza muda, gharama na idadi ya taratibu za kiutawala ambazo Wafanyabiashara na Wawekezaji hulazimika kuzifuata ili kufanya biashara nchini. Taratibu zinapokuwa ngumu na ndefu husababisha ongezeko la gharama za kufanya biashara na hivyo kuwakatisha tamaa wawekezaji. Taarifa ya Wepesi wa Kufanya Biashara duniani inayotolewa na Benki ya Dunia iliyochapishwa mwezi Novemba, 2015 inaonesha kwamba katika mwaka 2016, Tanzania imeshika

nafasi ya 139 kati ya Nchi 189 Duniani. Hali hii haikubaliki kabisa. Hivyo, eneo hilo litafanyiwa kazi haraka ili kuharakisha mapinduzi ya viwanda.

21. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Serikali itaimarisha utekelezaji wa Mpangokazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini. Utekelezaji huo utazingatia maelekezo aliyoyatoa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati wa mkutano na Wafanyabiashara uliofanyika mwezi Desemba, 2015. Katika mkutano huo, pamoja na mambo mengine, Mheshimiwa Rais aliwataka watendaji kupunguza urasimu usio wa lazima kwa wafanyabiashara na wawekezaji. Nitumie fursa hii kuwataka Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuyatumia mabaraza ya biashara ya Mikoa na Wilaya ili kuhakikisha juhudi shirikishi za uboreshaji wa mazingira ya biashara zinatekelezwa hadi ngazi ya chini. Pia, nawataka watumishi wa umma kuepuka kuwachelewesha kwa uzembe au makusudi wawekezaji wenye nia njema ya kuwekeza nchini ili kuleta maendeleo endelevu kwa wakati. Mtumishi yeyote wa umma atakayeendeleza urasimu usio wa lazima hatavumiliwa.

Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

22. Mheshimiwa Spika, azma ya kuwawezesha Watanzania kushiriki kikamilifu kwenye uchumi wa viwanda ni jambo la msingi. Hivyo, Serikali itaendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kuwadhamini wajasiriamali wenye miradi inayokidhi vigezo kwenye Taasisi za Fedha ili wapate mikopo yenye masharti nafuu. Pamoja na hatua hizo, Mpango Maalum wa Ushiriki wa Watanzania katika miradi mikubwa ya uwekezaji ulioandaliwa utatekelezwa. Mpango huo unalenga kuhakikisha kwamba Watanzania wananufaika zaidi na rasilimali za Nchi yao kwa njia ya ubia kwenye miradi ya uwekezaji, ajira na kandarasi mbalimbali zitakazotolewa na kampuni kubwa kwa Wazawa. Wananchi pia wataendelea kuwezeshwa kupitia mikopo yenye masharti nafuu kwa vikundi mbalimbali vya kiuchumi vya wakulima, wafugaji, wavuvi, wafanyabiashara na wachimbaji wadogo wa madini inayotolewa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Serikali imeruhusu Mifuko hiyo kutoa mikopo nafuu kwa wanachama wa vikundi vinavyojiunga na Mifuko kunufaika na mafao ya afya na pensheni yanayotolewa na mifuko husika.

23. Mheshimiwa Spika, Serikali imehamasisha uanzishaji na usajili wa Vikundi vya Kiuchumi kama vile Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa (SACCOs) na Benki za Jamii Vijijini (VICOBA). Serikali pia imesimamia uanzishwaji wa Taasisi Mwavuli ya kusimamia VICOBA inayoitwa VICOBA FETA. Takwimu zilizotolewa mwezi Februari 2016 na Taasisi hiyo zinaonesha kuwa kuna vikundi 100,000 vya VICOBA vyenye wanachama Milioni 2.2 na mtaji wa Shilingi trilioni

1.2. Ni jambo la kujivunia kwamba asilimia 79 ya wanachama wa VICOBA ni wanawake.

24. Mheshimiwa Spika, moja ya ahadi muhimu iliyopo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 ni kutenga Shilingi Milioni 50 kwa kila kijiji nchini zitakazotumika kwa utaratibu wa mzunguko (Revolving Fund). Lengo ni kuwawezesha wananchi kuanzisha na kuendeleza shughuli za uzalishaji kupitia Ushirika wa Kuweka na Kukopa na vikundi vingine vya kiuchumi.

Uhakiki wa Vyama vya Ushirika wa Kuweka na Kukopa uliofanywa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika unaonesha kwamba idadi ya SACCOs zinazokidhi vigezo vya usajili nchini imepungua kutoka 5,559 mwaka 2013 hadi 3,856 mwaka 2015. Kati ya hizo, SACCOs 2,125 sawa na asilimia 55 zipo Vijijini na 1,740 zipo Mijini. Ni dhahiri kwamba Mpango wa Shilingi Milioni 50 kwa kila Kijiji unahitaji maandalizi mazuri, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uanzishaji na usajili wa SACCOs na vikundi vya kiuchumi vinavyokidhi vigezo, ili kuhakikisha kwamba fedha zinazotolewa zinawafikia walengwa na zinatumiwa kwa shughuli zilizokusudiwa. Ninaziagiza Halmashauri zote nchini ziweke orodha sahihi ya Vyama vya Ushirika wa Kuweka na Kukopa vilivyosajiliwa kwa kila Kijiji na kuchukua hatua za kuwezesha uanzishaji na usajili wa SACCOs zinazokidhi vigezo kulingana na shughuli za uzalishaji katika Halmashauri husika.

25. Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, maandalizi ya utekelezaji wa Mpango huo yanaendelea vizuri katika kila Halmashauri. Tutatumia uzoefu uliopatikana kwenye utekelezaji wa mifuko mingine, ukiwemo Mfuko wa Kuwawezesha Wananchi na Kuongeza Fursa za Ajira maarufu kama “Mabilioni ya JK”, ili changamoto zilizojitokeza zitusaidie kuboresha Mpango huu mpya.

26. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuziwezesha Kaya maskini ili ziweze kupata mahitaji yao ya msingi na kuongeza kipato kupitia Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III). Tangu utekelezaji wa Mpango huo uanze kaya maskini 1,099,289 zimepokea kiasi cha Shilingi Bilioni 164.8 kama ruzuku katika Halmashauri 159 za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Aidha, kupitia Mpango wa Ajira za Muda kwa Kaya Maskini, iliandaliwa miradi 1,880 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 42.6 kutoka Halmashauri 40 za Tanzania Bara na Zanzibar. Katika mwaka 2016/2017, Serikali itaendelea kufanya utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini katika maeneo ambayo hayakufikiwa.

Ajira

27. Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 imeweka umuhimu katika kupanua fursa za ajira kwa kutumia rasilimali zilizopo nchini ili kila mwenye uwezo wa kufanya kazi achangie kwenye uchumi na kupata kipato halali. Msisitizo huo wa Ilani ya Uchaguzi unatokana na ukweli kwamba Utafiti wa Hali ya Ajira Nchini wa mwaka 2014 umeonesha kuwa kiwango cha ukosefu wa ajira kimepungua kutoka asilimia 11.7 mwaka 2006 hadi asilimia 10.3 mwaka 2014. Aidha, ukosefu wa ajira kwa vijana umepungua kutoka asilimia 14.2 mwaka 2006 hadi asilimia 11.7 mwaka 2014. Kiwango hicho bado ni kikubwa na tunaweza kufanya vizuri zaidi. Jitihada za Serikali za kuvutia uwekezaji kwenye sekta mbalimbali na urasimishaji wa sekta isiyo rasmi zitaendelezwa ili kupunguza zaidi kiwango cha ukosefu wa ajira nchini.

28. Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto zinazosababisha ukosefu wa ajira ni vijana wetu kutojengewa maarifa na ujuzi wa kuajiriwa na kuajirika. Hivyo, Serikali itaendelea kutekeleza Programu ya Miaka Mitano ya Kukuza Ujuzi Nchini (2015/2016 – 2019/2020). Programu hiyo inalenga kuongeza idadi ya watu wenye kiwango cha juu cha ujuzi kutoka asilimia 3 ya sasa hadi asilimia 12 inayotakiwa kuendesha uchumi wa viwanda. Vilevile, kupunguza idadi ya watu wenye kiwango cha ujuzi wa chini kutoka asilimia 75 ya sasa hadi 54. Utekelezaji wa Programu hiyo utasaidia kupunguza pengo la mahitaji ya rasilimali watu nchini ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya haraka ya uchumi wa viwanda. Serikali itahakikisha kuwa suala la ukuzaji ajira linazingatiwa katika mipango yote ya uwekezaji pamoja na mipango ya maendeleo ya kisekta katika ngazi zote. Hivyo, naziielekeza Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi za Umma, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha ukuzaji wa ajira unakuwa ni agenda ya msingi ya kudumu katika utekelezaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo. Tayari Mheshimiwa Rais amewaagiza Wakuu wa Mikoa kuhakikisha kwamba vijana ambao ndiyo nguvu kazi kuu ya Taifa wanatumia fursa itakayopatikana kutokana na Shilingi Milioni 50 zitakazotolewa kwa kila kijiji kuanzisha miradi ya maendeleo ya kujipatia kipato.

VIJANA

29. Mheshimiwa Spika, vijana ni hazina na rasimali watu muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, inaonesha kuwa idadi ya vijana wenye umri kati ya miaka 15 na 35 ni takribani Milioni 16.2, sawa na asilimia 35.1 ya Watanzania wote. Aidha, Utafiti wa Nguvu Kazi wa mwaka 2014 unaonesha kuwa vijana ni asilimia 59 ya nguvu kazi ya Taifa. Matokeo ya tafiti hizo yanathibitisha kuwa kuna umuhimu wa kuzingatia mahitaji ya vijana na ushirikishwaji wao katika mipango ya maendeleo. Katika mwaka

2014/2015 hadi 2015/2016, Serikali imewawezesha vijana kiuchumi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Hadi kufikia mwezi Machi 2016, mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 1.6 imetolewa na Mfuko huo kwa vikundi vya vijana 284 na mafunzo yametolewa kwa viongozi wa vikundi 2,552 kutoka Halmashauri 59. Vilevile, Serikali imetenga maeneo maalum ya shughuli za kiuchumi na huduma kwa vijana katika Halmashauri 30 nchini.

30. Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha dhana ya ushiriki na ushirikishwaji wa vijana katika shughuli za maendeleo, Bunge la Kumi lilitunga Sheria Na. 12 ya Baraza la Taifa la Vijana ya mwaka 2015. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba sasa Kanuni za utekelezaji wa Sheria hiyo zimekamilika. Hivyo, katika mwaka 2016/2017, Serikali itaendelea kuratibu uanzishwaji wa Baraza la Vijana la Taifa na kuhimiza uanzishaji na uimarishaji wa SACCOs za vijana katika Halmashauri zote nchini na kuziwezesha kupitia Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Vijana na Taasisi za fedha.

31. Mheshimiwa Spika, Maadili na Makuzi ya Vijana ni suala linalopewa kipaumbele na Serikali ya Awamu ya Tano. Hatuwezi kujenga uchumi imara wa viwanda, kuongeza fursa za ajira na kuwa na matumizi sahihi ya rasilimali za umma kama jamii yetu, hasa vijana hawatajitambua kwa kuwa waadilifu, wazalendo na wachapakazi. Serikali, itaendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Stadi za Maisha na Programu ya kujitolea kwa vijana ili kukuza maadili, uzalendo na kujenga utamaduni wa kuchapa kazi kwa vijana.

WATU WENYE ULEMAVU

32. Mheshimiwa Spika, Serikali inathamini mchango mkubwa wa watu wenye ulemavu katika maendeleo na kwamba wana haki sawa ya kutumia fursa mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Katika kuzingatia azma hiyo, Serikali inatekeleza Sheria ya Watu wenye Ulemavu Na. 9 ya mwaka 2010, ambayo, imewezesha kuundwa kwa Baraza la Kitaifa la Ushauri la Watu wenye Ulemavu ili kuongeza ushiriki wa Watu wenye Ulemavu katika maamuzi. Aidha, Kamati za kushughulikia masuala ya watu wenye ulemavu zimeundwa katika ngazi za Mikoa, Halmashauri, Kata, Mitaa na Vijiji kwa ajili ya kuratibu masuala muhimu kwa watu wenye ulemavu katika maeneo husika.

33. Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali kuwalinda na kuwapatia fursa, kumekuwepo na matukio ya vitendo vya ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu hususan wenye ualbino. Ukatili huo umesababisha watu wenye ualbino kupoteza maisha na wengine kupata aina nyingine ya ulemavu wa kudumu. Hali hiyo haikubaliki na haivumiliki katika jamii ya Watanzania. Serikali inafanya jitihada kubwa kukomesha vitendo hivyo ikiwa

ni pamoja na kuwakamata wote wanaojihusisha na vitendo hivyo na kuwafikisha katika vyombo vya sheria. Aidha, itaendelea kutoa elimu kwa jamii ili kubadili mitazamo na imani potofu kuhusu watu wenye ualbino na ulemavu kwa ujumla. Napenda kusisitiza kwamba watu wenye ulemavu wana haki ya kuthaminiwa utu wao na kulindwa dhidi ya ukatili na aina yoyote ya ubaguzi.

34. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Serikali itaviboresha Vyuo vya Ufundi na Marekebisho (*Vocational and Rehabilitation Training Centres*) vya watu wenye ulemavu nchini ili kutoa ujuzi unaoendana na mahitaji yao katika soko la ajira. Serikali pia, itaandaa walimu wa elimu maalum na kutoa vifaa saidizi kwa walimu na wanafunzi wenye ulemavu mashuleni. Kwa sasa Serikali imeanzisha utaratibu wa kuwahabarisha watu wenye usikivu hafifu kwa kuanzisha tafsiri za matangazo kwa njia za alama. Hivyo, wamiliki wote wa televisheni wametakiwa kuajiri wakalimani.

KAZI NA HIFADHI YA JAMII

Kazi

35. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa sheria na viwango vya kazi kwa kufanya kaguzi ili kuhakikisha waajiri wanazingatia mikataba ya ajira, masaa ya kazi, likizo na ujira kwa lengo la kupunguza migogoro na kuongeza tija. Hadi kufikia Machi 2016, jumla ya kaguzi za kazi 1,305 zilifanyika na migomo 23 katika sekta za usafirishaji, viwanda, ujenzi na kwenye migodi ilisuluhishwa na kupatiwa ufumbuzi. Aidha, kaguzi za kawaida 4,670 na kaguzi maalum 17,005 zilizojuumisha kaguzi za umeme, mitambo na vipimo vya mazingira ili kuhakikisha wafanyakazi wanakuwa na afya njema na usalama mahala pa kazi zilifanyika.

36. Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kuratibu Ajira ya Wageni Na. 1 ya Mwaka 2015 ilitungwa na kumpa Kamishna wa Kazi mamlaka ya kutoa vibali vya kazi nchini ili kukuza fursa za ajira kwa Watanzania. Tangu Sheria hiyo ianze kutumika rasmi tarehe 15 Septemba 2015 hadi mwezi Machi 2016, mapato yaliyopatikana kutokana na vibali vya kazi vilivyotolewa nchini ni Shilingi Bilioni 21.01, sawa na asilimia 356 ya lengo la makadirio ya Shilingi Bilioni 7.5 kwa mwaka 2015/2016. Serikali pia imefanya kaguzi katika makampuni na taasisi 400 zenye jumla ya wageni 3,939 na kubaini wageni 779 hawana vibali vya kuishi na kufanya kazi nchini. Kati ya hao, wageni 29 waliondolewa nchini, 317 walipewa hati maalum (*special pass*), 77 walifikishwa mahakamani na 356 walielekezwa kukamilisha taratibu za ukaazi wao kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Sheria ya Uhamiaji. Katika mwaka 2016/2017, Serikali itafanya kaguzi za kazi 56,200 katika

maeneo mbalimbali ya kazi nchini na itaanzisha Bodi mbili za kupanga kima cha chini cha mishahara kwa sekta ya umma na binafsi.

Hifadhi ya Jamii

37. Mheshimwa Spika, Sekta ya Hifadhi ya Jamii ina mchango mkubwa katika uchumi wa Nchi yetu. Kwa kutambua hilo, Serikali imeifanyia tathmini mifuko sita ambayo ni GEPP, LAPF, NHIF, NSSF, PPF na PSPF kwa lengo la kupima uendelevu wake. Tathmini hiyo imebainisha kuwa mifuko hiyo bado ni endelevu na rasilimali zake zimefikia Shilingi trilioni 8.8. Aidha, Mamlaka ya Usimamizi na Udhubiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii imetoa miongozo ya kupunguza gharama za uendeshaji wa Mifuko hiyo itakayoanza kutumika Julai, 2016. Serikali imekamilisha uhakiki wa madeni ya PSPF yaliyokuwepo kabla ya kuanzishwa kwa Mfuko huo mwaka 1999 yenye thamani ya Shilingi trilioni 2.9. Hadi sasa, Serikali imelipa sehemu ya deni la PSPF kiasi cha shilingi bilioni 180 ili kuhakikisha kwamba mafao ya wastaafu wa Mfuko huo yanalipwa kwa wakati. Serikali pia itaendelea kulipa deni la shilingi bilioni 840.4 linalotokana na miradi ya Serikali iliyogharamiwa na mifuko ya GEPP, LAPF, NHIF, NSSF na PPF.

38. Mheshimiwa Spika, hadi sasa asilimia 6.5 ya Watanzania wote ndiyo wanaofikiwa na huduma ya Hifadhi ya Jamii. Katika mwaka 2016/2017, Serikali itaendelea kutekeleza Programu ya Maboresho ya Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa kuongeza wigo wa wanaofikiwa na huduma hiyo. Hii ni pamoja na kujumuisha makundi mengine katika jamii kama vile wazee na watu wenye ulemavu ambapo rasimu ya andiko la mpango wa pensheni kwa makundi hayo imekamilika. Hatua inayoendelea hivi sasa ni ushirikishwaji wa wadau na taasisi zitakazohusika katika kutekeleza mpango huo. Aidha, Serikali itaendelea kuhamasisha uchangiaji wa hiari na kusimamia uendeshaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuhakikisha inaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kuchangia zaidi katika ukuzaji wa uchumi bila kuathiri mifuko.

SEKTA ZA UZALISHAJI MALI

(a) Uzalishaji wa Mazao na Akiba ya Chakula

39. Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo inayojumuisha uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na mazao ya misitu ndio tegemeo la maisha ya watanzania walio wengi. Hata hivyo, ukuaji wa sekta hiyo umekuwa siyo wa kuridhisha kutokana na matumizi ya teknolojia isiyoendana na wakati na pia kutegemea majaliwa ya Mwenyezi Mungu ya hali ya hewa. Pamoja na changamoto hizo, hali ya upatikanaji wa chakula imeendelea kuwa ya kuridhisha katika maeneo mengi hapa nchini. Katika msimu wa 2014/2015,

wakulima walizalisha Tani Milioni 15.5 za mazao ya chakula. Kutokana na uzalishaji huo, Nchi imejitosheleza kwa chakula kwa asilimia 120 kwani mahitaji ya chakula kwa mwaka 2015/2016 ni Tani Milioni 12.95. Hali hii pia imetuwezesha katika msimu huu kutoa chakula cha msaada na cha bei ya chini katika maeneo yaliyopata upungufu wa chakula. Aidha, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula - NFRA iliuzia jumla ya Tani 239,322 ya akiba yake kwa wafanyabiashara nchini ili kukabiliana na mfumuko wa bei za vyakula hususan unga wa sembe katika masoko ya mijini. Hadi kufikia mwezi Aprili 2016, NFRA ilikuwa na akiba ya Tani 67,895 za chakula. Katika mwaka 2016/2017, Serikali itanunua Tani 100,000 kwa ajili ya hifadhi ya chakula.

40. Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuleta mapinduzi katika sekta ya kilimo kwa kupanua na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji ili kuzalisha zaidi kwa ajili ya usalama wa chakula, kuuza ziada nje na kupata malighafi za viwandani. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, inalenga kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka Hekta 461,326 za sasa hadi Hekta Milioni moja ifikapo mwaka 2020. Ili kufikia lengo hilo, Serikali itashirikiana na sekta binafsi katika kujenga, kukarabati na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji nchini.

(b) Ruzuku za Pembejeo

41. Mheshimiwa Spika, ongezeko la tija katika uzalishaji wa mazao unategemea kwa kiasi kikubwa matumizi ya pembejeo zikiwemo mbolea na mbegu bora zenye ukinzani na ustahimilivu wa magonjwa na ukame; na zenye uwezo mkubwa wa kutoa mavuno. Katika msimu wa 2015/2016, Serikali imetoa vocha milioni tatu za pembejeo za kilimo zikiwemo Tani 10,271 za mbegu bora za mahindi na mpunga na Tani 99,923 za mbolea ambazo zimesambazwa katika mikoa 24 ya Tanzania Bara na kunufaisha kaya 999,926. Ninawaagiza Wakuu wa Mikoa hiyo kuhakikisha kuwa pembejeo hizo zinawafikia walengwa kwa wakati na zinatumiwa kama ilivyotarajiwa na kuwachukulia hatua wale wote watakaohujumu mpango huu.

(c) Benki ya Maendeleo ya Kilimo

42. Mheshimiwa Spika, mwezi Agosti 2015, Serikali ilizindua Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili kuwawezesha wakulima kupata mikopo yenye riba nafuu. Benki hiyo inatoa mikopo ya muda mfupi na muda mrefu kwa riba kati ya asilimia saba na 12 imeanza na mtaji wa Shilingi Bilioni 60. Mikopo inayotolewa na Benki hiyo inalenga kusaidia kugharamia uandaaji wa mashamba, ununuzi wa pembejeo za kilimo, usindikaji wa mazao pamoja na hifadhi ya mazao. Serikali itaendelea kuiongezea mtaji Benki hiyo ili ikopeshe wakulima wengi zaidi hasa kupitia vikundi vya wanawake na vijana

vinavyojihusisha na kilimo. Benki hiyo itasimamia kiasi cha Dola za Marekani Milioni 25 kwa ajili ya kudhamini mabanki ya biashara ili yaongeze ukopeshaji kwenye miradi ya miundombinu ya masoko na kuendeleza ubunifu kwenye miradi ya maendeleo vijijini chini ya Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji wa Thamani na Huduma za Kifedha Vijijini (MIVARF). Vilevile, Benki hiyo itakuwa Wakala wa Serikali wa kusimamia fedha za ruzuku ya pembejeo.

(d) Miundombinu ya Masoko

43. Mheshimiwa Spika, Serikali itaimarisha utekelezaji wa Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani na Huduma za Kifedha Vijijini (MIVARF) inayotekelezwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Programu hiyo inasaidia kuboresha miundombinu ya masoko, zikiwemo barabara na maghala ya kuhifadhia mazao; kuwawezesha wananchi waishio vijijini kuongeza thamani ya mazao ya kilimo; lakini pia kuwajengea wananchi uwezo wa kuyafikia masoko na kupanua wigo wa huduma za kifedha vijijini.

44. Mheshimiwa Spika, chini ya Programu hiyo katika mwaka 2015/2016, Serikali imekarabati barabara za vijijini zenye urefu wa kilomita 180 kwa kiwango cha changarawe zikiwemo kilomita 63.6 za Zanzibar. Aidha, imejenga maghala matano yenye uwezo wa kuhifadhi Tani 1,000 za mazao kila moja na kuvijengea uwezo wa kufikia masoko vikundi 780, vikiwemo vikundi 101 vya Tanzania Zanzibar. Vilevile, imezijengea uwezo Asasi ndogo za Kifedha, zikiwemo SACCOs 291 na Benki tisa za Wananchi ili ziweze kutoa huduma endelevu za kifedha.

Katika mwaka 2016/2017, Serikali itaendelea na uboreshaji wa miundombinu ya masoko katika Halmashauri 38 za Tanzania Bara na Wilaya 10 za Zanzibar. Aidha, itaendelea kuwajengea wazalishaji wadogo uwezo wa kuhifadhi na kusindika mazao, mbinu za kufikia masoko na Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

Mifugo

45. Mheshimiwa Spika, tunayo fursa ya kufanya mageuzi makubwa kwenye sekta ya mifugo kama tutawekeza kwenye viwanda vya kusindika nyama ili kuongeza thamani na kuzalisha bidhaa za aina mbalimbali kutokana na mifugo iliyopo nchini. Hali ilivyo sasa siyo nzuri kwani tunauza mifugo mingi nje ya nchi ikilinganishwa na nyama. Mathalan, katika mwaka 2015/2016 hadi kufikia mwezi Machi 2016, ng'ombe milioni 1.5, mbuzi milioni 1.2 na kondoo 253,243 wenye thamani ya Shilingi Bilioni 976.5 waliuzwa nje ya nchi. Hii ina maana kuwa mazao kama ngozi, kwato na damu za wanyama hao, ambazo zingeweza kutumika kuzalisha bidhaa nyingine za viwandani, yamekwenda nje

badala ya kutumika hapa nchini. Tunaweza kabisa kugeuza hali hii haraka kwa kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani mifugo. Nashauri wawekezaji binafsi kwenye sekta ya mifugo kuchangamkia fursa ya kufufua viwanda vya nyama vilivyopo na kujenga vingine vipya ili kuongeza thamani ya mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuanze kubadili fikra za wafugaji wetu ili ufugaji uwe na tija kwa kuwa na idadi ndogo ya mifugo yenye ubora wa kisasa na inayoendana na uwezo wa eneo la malisho. Serikali itaweka msisitizo wa kipekee katika kuboresha kosaafu za mifugo ili kuzalisha mifugo yenye tija kwa kusambaza ng'ombe bora kwa ajili ya uzalishaji wa maziwa na nyama kutoka katika mashamba ya kuzalisha mifugo na kuimarisha uwekezaji katika viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo. Vilevile, juhudi za kudhibiti magonjwa ya mifugo yasiyokuwa na mipaka na yenye athari kubwa katika uchumi wa Taifa zitaongezwa.

Serikali itaendelea kufanya tathmini ya uendeshaji wa ranchi za Taifa zilizobinafsishwa ili kuhakikisha kwamba wale waliopewa vitalu vya mifugo wanavitumia kwa mujibu wa mikataba ya mauzo au vinginevyo kuwanyang'anya na kuwapa wengine wenye uwezo.

Viwanda

46. Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuweka nguvu kubwa katika sekta ya viwanda ili kufikia lengo la kuwa Nchi ya uchumi wa viwanda. Azma hiyo imesisitizwa sana na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Ili kufikia uchumi wa viwanda, kuanzia mwaka 2016/2017 jitihada kubwa itawekwa katika kutenga na kuendeleza maeneo maalum ya viwanda; kuweka miundombinu muhimu ya nishati, usafirishaji, maji na maghala. Aidha, tutaweka utaratibu endelevu wa upatikanaji mitaji na teknolojia ikiwemo kuanzisha dirisha maalum katika Benki ya Maendeleo TIB na Benki ya Maendeleo ya Kilimo. Serikali pia itapitia mifumo ya kodi, tozo na taratibu mbalimbali kwa lengo la kuzipunguza na kuondoa urasimu ili kupunguza gharama za uzalishaji wa ndani na kuwezesha bidhaa zetu kushindana katika soko la ndani na kimataifa. Aidha, Serikali itaifanyia mapitio ya Sera ya Uwekezaji ya mwaka 1996 na Sheria yake ya mwaka 1997 ili kuendana na wakati.

Masoko

47. Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa masoko ya uhakika unategemea mambo makuu manne. Ubora wa bidhaa au mazao; uhakika wa kupatikana kwa mazao au bidhaa wakati wote; unafuu wa bei dhidi ya washindani wengine katika soko; na ufungashaji na ujenzi wa jina la bidhaa (branding). Hivyo, ni lazima mlolongo wote wa uzalishaji, uongezaji thamani na usafirishaji uwe mzuri kuwezesha uwepo wa soko la uhakika. Mtiririko huo katika mnyororo wa thamani wa bidhaa zenye uhakika wa soko ndio msisitizo wa Serikali ya Awamu ya Tano na msingi wa kuhamasisha mapinduzi ya viwanda kwa lengo la kuongeza thamani bidhaa zetu kabla ya kuuzwa. Msukumo mkubwa utawekwa katika uendelezaji na upatikanaji wa soko la ndani na nje kwa bidhaa zinazozalishwa nchini, hususan katika masoko ya upendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na masoko mengine ya kimkakati ya Kikanda na Kimataifa. Vivyo hivyo, uondoaji wa vikwazo vya kibiashara pamoja na kusimamia viwango na ubora wa bidhaa za ndani na nje ya nchi utaendelezwa.

48. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2015/2016, Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwemo Tanzania zimekamilisha mkataba mwingine wa kutumia Soko la Marekani bila ushuru chini ya Mpango wa AGOA, kwa kipindi kingine cha miaka 10 kuanzia tarehe 30 Septemba, 2015 hadi 30 Septemba, 2025. Ni muhimu sana kutumia fursa hii mpya ya AGOA kufanya biashara na Marekani katika kipindi cha miaka 10 ijayo. Vyama vya wafanyabiashara ni lazima viwaandae wanachama wao kupata taarifa kamili kuhusu bidhaa zinazohitajika na ubora unaotakiwa. Aidha, Serikali itasimamia uzalishaji wa bidhaa bora kulingana na ubora unaotakiwa na masoko.

Madini

49. Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa uchimbaji madini mdogo kama kichocheo cha kuongeza ajira na kukuza kipato cha wachimbaji wadogo wa madini na wananchi wanaozunguka maeneo husika ya madini. Aidha, uchimbaji mdogo wa madini unachangia kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kuwatengea maeneo, kuwapatia ruzuku na kutoa mafunzo ya kuwawezesha kutekeleza kazi zao kwa ufanisi na tija. Katika mwaka 2015/2016, Serikali ilitenga Hekta 7,731 kwa ajili ya uchimbaji madini mdogo katika maeneo ya Nyamongo (Tarime) na Muhintiri (Singida). Aidha, Serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya TIB imetoa mikopo ya masharti nafuu yenye thamani ya Shilingi Bilioni 7.2 kwa ajili ya kukuza mitaji ya wachimbaji wadogo. Pia mafunzo yametolewa kwa wachimbaji wadogo 1,520.

Mikopo hiyo pia inaweza kutolewa kupitia benki ya TIB Corporate na TIB Development.

50. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Serikali itatenga zaidi maeneo tengefu kwa ajili ya uchimbaji madini mdogo na kuongeza kiasi cha ruzuku inayotolewa kwa Wachimbaji Wadogo. Serikali imetenga Shilingi Milioni 900 kwa ajili ya ruzuku na Benki ya Dunia imeridhia kutoa Dola za Marekani Milioni Tatu kuchangia kwenye ruzuku hiyo. Aidha, Serikali itaimarisha usimamizi katika biashara ya madini ya Tanzanite na kutoa mwongozo mpya wa namna ya kuendesha uchimbaji madini mdogo kwa tija. Mafunzo kuhusu namna ya kufanya utafiti wa awali wa madini na uchenjuaji bora wa madini yataendelezwa ili kazi za wachimbaji madini wadogo zifanyike kwa ufanisi na tija.

Utalii

51. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utalii ni moja ya sekta muhimu ambazo fursa zilizopo zikitumika vizuri zitasaidia sana kukuza ajira na kupunguza umaskini. Juhudi kubwa ambazo zimefanywa na Serikali katika kuboresha huduma na miundombinu ya kitalii pamoja na kutangaza vivutio vya utalii zimeiwzesha Sekta ya Utalii kuchangia asilimia 17 ya Pato la Taifa na zaidi ya asilimia 25 ya mapato yanayotokana na mauzo ya nje mwaka 2015. Aidha, mwezi Julai 2015 Serikali ilizindua Kampeni Maalum ya Kukuza Utalii wa Ndani ili kuhamasisha wananchi kutembelea vivutio vilivyopo katika Hifadhi zetu. Kampeni hiyo imeongeza idadi ya watalii wa ndani kutoka watalii 115,913 mwezi Septemba 2014 hadi 148,406 Septemba 2015. Mafanikio hayo yanadhihirisha kwamba Sekta ya Utalii ikiboreshwa ina fursa nyingi za kuchangia Pato la Taifa na kuongeza ajira na kipato cha wananchi. Hata hivyo, unahitajika uwekezaji mkubwa kwenye miundombinu ya utalii ikiwemo hoteli, usafirishaji na rasilimali watu imara na yenye weledi katika kuwahudumia watalii wa ndani na nje.

52. Mheshimiwa Spika, tunahitaji kufanya vizuri zaidi kwa kupanua vyanzo vya utalii na kuhakikisha fedha nyingi wanazotumia watalii kuja Tanzania zinalipwa hapa nchini badala ya utaratibu wa sasa wa malipo hayo kufanyika Nchi wanazotoka watalii. Tunahitaji pia kupanua na kuvutia utalii wa kihistoria na malikale kama vile miji mikongwe ya Kilwa, Mikindani, Bagamoyo na Mjimkongwe Zanzibar na vivutio vingine visivyo na mfano Barani Afrika; kuliko kuegemea tu utalii wa wanyamapori na maliasili nyingine. Katika mwaka 2016/2017, Serikali itaandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kuendeleza Utalii Nchini pamoja na kuendelea kutangaza vivutio maafufu kama Mlima Kilimanjaro, Mbuga za Serengeti na Mapango ya Olduvai.

Kudhibiti Ujangili

53. Mheshimiwa Spika, Nchi yetu inakabiliwa na tatizo la ujangili hasa wa tembo, faru na biashara haramu ya nyara za Serikali. Katika kukabiliana na tatizo hilo, Serikali ilizindua Mkakati wa Kupambana na Ujangili na Biashara haramu ya Nyara za Serikali ulioanza kutekelezwa mwaka 2015, kwa kuchukua hatua mbalimbali. Hatua hizo ni pamoja na kutumia vifaa na teknolojia ya kisasa kama vile “*Geographical Information System - GIS*” na “*Global Positioning System - GPS*”; kuimarisha mfumo wa mawasiliano ya radio kutoka mfumo wa analogia kwenda kidigitali; na kuanza kutekeleza Mpango wa Kikanda wa kukusanya taarifa za kiintelijensia zinazoongoza doria katika kukamata watuhumiwa na wahalifu.

54. Mheshimiwa Spika, Serikali itaimarisha utekelezaji wa Mkakati huo hususan kwa kuzingatia ukubwa wa changamoto ya vitendo vya uwindaji haramu vinavyofanywa na majangili kwa kushirikiana na baadhi ya watumishi wa Idara ya Wanyamapori wasio waaminifu na baadhi ya wananchi wanaoishi maeneo yanayozunguka mapori. Serikali ya Awamu ya Tano itahakikisha kwamba ujangili huu unakomeshwa haraka. Nichukue fursa hii kuziomba jamii zinazozunguka hifadhi zetu kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Serikali katika vita hii.

HUDUMA ZA KIUCHUMI

Ardhi

55. Mheshimiwa Spika, ili azma yetu ya kufanya mapinduzi ya viwanda ifanikiwe, inahitajika ardhi iliyopimwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda. Changamoto tuliyonayo hivi sasa ni kwamba sehemu kubwa ya ardhi yetu haijapimwa na kupatiwa hatimiliki. Hivyo, tumeanza kuchukua hatua za haraka zitakazowezesha kupatikana kwa ardhi ya kutosha kwa ajili ya ujenzi wa viwanda. Wakuu wa Mikoa na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa walishaagizwa kutenga maeneo ya viwanda na biashara katika Mipango Miji. Napenda kutumia fursa hii kuitaka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutopitisha maombi yoyote ya Mipango Miji yasiyokuwa na maeneo ya Viwanda na Biashara. Nimefarijika kuona kwamba chini ya Mpango wa Maeneo Huru ya Biashara, baadhi ya mikoa imeshatenga ardhi ambayo itaweza kuanza kutumika mara moja kutekeleza Mpango huo kwa kuwekewa miundombinu muhimu na kukamilisha upimaji. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji zishirikiane kufanya uhakiki wa haraka wa maeneo hayo ili wawekezaji watakaoonsesha nia ya kuwekeza kwenye viwanda wapatiwe maeneo yenye hatimiliki kwa haraka.

56. Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba kuna migogoro ya ardhi katika baadhi ya maeneo nchini. Migogoro hiyo, wakati mwingine imesababisha uharibifu wa mali, majeruhi na mauaji ya binadamu na mifugo. Njia muafaka ya kudhibiti migogoro hiyo ni kupima kila kipande cha ardhi, kukimilikisha kwa mtumiaji kwa kumpatia hatimiliki na kusimamia matumizi yake. Kwa kutambua hilo, mwezi Februari 2016, Serikali ilizindua Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi (Land Tenure Support Programme) ambayo imeanza kutekelezwa kwa majaribio katika Wilaya za Ulanga, Kilombero na Malinyi mkoani Morogoro. Programu hiyo imelenga kuongeza kasi ya kupima ardhi na kutoa hakimiliki za kimila ambazo zinaweza kutumika kama dhamana kwa wakulima na wafugaji kupata mikopo; kupunguza au kuondoa migogoro ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi; na kuhifadhi kumbukumbu za ardhi kwa matumizi sahihi ya rasilimali hiyo. Programu hiyo itatekelezwa kwa muda wa miaka mitatu kwa gharama Dola za Marekani Milioni 15.2. Baada ya majaribio hayo, na mafanikio kuonekana katika wilaya hizo, Programu itatekelezwa katika wilaya zote nchini. Ninawaagiza viongozi wa Mkoa wa Morogoro na wilaya zinazohusika, kusimamia kwa karibu utekelezaji wa Programu hiyo kwani matokeo yake ni ya muhimu sana kwenye mustakabali wa upimaji na matumizi endelevu ya ardhi yetu.

57. Mheshimiwa Spika, mwaka 2015, Serikali iliwaomba Waheshimiwa Wabunge kuainisha na kuwasilisha Serikalini migogoro ya ardhi iliyopo kwenye majimbo yao. Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge walioitikia wito huo. Mchango wao katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016, umewezesha jumla ya migogoro 1,130 ya ardhi kupokelewa Serikalini kutoka katika Halmashauri zote nchini. Uchambuzi wa migogoro hiyo unaendelea ambapo taarifa za awali zinaonesha kwamba migogoro mingi iliyopo ni kati ya wakulima na wafugaji, uvamizi wa mashamba na viwanja, migogoro kati ya Mamlaka za Hifadhi za Taifa na wananchi na kati ya wawekezaji na wananchi.

58. Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, tayari Serikali imechukua hatua kali dhidi ya maafisa ardhi waliokiuka sheria na taratibu za usimamizi wa ardhi nchini. Hii ni pamoja na kuwasimamisha kazi ili kupisha uchunguzi. Kwa mfano, hatua kali zimechukuliwa katika Halmashauri za Majiji ya Mwanza na Arusha, Manispaa za Bukoba na Kahama na kutengua madaraka kwa afisa ardhi mteule wa Manispaa ya Temeke. Ninaendelea kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kushirikiana na Halmashauri zao hususan Maafisa Ardhi na kutumia Dawati Maalum la Kuratibu Migogoro ya Ardhi lililoanzishwa katika kila Halmashauri nchini ili kuendelea kubaini migogoro iliyopo na kuitafutia ufumbuzi.

59. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Serikali itaifanyia mapitio Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 ili kuweka vipengele muhimu vya kudhibiti migogoro baina ya watumiaji wa ardhi na kuunda na kuzipa nguvu zaidi Ofisi za Ardhi za Kanda zitakazosaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa kupima na kupanga matumizi ya ardhi na kutoa hati karibu zaidi na wananchi. Aidha, Serikali itapitia upya Sheria ya Ardhi Namba 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999 ili kuzifanyia marekebisho muhimu kuendana na wakati.

Barabara

60. Mheshimiwa Spika, miundombinu imara ni msingi muhimu wa maendeleo ya sekta nyingine zote, ikiwemo Sekta ya Viwanda na Biashara. Katika miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia uwekezaji mkubwa katika ujenzi wa barabara nchini. Mathalan katika mwaka 2015/2016, Serikali ililenga kujenga kilometa 523 za barabara kuu kwa kiwango cha lami. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016, jumla ya kilometa 414.3 za barabara zilikuwa zimekamilishwa kwa kiwango cha lami, sawa na asilimia 79 ya lengo lililowekwa. Aidha, jumla ya kilometa 82.4 za barabara kuu zilikarabatiwa kwa kiwango cha lami, ikiwa ni sawa na asilimia 73 ya lengo la kilometa 113. Kwa upande wa barabara za mikoa, jumla ya kilometa 52.19 zilijengwa kwa kiwango cha lami, sawa na asilimia 68 ya lengo la kilometa 77 na jumla ya kilometa 676 za barabara za mikoa zilifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe, sawa na asilimia 54 ya lengo la kilometa 1,252. Ujenzi wa madaraja makubwa 11 uliendelea ambapo Daraja la Kigamboni limekamilika na kufunguliwa rasmi.

Reli

61. Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu na Huduma za Reli ya Kati, lengo likiwa ni kuboresha reli iliyopo kwa kutandika reli mpya na nzito zaidi; kuimarisha matuta, mifereji na tabaka la kokoto. Aidha, tunaendelea na utekelezaji wa makubaliano baina ya Serikali yetu na Serikali za Rwanda na Burundi kuhusu ujenzi wa reli ya Dar es Salaam – Isaka – Keza - Kigali (Km. 1,464); na Keza – Musongati (Km. 197) kwa kiwango cha *Standard Gauge*. Mkakati wa ndani ni pamoja na kujenga reli ya *Standard Gauge* kuanzia Dar es Salaam hadi Kigoma na matawi yake mawili ya Kaliua-Mpanda-Karema na Tabora-Isaka-Mwanza. Lakini pia mradi wa pili ni wa reli ya Kusini ya kutoka Mtwara-Songea-Mbambabay na bado tuna kazi ya kuimarisha reli ya Kaskazini inayoanzia Pugu-Tanga-Moshi-Arusha.

Bandari

62. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Serikali imeanza kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha ufanisi wa bandari zetu kwa kuanzia na Bandari ya Dar es Salaam ambayo ni lango kuu la biashara katika Afrika Mashariki na Kati na kufuatiwa na Bandari za Mtwara na Tanga. Tumeanza kwa kuondoa watumishi wote wasio waaminifu ambao wanachangia kupoteza mapato ya Serikali yanayohitajika sana katika kutoa huduma muhimu kwa wananchi wetu. Vilevile, tumefanya kazi kubwa ya kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato kwa kuhakikisha kwamba malipo yote yanafanyika benki na kuoanisha mifumo ya Mamlaka ya Bandari Tanzania na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Niwahakikishie wananchi na wafanyabiashara kuwa Serikali itaendelea kuboresha huduma katika bandari zetu na hususan Bandari ya Dar es Salaam kwa kupunguza idadi ya siku za kutoa mizigo bandarini ili tufikie siku mbili au chini ya siku hizo. Aidha, tutaziondoa kero zote zilizoainishwa na Mawakala wa Forodha nilipokutana nao tarehe 21 Machi, 2016 Jijini Dar es Salaam. Vilevile, Serikali itaziba mianya yote ya upotevu wa mapato bandarini na wale wote watakaobainika kushiriki kwenye wizi wa aina yoyote wataondolewa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mawasiliano

63. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kukamilisha mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano nchini ikiwemo ujenzi wa Kituo Mahiri cha Kutunzia Kumbukumbu katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano vijijini ambapo hadi sasa tumefanikisha ujenzi wa kilometa 18,000 kati ya kilometa 20,000 za miundombinu ya mkongo katika wilaya zote nchini. Kazi nyingine zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano katika vijiji 4,000 visivyokuwa na mawasiliano, kuunganisha Ofisi zote za Wakuu wa Wilaya, Hospitali za Wilaya, Mahakama, Vituo vya Polisi vya Wilaya, Ofisi za Posta na kuziwesha shule 431 kupata huduma ya intaneti bila malipo.

Nishati

(a)Umeme

64. Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika, unaokidhi mahitaji na wenye gharama nafuu ili kusukuma mapinduzi ya viwanda kwa kasi zaidi. Ili kutekeleza azma hiyo, katika mwaka 2015/2016, Serikali imeongeza uwezo wa mitambo ya kufua umeme kutoka Megawati (MW) 1,226.24 mwaka 2015 hadi kufikia MW

1,516.24 mwezi Januari 2016, sawa na ongezeko la Asilimia 24. Ongezeko hilo limetokana na uamuzi sahihi wa Serikali wa kutekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa Bomba la Gesi pamoja na mradi wa kufua umeme wa Kinyerezi-I wenye uwezo wa kuzalisha MW 150. Mradi huo baadaye utapanuliwa na kuweza kufikia MW 335 ifikapo mwaka 2017/2018. Sambamba na hatua hiyo, tarehe 16 Machi 2016, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa kituo kingine cha Kinyerezi-II cha kufua umeme kutokana na gesi asilia ambao utakapokamilika utazalisha MW 240. Lengo la Serikali katika kipindi cha miaka mitano ijayo ni kuongeza uwezo wa uzalishaji umeme hadi kufikia MW 4,915 na hivyo, kuwezesha asilimia 60 ya watanzania kupata umeme wa uhakika ifikapo mwaka 2020 na kutekeleza ipasavyo azma ya kuongeza uwekezaji mkubwa kwenye viwanda.

65. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2015/2016, Wakala wa Nishati Vijijini (REA) umeendelea kusambaza na kuunganisha umeme kwa wananchi waishio vijijini. Katika kipindi hicho, idadi ya wananchi waliopata umeme kupitia mradi wa REA Awamu ya Pili ni 71,724 katika vijiji 1,669. Aidha, hadi mwezi Januari, 2016 Serikali imekamilisha ujenzi wa kilometa 12,193 za njia za msongo wa kati na kilometa 1,830 za msongo mdogo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Usambazaji wa Umeme Vijijini. Vilevile, umeme umefikishwa kwenye Makao Makuu ya Wilaya mpya 12 za Buhigwe, Busega, Chemba, Itilima, Kakonko, Kalambo, Kyerwa, Mkalama, Mlele, Nyasa, Nanyumbu na Uvinza. Utekelezaji wa miradi hiyo umeongeza kiwango cha wananchi wanaopata huduma ya umeme kufikia asilimia 40.

66. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Serikali itaendelea kutekeleza Mradi wa Kinyerezi-II pamoja na kuimarisha na kujenga njia za usafirishaji umeme katika Gridi ya Taifa za Msongo mkubwa wa kiloVolts 400 kutoka Iringa kupitia Dodoma na Singida hadi Shinyanga na kutoka Dar-es-Salaam kupitia Chalinze na Tanga hadi Arusha pamoja na mradi wa kiloVolts 220 kutoka Makambako hadi Songea. Aidha, Serikali itakamilisha Awamu ya Pili ya mradi wa usambazaji umeme vijijini na kuanza utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya miradi ya REA.

(b) Gesi Asilia na Mafuta

67. Mheshimiwa Spika, baada ya ugunduzi mkubwa wa Gesi Asilia nchini, mikakati ya Serikali inayoendelea ni kubuni miradi mbalimbali hasa ile itakayoendeshwa na wafanyabiashara wazawa ili rasilimali hiyo iweze kuwanufaisha Watanzania na kuwawezesha kumiliki uchumi wa Taifa lao. Serikali imetenga eneo la ardhi huko Likongo Mkoani Lindi kwa ajili ya kujenga

miundombinu ya kuchakata Gesi Asilia ikiwa ni sehemu ya kutekeleza azma hiyo ya kuwawezesha wazawa. Serikali itaanza utekelezaji wa mradi huo katika mwaka 2016/2017.

68. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba Nchi inakuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta kwa ushindani na gharama nafuu, Serikali imeanzisha Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja yaani *Petroleum Bulk Procurement Agency*, ulioanza kazi rasmi mwezi Januari, 2016. Utaratibu huo utaiwezesha Serikali kusimamia vizuri udhibiti wa uagizaji wa mafuta nchini na kuwawezesha Wananchi kuwa na uhakika wa kupata mafuta bora yenye viwango vinavyokubalika kimataifa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo na kijamii.

HUDUMA ZA JAMII

Elimu

69. Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa elimu kama nyenzo imara ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii, Serikali ya Awamu ya Tano imeanza kuchukua hatua madhubuti za kuboresha na kuimarisha elimu ya awali, msingi, sekondari, ufundi na elimu ya juu. Hatua zinazochukuliwa zinalenga kuhakikisha kwamba elimu ya Tanzania ni ya viwango vya ubora wa hali ya juu ili kuwawezesha vijana wetu kukabiliana na changamoto za maisha kwa kujari wenyewe na kumudu ushindani katika soko la ajira la ndani, kikanda na kimataifa. Aidha, hatua hizo zitatuwezesha kuwa na rasilimali watu yenye weledi wa kutosha kujenga uchumi wa viwanda nchini. Moja ya hatua kubwa iliyochukuliwa na Serikali ni utekelezaji wa ahadi ya utoaji wa elimu bila malipo kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha nne kwa shule za umma kuanzia mwezi Januari 2016. Ahadi hiyo ilitolewa na mgombea Urais kupitia CCM wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba, 2015 ambaye kwa sasa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, ni matakwa ya Kifungu cha 52(a) cha Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2015 ambacho kinasisitiza kwamba Serikali itaandaa mfumo, muundo na taratibu nyumbufu za kutoa elimu ya awali na elimumsingi bila malipo ili kila Mtanzania apate fursa sawa ya kupata elimu.

70. Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kuwa hatua hiyo nzuri iliyochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano, itawapunguzia wazazi na walezi hasa wananchi maskini mzigo wa kugharamia elimu ya vijana wao. Kupitia Waraka wa Elimu Na. 5 wa mwaka 2015, Serikali imefuta michango ya maji, umeme, ulinzi, mitihani na ada iliyokuwa inachangishwa shuleni kwa idhini ya Kamati na Bodi za Shule. Hata hivyo, yapo majukumu yanayohusu mahitaji ya

msingi ya mtoto ambayo yataendelea kutekelezwa na wazazi na walezi kama ilivyokuwa inafanyika awali. Majukumu hayo ni pamoja na kumnunulia mtoto sare za shule na michezo, madaftari, kalamu na chakula kwa wanafunzi wa shule za kutwa kwa utaratibu utakaowekwa na wazazi na walezi wenyewe. Maeneo mengine ni kulipia nauli ya kwenda na kurudi shule mwanafunzi na mahitaji mengine kama vile kununua godoro, shuka na vifaa vya usafi binafsi. Vilevile, mzazi au mlezi ana wajibu wa kugharamia matibabu ya mtoto wake.

71. Mheshimiwa Spika, baada ya kuanza utekelezaji wa mpango wa elimu bila malipo, kumejitokeza changamoto kadhaa. Baadhi ya changamoto hizo ni uelewa wa jamii juu ya umuhimu wa kuweka utaratibu muafaka wa kutoa chakula cha mchana kwa wanafunzi wa kutwa na uendeshaji wa mabweni ambayo wazazi na walezi au jamii walikuwa wanachangia fedha za chakula. Changamoto nyingine ni pamoja na upungufu wa miundombinu kama madarasa, mabweni, maabara, nyumba za walimu na vyoo. Napenda kuwahakikishia wananchi kwamba Serikali inaendelea kuzifanyia kazi changamoto hizo na jitihada kubwa zimewekwa katika kuielimisha jamii na wadau mbalimbali kuhusu mpango mzima wa utoaji elimu bila malipo.

72. Mheshimiwa Spika, tunayo changamoto ya upungufu mkubwa wa madawati baada ya kuanza kuandikisha watoto shule bila malipo. Hili ni jambo kubwa na tulishatoa agizo kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi kuhakikisha kuwa kila Halmashauri inatumia rasilimali zake kutengeneza madawati kwa kila shule. Nitumie nafasi hii kuwashukuru wadau walioanza kuchangia madawati katika maeneo mbalimbali na ninawasihi wengine waendeleo kuunga mkono jitihada hizi za Serikali. Kuanzia leo hii, nawaagiza Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi waliokamata mbao ndani ya Halmashauri zao kuzitumia kutengenezea madawati na siyo kuzipiga mnada. Natumia nafasi hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Watendaji wa Bunge kwa Mkakati wa kubana matumizi uliowezesha kupata Shilingi Bilioni sita zitakazotumika kutengeneza madawati. SUMA JKT na Magereza wameanza kazi ya kutengeneza madawati hayo. Tunatarajia kupata madawati 80,000 ambayo tutawagawia Wabunge wa Majimbo yote na kwa wastani kila Jimbo litaweza kupata madawati 300.

73. Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote tushirikiane katika juhudi za kuunga mkono uamuzi wa Serikali kuhusu elimu bila malipo. Aidha, nawaomba wote kwa ujumla wetu kushirikiana katika kuwaelimisha wananchi kuhusu mpango huu na wajibu wa kila mmoja wetu katika kuhakikisha kwamba watoto wetu wanapata fursa za kupata elimu bora. Tukifanya hivyo, tutaweza kufikia lengo letu la kuwa Nchi yenye uchumi wa kipato cha kati kwa haraka zaidi.

74. Mheshimiwa Spika, elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ni nguzo muhimu ya kuwapatia ujuzi na kuwajengea uwezo na uzoefu wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi na sekondari. Uzoefu wa Nchi za Asia zilizowekeza katika elimu ya ufundi na ufundi stadi unaonesha kwamba maendeleo ya haraka waliyoyapata na hususan kufikia uchumi wa kati na wa viwanda umechangiwa sana na elimu ya ufundi. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali itaelekeza nguvu zake katika kujenga na kuimarisha miundombinu ya elimu ya ufundi na kuboresha mitaala ili iendane na mahitaji ya sasa ya uchumi wa viwanda. Kwa kuanzia, Serikali imeridhia vyuo vya maendeleo ya wananchi kuhamishiwa Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi na kufanyiwa ukarabati kwa ushirikiano na Sekta Binafsi ili viweze kutoa mafunzo ya ufundi. Hatua hiyo itaharakisha kufikiwa kwa lengo la Serikali la kuwa na chuo cha ufundi kwa kila Wilaya.

75. Mheshimiwa Spika, udahili katika vyuo vya elimu ya juu umeongezeka kutoka wanafunzi 214,722 mwaka 2014 hadi kufikia wanafunzi 220,531 mwaka 2015. Aidha, hadi kufikia Februari 2016, idadi ya wanafunzi waliopewa mikopo ya elimu ya juu ilifikia 122,886. Kiasi cha fedha za mikopo kilichotolewa kwa wanafunzi hao ni Shilingi Bilioni 207. Hata hivyo, hali ya urejeshaji wa mikopo iliyotolewa hairidhishi. Hivyo, naiagiza Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kufuatilia urejeshaji wa mikopo hiyo ili fedha hizo zitumike kuwakopesha wanafunzi wengine.

Afya

76. Mheshimiwa Spika, uimarishaji wa huduma za afya nchini, kwa maana ya kinga na tiba ni muhimu sana. Nguvukazi yenye afya njema hutoa mchango mkubwa kwenye uchumi ikilinganishwa na nguvukazi dhaifu kiafya. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma za kinga, uchunguzi na upatikanaji wa dawa na vifaa-tiba katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali Maalum, Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati. Aidha, Serikali imetoa maelekezo kwa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kufungua na kuendesha maduka ya dawa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali za Rufaa za Mikoa na Hospitali za Wilaya ili kuhakikisha kwamba dawa za kutosha zinapatikana wakati wote na kwa bei nafuu.

77. Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Bohari Kuu ya Dawa imefungua na inaendesha maduka ya dawa yanayouza bidhaa zake kwa bei nafuu ndani ya maeneo ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Sekou Toure (Mwanza), Mawenzi (Kilimanjaro) na Mount Meru (Arusha). Pamoja

na juhudi hizo za Serikali za kuimarisha huduma za afya nchini, milango ipo wazi kwa sekta binafsi ya ndani na nje ya nchi kuwekeza katika sekta ya afya.

78. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha wananchi kujiunga na huduma za Bima ya Afya ili kuongeza na kuimarisha upatikanaji wa huduma ya afya kwa watu wote. Idadi ya wanufaika wa Bima ya Afya tangu kuanzishwa kwake ni 11,729,281, sawa na asilimia 27 ya wataanzania wote kulingana na Sensa ya mwaka 2012. Kati ya hao, wanufaika 8,390,550 wako katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na 3,338,755 ni wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF). Hata hivyo, idadi ya wanufaika wa Bima bado ni ndogo, hivyo naagiza viongozi wa Mifuko hiyo kushirikiana pamoja kutoa elimu na kuhamasisha wananchi wengi zaidi kujiunga na Mifuko hiyo. Serikali inaendelea kuangalia uwezekano wa Hospitali za Rufaa za Mikoa kuwa chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili Katibu Tawala wa Mkoa aratibu maendeleo ya Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati.

Maji

79. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa lengo la kuwapatia wananchi huduma ya maji safi, salama na ya kutosha. Hadi kufikia Desemba 2015, Serikali imefikisha huduma ya maji safi na salama kwa asilimia 72 katika maeneo ya vijijini, asilimia 86 miji mikuu ya mikoa na asilimia 60 katika miji mikuu ya wilaya na miji midogo. Mafanikio hayo yametokana na utekelezaji wa miradi ya maji 1,143 kati ya miradi 1,855 ya maji mijini na vijijini ambayo imetekelezwa chini ya Awamu ya Kwanza ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Aidha, huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam na miji ya Bagamoyo na Kibaha imeongezeka na kufikia asilimia 68, lengo likiwa kufikia asilimia 95 ifikapo mwaka 2025. Katika mwaka 2016/2017, Serikali itatekeleza Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji pamoja na kukamilisha miradi 712 ambayo haikutekelezwa katika Awamu ya Kwanza. Natoa wito kwa wananchi wote kutunza vyanzo vya maji pamoja na miundombinu yake ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji vijijini na mijini.

80. Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kwamba maji ni moja ya vigezo muhimu katika kuanzisha na kuendeleza viwanda. Hivyo hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji nchini, pamoja na kuongeza huduma ya maji safi na taka, ina lengo la kuongeza mchango wa Sekta ya Maji katika Sekta ya Viwanda. Mathalan, ongezeko la maji kutokana na utekelezaji wa miradi ya kuboresha miundombinu ya maji ya Ruvu Juu na Ruvu Chini umesaidia kupunguza tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam.

Serikali itahakikisha kuwa maeneo yenye viwanda na yanayotegemewa kuwa na viwanda yanaunganishwa na miradi mikubwa ya maji ili kuongeza kasi ya uzalishaji.

SHERIA, ULINZI NA USALAMA

Sheria

81. Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuona kwamba kero ya mlundikano wa mashauri Mahakamani inakuwa historia na kwamba wananchi wanapata haki kwa wakati. Katika kufanikisha dhamira hiyo, Serikali imeimarisha utendaji wa Mhimili wa Mahakama kwa kuongeza rasilimali watu na fedha. Aidha, Serikali imeboresha na kuongeza ufanisi katika upelelezi na uendeshaji wa mashauri kwa kutenganisha jukumu la upelelezi na uendeshaji wa mashauri. Vilevile, uongozi wa Mahakama umejiwekea utaratibu wa Majaji na Mahakimu kuwa na malengo ya idadi ya mashauri ambayo wanapaswa kuyasikiliza kila mwaka.

82. Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kukabiliana na changamoto ya uhaba wa majengo ya Mahakama na vitendea kazi katika ngazi zote, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ametekeleza ahadi yake aliyoitoa tarehe 4 Februari 2016 ya kutoa fedha zote za maendeleo za Mahakama kiasi cha Shilingi Bilioni 12.3 kwa mwaka 2015/2016. Hatua hiyo imeiwezesha Mahakama kuendelea na ukarabati na ujenzi wa Mahakama katika ngazi mbalimbali na pia ununuzi wa vitendea kazi. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi huo.

83. Mheshimiwa Spika, wakati akihutubia Bunge lako Tukufu mwezi Novemba, 2015 Mheshimiwa Rais aliahidi kuwa katika mwaka 2016/2017, Serikali itaanzisha Mahakama Maalum ya Ufisadi. Napenda kuliarifu Bunge lako kwamba, Serikali imeanzisha Divisheni ya Mahakama ya Rushwa na Ufisadi katika Mahakama Kuu itakayoanza kufanya kazi mwezi Julai 2016. Aidha, Serikali itaimarisha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kwa pamoja ziweze kuharakisha utoaji wa haki.

Ulinzi na Usalama

84. Mheshimiwa Spika, vyombo vya ulinzi na usalama vimeendelea na jukumu la kulinda mipaka, raia na mali zao. Kwa jumla, hali ya ulinzi na usalama wa Nchi yetu ipo shwari. Napenda kutumia fursa hii kuvipongeza vyombo vyote vya ulinzi na usalama kwa kazi yao nzuri, weledi na uzalendo wa hali ya juu katika kuhakikisha Taifa letu lina usalama wa kutosha pia kuchangia usalama

wa mataifa mengine duniani yenye migogoro ya kisiasa. Mambo yote haya yanatokana na ukweli kwamba Serikali imekuwa ikiviwezesha vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kuwa na uwezo wa kulinda mipaka ya Nchi, raia na mali zao. Katika kujenga utayari wa Majeshi wakati wote, askari wetu wameshiriki kwa ufanisi katika majukumu ya kimataifa ya kulinda amani katika nchi zenye migogoro duniani, hususan Darfur, Sudan, Lebanon na Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

85. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, jumla ya vijana 27,463 walipatiwa mafunzo ya kujenga uzalendo, ukakamavu, maadili mema, utaifa pamoja na stadi za kazi na za kimaisha. Kati yao, vijana 7,517 ni wa kujitolea na 19,946 ni wa mujibu wa sheria. Ni jambo la kutia moyo kwamba vijana 5,453 waliopitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa wamenufaika na utaratibu wa kuajiriwa na vyombo vya ulinzi na usalama. Kati ya hao, vijana 3,521 wameajiriwa na JWTZ; Polisi 1,185; Usalama wa Taifa 106, Takukuru vijana 24 na Jeshi la Zimamoto vijana 617.

Aidha, Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kuishi kwa watumishi wa vyombo vya ulinzi na usalama ambapo ujenzi wa nyumba 4,744 za makazi zimekamilishwa kati ya nyumba 6,064 za awamu ya kwanza kwenye mradi wa nyumba 10,000 zinazotarajiwa kujengwa Nchi nzima.

86. Mheshimiwa Spika, Serikali italiimarisha Jeshi letu kwa kulipatia mafunzo, zana bora na za kisasa zaidi; kuboresha mazingira ya kufanyia kazi; na maslahi. Aidha, itaimarisha uwezo wa Jeshi katika utafiti na kuendeleza teknolojia kwa madhumuni ya kuongeza ubunifu katika kuzalisha bidhaa bora zaidi na huduma kwa ajili ya matumizi ya jeshi na raia nchini na nje ya nchi.

Udhibiti wa Uhalifu Nchini

87. Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limeendelea kulinda usalama wa raia na mali zao na kudumisha amani na utulivu nchini. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2015, jumla ya makosa makubwa ya jinai 68,814 yaliripotiwa katika Vituo vya Polisi kote nchini ikilinganishwa na makosa 70,153 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2014, sawa na upungufu wa asilimia 1.9. Upungufu huo wa makosa umetokana na kuongezeka kwa ushirikishwaji wa wananchi katika vita dhidi ya uhalifu na kuongezeka kwa taarifa za kiintelijensia. Aidha, Jeshi limeimarisha doria za Nchi kavu na majini pamoja na kufanya misako na operesheni maalum kwa ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya, Tarafa, Kata na Shehia. Katika mwaka 2016/2017, Jeshi la Polisi litaendelea kutoa elimu ya Ulinzi Shirikishi kwa wananchi ili waweze kuongeza ushirikiano na Jeshi la Polisi katika utekelezaji wa jukumu la kupambana na uhalifu.

MICHEZO

88. Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa michezo katika kuimarisha afya, kuongeza ajira, kujenga udugu na mshikamano miongoni mwa jamii na mataifa mbalimbali duniani, Serikali itaendelea kuimarisha michezo nchini ili wanamichezo wetu waweze kufanya vizuri katika medani za michezo ndani na kimataifa. Katika kufikia azma hiyo, mwaka 2016/2017, Serikali itakamilisha mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995 na kuendelea kutoa mafunzo ya michezo kwa walimu wa shule za msingi na sekondari ili kuibua vipaji. Serikali pia itaendelea kusimamia maendeleo ya michezo katika shule, vyuo, taasisi na vilabu. Lengo ni kuhakikisha kuwa michezo inatoa fursa kwa vijana kupata ajira na kuendeleza vipaji vyao.

HABARI

89. Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba Sekta ya Habari ni nguzo muhimu katika kuelimisha, kuhabarisha na kuburudisha umma. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeendelea kusimamia Sekta ya Habari kikamilifu na kuhakikisha vyombo vya habari vinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Maadili na Weledi. Uhuru wa vyombo vya habari ni mkubwa na wigo wa ushiriki wa Sekta Binafsi umeongezeka sana. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016 Serikali ilikuwa imesajili Vituo vya Televisheni 26, Vituo vya Redio 126 na Magazeti 833. Muhimu hapa ni matumizi mazuri ya kalamu na kuweka uzalendo wa Nchi mbele.

90. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Serikali itawasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Huduma za Habari kwa lengo la kuweka mazingira wezeshi kwa vyombo vya Habari. Aidha, itaboresha Idara ya Habari-Maelezo ili itimize jukumu lake kama Msemaji Mkuu na Mratibu wa Mawasiliano Serikalini. Vilevile, itaendelea kufuatilia kwa karibu maudhui ya vituo vyote vya utangazaji kupitia mtambo maalum wa ufuatiliaji wa maudhui na kuhakikisha vituo vya utangazaji vinakuwa na wakalimani wa lugha ya alama. Napenda nitumie fursa hii kuvitaka vyombo ya habari nchini, kufanya kazi zake kwa weledi na kwa mujibu wa Sheria na Taratibu zilizopo, mambo ambayo ni muhimu sana katika tasnia ya habari kama wafanyavyo wenzao katika Nchi zote duniani yaani uzingatiaji wa maadili katika tasnia ya habari. Aidha, niwaombe wamiliki wa vyombo vya habari na wanahabari kutanguliza uzalendo wa Nchi yao mbele.

MASUALA MTAMBUKA

Lishe

91. Mheshimiwa Spika, lishe bora ni nguzo muhimu katika kujenga Taifa lenye rasilimali watu wenye afya bora na uwezo mkubwa wa kufikiri na kufanya kazi. Ukosefu wa lishe bora husababisha utapiamlo ambao una madhara makubwa kiuchumi na kijamii kwa kaya, jamii na Taifa kwa ujumla. Hali hiyo ikitokea ndani ya kipindi cha siku 1,000 kuanzia ujauzito hadi miaka miwili ya ukuaji wa mtoto husababisha udumavu ambao madhara yake hayawezi kurekebishwa katika maisha yake yote. Udumavu unaathiri mwili na akili ya mtoto na hivyo hawezi kujifunza vizuri darasani na pia hupunguza uwezo wake katika kuchangia maendeleo ya Taifa lake hapo baadaye.

92. Mheshimiwa Spika, athari nyingine za utapiamlo ni pamoja na watoto kuugua mara kwa mara, hali inayochangia ongezeko la gharama za matibabu kwa familia, jamii na Taifa; na wazazi kutumia muda mwingi kuuguza watoto badala ya kufanya shughuli za kukuza uchumi. Hali hiyo inatutaka sote tuwe mabalozi wa kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa lishe bora. Vilevile, ni muhimu kwa wajawazito kuhudhuria kliniki ili kuchunguzwa afya zao na pia kupata ushauri wa kitaalam utakaowawezesha kupata watoto wenye afya njema. Wakina mama waelimishwe kunyonyesha watoto wao kwa kipindi kisichopungua miezi sita mfululizo na kuwapatia vyakula vyenye viini lishe vya kutosha baada ya hapo. Masuala haya yanahitaji elimu zaidi kwa sababu vyakula hivyo vinapatikana kwenye jamii na kaya zetu na siyo ghali kuvipata.

Vita Dhidi ya Rushwa

93. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kupambana na rushwa kwa kuchunguza tuhuma za rushwa na kuwafikisha watuhumiwa mbele ya vyombo vya sheria. Katika mwaka 2015/2016, Serikali imeshughulikia tuhuma 3,911 ambapo uchunguzi wa tuhuma 324 ulikamilika. Kati ya tuhuma hizo, majalada 252 yaliombewa kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka ambapo majalada 156 yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa Mahakamani. Aidha, Majalada 329 yaliyotokana na taarifa ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yalichunguzwa. Majalada 19 yalikamilika na kuombewa kibali kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ambapo majalada 12 yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani. Vilevile, majalada nane yaliyohusu tuhuma za rushwa kubwa yalifikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka. Kati ya hayo, majalada mawili yamepata kibali na watuhumiwa wamefikishwa Mahakamani.

94. Mheshimiwa Spika, Miradi ya Maendeleo 284 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 41.63 ilikaguliwa kupitia ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo katika Serikali za Mitaa. Miradi 69 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 8.32 ilibainika kuwa na kasoro ambapo miradi 10 wahusika walishauriwa namna ya kurekebisha kasoro zilizojitokeza wakati miradi 59 uchunguzi wa kina umeanzishwa ili wahusika wachukuliwe hatua. Aidha, ufuatiliaji maalum wa miradi ya afya inayofadhiliwa na Benki ya Dunia unaendelea kufanyika ambapo hatua mbalimbali zimechukuliwa kwenye maeneo yaliyobainika kuwa na kasoro, ikiwemo kuanzisha uchunguzi wa awali ambapo majalada 85 yamefunguliwa.

95. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuchunguza tuhuma 3,444 zilizopo na mpya zitakazojitokeza na kukamilisha uchunguzi wa tuhuma 10 za rushwa kubwa. Aidha, itawajengea uelewa wa masuala ya rushwa makundi mbalimbali katika jamii na hususan Asasi za Kiraia, madhehebu ya dini na wanahabari ili washiriki kikamilifu kuwaelimisha wananchi kuhusu kudhibiti rushwa na kuendelea kufungua na kuimarisha klabu za wapinga rushwa katika shule za msingi, sekondari na vyo vya juu ili kuendelea kujenga jamii inayochukia rushwa.

Kudhibiti UKIMWI

96. Mheshimiwa Spika, maambukizo mapya ya Virusi vya UKIMWI yanaendelea kupungua kutoka asilimia 5.7 mwaka 2008 hadi 5.1 kwa takwimu za 2011/2012. Vifo vitokanavyo na UKIMWI navyo vimeendelea kupungua kutoka wastani wa vifo 79,338 mwaka 2012/2013 hadi vifo 50,219 mwaka 2014/2015. Maambukizi mapya ya UKIMWI nayo yamepungua kutoka wastani wa 78,843 mwaka 2012/2013 hadi 69,000 mwaka 2014/2015. Idadi ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI inakadiriwa kuwa milioni 1.4 kwa mwaka 2012/2013 na watu milioni 1.5 mwaka 2014/2015.

97. Mheshimiwa Spika, pamoja na kupungua kwa kasi ya maambukizi, UKIMWI bado ni tishio linaloathiri maendeleo na maisha ya wananchi. Hatuna budi kuendelea kuchukua hatua za dhati na madhubuti za kudhibiti maambukizi mapya, kutoa huduma za afya na matibabu kwa wale walioambukizwa na kuwahudumia wale wenye mahitaji kutokana na vifo vya wazazi hususan watoto yatima. Hatua hizo ni pamoja na kutekeleza Mkakati wa Tatu wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI wa mwaka 2013/2014 hadi 2017/2018 unaolenga kupunguza maambukizi mapya kwa asilimia 50, kupunguza vifo vitokanavyo na UKIMWI na kuondoa unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI ifikapo 2018.

98. Mheshimiwa Spika, huduma za upimaji wa virusi vya UKIMWI na uingizwaji kwenye mpango wa matunzo na matibabu kwa wale wanaogundulika na maambukizi ya VVU zinaendelea kutolewa. Jumla ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI wanaopata dawa za ARV ni 640,084, sawa na asilimia 43 ya watu wote wenye maambukizi. Kati yao, asilimia 69 ni wanawake na watoto. Serikali imeanza utaratibu mpya wa kutoa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI kwa yeyote atakayepimwa na kukutwa na maambukizi ya virusi vya UKIMWI tofauti na utaratibu wa awali ambao mwathirika alianzishiwa dawa kutegemea idadi ya CD4. Utaratibu huo umeanza katika Halmashauri 48 zenye kiwango kikubwa cha maambukizi na hatimaye kueneza huduma hii Nchi nzima. Katika juhudi za kupunguza maambukizi ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, Serikali imeendelea kutoa huduma katika vituo 5,361 kati ya 5,863 vinavyotoa huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto nchini. Vilevile, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa umma katika masuala ya VVU, UKIMWI, Afya ya Uzazi na Ujinsia. Kuanzia mwezi Julai 2016, Serikali itaanza zoezi la kupima kiwango cha maambukizi kwa Nchi nzima, kila Mkoa, ikiwa ni mara ya nne zoezi hili kufanyika nchini.

Hifadhi ya Mazingira

99. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuweka na kutekeleza mipango na mikakati thabiti ya kutunza mazingira kwa lengo la kutunza vyanzo vya maji, Bioanuai, kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa na uharibifu wa misitu. Aidha, Serikali imeandaa Kanuni mpya ya Mifuko ya Plastiki ya mwaka 2015 inayokataza kuzalishwa na kuingizwa nchini matumizi ya mifuko ya plastiki yenye unene chini ya mikroni 50. Vilevile, Serikali imeendelea kufanya kaguzi katika maeneo mbalimbali ili kubaini iwapo sheria za mazingira zinazingatiwa na kuchukua hatua za kuvifungia viwanda tisa na kutoa onyo kwa viwanda 63. Taasisi zinazohusika na usimamizi wa Sheria ya Mazingira hazina budi kuvisaidia kiufundi viwanda husika ili visifungwe kwa muda mrefu kwani ni hasara kwa Taifa.

100. Mheshimiwa Spika, wakati wa maadhimisho ya 54 ya Uhuru, tarehe 9 Desemba, 2015 Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alifanya uamuzi wa busara wa kuwataka wananchi wote kuyatumia maadhimisho hayo kwa kufanya usafi wa mazingira katika maeneo yao yanayowazunguka na maeneo ya Taasisi za Umma. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza kwa dhati wananchi wote, Taasisi za Umma na Sekta Binafsi na Asasi za kiraia kwa mwitikio mkubwa waliouonesha katika kushiriki na kufanikisha zoezi hilo la usafi.

101. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa usafi wa mazingira, Serikali imeamua kwamba zoezi la usafi wa mazingira litakuwa endelevu. Hivyo, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, tayari zimetoa Waraka maalum wa kuifanya kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi kuwa siku maalum ya wananchi wote kufanya usafi wa mazingira nchini kote. Napenda kuwahimiza Viongozi na Watendaji wote wa Wizara, Mashirika na Taasisi za Umma na Sekta Binafsi, Mikoa, Wilaya na Halmashauri zote nchini pamoja na Watendaji wa Mitaa, Kata na Vijiji na Vitongoji na Wakuu wa Kaya kusimamia usafi wa mazingira katika maeneo yao. Aidha, nawasihi Wananchi wote kudumisha utamaduni na tabia nzuri ya kuhakikisha kuwa maeneo yao yanakuwa safi wakati wote ili kuboresha afya zao na kuleta maendeleo endelevu nchini.

Menejimenti ya Maafa

102. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza jukumu la kuwalinda na kuwasaidia wananchi dhidi ya maafa yaletwayo na matukio mbalimbali ya kiasili. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na Serikali kutoa Tani 31,184 za chakula kwa halmashuri 69 zilizokumbwa na tatizo la upungufu wa chakula katika mwaka 2015/2016. Kati ya hizo, Tani 7,727 zilitolewa bure kwa kaya zisizo na uwezo na Tani 23,457 zilitolewa kwa bei nafuu ya Shilingi 50 kwa Kilo.

103. Mheshimiwa Spika, Serikali pia imetoa misaada mbalimbali ya kibinadamu yenye thamani ya Shilingi Milioni 42.5 na kiasi cha Shilingi Milioni 143.5 kwa ajili ya ununuzi wa mbegu za mihogo na mtama kwa waathirika wa maafa ya mafuriko, mvua ya mawe na upepo mkali. Mikoa iliyopata misaada hiyo ni Mtwara, Mara, Dodoma, Shinyanga, Iringa, Tanga, Pwani, Lindi na Tabora. Pia Shilingi Milioni 516 zilitolewa kama fidia kwa watu waliotakiwa kupisha ujenzi wa upanuzi wa mtaro katika eneo la Buguruni - Mnyamani. Serikali imeimarisha Mfumo wa Upatikanaji wa Taarifa za Tahadhari za majanga kwa haraka kwa kujenga vituo 16 vya upimaji wa hali ya hewa na kuweka vifaa vya kupima wingi na kasi ya maji katika vituo 10 vilivyopo katika mabonde ya mto Pangani na mto Ruvuma.

Aidha, Serikali imetoa mafunzo kwa Kamati za Maafa katika wilaya 14 za mikoa mitano nchini. Katika mwaka 2016/2017, Serikali itaendelea kuimarisha uratibu na menejimenti ya maafa nchini kwa kuanzisha Wakala wa Usimamizi wa Maafa, kujijengea uwezo Kamati za Maafa za Mikoa na Wilaya na kuendelea kuimarisha Mfumo wa Taarifa za Tahadhari ya Awali.

Kudhibiti Dawa za Kulevya

104. Mheshimiwa Spika, dawa za kulevya ni changamoto kubwa kwani huwaathiri watu wengi hasa vijana ambao ni nguvu kazi ya Taifa. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali kupitia Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawa za Kulevya ilifanya marekebisho ya Sera ya Kupambana na Dawa za Kulevya na kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria Mpya ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na kupitishwa na Bunge lako Tukufu na kuanza kutumika tarehe 15 Septemba 2015. Sheria hiyo inaipa Tume nguvu zaidi ya kudhibiti na kupambana na tatizo hilo.

105. Mheshimiwa Spika, Tume imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu athari za biashara na matumizi ya dawa za kulevya na kutoa huduma za matibabu kwa waathirika. Hadi kufika mwezi Februari 2016, zaidi ya watumiaji 2,223 wamepata huduma katika Hospitali za Muhimbili, Temeke na Mwananyamala. Tume kwa kushirikia na Jeshi la Polisi wameendesha misako, doria na operesheni nchini kwa lengo la kudhibiti uuzaji, utumiaji na usafirishaji wa dawa za kulevya, ambapo wamefanikiwa kuteketeza mashamba ya bangi na mirungi katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Mara. Katika mwaka 2015/2016, jumla ya watuhumiwa 43 walikamatwa na kiasi cha kilo 37.2 na kete 156 za dawa aina ya heroin na bangi. Pamoja na ukamataji huo, Mahakama Kuu ya Tanzania imetoa hukumu kwa kesi kubwa nne za dawa za kulevya. Katika mwaka 2016/2017, Serikali itakamilisha utaratibu wa kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ili kuongeza ufanisi. Mamlaka itashirikiana na Jeshi la Polisi kubaini mtandao wa wahalifu wa ndani na nje ya nchi unaojihusisha na uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini na kuwafikisha wahusika Mahakamani.

USTAWISHAJI MAKAO MAKUU DODOMA

106. Mheshimiwa Spika, mwaka 2015/2016, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu imepima viwanja 957 katika maeneo ya Mkalama, Nkuhungu Kusini na Mahungu. Vilevile, jumla ya viwanja 6,599 vilisanifiwa katika eneo la ukubwa wa Hekta 493 na kutoa vibali 275 vya ujenzi. Katika mwaka 2016/2017, Mamlaka inatarajia kuandaa ramani za jumla na ramani za kina katika maeneo ya lhumwa na Hombolo pamoja na kupima viwanja vipya 4,000 katika maeneo mbalimbali ya Mji wa Dodoma na kujenga kwa kiwango cha lami barabara zenye urefu wa kilometa 23.

USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

107. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kushiriki kwenye utengamano wa kikanda na kimataifa na kuendeleza Diplomasiya ya Uchumi na Siasa kwa kuzingatia maslahi muhimu ya Nchi yetu. Mathalani, Serikali imeandaa Mpango Kazi wa Miaka Mitatu (2016-2018) wa Ushirikiano kati ya Tanzania na China. Mpango huo umeainisha miradi ya kipaumbele ya uwekezaji wa viwanda mbalimbali nchini. Ushirikiano huo umelenga kutumia fursa ya Dola za Marekani Bilioni 10 zitakazotolewa na Serikali ya China chini ya Mpango wa kuzisaidia Nchi nne za Afrika, ikiwemo Tanzania. Makubaliano hayo yalifikiwa katika Mkutano wa Sita wa Wakuu wa Nchi wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika uliofanyika Jijini Johannesburg, Afrika Kusini tarehe 5 Desemba 2015. Nchi nyingine zitakazofaidika na Mpango huo ni Afrika Kusini, Ethiopia na Kenya.

Serikali pia imesaini Mkataba wa ushirikiano na Serikali ya Japan kwa ajili ya ujenzi wa Gridi ya umeme na Serikali ya Ufaransa kwa ajili ya kusaidia mpango wa maboresho ya *Terminal Two* ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere.

108. Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha Nchi kufikia uchumi wa kati ifikapo 2025, Serikali itaendelea kusimamia na kutekeleza diplomasiya thabiti ambayo itachangia katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo endelevu ya Tanzania. Aidha, itakuza ubia wa kimataifa na kuimarisha ushirikiano wa kikanda, Barani Afrika na wadau wengine wa maendeleo ili kuhakikisha kuwa Tanzania inapata manufaa ya fursa za utandawazi.

URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI

109. Mheshimiwa Spika, ili kazi zote zilizopangwa kutekelezwa zifanyike kwa ufanisi, tunahitaji uratibu mzuri wa sekta zote ili kila mmoja atekeleze wajibu wake kikamilifu. Hivyo, kuanzia mwezi Julai, 2016 Serikali itaanza kutumia mfumo wa wazi wa kielektroniki wa kufuatilia uwajibikaji na utendaji kazi kwa mujibu wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Mfumo huo ni muhimu ili kuhakikisha kuwa utendaji kazi unaendana na kasi ya Serikali ya Awamu ya Tano katika kufikia malengo yaliyopangwa. Mfumo huo utarahisisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Serikali kulingana na Ilani ya Chama Mapinduzi ya mwaka 2015, Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa, Ahadi na Maagizo ya Viongozi Wakuu. Aidha, Mfumo huo utapunguza ucheleweshaji wa utekelezaji, mwingiliano wa majukumu na gharama zisizo za lazima katika utendaji kazi.

HITIMISHO

110. Mheshimiwa Spika, nimetumia muda mrefu kuelezea baadhi ya shughuli ambazo Serikali ya Awamu ya Tano itazipatia kipaumbele. Kabla ya kuhitimisha Hotuba yangu, napenda kuisitiza masuala machache yafuatayo:-

(i) Tunayo changamoto kubwa ya kutumia rasilimali fedha kidogo tuliyonayo kukidhi mahitaji makubwa ya kutoa huduma bora kwa wananchi. Mathalani, upo upotevu wa mapato kwa kushindwa kudhibiti na kusimamia mapato na matumizi ya fedha za umma. Serikali ya Awamu ya Tano itasimamia na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato na kuhakikisha kwamba fedha za umma zinatumika kulingana na sheria na kanuni za matumizi ya fedha za Serikali;

(ii) Tumedhamiria kufanya mapinduzi ya viwanda ili kujenga uchumi imara kwa faida ya wananchi. Hata hivyo, tunalo jukumu kwa kila mmoja wetu kuunga mkono dhamira ya kweli ya Serikali ili kufikia lengo hili. Tuungane na Mheshimiwa Rais kuondoa kasoro zilizopo kwa kupunguza urasimu katika kuwawezesha wawekezaji wa ndani na nje; kuimarisha huduma na miundombinu ya kiuchumi kama vile umeme, barabara, reli, maji na rasilimali watu yenye ujuzi kuhakikisha viwanda vilivyobinafsishwa na ambavyo havifanyi kazi vianze kufanya kazi. Ni muhimu kuhimiza na kuhamasisha ujenzi wa viwanda vyenye kutumia malighafi iliyopo nchini kwa faida na maendeleo ya wananchi wetu. Watanzania na wawekezaji kutoka nje mnakaribishwa kuwekeza;

(iii) Tunahitaji kuboresha Sekta za Kilimo, Mifugo, Uvuvi na bidhaa za masoko kama njia ya kujenga muunganisho wa sekta hizi na viwanda ili kuongeza thamani kwa lengo la kuondoa umaskini kwa wananchi wetu ambao wengi wao ni wakulima, wafugaji na wavuvi. Tutumie akili, maarifa na nguvu zetu kuhakikisha kwamba wananchi wanapata nyenzo na pembejeo za kuwaongezea uwezo wa uzalishaji wenye tija kwa mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu. Tumedhamiria kupitia mfumo wa masoko ya mazao yetu ili wakulima wauze kwa faida mazao yao;

(iv) Tunalo jukumu kubwa la kuboresha huduma za jamii, ikiwemo elimu, afya, upatikanaji wa maji safi na salama na miundombinu ya umeme hasa vijijini. Tumeanza utaratibu wa kutoa elimu bila malipo kwa wanafunzi, kuanzia darasa la awali hadi kidato cha nne; (v) Bado tunalo tatizo kubwa la biashara na matumizi ya Dawa za Kulevya. Tuunge mkono juhudi za Serikali katika vita hii kubwa ya kupambana na tatizo la Dawa za Kulevya ambazo zinaleta athari kubwa kwa wananchi hususan vijana;

(vi) Umuhimu wa kurejesha maadili katika utumishi wa umma ni suala la kipaumbele. Ni vyema kila mtumishi wa umma kuzingatia sera, sheria na kanuni kuhusu Maadili ya Viongozi na Watumishi wa Umma. Aidha, ni vyema viongozi na watumishi wa umma kila mmoja kwa nafasi yake, awajibike kwa cheo na dhamana aliyopewa katika kuwatumikia wananchi. Dhana ya **“Kutumbua Majipu”** iwe kichocheo cha kuwabaini na kuwarekebisha wale wote wenye dhamira ya kukiuka maadili kwenye nyadhifa zao na katika kuwatumikia wananchi;

(vii) Tunayo changamoto ya ukuaji wa uchumi ambao hauendi sambamba na kasi ya upatikanaji wa ajira. Aidha, zipo dalili kwamba vijana wetu wamekuwa wakitumia muda mwingi kufanya shughuli ambazo hazichangii sana katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. Tuendeele kuwahimiza vijana na kujenga utamaduni kwa kila mwananchi kufanya kazi kwa bidii ili kujenga uchumi kwa maendeleo yetu. Tuunge mkono falsafa ya **“Hapa Kazi Tu”** na kwamba **Asiyefanya kazi na Asile**; na

(viii) Mwisho, niwaombe Watanzania wote kuendelea kuishi kwa amani na utulivu. Tunayo Nchi nzuri na Watanzania wote ni watu wenye upendo. Tudumishe amani, umoja na mshikamano kwa kuwaunga mkono viongozi wetu ili tuongeze kasi ya kuleta maendeleo katika Nchi yetu kwa maana **Umoja ni Nguvu**. Sekta Binafsi, ambayo ndiyo Injini ya Ukuzaji Uchumi wa Taifa letu, isiwe na tashwishwi hata kidogo. Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kuienzi na kuisaidia Sekta Binafsi katika kuchangia maendeleo ya Taifa letu.

SHUKRANI

111. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii sasa kuwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa ushirikiano walionipa tangu wateuliwe. Aidha, nawashukuru Wafanyakazi wote wa Serikali na Taasisi zake chini ya Uongozi wa Katibu Mkuu Kiongozi, kwa kukamilisha Bajeti ya Serikali ya mwaka 2016/2017. Nawashukuru Watanzania wote kwa kushiriki katika ujenzi wa Taifa.

112. Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu); Mheshimiwa Dkt. Abdallah Saleh Possi, Mbunge, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Wenye Ulemavu); Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Mbunge wa Dodoma Mjini na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Vijana) kwa msaa na ushirikiano wao mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nawashukuru vilevile Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, chini ya Uongozi wa Makatibu Wakuu, Dkt. Hamisi H. Mwinyimvua; Bwana Uledi

A. Mussa na Bwana Eric F. Shitindi kwa ushauri wao wa kitaalam ambao wamenipa mimi na Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi katika kipindi hiki. Nawashukuru kwa kukamilisha kwa wakati maandalizi yote ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2016/2017.

113. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Nchi yetu imepata misaada na mikopo kutoka kwa Wahisani wetu mbalimbali. Misaada na mikopo hiyo imetoka kwa Nchi rafiki, Nchi fadhili, Taasisi za Fedha duniani, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Mifuko mbalimbali ya Fedha duniani, madhehebu ya dini na Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Misaada na mikopo hiyo imechangia sana katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Napenda kuwashukuru wote kwa dhati na kuwahakikishia kuwa Watanzania tunathamini misaada na mikopo waliyotupatia na tutaendelea kushirikiana nao katika harakati za kuleta maendeleo ya Taifa letu.

114. Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati wapiga kura wangu wa Jimbo la Ruangwa kwa imani na heshima kubwa waliyonipa ya kunikubali na kunichagua kuwa Mbunge wao. Napenda kuwaahidi kuwa sitawaangusha. Ninawashukuru viongozi wenzangu wote wa Kitaifa na wa ngazi nyingine zote kwa ushirikiano mkubwa ninaoupata kutoka kwao ambao umeniwezesha kutekeleza jukumu hili kubwa la kusimamia utendaji wa Serikali katika sekta zote na kuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. **Asanteni sana!**

115. Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kuishukuru familia yangu hususan mke wangu Mary Majaliwa na watoto wangu wote kwa kuniombea na kunipa moyo mara baada ya kuteuliwa kushika wadhifa huu. Maombi yao yamenipa nguvu ya kutekeleza majukumu yangu.

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA 2016/2017 116.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2016/2017, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Mbili Thelathini na Sita, Milioni Mia Saba Hamsini na Tisa, Mia Nane Sabini na Nne Eflu, Mia Saba na Sita** (236,759,874,706). Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Sabini na Moja, Milioni Mia Tano Sitini na Nne, Mia Mbili Tisini na Tatu Eflu, Mia Saba Sabini na Tatu** (71,564,293,773) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi Bilioni Mia Moja Sitini na Tano, Milioni Mia Moja Tisini na Tano, Mia Tano Themanini Eflu, Mia Tisa Thelathini na Tatu** (165,195,580,933) ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

117. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono kwa wingi mkubwa sana. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba muhimu kabisa ambayo inatufungulia shughuli zetu hapa Bungeni. Waheshimiwa Wabunge wamekusikiliza kwa umakini mkubwa, japo muda haukutosha kwa hotuba nzima kuwa covered lakini kama alivyoshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakala tunazo tuzipitie sisi wenyewe, yale maeneo machache ambayo yamebakia tujielimishe wenyewe kwa wakati wetu, vitabu vimeshagawiwa.

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo moja lilisahuliwa la Mheshimiwa Chegeni, Mwenyekiti wa tawi la CPA, anaomba Kamati yake ya Utendaji ikutane pale Ukumbi wa Spika saa nane, leo mchana. Kamati ya Utendaji ya CPA mkutane pale ukumbi wa Spika saa nane mchana.

Waheshimiwa Wabunge, nimuite moja kwa moja Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria ili aje atoe maoni ya Kamati yake kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu, anakuja Mwenyekiti mwenyewe Mheshimiwa Mchengelwa. Mheshimiwa Mwenyekiti karibu na una nusu saa tu.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kwa kipindi cha dakika mbili nimshukuru kwanza Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujalia afya njema siku ya leo ikiwa ni siku maalum kwangu siku ya Ijumaa, kuwepo hapa kwa ajili ya kutoa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Lakini pia shukrani hizo zinakwenda moja kwa moja kwa Waheshimiwa Wabunge wote bila kujali itikadi zao.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa namna ya pekee kabisa ninaomba nichukue fursa hii kumshukuru sana na kumtakia afya njema Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kukuza demokrasia nchini ambayo imepelekea leo hii kuwa na Wabunge wengi vijana kwa takriban asilimia 67. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu za hivi karibuni za Mabunge ya dunia ambapo mimi ni Mjumbe na nilihudhuria Lusaka - Zambia, taarifa za Mabunge mbalimbali duniani zilionesha kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi chache duniani ambazo zina Wabunge wengi vijana, na tuna sera nzuri kabisa za kuwasaidia vijana duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo pia inajionesha kwamba Tanzania tunaye Mbunge kijana mdogo kuliko wote duniani ambaye anapatikana hapa Tanzania. Tunamtakia afya njema Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Pia nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa wapigakura wangu wa Jimbo la Rufiji kwa namna ya kipekee kunichagua kuwa Mbunge wao na kunipa heshima leo kusimama mbele ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kwa mara ya kwanza katika historia ya mfumo wa vyama vingi Chama cha Mapinduzi mgombea wa Urais amepata kura nyingi kabisa katika Jimbo la Rufiji, kwa mara ya kwanza katika historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni heshima waliyonayo, lakini pia niseme tu kwamba imedhihirisha wazi kabisa kwamba Watanzania katika Jimbo la Rufiji wana imani kubwa na Rais wao Dkt. John Pombe Magufuli. Japokuwa changamoto zilizopo za barabara, afya na elimu ni nyingi lakini tunaamini kwamba changamoto hizo Rais Dkt. John Pombe Magufuli atazitatia. Pia tunaamini Tanzania hii Rais Dkt. John Pombe Magufuli ni miongoni mwa watu wachache duniani kuzaliwa...

SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, jielekeze zaidi kwenye hotuba yako kama ilivyoandikwa. *(Kicheko)*

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, huo ulikuwa ni utangulizi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6(2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 kimeipa Kamati ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na watu wenye Ulemavu. Kamati imetekeleza jukumu hili kwa kipindi cha miezi miwili ambapo ilipokea kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu taarifa za utekelezaji za nusu mwaka (*mid year performance report*), taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengwa na kupokea fedha katika mwaka wa fedha 2015/2016, taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu katika

mwaka wa fedha 2015/2016 na taarifa ya Mpango wa Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo chini ya ofisi hii iliyotengewa na kupokea fedha katika mwaka wa fedha 2015/2016 tarehe 29 Machi hadi tarehe 4 Aprili, 2016. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya Wizara, Taasisi inazosimamia tarehe 8 hadi 13 Aprili 2016, ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Vijana Ajira na Watu wenye Ulemavu ina mafungu sita ya bajeti kama ifuatavyo:-

- (i) Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu;
- (ii) Fungu 25 - Ofisi Binafsi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu;
- (iii) Fungu 65 - Kazi na Ajira;
- (iv) Fungu 15 - Tume ya Upatanishi na Usuluhishi;
- (v) Fungu 61 - Tume ya Uchaguzi; na
- (vi) Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo makubwa manne yafuatayo:-

- (i) Ukaguzi wa miradi ya maendeleo;
- (ii) Mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016;
- (iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa Fedha 2016/2017; na
- (iv) Maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka fedha 2015/2016. Kanuni ya 98(1) na (2) inazitaka Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha unaoisha. Katika kutekeleza masharti ya Kanuni hiyo, Kamati ya Katiba na Sheria ilitembelea, kukagua na kupokea taarifa ya utekelezaji wa miradi inayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu tarehe 29 Machi, tarehe 31 Machi hadi tarehe 04 Aprili 2016. Miradi hiyo ni pamoja na daraja la Mwalimu Nyerere - Kigamboni, mradi wa Nyumba za Makazi Mtoni Kijichi, mradi namba 6575, mradi wa kuboresha uwezo wa kukabiliana na majanga, nne ni mradi namba 5306

mradi wa kuboresha mfumo wa taarifa za hali ya hewa, na tano ni mradi namba 4494 mradi wa kuboresha miundombinu na thamani ya masoko vijijini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara katika Ofisi ya Mamlaka ya usimamizi na Uthibiti wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (SSRA) tarehe 4 Aprili, 2016 ili kujionea jinsi ambavyo Mamlaka hiyo inatekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, yatokanayao na ukaguzi wa miradi:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Nyumba za Makazi Mtoni Kijichi. Mradi huu ni uwekezaji uliofanywa na NSSF ili kuwasaidia Watanzania wengi kumiliki nyumba zao wenyewe kwa gharama nafuu. Kamati iliridhika na ujenzi wa nyumba hizi ambao umefanyika kwa awamu mbili mpaka sasa na kuishauri NSSF kuendeleza kujenga nyumba zaidi za namna hii ili Watanzania wengi waweze kuwa na nyumba zao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba endapo ujenzi wa barabara kutoka nyumba za NSSF za Mtoni Kijichi kuingia katika Mji utakamilika mapema wakazi wa eneo la mradi wataweza kupunguza adha ya umbali wa kuingia na kutoka katika Mji kwa kuzunguka daraja la Mwalimu Nyerere au Kivukoni. Kamati ina maoni kuwa ni vyema ofisi ya Rais - TAMISEMI na Manispaa ya Tameke wakakamilisha haraka ujenzi wa barabara hii kwa kushirikana na NSSF ili kuwasaidia wakazi wa eneo hili.

Mheshimiwa Spika, Daraja la Mwalimu Nyerere Kigamboni: Mradi wa daraja la Mwalimu Nyerere uliendeshwa kiubia kati ya Serikali na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi za Jamii (NSSF) chini ya mfumo wa *Public Private Partnership (PPP)*. Thamani ya mradi huu ni kiasi cha shilingi bilioni 214 ambapo asilimia 25 ya fedha hizo ni fedha za Tanzania na asilimia 75 ni fedha za Dola za Kimarekani. Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia Machi, 2016 asilimia 86 ya fedha zote zilikuwa zimeshalipwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba na Sheria inatoa pongezi za dharti kabisa kwa Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ambaye alianzisha mchakato huu na Rais wa Awamu ya Tano Dkt. John Pombe Magufuli kwa kukamilisha ufunguzi wa daraja hili. Aidha, Kamati inawapongeza Watendaji wote wa NSSF kwa ushiriki wao katika kufanikisha, kukamilisha na hatimae kufunguliwa kwa mradi huu tarehe 19 Aprili, 2016.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi za dharti kukamilika kwa mradi huu, Kamati inaelewa juu ya taarifa ya Mamlaka ya Usimamizi wa Mhibiti wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya tarehe 20 Aprili, 2016 iliyochapishwa katika gazeti

la *The Gurdian*, kuhusu Mfuko wa Jamii (NSSF), ambayo imeuhakikishia umma wa Watanzania kwamba fedha za wanachama katika Mfuko wa NSSF ziko salama na kwamba Mamlaka ya Usimamizi wa Udhibiti wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii itaendelea kusimamia usalama wa fedha za wanachama katika mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii.

Pamoja na taarifa hii ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii, Kamati inatambua pia umuhimu wa sera za uwekezaji katika mifuko yote inayosimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Mifuko ya Jamii hususani kaguzi za NSSF ambazo hufanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa Udhibiti wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Wakaguzi wa Nje na wakaguzi wa Ndani, pamoja na taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ambayo Kamati inaona ni muhimu kwa sasa ikafanyiwa kazi na Kamati ikapata fursa ya kupitia taarifa husika ili kutoa maoni na kuishauri Serikali juu ya hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Spika, miradi iliyopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Miradi yote ya maendeleo iliyokaguliwa na Kamati kwa kipindi hiki chini ya ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ipo katika Fungu 37, Fungu 61- Tume ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na Fungu 65 - Kazi na Ajira. Miradi hiyo ni pamoja na mradi namba 6575 wa kuboresha uwezo wa kukabiliana na majanga.

Mheshimiwa Spika, mradi huu umekuwa ukifadhiliwa na UNDP pamoja na UNICEF toka mwaka wa fedha 2011/2012 na umeendelea kwa muda wa miaka mitano hadi mwaka wa fedha 2015/2016. Mradi huu ulipangwa kutekelezwa kwa gharama ya shilingi billion 4.8 hadi kufikia Februari 2016. Hadi kufikia Februari 2016 fedha ambayo imekwishatumika katika mradi huu ni shilingi bilioni 2.7 sawa na asilimia 56.25 ya fedha zote, mradi huu ulifikia ukomo wa utekelezaji wake tarehe 04 Februari, 2016.

Mheshimiwa Spika, mradi namba 5506, mradi wa kuboresha mfumo wa taarifa za hali ya hewa. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 mradi huu ulitengewa shilingi bilioni 2.6 ambazo ni fedha za nje. Mpaka Februari 2016 mradi huu ulikuwa umepokea shilingi bilioni 2.6 ambazo ni sawa na asilimia 100 ya fedha zote za mradi. Kazi zilizotekelezwa katika mradi huu ni pamoja na kujenga vituo 16 vya kisasa vya hali ya hewa, kununua mitambo na vitendea kazi vya hali ya hewa na kutoa mafunzo kwa wataalam kuhusu utumiaji na uendeshaji wa mitambo wa hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, Mradi namba 4494, mradi wa kuboresha miundombinu ya masoko, uongezaji wa thamani, mazao na huduma za kifedha

vijijini. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 mradi huu ulitengewa shilingi milioni 100 fedha za ndani na shilingi 19, 992,942,000 kama fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi kufika Machi 2016 fedha ambayo imekwisha pokelewa kwenye mradi huu ni shilingi 37,878,269,956 sawa na asilimia 189.5 ya bajeti. Mpaka kufika Machi, 2016 kiasi ambacho tayari kimetumika katika mradi huu ni shilingi 31,402,016,599 sawa na asilimia 82.9 ya kiasi kilichopokelewa. Fedha za mradi huu ni Mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika yaani ADB na Mfuko wa Kimataifa wa Uendelezaji Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kazi ambazo zimetetelezwa katika mradi huu mpaka sasa ni kama ifuatavyo:-

(i) Ukarabati wa barabara za vijijini zenye urefu wa kilomita 180 zikiwepo kilomita 63.6, ambazo zipo Zanzibar;

(ii) Ujenzi wa maghala matano yenye uwezo wa kuhifadhi tani 1000 za mazao kila moja;

(iii) Kuvijengea uwezo wa kufikia masoko vikundi 780, ambapo vikundi 101 vyenye wanachama 2000 ni vikundi vya Zanzibar;

(iv) Kujenga uwezo wa asasi ndogo ndogo za kifedha kama Benki za wananchi ili ziweze kutoa huduma endelevu Vijijini; na

(v) Kushirikiana na taasisi mbalimbali zinazohusika na kuimarisha mfumo wa kifedha vijijini. Jumla ya SACCOS 391 zimefikwa katika mradi huu na kwamba SACCOS 291 ni za Tanzania Bara na SACCOS 100 ni kwa upande wa Zanzibar. Pia viongozi 1568 walipatiwa mafunzo na jumla ya SACCOS 44 zilikaguliwa.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa Fedha 2015/2016. Pamoja na kuipongeza Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutekeleza ipasavyo miradi ya maendeleo kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa kuna umuhimu mkubwa wa Serikali kuipa msukumo wa kutosha miradi ambayo ilidhinishwa fedha katika Fungu la 37 katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 ambalo haijapokea kiasi chochote cha fedha mpaka sasa kutokana na ufinyu wa bajeti.

Miradi hii ni pamoja na mradi wa Uendelezaji wa Makao Makuu ya Nchi, Dodoma (CDA), Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Mradi wa Kimarisha Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Aidha, Kamati ina maoni kuwa ni vizuri ofisi ya Waziri Mkuu ikaongeze nguvu katika Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kuboresha Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ili iweze kujiendesha kisasa na kibiashara zaidi hasa kutokana na mazingira ya ushindani yaliyopo katika sekta ya uchapishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati inatoa pongezi za dhati kabisa kwa uamuzi wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuongeza bajeti ya maendeleo hadi kufikia asilimia 40 katika mwaka wa fedha 2016/2017 na imani ya Kamati kwamba hatua hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuhuisha miradi ya maendeleo ambayo ilisimama na utekelezaji wake haukufanyika kutokana na ufinyu wa Bajeti katika mwaka fedha uliyopita.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa ya ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu utekelezaji wa mpango wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ni kuwa Kamati ilifanya vikao Jijini Dara es Salaam kuanzia tarehe 5 hadi 18 Aprili, 2016, kwa ajili ya kuchambua taarifa za utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa mwaka wa Fedha wa 2015/2016 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017. kwa mujibu wa Kanuni ya 68(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Katika kipindi hicho Kamati ilipata fursa ya kuchambua taarifa za Bajeti na mafungu yalio chini ya ofisi ya Waziri Mkuu, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliyofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Mei, 2015 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Machi, 2016, katika robo tatu ya mwaka huu wa fedha 2015/2016. Uchambuzi huu pia ulitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 na kiasi cha fedha kilichopokelewa katika mradi wa maendeleo hadi kufikia mwezi Machi, 2016. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu mwelekeo wa Mpango wa Bajeti wa Mapato na Matumizi ya Serikali katika mwaka wa fedha 2015/2016, ili kujua vipaumbele vya kibajeti katika mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati ulitazama pia eneo la ukusanyaji wa maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanywa hadi Machi 2016 na lengo la ukusanyaji lililowekwa wakati wa kupitisha bajeti. Lengo la

uchambuzi wa namna hii ni kufahamu uwezo wa Serikali katika kukusanya maduhuli. Kamati ilitumia njia mbalimbali katika uchambuzi wake katika kutazama hali halisi ya kila taasisi, kujiridhisha na taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikana wa taarifa muhimu kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Bunge la Kumi liliidhinisha makadirio ya makusanyo ya maduhuli yenye jumla ya shilingi 12,487,261,000 hadi kufikia 31 Machi, 2016 kiasi cha maduhuri kilichokusanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake ni shilingi 22,173,471,166 ambazo ni sawa na asilimia 178 ya lengo lililokusudiwa. Kamati inaipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake zote kwa ukusanyaji mzuri wa maduhuli katika mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Mafungu yanayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zilizo chini yake, zilitengewa shilingi 349,247,482,857 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016 taasisi hizo zilipokea kiasi cha asilimia 87 ya fedha iliidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Ofisi ya Waziri Mkuu Fungu - 37, Tume ya Taifa ya Uchaguzi Fungu - 61 na Fungu - 65 linalohusika na Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu kwa pamoja lilitengewa jumla ya shilingi 63,874,465,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016 jumla ya shilingi 54,910,620,462 sawa na asilimia 86 ya fedha iliyoidhinishwa... Mwenendo huu ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na fedha za nje, ambazo ni mikopo mbalimbali hasa fedha za miradi na uendelezaji wa miundombinu ya masoko, uongezaji thamani wa mazao na huduma za kifedha vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika kiasi cha fedha ambacho hakikupokelewa kutoka Hazina zipo shilingi bilioni tatu kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa makazi ya Waziri Mkuu unaoendelea eneo la Mlimwa - Dodoma hadi wakati Kamati inakutana mradi huu haukupokea kiasi chochote cha fedha kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Kamati ilibaini kuwa licha ya mradi huu kutengewa fedha kwa miaka mitatu mfululizo, utekelezaji wake umekuwa ni wa kusuasua!

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipokea na kuchambua Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017, tarehe 12 na tarehe 13 Aprili, 2016. Mapango huu wa bajeti ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 umezingatia mwongozo wa mpango wa bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha

na Mipango ambao umelenga utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2016/2017 hadi 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kumwezesha Mheshimiwa Waziri Mkuu kufanya ziara za kikazi ndani na nje ya nchi, pamoja na kuongoza shughuli za Serikali katika Mikutano minne ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(ii) Kuratibu shughuli za maafa nchini na kuelimisha, kuhamasisha na kuwawezesha wadau wa maafa juu ya kuzuia kujiandaa kukabili maafa na kurudisha hali baada ya maafa kutokea kwa kuzingatia sheria mpya ya maafa,

(iii) Kuchapa nyaraka mbalimbali za uendeshaji wa shughuli za Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Bunge.

(iv) Kuratibu na kusimamia shughuli zote zinazohusiana na Vyama vya Siasa.

(v) Kufanya tathmini na kuandaa taarifa ya Uchaguzi Mkuu.

(vi) Kuzuia na kutatua migogoro ya kikazi, kukuza majadiliano kati ya wafanyakazi na waajiri kwa adhima ya kuwezesha ukuaji wa uchumi, ajira, tija na kulinda haki za msingi za wafanyakazi kama zilivyoainishwa katika Mikataba mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa.

(vii) Kuhakikisha wafanyakazi na wananchi kwa ujumla wanapata huduma endelevu za Hifadhi ya Jamii kama vile pensheni, huduma za afya, fidia kwa wafanyakazi watakaoumia kazini na kupanua wigo wa hifadhi ya jamii nchini.

(viii) Kuainisha na kupendekeza maeneo muhimu ya kukuza ajira na hatimaye kuondoa umaskini wa kipato ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa za soko la ajira nchini.

(ix) Kuendelea kushughulikia maendeleo ya vijana nchini katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kimaadili ili kujenga Taifa lenye vijana wenye nguvu, ari, wanaojitambua na wanaojitegemea na kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Taifa.

(x) Kusimamia na kuratibu masuala mbalimbali ya watu wenye ulemavu.

(xi) Kuajiri; kusimamia utendaji wa kazi, kusimamia na kuendeleza rasilimali watu, kuratibu masuala ya kijinsia, kutoa mafunzo ya utendaji kazi, kupambana na rushwa na janga la UKIMWI mahala pa kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhishwa na vipaumbele vilivyowekwa na ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa mwaka 2016/2017 na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Kamati pia imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya msingi ambayo yapo katika ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, ofisi ya Waziri Mkuu inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 38, 051,233, 400. Maduhuli haya yatakusanywa chini ya Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Ofisi ya Waziri Mkuu - Fungu 37, Tume ya Taifa ya Uchaguzi - Fungu 61 na Fungu 65 - Kazi, Ajira, Vijana, na Wenye Ulemavu. Sehemu kubwa ya makadirio ya maduhuli haya yanatokana na shughuli za Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali katika kuchapa nyaraka mbalimbali za Selikali Kuu, Serikali za Mitaa pamoja na nyaraka za matukio maalum.

Mheshimiwa Spika, ufanisi wa Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali unategemea fedha inayotengwa na Serikali katika Bajeti ya Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Ili Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali iweze kufanikisha ukusanyaji mzuri wa maduhuli ni vema Serikali ikataenga fedha za kutosha kwa Idara hii ili iweze kufanya kazi katika mazingira ya kibiashara na kisasa zaidi katika dunia hii ya ushindani wa biashara katika sekta upigaji chapa. Pamoja na maduhuli yanayokusanywa na Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, Fungu 65 - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu linategemea kukusanya maduhuli ya shilingi 35,029,000,400 kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 236,759,874,706, kati ya fedha hizo shilingi 71,564,293,773 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 165,195,580,933 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika katika, mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Waziri Mkuu Fungu - 37 limetengewa shilingi 23,857,728,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 5,131,644,000 ni mishahara ya watumishi na

shilingi 12, 310,210,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 6,415,874,000 ni ruzuku ya taasisi.

Mheshimiwa Spika, jedwali namba moja linaonyesha mgawanyo wa fedha na Matumizi wa Kawaida.

Mheshimiwa Spika, katika mchanganuo wa mapato na matumizi kwa mafungu ambayo yametengewe fedha nyingi kuliko mengine ni ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa - Fungu 27 ambalo limetengewa shilingi 18,793,791,272 na Ofisi ya Waziri Mkuu - Fungu 37 ambalo limetengewa shilingi 23,857,728,000.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi ya kawaida kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi yamepungua kwa asilimia 88 katika Bajeti ya mwaka huu ikilinganishwa na bajeti ya mwaka uliopita kama inavyoonekana katika jedwali namba mbili.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na dhana kwamba Tume ya Taifa Uchaguzi haina kazi baada ya Uchaguzi na hii inaweza kupata nguvu kwa tofauti kubwa ya bajeti inayotengewa kwa matumizi ya kawaida, wakati wa uchaguzi na wakati ambao hakuna uchaguzi. Kamati inatoa rai kwamba bajeti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi iongezwe ili Tume iwe na uwezo wa kusimamia chaguzi za mara kwa mara kwa ufanisi na kuratibu mipango ya muda mrefu ya Tume.

Aidha, Kamati inashauri Serikali kuanza mapema maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kwa kuboresha Daftari la Wapiga Kura na Mfumo wa BVR. Mambo kama haya yanahitaji bajeti ya kutosha kwa kila mwaka ili Tume iweze kuratiba shughuli hizi zote kwa wakati na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zake zote kwa ujumla, inaomba kuidhinishiwa shilingi 140,467,620,000 kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni tano ni fedha za ndani na shilingi 135,467,620,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, fedha iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2016/2017 ni zaidi ya mara tatu ya fedha iliyotengwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 kwa mafungu yote ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kiasi kilichotengwa 2015/2016 kilikuwa shilingi 42,678,055,000.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa fedha za matumizi ya maendeleo ya miaka michache iliyopita inaonyesha kwamba nchi imekuwa ikitenga fedha kidogo, huu siyo mwenendo sahihi kwa nchi ambayo ina maono ya kuelekea

uchumi wa kati. Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuongeza asilimia ya bajeti ya maendeleo hadi kufikia asilimia 40 ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha iliyotengwa kwa ajili ya bajeti ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2016/2017 ni mara tatu zaidi ya fedha iliyotengwa katika mwaka wa fedha unaoisha. Hii inatokana pamoja na mambo mengine na uamuzi wa Serikali ya Awamu ya Tano kuongeza bajeti ya fedha ya Maendeleo kutoka asilimia 26 kwa mwaka wa fedha 2015/2016 mpaka asilimia 40 kwa mwaka fedha 2016/2017 kwa Wizara na taasisi zote za Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2016/2017, kwa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zote na maoni na ushauri wa Kamati pia umezingatia ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2015/2016. Maoni na ushauri huu unajikita katika Fungu 37 ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ili kusimamia matumizi mazuri ya fedha za umma, Kamati inashauri Serikali:

(i) Kusimamia kwa ukaribu fedha zote zinazopelekwa katika miradi ya maendeleo na kufanya ukaguzi wa hesabu wa mara kwa mara ili kujiridhisha kwamba fedha hizo zinatumika kwa mujibu wa sheria na taratibu za matumizi ya fedha ya Serikali;

(ii) Serikali kuifanyia kazi ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kubaini ukweli juu ya tuhuma za ubadhirifu wa fedha za miradi ya mifuko ya Hifadhi ya Jamii *NSSF* na kuwachukulia hatua za kisheria kiutaratibu na kinidhamu watu wote watakaonekana kuhusika na ubadhirifu wa fedha za umma za wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)*;

(iii) Serikali ichukue hatua za maksudi katika ukaguzi wa Sera za Uwekezaji katika Mifuko yote ya Hifadhi za Jamii iliyo chini yake;

(iv) Mamlaka ya Usimamizi ya uthibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii *(SSRA)* iendele kusimamia na kuchukua hatua kali za kisheria kwa Waajiri wote ambao hushindwa kutoa michango ya wanachama wakiwemo Waajiri wa sekta binafsi pamoja na Serikali;

(v) Ofisi ya Waziri Mkuu kuboresha mitambo na mazingira ya Idara ya Mpira Chapa Mkuu wa Serikali na kuiwezesha Idara hii kufanya shughuli zake kibiashara zaidi;

(vi) Serikali kumaliza kwa haraka jengo la Ofisi ya Waziri Mkuu Dodoma katika mwaka huu wa fedha ambalo halijakamilika kwa kipindi kirefu sasa;

(vii) Ofisi ya Waziri Mkuu kuharakisha mpango wa Sheria ambayo itaifanya Dodoma kuwa Mji Mkuu wa Tanzania;

(viii) Serikali kuchukua hatua za ziada kuboresha kitengo cha maafa na kukiwezesha kutoa msaada wa haraka kadri inavyowekana mara maafa yanapotokea;

(ix) Kamati inaishauri Serikali kuanzisha vituo vya Kitaifa vyenye vifaa vya kisasa na kisayansi vitakavyoweza kukabiliana na majanga mbalimbali;

(x) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya maendeleo, hata hivyo, inaishauri Serikali kupunguza asilimia ya utegemezi wa fedha za nje katika mpango wake wa maendeleo;

(xi) Ili kuboresha kitengo cha maafa, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kuwajengea uwezo wataalam mbalimbali wa fani ya usimamizi wa fedha;

(xii) Kamati kwa dhafi kabisa inaipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kutenga fedha ya kununua bajaji na pikipiki kwa ajili ya usafiri katika mwaka huu wa fedha. Uamuzi wa namna hii unaendana na dhana ya kubana matumizi ya fedha za Serikali katika Awamu ya Tano; na *(Makofi)*

(xiii) Serikali itoe tamko kuhusu maandalizi ya utekelezaji wa mchakato wa Kura ya Maoni ya Katiba inayopendekezwa.

Kuhusu Fungu 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi:-

(i) Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi iweke utaratibu mpya wa ratiba ya upigaji kura ili chaguzi zote za Rais, Wabunge, Madiwani na Serikali za Mitaa zifanyike kwa wakati mmoja. Hii itasaidia kupunguza gharama zinazotumika kwa nyakati mbili tofauti, pamoja na kusaidia kupunguza mtikisiko wa amani nchini.

(ii) Kwa kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi haina uwezo wa kusambaza elimu ya uchaguzi katika kila sehemu nchini, Asasi za Kiraia zipewe fedha kupitia Tume hii, ili ziweze kusaidia katika utoaji wa elimu hiyo kwenye sehemu ambazo hazawezi kufikika kwa urahisi hasa vijijini. Vilevile elimu ya mpigakura ifanyike wakati wote na siyo kusubiri wakati wa uchaguzi tu.

(iii) Tume ya Taifa ya Uchaguzi iendelee kufanya ukaguzi wa daftari la kupiga kura mara kwa mara hata baada ya uchaguzi kuisha na kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kujiandikisha.

(iv) Muda wa uhakiki wa majina kabla ya kupiga kura uongezwe kwani ni muda mfupi na umesabaisha wananchi wengi wameshindwa kupiga kura kutokana na majina yao kutokuwepo kwenye daftari na iwapo wangepata muda wa kutosha wa uhakiki wangeweza kupata nafasi ya kufanya utaratibu wa kujiandikisha tena.

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa iangalie pia uwezekano wa kuweka masharti mapya ili kupunguza utitiri wa vyama vya siasa ambavyo havina tija.
(Makofi)

Kuhusu Fungu 65- Kazi na Ajira

Serikali kuendelea kujenga uwezo wa Maafisa Vijana wa Halmashauri, Sekeretarieti ya Mikoa pamaoja na Viongozi, SACCOS ya vijana pia...

SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru...

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI KAMATI YA KATIBA NA SHERIA: Hitimisho.

SPIKA: Utakubaliana nami kwamba muda sasa umeisha.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI KAMATI YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza kwa kuniongezea muda, lakini pia napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jahmuri ya Muungano wa Tanzania...

SPIKA: Omba fedha, nenda katika yale mafungu moja kwa moja.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI KAMATI YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie!

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhisha maombi ya Makadirio ya Mapato ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naonga mkono hoja na kwa yoyote ambayo sikuyasema naomba yaingie kwenye *Hansard*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru! (Makofi)

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kimeipa Kamati ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu. Kamati imetekeleza jukumu hili kwa kipindi cha miezi miwili ambapo Kamati ilipokea kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu taarifa za utekelezaji za Nusu Mwaka (Mid-Year Performance Report), Taarifa za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2015/2016, Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako tukufu katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 na Taarifa ya Mpango wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi hii, iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 tarehe 29 Machi na 04 Aprili 2016. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa

bajeti za Wizara na Taasisi inazosimamia tarehe 08 hadi 13 Aprili 2016 ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu ina mafungu 6 ya bajeti kama ifuatavyo;

- i) Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu
- ii) Fungu 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu
- iii) Fungu 65 - Kazi na Ajira
- iv) Fungu 15 - Tume ya Upatanishi na Usuluhishi
- v) Fungu 61 -Tume ya Uchaguzi
- vi) Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo makubwa manne yafuatayo:-

- i) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
- ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016;
- iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
- iv) Maoni na Ushauri wa Kamati

2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 98 (1) na 98 (2) inazitaka Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Katika kutekeleza masharti ya Kanuni hiyo, Kamati ya Katiba na Sheria ilitembelea, kukagua na kupokea taarifa ya utekelezaji wa miradi inayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu tarehe 29, Machi, 31 Machi na 04 Aprili 2016. Miradi hiyo ni:-

- I. Daraja la Mwalimu Nyerere (Kigamboni)
- II. Mradi wa nyumba za Makazi za Mtoni Kijichi
- III. Mradi Na. 6575 - Mradi wa Kuboresha Uwezo wa Kukabiliana na Majanga (*Strengthening National Disaster Preparedness and Response Project*);
- IV. Mradi Na. 5306 - Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Taarifa za Hali ya Hewa (*Strengthening Climate Information and Early Warning System*);

- V. Mradi Na. 4494 - Mradi wa Kuboresha Miundombinu na Thamani ya Masoko Vijijini (*Market Infrastructure and Value Addition Rural Finance-MIVARF*)

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilifanya ziara katika Ofisi ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) tarehe 04/04/2016 ili kujionea jinsi ambavyo Mamlaka hiyo inatekeleza majukumu yake.

2.1 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi

2.1.1 Mradi wa Nyumba za Makazi Mtoni Kijichi

Mheshimiwa Spika, Mradi huu ni uwekezaji uliofanywa na NSSF ili kuwasaidia Watanzania wengi kumiliki nyumba zao wenyewe kwa gharama nafuu. Kamati iliridhika na ujenzi wa nyumba hizi ambao umefanyika kwa awamu mbili mpaka sasa na kuishauri NSSF kuendelea kujenga nyumba zaidi za namna hii ili Watanzania wengi waweze kuwa na nyumba zao wenyewe. Hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba endapo ujenzi wa barabara kutoka nyumba za NSSF za Mtoni Kijichi kuingia katikati ya mji utakamilika mapema wakazi wa eneo la mradi wataweza kupunguza adha ya umbali wa kuingia na kutoka katikati ya mji kwa kuzungukia daraja la Mwalimu Nyerere au Kivukoni. Kamati ina maoni kuwa ni vema Ofisi ya Rais TAMISEMI na Manispaa ya Temeke wakakamilisha haraka ujenzi wa barabara hii kwa kushirikiana na NSSF ili kuwasaidia wakazi wa eneo hili.

2.1.2 Daraja la Mwalimu Nyerere (Kigamboni)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Daraja la Mwalimu Nyerere uliendeshwa kiubia kati ya Serikali na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) chini ya Mfumo wa Public Private Partnership. Thamani ya Mradi huu ni kiasi cha Shilingi Bilioni 214 ambapo asilimia 25 ya fedha hizo ni fedha za Tanzania na asilimia 75 ni fedha za Dola za Kimarekani. Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia Machi 2016 asilimia 86 ya fedha zote ilikuwa imekwishalipwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba na Sheria inatoa pongezi za dhati kwa Rais wa Awamu ya Nne Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete ambaye alianzisha mchakato huu na Rais wa Awamu ya Tano Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa kukamilisha ufunguzi wa Daraja hili. Aidha, Kamati inawapongeza watendaji wote wa NSSF kwa ushiriki wao katika kufanikisha, kukamilika na hatimaye kufunguliwa kwa mradi huu tarehe 19 Aprili 2016.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi za dhiti kwa kukamilika kwa mradi huu, Kamati inatambua taarifa ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya Tarehe 20 Aprili 2016 iliyochapishwa katika gazeti la The Guardian kuhusu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ambayo imeuhakikishia Umma wa Watanzania kwamba fedha za Wanachama katika Mfuko wa NSSF ziko salama na kwamba Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii itaendelea kusimamia usalama wa fedha za Wanachama katika Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na taarifa hii ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Kamati inatambua pia umuhimu wa Sera za Uwekezaji katika Mifuko yote inayosimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, hususan kaguzi za NSSF, ambazo hufanywa na Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, wakaguzi nje, na wa ndani na taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ambayo kamati inaona ni muhimu kwa sasa ikafanyiwa kazi na Kamati ikapata fursa ya kupitia taarifa husika, ili kutoa maoni na kuishauri Serikali juu ya hatua za kuchukua.

2.1.3 Miradi iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu

Mheshimiwa Spika, miradi yote ya maendeleo iliyokaguliwa na Kamati kwa kipindi hiki chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ipo katika Mafungu 37 (Ofisi ya Waziri Mkuu), 61 (Tume ya Taifa ya Uchaguzi) na 65 (Kazi na Ajira). Miradi hiyo ni:-

i) Mradi Na. 6575 - Mradi wa Kuboresha Uwezo wa Kukabiliana na Majanga (*Strengthening National Disaster Preparedness and Response Project*)

Mheshimiwa Spika, Mradi huu umekuwa ukifadhiliwa na UNDP na UNICEF toka Mwaka wa Fedha 2011/2012 na umeendelea kwa muda wa miaka 5 hadi Mwaka wa Fedha 2015/2016. Mradi huu ulipangwa kutekelezwa kwa gharama ya Shilingi Bilioni 4.8 hadi kufikia Februari, 2016 fedha ambayo imekwishatumika kwenye mradi huu ni Shilingi Bilioni 2.7 sawa na asilimia 56.25 ya fedha zote. Mradi huu ulifikia ukomo wa utekelezaji wake tarehe 04 Februari 2016.

ii) Mradi Na. 5306 - Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Taarifa za Hali ya Hewa (*Strengthening Climate Information and Early Warning System*)

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 mradi huu ulitengewa Shilingi Bilioni 2.6 ambazo ni fedha za nje. Mpaka Februari 2016 mradi ulikua umepokea Shilingi Bilioni 2.6 ambazo sawa na asilimia 100 ya fedha

zote za mradi. Kazi zilizotekelezwa katika mradi huu ni pamoja na kujenga vituo 16 vya kisasa vya hali ya hewa (Automatic Weather Stations), kununua mitambo na vitendea kazi vya hali ya hewa na kutoa mafunzo kwa wataalamu kuhusu utumiaji na uendeshaji wa mitambo ya hali ya hewa.

iii) Mradi Na. 4494 - Mradi wa Kuboresha Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani ya Mazao na Huduma za Kifedha Vijijini (*Marketing Infrastructure, Value Addition and Rural Financing - MIVARF*)

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 mradi huu ulitengewa Shilingi Milioni Mia moja (100,000,000/=) fedha za ndani na Shilingi Bilioni Kumi na Tisa, Milioni Mia tisa Tisini na Mbili, Laki Tisa na Arobaini na Mbili Eflu (19,992,942,000/=), fedha za nje. Hadi kufikia Machi 2016 fedha ambayo imekwishapokelewa kwenye mradi ni Shilingi Bilioni Thelathini na Saba, Milioni Mia nane Sabini na Nane, Laki Mbili Sifini na Tisa Eflu Mia tisa Hamsini na Sita (37,878,269,956) sawa na asilimia 189.5 ya bajeti. Mpaka kufikia Machi 2016 kiasi ambacho tayari kimetumika katika mradi huu ni Shilingi Bilioni Thelathini na Moja, Milioni Mia nne na Mbili, Kumi na Sita Eflu, Mia tano Tisini na Tisa (31,402,016,599) sawa na asilimia 82.9 ya kiasi kilichopokelewa. Fedha za mradi huu ni mkopo kutoka Benki ya Maendeleo Afrika (ADB) na Mfuko wa Kimataifa wa Uendelezaji Kilimo (IFAD).

Mheshimiwa Spika, kazi ambazo zimeteketelezwa katika mradi huu mpaka sasa ni kama ifuatavyo:- Ukarabati wa barabara za vijijini zenye urefu wa kilomita 180 zikiwemo km 63.6 ambazo zipo Zanzibar, ujenzi wa maghala matano yenye uwezo wa kuhifadhi tani 1000 za mazao kila moja, kuvijengea uwezo wa kufikia masoko vikundi 780 ambapo vikundi 101 vyenye wanachama 2,000 ni vya Zanzibar, kujenga uwezo wa Asasi ndogo ndogo za kifedha kama vile Benki za Wananchi/Ushirika ili ziweze kutoa huduma endelevu vijijini na kushirikiana na Taasisi mbalimbali zinazohusika na kuimarisha Mfumo wa Kifedha Vijijini. Jumla ya SACCOS 391 zimefikwa na mradi huu; 291 Tanzania Bara na 100 kwa upande wa Zanzibar. Pia kwa upande wa Zanzibar viongozi 1,568 walipatiwa mafunzo na jumla ya SACCOS 44 zilikaguliwa.

2.2 Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2015/2016

2.2.1 Maoni na Mapendekezo ya Jumla Kuhusu Miradi

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kutekeleza ipasavyo miradi ya maendeleo kwa asilimia kubwa, Kamati ina maoni kuwa kuna umuhimu mkubwa kwa Serikali kuipa msukumo wa kutosha miradi ambayo iliidhinishwa fedha katika Fungu 37 katika Mwaka wa Fedha

2015/2016 ambayo haijapokea kiasi chochote cha fedha mpaka sasa kutokana na ufinyu wa bajeti. Miradi hii ni pamoja na mradi wa Uendelezaji wa Makao Makuu ya Nchi Dodoma (CDA), Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na mradi wa Kuimarisha Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

Aidha, Kamati ina maoni kuwa ni vizuri Ofisi ya Waziri Mkuu ikaongeze nguvu katika Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kuboresha Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ili iweze kujiendesha kisasa na kibiashara zaidi hasa kutokana na mazingira ya ushindani yaliyopo katika sekta ya uchapishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati inatoa pongeza za dhati kwa uamuzi wa Serikali ya Awamu ya Tano wa kuongeza bajeti ya maendeleo hadi asilimia 40 katika Mwaka wa Fedha 2016/2017. Ni imani ya Kamati kwamba hatua hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuhuisha Miradi ya Maendeleo ambayo ilisimama au utekelezaji wake haukufanyika kutokana na ufinyu wa bajeti katika Mwaka wa Fedha uliopita.

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA OFISI YA WAZIRI MKUU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikaa vikao Jijini Dar es Salaam, kuanzia tarehe 08 hadi 15 Aprili 2016 kwa ajili ya kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Mipango ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na uchambuzi wa makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016. Katika kipindi hiki Kamati ilipata fursa ya kuchambua taarifa za bajeti za Mafungu yaliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Mei 2015 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Machi 2016 katika robo ya tatu ya mwaka huu wa fedha 2015/2016. Uchambuzi huu pia ulitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 na kiasi cha fedha kilichopokelewa katika Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Mwezi Machi 2016. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa

Mpango na Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 ili kujua vipaumbele vya kibajeti katika mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati ulitazama pia eneo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanywa hadi Machi 2016 na lengo la ukusanyaji lililowekwa wakati wa kupitisha bajeti. Lengo la uchambuzi wa namna hii ni kufahamu uwezo wa Serikali katika kukusanya Maduhuli. Kamati ilitumia njia mbalimbali katika uchambuzi wake kama kutazama hali halisi ya kila Taasisi, kujiridhisha na taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu kwenye Kamati.

3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa Kuhusu Ukusanyaji Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Bunge la 10 liliidhinisha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yenye jumla ya Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia nne Themanini na Saba, Laki Mbili Sitini na Moja Eflu (12,487,261,000/=). Hadi kufikia Machi 31 2016 kiasi cha Maduhuli kilichokusanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake ni Shilingi Bilioni Ishirini na Mbili, Milioni Miamoja Sabini na Tatu, Laki Nne Sabini na Moja Eflu Miamoja Sitini na Sita (22,173,471,166/=) ambazo sawa na asilimia 178 ya lengo lililokusudiwa. Kamati inaipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa ukusanyaji mzuri wa Maduhuli katika Mwaka wa Fedha 2015/2016.

3.1.2 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Mafungu yanayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake yalitengewa Shilingi Bilioni Mia tatu Arobaini na Tisa, Milioni Miambili Themanini na Saba, Laki Nne Themanini na Mbili Eflu Mia nane Hamsini na Saba (349,287,482,857 /)=) kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2016 Taasisi hizo zilipokea kiasi cha asilimia 87 ya fedha iliyoidhinishwa.

3.1.3 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 37), Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Fungu 61) na Fungu 65 linalohusika na Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa pamoja yalitengewa jumla ya Shilingi bilioni Sitini na Tatu, Milioni Mia nane Sabini na Nne, Laki Nne Sitini na Tano Eflu (63,874,465,000/=) kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Mwezi Machi 2016 jumla ya Shilingi Bilioni Hamsini na Nne, Milioni Mia tisa na Kumi, Laki

Sita Ishirini Efu Mia Nne Sitini na Mbili (54,910,620,462/=) sawa na asilimia 86 ya fedha iliyoidhinishwa. Mwenendo huu ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na fedha za nje amabazo ni mikopo mbalimbali na hasa fedha za mradi wa uendelezaji wa Miundo mbinu ya Masoko, Uongezaji Thamani ya Mazao na Huduma za Kifedha Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Katika kiasi cha fedha ambacho hakikupokelewa kutoka hazina zipo Shilingi Bilioni Tatu (3,000,000,000/=) kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa makazi ya Waziri Mkuu unaoendelea eneo la Mlimwa Dodoma. Hadi wakati Kamati inakutana Mradi huu haukupokea kiasi chochote cha fedha kwa mwaka 2015/2016. Kamati ilibaini kuwa licha ya Mradi huu kutengewa fedha kwa miaka mitatu mfululizo, utekelezaji wake umekuwa ukisuasua.

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 tarehe 12 na 13 April 2016. Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 umezingatia Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mpango ambao umelenga utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/2021).

4.1 Uchambuzi wa Vipaumbele vya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Mpango wa Bajeti wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ni kama ifuatavyo:-

- i) Kumwezesha Mheshimiwa Waziri Mkuu kufanya ziara za kikazi ndani na nje ya nchi pamoja na kuongoza shughuli za Serikali katika Mikutano 4 ya Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania;
- ii) Kuratibu shughuli za maafa nchini kwa kuelimisha, kuhamasisha na kuwawezesha wadau wa maafa juu ya kuzuia, kujiandaa, kukabili maafa na kurudisha hali baada ya maafa kutokea kwa kuzingatia Sheria mpya ya maafa;
- iii) Kuchapa nyaraka mbalimbali za uendeshaji wa shughuli za Serikali Kuu, Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Bunge;

iv) Kuratibu na kusimamia shughuli zote zinazohusiana na Vyama vya Siasa;

v) Kufanya tathmini na kuandaa taarifa ya Uchaguzi Mkuu;

vi) Kuzuia na kutatua migogoro ya kikazi, kukuza majadiliano kati ya Wafanyakazi na Waajiri kwa azma ya kuwezesha ukuaji wa uchumi, ajira, tija na kulinda haki za msingi za wafanyakazi kama zilivyodainishwa katika Mikataba mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa;

vii) Kuhakikisha Wafanyakazi na Wananchi kwa ujumla wanapata huduma endelevu za hifadhi ya jamii kama vile Pensheni, huduma za afya, fidia kwa wafanyakazi watakaoumia kazini na kupanua wigo wa hifadhi ya jamii nchini;

viii) Kuainisha na kupendekeza maeneo muhimu ya kukuza ajira na hatimaye kuondoa umaskini wa kipato ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa za soko la ajira nchini;

ix) Kuendelea kushughulikia maendeleo ya vijana nchini katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kimaadili ili kujenga Taifa lenye vijana wenye nguvu, ari, wanaojitambua, wanaojitegemea na kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Taifa;

x) Kusimamia na kuratibu masuala mbalimbali ya Watu wenye Ulemavu;

xi) Kuajiri, kusimamia utendaji wa kazi, kusimamia na kuendeleza rasilimali watu, kuratibu masuala ya kijinsia, kutoa mafunzo ya utendaji kazi, kupambana na rushwa na janga la UKIMWI/VVU mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhishwa na Vipaumbele vilivyowekwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2016/2017 na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017-2020/2021). Kamati pia imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya msingi ambayo yapo katika Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Ofisi ya Waziri Mkuu inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi Bilioni Thelathini na Nane, Milioni Hamsini na Moja, Laki Mbili Thelathini na Tatu Eflu na Mia nne (38,051,233,400/=). Maduhuli haya yatakusanywa chini ya Fungu 27 (Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa), Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 37), Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Fungu 61) na Fungu 65 (Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu). Sehemu kubwa ya Makadirio ya Maduhuli haya yatatokana na shughuli za Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali katika kuchapa Nyaraka mbalimbali za Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, pamoja na Nyaraka za matukio maalumu.

Mheshimiwa Spika, ufanisi wa Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali unategemea fedha inayotengwa na Serikali katika bajeti ya Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Ili Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali iweze kufanikisha ukusanyaji mzuri wa Maduhuli ni vema Serikali ikatenga fedha za kutosha kwa Idara hii ili iweze kufanya kazi katika mazingira ya kibiashara na kisasa zaidi katika dunia hii ya ushindani wa biashara katika sekta ya upigaji chapa. Pamoja na Maduhuli yanayokusanywa na Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali Fungu 65 (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) linategemea kukusanya Maduhuli ya Shilingi Bilioni Thelathini na Tano, Milioni Ishirini na Tisa, na Mia nne (35,029,000,400/=) kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato.

4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake b inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni Mia Mbili Thelathini na Sita, Milioni Miasaba Hamsini na Tisa, Mianane Sabini na Nne Eflu, Mia Saba na Sita, (236,759,874,706/=), kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Sabini na Moja, Milioni Mia Tano Sitini na Nne, Mia Mbili Tisini na Tatu Eflu, Mia Saba Sabini na Tatu (71, 564, 293,773/=) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi Bilioni Mia Moja Sitini na Tano, Milioni Mia Moja Tisini Na Tano, Mia Tano Themanini Eflu, Mia Tisa Thelathini na Tatu (165, 195, 580,933/= ni kwa Maendeleo.

4.3.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya kawaida Fungu 37 (Ofisi ya Waziri Mkuu) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 37) limetengewa Shilingi Bilioni Ishirini na Tatu, Milioni Mia Nane

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Hamsini na Saba, Mia Saba Ishirini na Nane Efu, (23,857,728,000/=). Kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Moja Thelathini na Moja, Mia sita Arobaini na Nne Efu (5,131, 644,000/=) ni mishahara ya Watumishi na Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Tatu na Kumi, Mia Mbili na Kumi Efu (12, 310,210,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi Bilioni Sita Milioni Mia Nne Kumi na Tano, Mia Nane Sabini na Nne Efu (6,415, 874,000/=) ni Ruzuku za Taasisi

Jedwali Na. 01: Mgawanyo wa fedha ya Matumizi ya kawaida Ki - Taasisi mwaka 2016/2017

KASMA	TAASISI	MISHAHARA	MATUMIZI MENGINEYO	JUMLA YA MAKADIRIO
1001	Uendelezaji wa Makao Makuu Dodoma (CDA)	3,723,632,000	0	3,723,632,000
4001	Baraza la Biashara la Taifa (TNBC)	825,480,000	400,153,000	1,225,633,000
	Baraza la Uwezesaji (NEEC)	614, 286,000	852,323,000	1,466,609,000
JUMLA		5,163,398,000	1,252,476,000	6,415,874,000

Mheshimiwa Spika, katika mchanganuo wa mapato na matumizi kwa Mafungu, ambayo yametengewa fedha nyingi kuliko mengine ni Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa (Fungu 27) ambalo limetengewa Shilingi Bilioni Kumi na Nane, Milioni Mia saba Tisini na Tatu, Mia Saba Tisini na Moja Eflu, Mia Mbili Sabini na Mbili (18,793,791,272/=) na Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 37) ambalo limetengewa Shilingi Bilioni Ishirini na Tatu, Milioni Mia Nane Hamsini na Saba, Mia Saba Ishirini na Nane Eflu, (23,857,728,000/=).

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi yamepungua kwa asilimia 88 katika bajeti ya mwaka huu ikilinganishwa na bajeti ya mwaka uliopita kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 02.

Jedwali Na. 02: Ulinganisho wa Bajeti ya Matumizi ya kawaida ya Tume ya Uchaguzi kati ya mwaka 2015/2016 na mwaka 2016/2017

a) 2015/2016	b) 2016/2017	TOFAUTI (a)– (b)	ASILIMIA
276,842,591,872	3,145,814,000	273,696,777,872	88

Mheshimiwa Spika, kumekua na dhana kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi haina kazi baada ya uchaguzi. Dhana hii inaweza kupata nguvu kwa tofauti kubwa ya bajeti inayotengwa kwa Matumizi ya Kawaida ya Tume wakati wa uchaguzi na wakati ambapo hakuna uchaguzi. Kamati inatoa rai kwamba bajeti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi iongezwe ili Tume iwe na uwezo wa kusimamia chaguzi za mara kwa mara kwa ufanisi na kuratibu mipango ya muda mrefu ya Tume. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuanza mapema maandalizi ya Uchaguzi wa Mwaka 2020 kwa kuboresha Daftari la Wapiga Kura na Mfumo wa BVR. Mambo kama haya yanahitaji bajeti ya kutosha kwa kila mwaka ili Tume iweze kuratibu shughuli hizi zote kwa wakati na kwa ufanisi.

4.3.2 Mpango wa Matumizi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zake kwa ujumla inaomba kuidhinishiwa Shilingi Bilioni Mia Moja Arobaini, Milioni Mia Nne Sitini na Saba, Mia Sita Ishirini Eflu, (140,467,620,000/=) kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo.

Kati ya fedha hizi Shilingi Bilioni Tano, (5,000,000,000/=) ni fedha za ndani na Shilingi Bilioni Mia Moja Thelathini na Tano, Milioni Mia Nne Sifini na Saba, Mia Sita Ishirini Efu (135, 467,620,000/=) ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, fedha iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 ni zaidi ya mara tatu ya fedha iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 kwa Mafungu yote ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kiasi kilichotengwa 2015/2016 kilikuwa Shilingi Bilioni Arobaini na Mbili, Milioni Mia Sita Sabini na Nane, Hamsini na Tano Efu (42,678,055,000/=).

Jedwali Na. 03: Ulinganisho wa Fedha ya Matumizi ya Maendeleo kati ya mwaka 2015/2016 na mwaka 2016/2017 kwa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake.

2015/2016		2016/2017	
FEDHA ZA NDANI	FEDHA YA NJE	FEDHA YA NDANI	FEDHA YA NJE
5,000,000,000/=	37,678,055,000/=	5,000,000,000/=	135, 467,620,000/=
JUMLA	42,678,055,000/=	140,467,620,000/=	

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa fedha za matumizi ya maendeleo kwa miaka michache iliyopita inaonyesha kwamba nchi imekua ikitenga fedha kidogo. Huu sio mwenendo sahihi kwa nchi ambayo ina maono ya kuelekea uchumi wa kati. Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuongeza asilimia ya bajeti ya Maendeleo hadi kufikia asilimia 40 ya bajeti ya Serikali kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, fedha iliyotengwa kwa ajili ya bajeti ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2016/2017 ni mara tatu zaidi ya fedha iliyotengwa katika mwaka wa fedha unaoisha.

Hii inatokana, pamoja na mambo mengine, na uamuzi wa serikali ya awamu ya tano kuongeza bajeti ya fedha za maendeleo kutoka asilimia 26 kwa mwaka wa fedha 2015/2016 mpaka asilimia 40 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa Wizara na Taasisi zote za Serikali.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na Taarifa za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake. Maoni na Ushauri wa Kamati pia umezingatia ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Maoni na Ushauri huo ni kama ifuatavyo:-

5.1 Fungu 37 – OFISI YA WAZIRI MKUU

i) Ili kusimamia matumizi mazuri ya fedha za Umma Kamati inaishauri Serikali kusimamia kwa ukaribu fedha zote zinazopelekwa katika Miradi ya Maendeleo na kufanya ukaguzi wa Hesabu wa mara kwa mara ili kujiridhisha kwamba fedha hizo zinatumika kwa mujibu wa sheria na taratibu za matumizi ya fedha za Serikali;

ii) Serikali kuifanyia kazi ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali ili kubaini ukweli juu ya tuhuma za ubadhirifu wa fedha katika miradi ya NSSF na kuwachukulia hatua kali za kisheria, kiutaratibu na kinidhamu watu wote watakaonekana kuhusika na ubadhirifu wa fedha hizi za Umma na Wanachama wa Mfuko wa NSSF;

iii) Serikali ichukue hatua za makusudi katika ukaguzi wa Sera za Uwekezaji katika Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii iliyo chini yake;

iv) Mamlaka ya Usimaizi na Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iendelee kusimamia na kuchukua hatua kali za kisheria kwa waajiri wote ambao hushindwa kutoa michango ya wanachama, wakiwemo Waajiri wa Sekta binafsi pamoja na Taasisi za Serikali;

v) Ofisi ya Waziri Mkuu kuboresha mitambo na mazingira ya Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na kuiwezesha Idara hii kufanya shughuli zake kibiashara zaidi;

vi) Serikali kumaliza kwa haraka jengo la Ofisi ya Waziri Mkuu Dodoma katika mwaka huu wa fedha ambalo halijakamilika kwa kipindi kirefu sasa;

vii) Ofisi ya Waziri Mkuu kuharakisha Mpango na Sheria ambayo itaifanya Dodoma kuwa Mji Mkuu wa Tanzania;

viii) Serikali kuchukua hatua za ziada kuboresha kitengo cha Maafa na kukiwezesha kutoa msaada wa haraka kadri inavyowezekana mara Maafa yanapotokea;

ix) Kamati inaishauri serikali kuanzisha vituo vya kitaifa vyenye vifaa vya kisasa na kisayansi vitakavyoweza kukabiliana na majanga mbalimbali;

x) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya maendeleo hata hivyo, inashauri Serikali kupunguza asilimia ya utegemezi wa fedha za nje katika Mpango wake wa Maendeleo;

xi) Ili kukiboresha kitengo cha Maafa, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kuwajengea uwezo wataalamu mbalimbali wa fani ya usimamizi wa maafa;

xii) Kamati kwa dhati kabisa inaipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kutenga fedha ya kununua Bajaji na Pikipiki kwa ajili ya usafiri katika mwaka huu wa fedha. Uamuzi wa namna hii unaendana na dhana ya kubana matumizi ya fedha ya Serikali katika Awamu ya Tano;

xiii) Serikali itoe Tamko kuhusu Maandalizi na Utekelezaji wa Mchakato wa Kura ya Maoni ya Katiba inayopendekezwa;

5.2 Fungu 61 – TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

i) Tume ya Taifa ya Uchaguzi iweke utaratibu mpya wa ratiba ya upigaji kura ili chaguzi zote za Rais, Wabunge, Madiwani na Serikali za Mitaa zifanyike kwa wakati mmoja. Hii itasaidia kupunguza gharama zinazotumika kwa nyakati mbili tofauti pamoja na kusaidia kupunguza mtikisiko wa amani nchini;

ii) Kwa kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi haina uwezo wa kusambaza elimu ya Uchaguzi katika kila sehemu nchini, Asasi za Kiraia zipewe fedha kupitia Tume ili ziweze kuisaidia katika utoaji wa elimu hiyo kwenye sehemu ambazo hazawezi kufikika kwa urahisi hasa vijijini. Vilevile elimu ya Mpiga Kura ifanyike wakati wote na sio kusubiri wakati wa uchaguzi tu;

iii) Tume ya Taifa ya Uchaguzi iendelee kufanya Ukaguzi wa Daftari la Kupiga Kura mara kwa mara hata baada ya uchaguzi kuisha na kuwaelimisha Wananchi umuhimu wa kujiandikisha;

iv) Muda wa uhakiki wa majina kabla ya kupiga kura uongezwe kwani ni mfupi na umesababisha Wananchi wengi washindwe kupiga kura kutokana na majina yao kutokuwepo kwenye Daftari. Iwapo wangepata muda wa kutosha wa uhakiki wangeweza kupata nafasi ya kufanya utaratibu wa kujiandikisha tena;

5.3 Fungu 27 – OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA

Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa iangalie uwezekano wa kuweka masharti mapya ili kupunguza utitiri wa Usajili wa Vyama ambavyo havina tija; na

5.4 Fungu 65 – KAZI NA AJIRA

Serikali kuendelea kujenga uwezo wa Vijana, Maafisa Vijana wa Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa pamoja na Viongozi wa SACCOS za Vijana katika kuhamasisha uundwaji na usimamizi wa SACCOS imara na endelevu pamoja na kujifunza namna nzuri ya matumizi ya fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Kiongozi katika Mhimili huu muhimu wa kutetea haki za Wananchi. Nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Napenda nikupongeze pia kwa umahiri wako katika kasi ya kuliendesha Bunge hili katika kutekeleza Kauli Mbiu ya **HAPA KAZI TU** na kuishauri vema Serikali kwa manufaa ya Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru na kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Tulia Ackson kwa kuchaguliwa kwake kuwa Naibu Spika wa Bunge hili la Kumi na Moja, Aidha, nimpongeze kwa kazi nzuri anayoifanya ya kukusaidia katika kuendesha Bunge letu. Niwapongeze Wenyeviti wa Bunge kwa kuchaguliwa kwao naamini watafanya kazi nzuri ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge ili kuwa na Bunge lenye ufanisi mkubwa na la wazi kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa ya pekee kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, na nimtakie kazi njema ya kuliongoza Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Nimpongeze Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Majaliwa Kassimu Majaliwa kwa kuteuliwa kwake kuwa kushika Wadhifa huu mkubwa wa kuwa Mtendaji Mkuu wa Shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge Kazi, Ajira, Vijana, na Walemavu, Mhe. Jenista J. Mhagama, (Mb) Naibu Mawaziri, Mhe. Antony Mavunde, (Mb), na Mhe. Dr.Abdallah Possi, (Mb), Makatibu Wakuu Ndg. Erick Shitindi, Ndg. Hamisi H. Mwinyimkuu, Ndg. Uledi A. Mussa pamoja na Wataalam wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa kuchambua na kujadili bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu.

Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb - Mjumbe;
4. Mhe. Ally Saleh Ally, Mb - Mjumbe;
5. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Dkt.Godwin Oloyce Mollel, Mb - Mjumbe;
9. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb - Mjumbe;
- 10.Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb - Mjumbe;
- 11.Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb - Mjumbe;
- 12.Mhe. Makame Mashaka Fom, Mb - Mjumbe;-
- 13.Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb - Mjumbe;
- 14.Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb - Mjumbe;
- 15.Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb - Mjumbe;
- 16.Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb - Mjumbe;
- 17.Mhe. Riziki Shahari Mngwali, Mb - Mjumbe;
- 18.Mhe. Saumu Heri Sakala, Mb - Mjumbe;
- 19.Mhe. Seif Ungando Ally, Mb - Mjumbe;

- 20.Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe;
- 21.Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb - Mjumbe;
- 22.Mhe. Twahir Awesu Mohammed, Mb - Mjumbe;
- 23. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb - Mjumbe;
- 24.Mhe. David Mathayo David, Mb - Mjumbe;

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kasilillah kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, nawashukuru Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Angelina Sanga, Ndg. Stella Bwimbo, Ndg. Stanslous Kagisa, Ndg. Dunford Mpelumbe na Muhudumu wa Kamati Ndg. Gaitana Chima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha maombi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, na naunga mkono hoja hii.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.

**MWENYEKITI,
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA
22 Aprili, 2016**

SPIKA: Ahsante Mwenyekiti. Nina tangazo moja tu kutoka kwa Mheshimiwa Ally Saleh, Naibu Mnadhimu upande wa Upinzani anaomba Wabunge wa Kambi ya Upinzani wote mkutane baadaye tutakapoahirisha kikao hiki kwenye saa nane katika Ukumbi wa Msekwa. *Opposition* wote Ukumbi wa Msekwa saa nane mchana.

Waheshimiwa Wabunge, bado tunaendelea, nitamuita Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI sasa hivi. Lakini nitoe ushauri kwa Wenyeviti wa Kamati wote, kwenye hotuba zenu, kitu muhimu kuliko vyote ni ushauri na maoni ya Kamati, ndiyo kitu muhimu sana. Kwa hiyo utangulizi, ukichukua nusu saa yako ukajaza utangulizi au ukajaza hitimisho, unajikuta umepoteza lengo lako. Kwa vyovyote vile jitahidi uhakikishe maoni na ushauri wa Kamati Wabunge wameusikia halafu haya mengine unaweza ukajaziajazia unavyojua wewe mwenyewe. Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI! (Makofi)

Waheshimiwa Wenyeviti ambao mnajua mnatoa hotuba zenu hapa muwe mnasogea mbele, mnakuwa karibu hivi.

Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya UKIMWI karibu sana!

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MASUALA YA UKIMWI: Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya ofisi ya Waziri Mkuu, Tume ya Kuratibu na Kudhibiti UKIMWI/ Dawa za Kulevya, Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) kwa mwaka wa fedha 2015/16 na Makadirio na Mapato na Matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu utekelezaji wa majukumu ya bajeti ya Tume ya Uratibu ya Kudhibiti UKIMWI/ Dawa za Kulevya kwa Fungu 91 na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) Fungu 92, kwa mwaka wa fedha wa mwaka 2015/16, pamoja na Makadirio na Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2016/17 kwa Tume hizo mbili.

Mheshimiwa Spika, maoni yatakayotolewa katika taarifa ni kutokana na majukumu ya Kamati kama yalivyoainishwa katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili 2016, majukumu ya Kamati yaliyotekelezwa kwa njia ya vikao na ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali. Aidha, mtiririko wa taarifa umezingatia maeneo makubwa manne yafuatayo:-

Utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya kipindi kilichopita, utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/16, makadirio ya mapato na matumizi ya 2016/17, Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawa za Kulevya, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza ya utangulizi inaeleza mtiririko wa taarifa itakavyokuwa, na sehemu ya pili ina masuala muhimu yaliyojitokeza katika kipengele kilichotajwa sehemu ya kwanza hapo juu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ni kuhusu masuala muhimu yaliyobainika. Kama ilivyoelezwa hapo awali katika kipengele cha 1.3. sehemu hii inaeleza mambo muhimu yaliyobainika katika utekelezaji wa shughuli za Kamati. Kutokana na mambo hayo Kamati inatoa maoni na mapendekezo yatakayotolewa katika sehemu ya tatu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati. Katika mwaka wa fedha 2015/16, Kamati ilitoa maoni sita kwa ajili ya kutekelezwa na Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya, mahusiano na bajeti yake. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Tume imetekeleza vizuri maoni tano kasoro moja linalohusu kuongeza bajeti yake. Bajeti ya Tume imeendelea kuwa ndogo kiasi cha kuathiri ufanisi katika utekelezaji wa mipango yake, kwani kiasi cha fedha kilichotengwa kwa mwaka wa fedha, shilingi 2,340,236,000 ambacho ni kidogo ikilinganishwa na mwaka uliopita shilingi 3,974,822,359 sawa na asilimia tisa.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Bajeti wa Mwaka wa Fedha 2015/16. Katika eneo hili Kamati iliainisha Mpango wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI nchini na Mipango ya Tume ya Kuratibu Udhubiti wa Dawa za Kulevya ili kuona kama mipango ya Tume hizo ina uwiano moja kwa moja na matakwa ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2016/17- 2020/2021. Kilichobainika ni kwamba mipango na vipaumbele vya Tume zote mbili ni vema, tatizo lipo kwenye kiasi kidogo cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa vipaumbele hivyo.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kudhibiti UKIMWI; Katika mwaka wa fedha 2015/2016 Tume ya Kudhibiti UKIMWI nchini (TACAIDS), ilitengewa jumla ya shilingi 9,131,509,000 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo shilingi 6,300,068,000 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 2,744,438,000 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hata hivyo hadi kufikia tarehe 31 Machi 2016, Tume ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 1,964,435,212 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, hii ikiwa ni pungufu ya shilingi 4,422,632,780 sawa na asilimia 30.7 ya kiasi chote kilichotengwa kwa ajili ya shughuli hiyo.

Aidha, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016 Tume ilipokea jumla ya shilingi 1,198,928,740, sawa na asilimia 43 kwa ajili ya shughuli za maendeleo, hii ikiwa ni pungufu ya shilingi 1,545,509,206 ya kiasi chote kilichotengwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kupewa fedha chini ya kilichoombwa Tume imelegalega katika utekelezaji wa majukumu yake. Kwa mfano, imeshindwa kusambaza kikamilifu miongozo ya kimkakati kama sheria, imeshindwa kuratibu vikao vya wadau, imeshindwa kufanya vikao vya kisheria na bodi na mifuko imekosa fedha kwa ajili ya kulipa stahili za Watumishi wanaotoa huduma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Kuratibu Udhubiti wa Dawa za Kulevya, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Tume ya Kuratibu Udhubiti wa Dawa za Kulevya ilitengewa kiasi cha shilingi 2,150,484,350 kwa ajili ya matumizi

mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi 2016, kiasi kilichopokelewa ni shilingi 777,188,000 ambayo ni sawa na asilimia 35. Aidha, fedha za mishahara zilizoidhinishwa ni shilingi 950,805,023, kiasi kilichopokelewa hadi kufikia mwezi Machi 2016 ni sawa na shilingi 471,473,010 sawa na 49%.

Mheshimiwa Spika, Kamati haijaridhishwa na mwenendo wa utoaji huu wa fedha kwani ikumbukwe kuwa dawa za kulevya ni janga la Taifa linalowaathiri zaidi vijana ambao ndiyo nguvukazi ya nchi yetu. Mwenendo huu wa utoaji wa fedha kidogo unachangia mapambano dhidi ya dawa za kulevya kuwa magumu zaidi na hivyo kuendelea kupoteza nguvukazi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, makadirio na matumizi mwaka 2016/2017. Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) vipaumbele; Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imeainisha maeneo yaliyopewa kipaumbele katika mpango wa bajeti kama ifuatavyo:-

Kuboresha utaratibu wa wadau wa UKIMWI na uendeshaji wa Afua VVU/ UKIMWI katika ngazi zote, kuboresha ushiriki wa Sekta Binafsi ili kuleta ufanisi katika kuchangia mwitikio wa Taifa dhidi ya UKIMWI, kuboresha upatikanaji wa taarifa za mikakati ya VVU ili kusaidia kufanya maamuzi sahihi, kutafuta rasilimali fedha ndani kwa ajili ya ugharamiaji wa programu ya UKIMWI na kuimarishwa kwa uwezo wa ufanisi wa Tume katika kusimamia utaratibu na mwitikio dhidi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania inaomba jumla ya shilingi 10,949,681,193 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake, kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi 5,385,974,601 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 5,553,706,582 ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhika na mpangilio wa vipaumbele vya Tume japokuwa kilichoombwa kwa kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele hivyo, wimbo wa ufinyu wa bajeti umekuwa ukiimbwa kila mwaka, haijulikani utaisha lini.

Mheshimiwa Spika, Tume imekuwa ikijitahidi katika kutoa huduma zilizo chini ya mamlaka yake, hata hivyo kiasi cha fedha kinachotengwa na kutolewa ni kidogo sana ikilinganishwa na kiasi cha uzito na majukumu yake. Kwa mfano katika mwaka wa fedha 2015/16, kati ya shilingi bilioni 9.8 zilizokuwa zimetengwa, shilingi 3,163,363,132 sawa na asilimia 33 zilikuwa zimetolewa hadi kufikia Machi 2016. Hali hii huathiri kiasi kikubwa cha utekelezaji wa majukumu ya Tume na morali ya Watumishi kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawa za Kulevya; vipaumbele vya Bajeti. Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imeainisha maeneo yaliyopewa kipaumbele katika mpango wa bajeti kama ifuatavyo:-

Kukamilisha mchakato wa kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti/Kupambana na Dawa za Kulevya, kutoa elimu kwa Umma juu ya athari zinazopatikana na biashara na matumizi ya dawa za kulevya, kuendelea kuwawezesha kikosikazi cha kupambana na dawa za kulevya chini ya ushiriki wa operesheni ya dawa za kulevya, kuendelea kuboresha Kanuni na Sheria na mapambano ya dawa za kulevya, kufuatilia kwa karibu kesi zinazohusiana na dawa za kulevya, kuandaa rasimu ya mpango mkakati wa Sera za Taifa kudhibiti dawa za kulevya, kudumisha ushirikiano wa nchi nyingine katika mapambano ya dawa za kulevya, kuwezesha Asasi za Kiraia zinazojihusisha na mapambano dhidi ya dawa za kulevya, kufuatailia kwa karibu kazi za udhibiti wa dawa za kulevya zinanzofanywa na Kamati ya Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya, kuandaa na kuwasilisha Bungeni taarifa ya hali ya dawa za kulevya nchini mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya bajeti; Katika mwaka huu wa fedha 2016/17, Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawa za Kulevya inaomba jumla ya shilingi 2,342,086,000 kati ya fedha hizo shilingi 610,790,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na 1,729,487,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Tume imetengewa kiasi cha shilingi 2,340,286,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida tu, hapatakuwa na shughuli ya maendeleo. Kiasi kilichotengwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni kidogo kuliko kiasi kilichotengwa mwaka uliopita shilingi 3,978,350,000, imepungua kwa asilimia 59.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhishwa na vipaumbele na malengo yaliyowekwa na Tume zote mbili kwa kuwa yanaendana na Mpango wa Taifa wa mwaka 2016/2017 na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017 hadi 2020/2021. Hata hivyo, swali ambalo Kamati inajjuliza ni kuhusiana na kupungua kwa bajeti katika masuala ya dawa za kulevya, na je, matumizi ya dawa za kulevya nchini kwa sasa yamepungua kuliko ilivyokuwa mwaka jana au athari zake kwa mwaka ujao ni kubwa kuliko zilizokuwepo mwaka uliopita.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati. Sehemu ya kwanza ya taarifa hii ilibainisha namna shughuli za Kamati zilivyotajwa katika

Nyongeza ya Nane ya Kamati za Kudumu ya Bunge zilivyotekelezwa, Sehemu ya Pili inabainisha masuala yaliyobainika katika utekelezaji wa shughuli hizo, kimsingi shughuli kubwa ya uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya nchini. Katika Sehemu hii ya Tatu naomba kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kamati imebaini kuwa fedha zinazotengwa na kutolewa na Serikali kwa ajili ya TACAIDS na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya ni kidogo, wakati tatizo la UKIMWI na dawa za kulevya nchini bado ni kubwa, Kamati inashawishi Bunge kuitaka Serikali kuipatia fedha TACAIDS na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa wakati na kwa kiasi kitakachokuwa kimeidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa MSD ina uhaba mkubwa wa fedha kuna uwezekano wa kushindwa kupakua mizigo ya dawa kutoka bandarini kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI na kwa kuwa MSD inaidai Serikali kiasi cha shilingi bilioni 130, pamoja na shughuli zingine zingesaidia shirika kutoa mizigo bandarini. Kamati inatoa ushauri kwa Serikali kulipa deni hilo la MSD ili iweze kutekeleza shughuli zake ikiwa ni pamoja na usambazaji wa dawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika, kutokana na UKIMWI na dawa za kulevya kuwa na athari mbaya kwa Taifa na ili kulinda mustakabali wa Taifa, Kamati inatoa ushauri kwamba makongamano na semina mbalimbali ikiwa ni pamoja na mikutano kuzungumzia masuala haya, hii ni njia ya kuelimisha watu na kuwakumbusha baadhi ya walioelewa kuhusu masuala hayo. Aidha Kamati inashauri kuwa shughuli zisizo za ulazima kufanyika nyakati za usiku zifanyike mchana ili kupunguza kuwepo kwa vitendo vya matumizi ya dawa za kulevya na ngono zembe zinazochangia na maambukizi ya UKIMWI. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchache wa ajira kupelekea vijana wengi kujiingiza katika tabia hatarishi kama utumiaji wa dawa za kulevya na vitendo vingine vinavyoweza kuchangia maambukizi ya UKIMWI, Kamati inashauri Serikali ifufue viwanda vilivyokufa ili viweze kuongeza ajira kwa vijana kuwalinda na kujiingiza katika tabia hatarishi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na baadhi ya Mikoa na Halmashauri kushindwa kusimamia utekelezaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) katika maeneo ambayo yanajishughulisha na UKIMWI au dawa za kulevya, Kamati inashauri Serikali kubuni utaratibu wa kusimamia matumizi mazuri ya fedha zinazotumwa moja kwa moja kwenye mashirika hayo ikiwa ni pamoja na kubaini kiasi cha fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga kiasi cha shilingi bilioni sita, kwa ajili ya Mfuko wa Taifa wa Kupambana na UKIMWI (*AIDS Trust Fund*) kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kwa maana hiyo kutekeleza agizo muhimu la Kamati ya Bunge kwa ujumla wake. Hata hivyo, Mfuko huu ulioanzishwa kwa Sheria iliyorekebisha na Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI bado haijawa na Kanuni ya kuendelea na Mfuko huo. Kamati inasisitiza kuwa Serikali ifanye kila linalowezekana kuhakikisha kuwa Kanuni hizi zinatungwa na mfumo wake uanze kufanya kazi iliyokusudiwa. Aidha, fedha hizi zilizotengwa bado ni kidogo ikilinganishwa na ukubwa wa tatizo, hivyo Kamati inashauri Serikali ibuni vyanzo vingine vya mapato kutunisha mfuko huu ambao ni muhimu kwa mustakabali wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mfuko wa Taifa wa Kupambana na UKIMWI bado hauna fedha za kutosha kupambana na janga hili Kamati inaishauri Serikali kushirikiana na taasisi na Mashirika yasioyo ya Kiserikali na watu binafsi kuchangia Mfuko wa Mapambano Dhidi ya UKIMWI (*AIDS Trust Fund*) kwa lengo la kutunisha Mfuko huu kupambana na UKIMWI na hivyo kupunguza maambukizi mapya. Aidha, katika utumiaji wa rasilimali itakayopatikana kuwepo na vigezo maalum vitakavyotumika katika kugawanya rasilimali hizo zinazotokana na wafadhili wanaoshughulikia masuala ya UKIMWI na kutoa vipaumbele katika maeneo ya maambukizi zaidi.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazopelekwa katika Halmashauri kwa ajili ya kupambana na UKIMWI zimekuwa hazitumiki kama ilivyokusudiwa, hivyo Kamati inashauri kwamba uwepo ufuatiliaji kutoka Wizara ya Afya kwa kushirikiana na TAMISEMI kuhakikisha fedha hizi zinatumika kama ilivyopagwa, Halmashauri zozote zitakazobainika kutumia fedha hizo vibaya zichukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutokutolewa mkazo elimu ya UKIMWI na dawa za kulevya kwenye mitaala ya elimu ya msingi na sekondari, Kamati inaishauri Serikali kuwa ni vema sasa elimu hii ikafundishwa katika shule zote nchini kuanzia msingi, sekondari hadi vyuo, vilevile vilabu vya kuhamasisha mapambano dhidi ya UKIMWI viwepo katika shule zote nchini.

Mheshimiwa Spika, suala la kupima afya ni jema ili kubaini afya yako na hivyo kuchukua hatua mara moja iwapo utabainika na tatizo. Kwa kuzingatia ukweli huu Kamati inaona upo umuhimu wa Serikali kuwashawishi wananchi, watumishi wake ikiwemo kwa Waheshimiwa Wabunge kujenga tabia ya kupima afya zao, ikiwa pamoja na UKIMWI na magonjwa sugu yasioyoambukiza ili kuchukua hatua mapema iwapo watabainika kuwa na tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, UKIMWI ni janga la Taifa ambapo nguvukazi itapotea na uchumi wa Taifa utashuka kama Taifa litakuwa na idadi kubwa ya watu wanaougua UKIMWI. Kwa kuwa ongezeko la maambukizi kwa vijana na wanawake, watoto na watu wa makundi maalum, aidha watu wanaoishi na VVU wanaosubiri kupata dawa za kufubaza makali ya virusi (ARVs) ni wengi na kwa bahati mbaya fedha za kununulia dawa kwa asilimia 100 zinatoka kwa wafadhili ambazo pia hazitoshi kukidhi haja ya watu wote wanaohitaji dawa hizo, Kamati inaishauri Serikali kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo katika vita hii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matumizi ya dawa za kulevya kuchangia ongezeko la maambukizi ya UKIMWI, Kamati inashauri kwamba ni vema Asasi Zisizo za Kiserikali (NGOs) zinazojishughulisha na dawa za kulevya na VVU badala ya kujikita kwenye maambukizi ya UKIMWI pekee, zijishughulishe pia na masuala ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi yetu imekuwa ikitajwa kama kituo kikuu cha kupitisha dawa za kulevya, Kamati inaiagiza Serikali kuweka mbwa wa kunusa katika viwanja vya ndege, mashine za X ray kwa ajili ya kukagua watu waliomeza vidonge kwenye viwanja vya ndege, bandari mipakani, boti za kufanya doria katika fukwe zetu, kuwaongezea fedha askari waweze kufanya ulinzi. Aidha, kuwepo na mikakati madhubuti ya upekuzi wa magari, vipuri na mizigo inayoingia nchini kutoka nje ya nchi kupitia kwenye bandari na viwanja vya ndege, kwa kuwa baadhi ya waingizaji wa biashara hiyo haramu wanatuminja mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kuwa wananchi wakihakikishiwa usalama wao na kupewa motisha watakuwa tayari kutoa ushirikiano na vyombo vya dola, bila kuhakikisha usalama siyo rahisi kuwataja wauza dawa za kulevya kwani ni watu wenye fedha nyingi ambao mara nyingi jamii imekuwa ikiwaogopa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ongezeko kubwa la vijana wanaojijua na kutumia dawa za kulevya, hali ambayo imehatarisha mustakabali wa maisha ya vijana wetu. Kamati inaishauri Serikali itoe semina elimishi mara kwa mara kwa makundi hatarishi ambayo ni *sex workers, injection drug users (IDU), men sex to men*, ili kupunguza au kuondoa ongezeko la maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI. Aidha, elimu itolewe na maeneo ambayo pia ni hatarishi kama vile maeneo ya migodi, barabara kuu za nchi na vituo vikubwa vya stesheni na reli.

Mheshimiwa Spika, kituo cha kuhifadhia dawa za kulevya kinakabiliwa na changamoto ya upungufu wa fedha kujenga ghala kubwa la kisasa lenye vifaa vya utaalum na viyoyoz, makabati na milango.

Aidha, kukosekana kwa vifaa kama magari ya kuwafanya askari kushindwa kufika kwa wakati kwenye matukio ya ukamataji. Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele kwa kutenga bajeti ya kutosha itakayowawezesha kununua vifaa na kufanikisha azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji wa Kamati wa dawa hizo, aidha kitengo kinahitaji chombo maalum cha kuchomea dawa za kulevya. Kamati inaishauri Serikali kununua chombo hicho ili kurahisisha utekelezaji wa uteketezaji wa dawa bila kusababisha madhara kwa wateketezaji na jamii inayozunguka.

Mheshimiwa Spika, kesi za dawa za kulevya zimekuwa zikichukua muda mrefu sana kumalizika, japokuwa wakati mwingine ushahidi huwa bayana. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha usikilizwaji wa kesi za dawa za kulevya uishe haraka na hatua zichukuliwe kwa wahusika kwa kuwa zinapochelewa kumalizika kunakuwepo na wingi wa dawa za kulevya zilizohifadhiwa katika ghala na kusababisha hatari ya kiafya kwa watumishi katika kituo kutokana na kemikali zinazotumika kutengenezewa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vituo vya kutolea matibabu ya *methadone* vipo vinne tu hapa nchini, Muhimbili, Mwananyamala, Temeke na Zanzibar na kwa maana hiyo siyo rahisi kuwafikia waathirika wote nchini, Kamati inaishauri Serikali kuongeza vituo vya matibabu *methadone*, angalau kituo kimoja katika kila Mkoa ili huduma hii iwafikie wananchi kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inatumia rasilimali kupambana na dawa za kulevya na pia katika kuwahudumia waathirika, Kamati inaishauri Serikali iwashughulikie bila aibu na wala urafiki wowote wanaojishughulisha na kuingiza dawa za kulevya haramu hapa nchini ambayo yameathiri Watanzania wengi kuanzia watoto hadi watu wazima. Kwa kutokuchukua hatua nchi yetu itajaa mazezeta na hivyo uzalishaji wa mali hautakuwa na ufanisi na wategemezi watakuwa wengi kutokana na athari za dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la dawa za kulevya kwa Tanzania ni tishio kubwa kwa vizazi vilivyopo na vijavyo, suala linalohitaji nguvu ya Wabunge katika kulisemea jambo hili katika Majimbo yao, Kamati inaishauri Serikali itoe semina kwa Wabunge wote ili wajue ukubwa wa tatizo la dawa za kulevya na hivyo kuwa na sauti moja na namna ya kukabiliana na janga hili Tanzania.
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, hitimisho, kwa dhati ya moyo napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo bila kuchoka na napenda kuwatambua kwa majina kama yalivyoorodheshwa kwenye kitabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa utendaji wako mzuri na kuliongoza ipasavyo Bunge hili kuwa Bunge mahiri, umekuwa mtu wa busara sana wakati wote wa uongozi wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu, Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Naibu wake Dkt. Abdallah Possi kwa kutoa ufafanuzi mzuri katika uchambuzi wa bajeti hii lakini pia kutoa ushirikiano mzuri kipindi chote cha utendaji wa Kamati.

Aidha napenda kuwashukuru watendaji wote wa Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Tume ya Kudhibiti UKIMWI na uongozi wa Dkt. Hamisi Mwinyimvua, Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah kwa ushirikiano ambao amekuwa akiipa Kamati, pamoja na yeye namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati yetu, Ndugu Athumani Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi wa Kamati pamoja na Makatibu wetu.

Mheshimiwa Spika, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio na mapato ya matumizi ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya - Fungu 91 kiasi cha shilingi 2,340,236,000 na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - Fungu 92 kiasi cha shilingi 10,949,681,193.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU (TUME YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA NA TUME YA KUDHIBITI UKIMWI (TACAIDS) KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Bajeti ya Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawa za Kulevywa – Fungu 91 na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) – Fungu 92 kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa Tume hizo mbili.

1.2 Mheshimiwa Spika, maoni yatakayotolewa katika Taarifa ni kutokana na majukumu ya Kamati kama yanavyobainishwa katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2016. Majukumu ya Kamati yalitekelezwa kwa njia ya vikao na ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo katika maeneo mbalimbali.

1.3 Aidha, mtiririko wa Taarifa umezingatia maeneo makubwa manne (4) yafuatayo: -

- (a) Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati kwa kipindi kilichopita.
- (b) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.
- (c) Makadirio ya Mapato na Matumizi (2016/2017).
- (i) Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawa za Kulevywa.
- (ii) Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS).
- (d) Maoni na Ushauri wa Kamati.

1.4 Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza (Utangulizi) imeeleza mtiririko wa Taarifa utakavyokuwa. Sehemu ya Pili itabainisha masuala muhimu yaliyojitokeza kwa kila kipengele kilichopo katika 1.3 hapo juu.

SEHEMU YA PILI

2.0 MASUALA MUHIMU YALIYOBAINIKA (FINDINGS)

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo awali katika kipengele 1.3, Sehemu hii inaeleza mambo muhimu yaliyobainika katika utekelezaji wa shughuli za Kamati. Kutokana na mambo hayo, Kamati inatoa Maoni na Mapendekezo yatakayotolewa katika Sehemu ya Tatu.

2.1 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Kamati ilitoa maoni sita (6) kwa ajili ya kutekelezwa na Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawu za Kulevya kuhusiana na bajeti yake.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Tume imetekeleza vizuri maoni matano (5), kasoro moja (1) linalohusu kuongeza bajeti yake. Bajeti ya Tume imeendelea kuwa ndogo kiasi cha kuathiri ufanisi katika utekelezaji wa mipango yake, kwani kiasi cha fedha kilichotengwa kwa mwaka huu TShs. **2,340,236.000/= (bilioni mbili, milioni mia tatu na arobaini, laki mbili thelathini na sita)** ambacho ni kidogo ikilinganishwa na mwaka uliopita TShs. **3,974,822,359./= (bilioni tatu, milioni mia tisa sabini na nne, laki nane ishirini na mbili na mia tatu hamsini na tisa) sawa na asilimia hamsini na tisa.**

2.2 Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili, Kamati kuianisha Mipango ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI nchini na Mipango ya Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawu za Kulevya ili kuona kama mipango ya Tume hizo ina uwiano wa moja kwa moja na matakwa ya Mpango wa maendeleo wa Taifa (2016/2017- 2020/2021). Kilichobainika ni kwamba mipango na vipa umbele vya Tume zote mbili viko vema. Tatizo lipo kwenye kiasi kidogo cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mipango na vipaumbele hivyo. Kwa mfano:

a) Tume ya Kudhibiti UKIMWI

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Nchini (TACAIDS), ilitengewa jumla ya shilingi **9,131,506,000/=(bilioni tisa ,milioni mia moja na thelathini na moja laki tano na tisa)** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, shilingi **6,387,068,000/=(bilioni sita, milioni mia tatu na elfu sitini na nane)** zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **2,744,438,000/=(bilioni mbili, milioni mia saba na arobaini na nne,laki nne na thelathini na nane elfu)** zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016, Tume ilikuwa imepokea jumla ya shilingi **1,964,435,212/=(bilioni moja, milioni mia tisa sitini na nne, laki nne thelathini na tano na mia mbili kumi na mbili)** kwa ajili ya matumizi ya kawaida, hii ikiwa ni pungufu ya shilingi **4,422,632,788/=(billioni nne,milioni mia nne ishirini na mbili na laki sita thelathini na mbili , mia saba themanini na nane)** sawa na asilimia **30.7%** ya kiasi chote kilichotengwa kwa ajili hiyo. Aidha, hadi

kufikia tarehe 31 Machi, 2016 Tume ilipokea jumla ya shilingi **1,198,928,740/= (bilioni moja, milioni mia moja na tisini na nane, laki tisa na ishirini na nane na mia saba arobaini)** sawa na asilimia **43.7%** kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Hii ikiwa ni pungufu ya shilingi **1,545,509,206/=(bilioni moja, milioni mia tano na arobaini na tano,laki tano na tisa, mia mbili na sita)** ya kiasi chote kilichotengwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kupewa fedha chini ya kiasi kilichoombwa, Tume imelegalega katika utekelezaji wa majukumu yake. Kwa mfano, imeshindwa kusambaza kikamilifu miongozo ya kimkakati kama sheria, imeshindwa kuratibu vikao na wadau, imeshindwa kufanya vikao vya kisheria vya Kamisheni na Bodi ya Mfuko na imekosa fedha za kulipa stahili za watumishi na watoa huduma.

b) Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya ilitengewa kiasi cha shilingi **2,159,488,359/=(bilioni mbili,milioni mia moja na hamsini laki nne na elfu themanini na nane na mia tatu na hamsini na tisa)** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016, kiasi kilichopokelewa ni shilingi **771,407,188/=(milioni mia saba sabini na saba na moja na mia moja themanini na nane)** ambayo ni sawa na **35.7%**. Aidha, fedha za mishahara zilizoidhinishwa ni shilingi **954,523,000/=(milioni mia tisa hamsini na nne na laki tano na ishirini na tatu)** na kiasi kilichopokelewa hadi kufikia mwezi Machi, 2016 ni shilingi **471,473,010.00**, sawa na **49.4%**.

Mheshimiwa Spika, Kamati haijaridhishwa kabisa na mwenendo wa utoaji huu wa fedha kwani ikumbukwe kuwa dawa za kulevya ni Janga la Taifa linaloathiri zaidi vijana ambao ndiyo nguvu kazi katika nchi yetu. Mwenendo huu wa utengaji na utoaji wa fedha kidogo unachangia mapambano dhidi ya dawa za kulevya kuwa magumu zaidi na hivyo kuendelea kupoteza nguvu kazi ya Taifa.

2.2.1 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI (2016/2017)

2.2.2.1 Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS)

a) Vipaumbele vya Bajeti katika Tume

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 imeainisha maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Mpango wa Bajeti kama ifuatavyo:-

- i) Kuboresha uratibu wa Wadau wa UKIMWI na uendeshaji wa Afua za VVU/UKIMWI katika ngazi zote.
- ii) Kuboresha ushiriki wa Sekta Binafsi ili kuleta ufanisi katika kuchangia mweitikio wa Taifa dhidi ya UKIMWI.
- iii) Kuboresha upatikanaji wa taarifa za mkakati wa VVU/UKIMWI ili kusaidia kufanya maamuzi sahihi.
- iv) Kutafuta rasilimali fedha kutoka ndani kwa ajili ya ugharimiaji wa Programu za UKIMWI nchini.
- v) Kuimarishwa kwa uwezo na ufanisi wa Tume katika kusimamia uratibu wa mweitikio wa Taifa dhidi ya UKIMWI.

b) Mapitio ya Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania inaomba jumla ya shilingi **10,949,681,193/=(bilioni kumi, milioni mia tisa arobaini na tisa, mia sita themanini na moja na mia moja na tisini na tatu)** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi **5,395,974,601/=(bilioni tano, milioni mia tatu na thelathini na tano, laki tisa na sabini na nne na mia sita na moja)** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **5,553,706,582/=(bilioni tano, milioni mia tano na hamsini na tatu, laki saba na sita mia tano na themanini na mbili)** kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhika na mpangilio wa vipaumbele vya Tume japokuwa kilichoombwa na kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele hivyo. Wimbo wa ufinyu wa Bajeti umekuwa ukiimbwa kila mwaka. Haijulikani utahitimishwa lini.

Mheshimiwa Spika, Tume imekuwa ikijitahidi katika kutoa huduma zilizo chini ya mamlaka yake. Hata hivyo, kiasi cha fedha kinachotengwa na kutolewa ni kidogo sana, kikilinganishwa na kiasi na uzito wa majukumu yake. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2015/2016, kati ya shilingi **bilioni 9.8** zilizokuwa zimetengwa ni shilingi bilioni **3,163,363,952/=(bilioni tatu, milioni mia moja na sitini na tatu, laki tatu na sitini na tatu na mia moja na hamsini na mbili)** sawa na asilimia 33.% tu zilizokuwa zimetolewa hadi kufikia Machi, 2016.

Hali hii huathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa majukumu ya Tume na morali ya Watumishi wa Tume kutekeleza majukumu yao.

2.2.1.2 Tume ya Kuratibu Udhubiti wa Dawu za Kulevya

a) Vipaumbele vya Bajeti

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kuratibu Udhubiti wa Dawu za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 imeainisha maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Mpango wa Bajeti kama ifuatavyo:-

- i. Kukamilisha mchakato wa kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawu za Kulevya.
- ii. Kutoa elimu kwa Umma juu ya athari mbalimbali zitokanazo na biashara na matumizi ya dawu za kulevya.
- iii. Kuendelea kuwawezesha Kikosi Kazi cha Taifa cha Kupambana na Dawu za Kulevya nchini na kushiriki katika Operesheni ya Dawu za Kulevya.
- iv. Kuendelea kuboresha kanuni na sheria mpya katika mapambano ya dawu za kulevya.
- v. Kufuatilia kwa karibu kesi zinazohusiana na dawu za kulevya.
- vi. Kunda Rasimu ya Mpango Mkakati wa Sera ya Taifa ya Kudhibiti Dawu za Kulevya.
- vii. Kudumisha ushirikiano na nchi nyingine katika mapambano ya dawu za kulevya.
- viii. Kuwawezesha asasi za kiraia zinazojihusisha na mapambano dhidi ya dawu za kulevya.
- ix. Kufuatilia kwa ukaribu kazi za udhibiti wa dawu za kulevya zinazofanywa na Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya.
- x. Kuandaa na kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Hali ya Dawu za Kulevya Nchini ya Mwaka 2015.

b) Mapitio ya Bajeti ya Tume ya Kuratibu Udhubiti wa Dawu za Kulevya

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka huu wa Fedha wa 2016/2017, Tume ya Kuratibu Udhubiti wa Dawu za Kulevya inaomba jumla ya Shilingi **2,340,236/=(bilioni mbili, milioni mia tatu na arobaini na mia mbili na thelathini na sita)** Kati ya fedha hizo, Shilingi **610,799,000/=(milioni mia sita na kumi,laki saba na tisini na tisa)** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na Shilingi **1,729,**

437,000/=(bilioni moja, milioni mia saba na ishirini na tisa, laki nne na thelathini na saba) kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa fedha 2016/2017 Tume hii imetengewa kiasi cha shilingi **2,340,236,000/=(bilioni mbili,milioni mia tatu na arobaini,laki mbili na thelathini na sita)** kwa ajili ya matumizi ya kawaida tu! Hapatakuwa na shughuli za maendeleo. Kiasi kilichotengwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni kidogo kuliko kiasi kilichotengwa kwa mwaka uliopita Tsh.**3,974,359,000/=(bilioni tatu,milioni mia tisa na sabini nan ne, laki tatu na hamsini na tisa)** imepungua kwa asilimia **59%**.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhishwa na vipaumbele na malengo yaliyowekwa na Tume zote mbili kwa kuwa yanaandana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2016/2017 na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021). Hata hivyo, Swali ambalo Kamati inajiliza kuhusiana na kupungua kwa Bajeti katika masuala ya dawa za kulevya ni je, matumizi ya dawa za kulevya nchini kwa sasa yamepungua kuliko ilivyokuwa mwaka jana au athari zake kwa mwaka ujao ni kidogo kuliko zilizokuwepo mwaka uliopita?

SEHEMU YA TATU

4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza ya Taarifa hii ilibainisha namna shughuli za Kamati zilizotajwa katika Nyongeza ya Nane ya Kamati za Kudumu za Bunge zilivyotekelezwa. Sehemu ya Pili imebainisha masuala yaliyobainika katika utekelezaji wa shughuli hizo. Kimsingi shughuli kubwa ni uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawa za Kulevya Nchini.

Katika Sehemu hii ya Tatu,naomba kuwasilisha Maoni (Mapendekezo) ya Kamati kuhusiana na Masuala yote yaliyobainika kama ifuatavyo:

4.1 Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa Kamati imebaini kuwa fedha zinazotengwa na kutolewa na Serikali kwa ajili ya shughuli za TACAIDS na Tume Kudhibiti Dawa za Kulevya ni kidogo wakati tatizo na athari za UKIMWI na dawa za kulevya nchini bado ni kubwa, Kamati inalishawishi Bunge kuitaka Serikali kuipatia fedha TACAIDS na Tume ya kudhibiti Dawa za kulevya kwa wakati na kwa kiasi kinachokuwa kimeidhinishwa.

4.2 Mheshimiwa Spika,kwa kuwa MSD ina uhaba wa fedha na kuna uwezekano wa kushindwa kupakua mizigo ya dawa kutoka Bandarini kwa ajili

ya mapambano dhidi ya UKIMWI. Kwa kuwa MSD inaidai Serikali fedha nyingi kiasi cha sh. Bil. 1.13 fedha ambazo pamoja na shughuli nyingine zingelisaidia Shirika kutoa huduma kwa ukamilifu ikiwa ni pamoja na kutoa mizigo yake bandarini, Kamati inatoa ushauri kwa Serikali kulipa deni hilo ili MSD iweze kutekeleza shughuli zake ikiwa ni pamoja na usambazaji wa dawa na vifaa tiba.

4.3 Mheshimiwa Spika, kutokana na UKIMWI na Dawa za Kulevya kuwa na athari mbaya kwa Taifa na ili kulinda mustakabali wa Taifa, Kamati inatoa ushauri kwamba, makongamano na semina mbalimbali ikiwa ni pamoja na mikutano, kuzungumzia masuala haya hii ni njia ya kuwaelimisha watu na kuwakumbusha baadhi walio na uelewa kuhusu masuala hayo. Aidha Kamati inashauri kuwa, shughuli zisizo na ulazimaza kufanyika nyakati za usiku zifanyike mchana ili kupunguza kuwepo kwa vitendo vya matumizi ya dawa za kulevya na ngono zembe zinazochangia maambukizi ya VVU.

4.4 Mheshimiwa Spika, uchache wa ajira hupelekea vijana kujiingiza katika tabia hatarishi kama utumiaji wa dawa za kulevya na vitendo vingine vinavyoweza kuchangia maambukizi ya VVU/UKIMWI. Kamati inashauri kwamba, Serikali ifufue viwanda vilivyokufa ili viweze kuongeza ajira kwa vijana ili kuwalinda kujiingiza katika tabia hatarishi.

4.5 Mheshimiwa Spika, kutokana na baadhi ya Mikoa na Halmashauri kushindwa kusimamia utekelezaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) katika maeneo yao ambayo yanajishughulisha na UKIMWI au Dawa za Kulevya, Kamati inaishauri Serikali kubuni utaratibu wa kusimamia matumizi mazuri ya fedha zinazotumwa moja kwa moja kwenye Mashirika hayo ikiwa ni pamoja na kubaini kiasi cha fedha hizo.

4.6 Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga kiasi cha **shilingi bilioni 6** kwa ajili ya Mfuko wa Taifa wa Kupambana na UKIMWI (*Aids Trust Fund*) kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 na kwa maana hiyo kutekeleza agizo muhimu la Kamati na Bunge kwa ujumla wake. Hata hivyo, Mfuko huu ulioanzishwa kwa sheria iliyorekebisha Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI bado haijawa na kanuni za kuuendesha mfuko huo. Kamati inasisitiza kuwa Serikali ifanye kila linalowezekana kuhakikisha kuwa kanuni hizi zitanatungwa ili Mfuko uanze kufanya kazi iliyokusudiwa. Aidha, fedha hizi zilizotengwa bado ni kidogo ukilinganisha na ukubwa wa tatizo. Hivyo Kamati inashauri kwamba, serikali ibuni vyanzo vingine vya mapato ili kutunisha mfuko huu ambao ni muhimu kwa mustakabali wa Taifa.

4.7 Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mfuko wa Taifa wa Kupambana na UKIMWI hauna fedha za kutosha kupambana na Janga la UKIMWI, Kamati

inaishauri Serikali kushirikiana na Taasisi, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Watu Binafsi, kuchangia Mfuko wa Mapambano Dhidi ya UKIMWI (*AIDS Trust Fund*) kwa lengo la kutunisha Mfuko ili kupambana na UKIMWI na hivyo kupunguza maambukizi mapya ya VVU. Aidha, katika utumiaji wa rasilimali fedha itakayopatikana, kuwepo na vigezo maalum vitakavyotumika katika kugawanya rasilimali husika zinazotoka kwa wafadhili wanaoshughulikia masuala ya UKIMWI na kutoa vipaumbele kwenye maeneo yenye maambukizi zaidi.

4.8 Mheshimiwa Spika, fedha zinazopelekwa katika Halmashauri kwa ajili ya kupambana na UKIMWI zimekuwa hazitumiki kama zilivyopangwa. Hivyo, Kamati inashauri kwamba, uwepo ufuatiliaji kutoka Wizara ya Afya kwa kushirikiana na TAMISEMI ili kuhakikisha fedha hizi zinatumiwa kama ilivyopangwa. Halmashauri zozote zitakazobainika kutumia visivyo fedha hizo zichukuliwe hatua.

4.9 Mheshimiwa Spika, kutokana na kutofiliwa mkazo elimu kuhusu UKIMWI na dawa za kulevya kwenye mitala ya elimu ya msingi na sekondari, Kamati inaishauri Serikali kuwa ni vema sasa elimu hii ikafundishwa katika shule zote nchini kuanzia msingi, sekondari hadi vyuo vikuu. Vilevile vilabu vya kuhamasisha mapambano dhidi ya UKIMWI viwepo katika shule zote nchini.

4.10 Mheshimiwa Spika, suala la kupima afya ni jema ili kubaini afya yako na hivyo kuchukua hatua mara moja iwapo utabainika kuwa na tatizo. Kwa kuzingatia ukweli huu Kamati inaona upo umuhimu wa Serikali kuwashawishi wananchi, Watumishi wake ikiwemo na waheshimiwa wabunge kujenga tabia ya kupima afya zao ikiwa ni pamoja na UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza ili kuchukua hatua mapema ikiwa watabainika kuwa na tatizo.

4.11 Mheshimiwa Spika, UKIMWI ni Janga la Taifa ambapo nguvu kazi inapotea na Uchumi wa Taifa utashuka kama Taifa litakuwa na Idadi kubwa ya watu wanaougua UKIMWI. Kwa kuwa ongezeko la maambukizi kwa vijana, wanawake, watoto na watu wa Makundi Maalumu . Aidha, watu wanaoishi na VVU wanaosubiri kupata dawa za kufubaza makali ya virusi (ARVs) ni wengi na kwa bahati mbaya fedha za kununulia dawa kwa asilimia mia moja zinatoka kwa wafadhili ambazo pia hazitoshi kukidhi haja ya watu wote wanaohitaji dawa hizo. Kamati inaishauri Serikali kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo katika vita hii.

4.12 Mheshimiwa Spika, kutokana na matumizi ya dawa za kulevya kuchangia ongezeko la maambukizi ya VVU, inashauriwa kwamba, ni vema asasi za zisizo za kiserikali (NGOs) zikajihusisha kushughulikia madawa ya kulevya na VVU badala ya kujikita kwenye maambukizi ya VVU pekee.

4.13 Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi yetu imekuwa ikitajwa kama kituo kikuu cha kupitishia Dawa za Kulevya, Kamati inaiagiza Serikali kuweka mbwa wa kunusa katika viwanja vya ndege, mashine ya x ray kwa ajili ya kukagua watu waliomeza dawa za kulevya kwenye viwanja vya ndege, bandarini na kwenye mipakani, boti za kufanya doria katika bandari na fukwe zetu na kuwaongezea fedha askari waweze kufanya ulinzi. Aidha, kuwepo na mikakati madhubuti ya upekuzi wa magari, vipuri na mizigo inayoingia nchini kutoka nchi za nje kupitia kwenye bandari na viwanja vya ndege kwa kuwa baadhi ya waingizaji wa biashara hiyo haramu wanatumia mbinu mbalimbali.

4.14 Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kuwa Wananchi wakahakikishiwa usalama wao na kupewa motisha, watakuwa tayari kutoa ushirikiano kwa vyombo vya dola kwani bila kuhakikisha usalama siyo rahisi kuwataja wauzaji wa dawa za kulevya kwani ni watu wenye fedha nyingi ambao mara nyingi jamii imekuwa ikiwaogopa.

4.15 Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ongezeko kubwa la vijana wanaojiuza na kutumia madawa ya kulevya, hali ambayo inahatarisha mustakabali wa maisha ya vijana wetu. Kamati inaishauri Serikali itoe semina elimishi ya mara kwa mara kwa makundi hatarishi (*SW – Sex Workers, Injection Drug User – IDU, Men Sex to Men*) ili kupunguza au kuondoa ongezeko la maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI. Aidha, elimu itolewe kwa maeneo ambayo pia ni hatarishi kama vile maeneo ya migodi, barabara kuu za nchi na vituo vikubwa vya stesheni za reli.

4.16 Mheshimiwa Spika, Kituo cha Kuhifadhia Dawa za Kulevya kinakabiliwa na changamoto ya upungufu wa fedha za kujenga ghala kubwa la kisasa lenye vifaa vya kitaalam kama viyoyozi, makabati na milango. Aidha, kukosekana kwa vifaa kama magari kunawafanya askari kushindwa kufika kwa wakati kwenye matukio ya ukamataji. Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele kwa kutenga bajeti ya kutosha itakayowawezesha kununua vifaa mbalimbali na kufanikisha zoezi zima la ufuatiliaji na ukamataji wa dawa hizo. Aidha, Kitengo kinahitaji chombo maalum cha kuchomea dawa inapobidi kufanya hivyo. Kamati inaishauri Serikali kununua chombo hicho ili kurahisisha uteketezaji wa dawa bila kusababisha madhara kwa wateketezaji na jamii inayozunguka.

4.17 Mheshimiwa Spika, kesi za madawa ya kulevya zimekuwa zikichukua muda mrefu kumalizika ijapokuwa wakati mwingine ushahidi huwa bayana. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha usikilizwaji wa kesi za dawa za kulevya ziishe haraka na hatua zichukuliwe kwa wahusika kwa kuwa zinapochelewa kumalizika kunakuwepo na wingi wa dawa zilizohifadhiwa katika ghala na kusababisha hatari za kiafya kwa watumishi wa kituo hicho kutokana na kemikali zinazotumika kutengenezea.

4.18 Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vituo vya kutolea matibabu ya *methodane* vipo vinne tu hapa nchini; Muhimbili, Mwananyamala, Temeke na Zanzibar, na kwa maana hiyo siyo rahisi kuwafikia waathirika wote waliopo nchini; Kamati inaishauri Serikali kuongeza vituo vya matibabu ya *methodane* angalau kituo kimoja kwa kila mkoa ili huduma hii iwafikie Wananchi wengi zaidi.

4.19 Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inatumia rasilimali nyingi kupambana na Madawa ya Kulevya na pia katika kuwahudumia waathirika, Kamati inashauri kwamba, Serikali iwashughulikie bila aibu wala urafiki na wale wote wanaojihusisha na uingizaji wa biashara haramu ya dawa za kulevya hapa nchini ambayo yamewaathiri Watanzania wengi kuanzia watoto hadi watu wazima. Kwa kutochukua hatua, hii nchi yetu itajaa mazezeta na hivyo uzalishaji mali hautakuwa na ufanisi na wategemezi watakuwa wengi sana kutokana na athari ya dawa hizi.

4.20 Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la dawa za kulevya kwa Tanzania ni tishio kubwa kwa vizazi vilivyopo na vijavyo, suala linalohitaji nguvu ya Wabunge katika kulisemea jambo hili katika Majimbo yao inahitajika kwa kiasi kikubwa. Kamati inaishauri Serikali itoe semina kwa Wabunge wote ili wajue ukubwa wa tatizo hili la Dawa za Kulevya na hivyo kuwa na sauti moja ya namna ya kukabiliana na janga hili nchini Tanzania.

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa dhati ya moyo wangu napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo bila ya kuchoka. Napenda kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Kanyasu Constantine John, Mb - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Muhammed Amour Muhammed, Mb - Mjumbe

- 4.Mhe. Juma Kombo Hamad, Mb - Mjumbe
- 5.Mhe. John Wegesa Heche, Mb - Mjumbe
- 6.Mhe. Mattar Ali Salum, Mb - Mjumbe
- 7.Mhe. Savelina S. Mwijage, Mb - Mjumbe
- 8.Mhe. Khalifa Mohammed Issa, Mb - Mjumbe
- 9.Mhe. Abdalla Haji Ali, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Rhoda Edward Kunchela, Mb - Mjumbe
- 11.Mhe. Sikudhani Yassin Chikambo, Mb - Mjumbe
- 12.Mhe. Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mb - Mjumbe
- 13.Mhe. Mgeni Jadi Kadika, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Richard Phillip Mbogo, Mb - Mjumbe
- 15.Mhe. Grace Victor Tendega, Mb -Mjumbe
16. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Elibariki Immanuel Kingu, Mb - Mjumbe
- 18.Mhe. John Peter Kadutu, Mb - Mjumbe
- 19.Mhe. Khamis Yahya Machano, Mb - Mjumbe
- 20.Mhe. Hussein Nassoro Amar, Mb - Mjumbe
- 21.Mhe. Vuma Hole Augustine, Mb - Mjumbe
- 22.Mhe. Waitara Mwita Mwikwabe, Mb - Mjumbe
- 23.Mhe. Azza Hillal Hamad, Mb - Mjumbe
- 24.Mhe. Zainayb Matitu Vulu, Mb - Mjumbe
- 25.Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa utendaji wako mzuri na kuliongoza ipasavyo Bunge hili lenye Wabunge mahiri. Umekuwa mtu wa busara sana wakati wote wa uongozi wako.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Mhe. Jenista J. Mhagama (Mb), pamoja na Naibu Waziri Mhe. Dkt. Possy Abdallah kwa kutoa ufafanuzi mzuri wakati wa uchambuzi wa Bajeti hii, lakini pia kutoa ushirikiano mzuri kipindi chote cha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawa za Kulevya na Tume ya Kudhibiti UKIMWI nchini ya Uongozi wa Katibu Mkuu Dkt. Hamisi Mwinyimvua.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, kwa ushirikiano ambao amekuwa akiipa Kamati. Pamoja na yeye, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athumani Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi, Makatibu wa Kamati hii; Ndg. Asia Msangi, Ndg. Happiness Ndalu na Ndg. Susan Ngole pamoja na Msaidizi wao Ndg. Grace Mwenye, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na

kuhakikisha Taarifa hii inakamilika. Aidha, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, kwa ushirikiano wanaoipa Kamati katika majukumu yetu ya kila siku kama Wabunge na Wajumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawa za Kulevya (Fungu 91), kiasi cha Shilingi **2,340,236,000 (bilioni mbili, milioni mia tatu na arobaini, laki mbili na thelathini sita elfu)** na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (Fungu 92) kiasi cha Shilingi **10,949,681,193/= (bilioni kumi, milioni mia moja na tisini na mbili, mia tatu sabini na sita elfu)**.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Hasna Sudi Katunda Mwilima (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI

22 Aprili, 2016

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kanyasu, Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI. Tunawapongeza sana kwa kazi nzuri ambayo mmekuwa mkiifanya kupitia Kamati hiyo. Lakini pia tunashukuru kwa ajili ya ushauri muhimu ambao mmetupatia. Waheshimiwa tumeshauriwa wote tupime, sijui kama wenzangu mlisikia. Siyo kupima uzito, hapana. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, limetokea jambo kidogo siyo la kawaida lakini tuvumiliane. Katika utaratibu wetu wa kawaida ilitakiwa sasa hivi afuate Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini jinsi ambavyo hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ilivyokuwa nzito, Kambi ya Upinzani imesambaratika mpaka ninavyoongea meza yangu haina nakala ya hotuba yao, yaani kwa kweli bado hawajajipanga kidogo. *(Kicheko/ Makofi)*

Kwa hiyo, kwa kuwa ndugu zetu kidogo leo wamebanwa pabaya na mimi ni rafiki kwao, basi tumesema tuwavumilie ndugu zangu ili wajipange pange mchana huu na nini. Basi hotuba yao itasomwa kuanzia saa kumi kamili jioni tutakaporudi, tunarudi saa kumi kamili jioni.

Pia nitoe wito hapa, kwa sababu tuko mwanzoni mwa shughuli zetu, kwa wale wote ambao asubuhi kabisa mnaweka mezani jambo fulani la Kibunge, basi muweke mezani kweli kweli kwa kuhakikisha wakati huo nakala za jambo

hilo anazo Katibu wa Bunge ili Wabunge waweze kugawiwa mapema waweze kupitia mapema.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo naomba nisisitize tena Kambi ya Upinzani saa kumi kamili tutaanza na hotuba yenu. Naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili jioni siku ya leo.

(Saa 06.43 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tuketi. Katibu!

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI: Hoja za Serikali kwamba Bunge likubari kuptia mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Majadiliano yanaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba tulipositisha shughuli za Bunge, tulikuwa bado kwenye Kanuni ya ya 96 (9). Wenyeviti ambao Kamati zao za Kisekta zilizopelekewa makadirio ya matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, waliwasilisha taarifa zao tukabaki na taarifa ya Kambi ya Upinzani. Kwa hiyo, sasa tunaendelea katika hatua hii kupokea taarifa ya Kambi ya Upinzani. Msemaji wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

MHE. FREEMAN A. MBOWE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa Hotuba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni, nikiwakilisha maoni na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusiana na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha katika Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba moja, Sheria ya Utekelezaji wa majukumu ya Mawaziri yaani *(Ministers Discharge of Ministerial Functions Act,*

1980). Kifungu cha 5(1) kinaweka masharti kwa Rais kutengeneza muongozo wa muundo na utekelezaji wa majukumu wa Serikali yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya kifungu hicho nilichokitaja inasomeka ifuatavyo na ninanukuu; *“The President shall, from time to time, by notice published in the Gazette, specify the departments, business and other matters and responsibility for which he has retained for himself or he has assigned under his direction to any Minister and may in that notice specify the effective date of the assumption of that responsibility...”* Mwisho wa kunukuu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa tunapoongea Serikali ya Awamu ya Tano inafanyakazi bila ya kuwa na mwongozo huo wa utendaji wake wa kazi kwa Wizara mbalimbali. Hii ina maana kwamba Serikali inafanyakazi kwa kauli za Rais na kauli za Mawaziri bila kufuata mwongozo wowote wenye msingi wa uhalali wa kisheria. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa mwongozo wa utendaji wa Serikali kwa kila Wizara yaani *instrument* unaotumika ni ule uliochapishwa kwenye Gazeti la Serikali namba 494(a) la tarehe 17/12/2010. Kwa mujibu wa *instrument* hiyo majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba nisome kwa mujibu wa *instrument*:-

- i. *Coordination of Government Business;*
- ii. *Leader of Government Business in the National Assembly;*
- iii. *Link between Political Parties and Government;*
- iv. *National Festivals and Celebration of Management of Civic Contingencies and relief;*
- v. *Facilitation and Implementation of Plans for the Development of Dodoma as Capital of Tanzania;*
- vi. *Coordination and Supervision of Transfer of the Government to Dodoma;*
- vii. *Government Press Services, Investment;*
- viii. *Economic Empowerment;*

- ix. *Public-Private-Partnership (PPP);*
- x. *Poverty alleviation Policies and their Implementation;*
- xi. *Facilitation of the Development of Informal Sector;*
- xii. *Performance Improvement and Development of Human Resources under this Office;*
- xiii. *Extra – Ministerial Department;Parastatal Organisations; Agencies; Programmes and Projects under this Office.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Regional Administration and Local Government ambayo chini yake kuna Decentralization by Devolution (D by D), Rural Development, Urban Development Policies and their Implementation, Regional Administration, Primary and Secondary Education Administration, Dar Rapid Transport – DART, Performance Improvement and Development of Human Resources under this Office, Extra-Ministerial Departments, Parastatal Organisations, Agencies, Programmes and Projects under this Office.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Serikali kuendesha kazi zake kwa mwongozo wa mwaka 2010, inamaanisha kwamba majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo bado ni yale yale yaliyochapishwa mwaka 2010 kwa sababu Gazeti hilo la Serikali halijafutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili, uvunjwaji wa Katiba na Sheria za nchi kuhusiana na bajeti unaofanywa na Serikali. Hili ni Bunge la Bajeti ambalo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, limepewa mamlaka ya kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti kwa madhumuni ya kujadili na kuidhinisha bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge hazikutosha kutekeleza majukumu ya Serikali kifungu 41(1) cha sheria ya Bunge ya mwaka 2015 kinaelekeza kwamba nanukuu: “Serikali itawasilisha Bungeni kwa idhini bajeti ya nyongeza ya fedha zilizotumika ambazo zimezidi kiwango kilichoidhinishwa na Bunge, au kwa madhumuni ya kugharamia mahitaji ambayo hayakupangwa.” Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu unatiliwa nguvu na Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001, *Public Finance Act of 2001* ambapo kifungu cha 18(3) na (4) kinaitaka Serikali kuleta Bungeni bajeti ya nyongeza yaani *mini-*

budget kwa ajili ya kupata idhini ya Bunge ikiwa fedha zilizoidhinishwa awali hazikutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huo wa kisheria umekuwa ukivunjwa na Serikali kwa kufanya matumizi ya fedha ambazo hazikuidhinishwa na Bunge, jambo ambalo linaua dhana ya madaraka ya Bunge ya kuisimamia na kuishauri Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuthibitisha jambo hili kwa mfano, Bajeti ya Maendeleo iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2015/2016; ilikuwa ni shilingi bilioni 883.8 ambapo kati ya fedha hizo, fedha za ndani ilikuwa shilingi bilioni 191.6. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza ni kwamba hadi kufikia mwezi Machi 2016, Wizara ilikuwa imeshapokea kutoka Hazina shilingi bilioni 607 ikiwa ni fedha za ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama takwimu utaona kuwa kunaongezeko la fedha zilizotolewa na Hazina hadi kufikia mwezi Machi 2016 ukilinganisha na fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Tangu kuidhinishwa kwa bajeti ya Wizara ya Ujenzi hakuna bajeti ya nyongeza iliyoletwa Bungeni na Serikali kwa ajili ya kupata idhini kutokana na matakwa ya sheria ya bajeti ya 2015 au Sheria ya Fedha ya mwaka 2015. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Serikali kuamua kufanya *reallocation* ya bajeti bila kupata idhini ya Bunge ni dharau kwa Bunge, lakini mbaya zaidi ni uvunjaji wa Katiba na Sheria. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, uhuru na madaraka ya mhimili wa Bunge. Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania inalitaja Bunge kuwa ndicho chombo kikuu katika Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri wa Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake. Katika hali isiyo ya kawaida, kifungu hiki cha Katiba kimevunjwa na badala yake Serikali imelipoka Bunge madaraka yake na Bunge kwa maana.... (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie hapo. Katika hali isiyo ya kawaida Kifungu hiki cha Katiba kimevunjwa na badala yake Serikali imelipoka Bunge madaraka yake na Bunge kwa maana ya Uongozi wake; narudia, Bunge kwa maana ya Uongozi wake wanaonekana kushiriki na kukubali kupokwa huku kwa madaraka na uhuru wake. (Makofi)

Bunge ni chombo cha uwakilishi cha wananchi, na wananchi wana haki ya kujua Bunge lao linavyofanya kazi ili wawe na uwezo wa kuwawajibisha wawakilishi wao iwapo hawafanyi kazi inavyostahili. Katika hali isiyo ya kawaida, Serikali na uongozi wa Bunge imewapoka wananchi haki yao ya kupata habari za Bunge kwa kuzuia mijadala Bungeni kurushwa moja kwa moja na Televisheni ya Taifa na vyombo vyingine vya habari vya kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili pia ni uvunjwaji wa Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, ambayo inasema kwamba kila mtu anaouhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake, anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake na anayo haki ya kupewa taarifa wakati wowote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii. *(Makofi)*

katika mazingira kama haya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haiko tayari kuendelea kushiriki uvunjaji wa Katiba na haki za msingi za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaushauri Uongozi wa Bunge, kutafuta na kupata ufumbuzi wa haraka wa kadhia hii, ili kurejesha heshima ya Bunge na haki za msingi za wananchi. Hivyo basi, Kambi Rasmi bado inatafakari kwa kina na makini sana hatua za kufuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

HOTUBA YA KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI (KUB) MHESHIMIWA FREEMAN AIKAEI MBOWE (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge,
Toleo la Januari, 2016*

1. SHERIA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MAWAZIRI (MINISTERS – DISCHARGE OF MINISTERIAL FUNCTIONS – ACT, 1980.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 5(1) kinaweka masharti kwa Rais kutengeneza mwongozo wa muundo na utekelezaji wa majukumu ya Serikali yake. Inasomeka ifuatavyo: Nanukuu **“the President shall from time to time by notice published in the Gazette, specify the departments, business and other matters and responsibility for which he has retained for himself or he has assigned under his direction to any minister and may in that notice specify the effective date of the assumption of that responsibility.....”**mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Serikali inafanya kazi bila kuwa na mwongozo wa utendaji wake na kazi kwa wizara mbalimbali. Hii ina maana kwamba Serikali inafanya kazi kwa kauli za Rais na Mawaziri bila kufuata mwongozo wowote wenye msingi na uhalali wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa mwongozo wa utendaji wa Serikali kwa kila Wizara (Instrument) unaotumika ni ule uliochapishwa kwenye gazeti la Serikali namba 494A la tarehe 17/12/2010. Kwa mujibu wa *Instrument* hiyo, majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni:

- (i) Coordination of Government Business
- (ii) Leader of Government Business in the National Assembly
- (iii) Link between Political Parties and Government.
- (iv) National Festivals and Celebration of Management of Civic Contingencies (relief).
- (v) Facilitation and Implementation of Plans for the Development of Dodoma as Capital of Tanzania.
- (vi) Coordination and Supervision of Transfer of the Government to Dodoma.
- (vii) Government Press Services.

- (viii) Investment, Economic Empowerment, Public-Private-Partnership (PPP), Poverty alleviation Policies and their Implementation.
- (ix) Facilitation of the Development of Informal Sector.
- (x) Performance Improvement and Development of Human Resources under this Office
- (xi) Extra – Ministerial Department, Parastatal Organisations, Agencies, Programmes and Projects under this Office.

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT:

- (xii) Decentralization by Devolution (D by D), Rural Development, Urban Development Policies and their Implementation.
- (xiii) Regional Administration.
- (xiv) Primary and Secondary Education Administration
- (xv) Dar Rapid Transit – DART.
- (xvi) Performance Improvement and Development of Human Resources under this Office.
- (xvii) Extra-Ministerial Departments, Parastatal Organisations, Agencies, Programmes and Projects under this Office.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali hii kuendesha kazi zake kwa Mwongozo wa 2010 ina maanisha kwamba majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu bado ni yale yale yaliyochapishwa mwaka 2010, kwa sababu gazeti hilo la Serikali halijafutwa.

2. UVUNJWAJI WA KATIBA NA SHERIA ZA NCHI KUHUSIANA NA BAJETI UNAOFANYWA NA SERIKALI

Mheshimiwa Spika, hili ni Bunge la Bajeti ambalo kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, limepewa mamlaka ya kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaaka wa Bajeti kwa madhumuni ya kujadili na kuidhinisha Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ikiwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge hazikutosha kutekeleza majukumu ya Serikali, kifungu cha 41(1) cha Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015 kinaelekeza kwamba: “ Serikali itawasilisha Bungeni kwa idhini, bajeti ya nyongeza ya fedha zilizotumika ambazo zimezidi kiwango kilichoidhinishwa na Bunge au kwa madhumuni ya kugharamia mahitaji ambayo hayakupangwa”.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu unatiliwa nguvu na Sheria ya Fedha za Umma wa mwaka 2001 (Public Finance Act, 2001) ambapo kifungu cha 18 (3)

na (4) kinaitaka Serikali kuleta Bungeni bajeti ya nyongeza (mini-budget) kwa ajili ya kupata idhini ya Bunge ikiwa fedha zilizoidhinishwa awali hazikutosha.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huo wa kisheria umekuwa ukivunjwa na Serikali kwa kufanya matumizi ya fedha ambazo hazikuidhinishwa na Bunge jambo ambalo linaua dhana ya madaraka ya Bunge ya kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili kuthibitisha jambo hilo, kwa mfano bajeti ya maendeleo iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2015/16 ilikuwa ni **shilingi bilioni 883.8** ambapo kati ya fedha hizo, fedha za ndani zilikuwa ni **shilingi bilioni 191.6**

Mheshimiwa Spika, Jambo la kushangaza ni kwamba hadi kufikia mwezi Machi 2016 Wizara ilikuwa imeshapokea kutoka hazina **shilingi bilioni 607.4** ikiwani fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, ukitazama takwimu hizo utaona kuwa kuna ongezeko la fedha zilizotolewa na hazina hadi kufikia mwezi Machi 2016 ukilinganisha na fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Tangu kuidhinishwa kwa bajeti ya Wizara ya Ujenzi, hakuna bajeti ya nyongeza iliyoletwa Bungeni na Serikali kwa ajili ya kupata idhini kutokana na matakwa ya Sheria ya Bajeti ya 2015 au sheria ya Fedha ya 2015.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali kuamua kufanya re-allocation ya bajeti bila kupata idhini ya Bunge ni dharau kwa bunge lakini mbaya zaidi ni uvunjaji wa Katiba na Sheria.

3. UHURU NA MADARAKA YA MHIMILI WA BUNGE

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalitaja Bunge kuwa ndicho chombo kikuu katika Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake. Katika hali isiyo ya kawaida, kifungu hiki cha Katiba kimevunjwa na badala yake Serikali imelipoka bunge madaraka yake na Bunge kwa maana ya uongozi wake wanaonekana kushiriki na kukubali kupokwa huku kwa madaraka na uhuru wake.

Mheshimiwa Spika, Bunge ni chombo cha uwakilishi wa wananchi, na wananchi wana haki ya kujua Bunge lao linavyofanya kazi ili wawe na uwezo wa kuwawajibisha wawakilishi wao iwapo hawafanyi kazi inavyostahili. Katika

hali isiyo ya kawaida, Serikali na uongozi wa Bunge, imewapoka wananchi haki yao ya kupata habari za Bunge kwa kuzuia mijadala Bungeni kurushwa moja kwa moja na televisheni ya Taifa na vyombo vingine vya habari vya kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, Jambo hili pia ni uvunjwaji wa ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo inasema kwamba kila mtu anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake; anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi; anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake na anayo haki ya kupewa taarifa wakati wowote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, katika Mazingira kama hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haiko tayari kuendelea kushiriki uvunjaji wa Katiba Sheria na haki za msingi za wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya Upinzani haitakuwa tayari kuwasilisha hotuba yake katika mazingira haya na inaushauri uongozi wa Bunge kupata ufumbuzi wa haraka wa kadhia hii ili kurejesha heshima ya Bunge na haki za msingi za wananchi. Hivyo basi Kambi bado inatafakari kwa kina na makini hatua za kufuata.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Freeman Aikaeli Mbowe (Mb)
**KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI NA
MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI
KATIKA OFISI YA WAZIRI MKUU**
22 Aprili, 2016.

MWENYEKITI: Tunashukuru. Kwanza nikupatie pole sana Mheshimiwa Mbowe kwa kupotelewa na kaka yetu mpenzi, tunamwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi.

Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo taarifa ya Kambi ya Upinzani ambayo mmeisikia wote ninyi wenyewe, inajaribu kutuondoa kwenye reli, maana hoja iliyo mbele yetu ni Bunge lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa mwaka wa fedha 2016/2017. (Makofi)

Taarifa za awali za Kamati za kisekta zimejielekeza katika hoja iliyo mbele yetu. Taarifa iliyowasilishwa na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni

imejielekeza kwingine kabisa na ina tuhuma nzito kidogo, kwa sababu imetumia maneno ambayo kwa nchi kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inaongozwa kwa misingi ya Katiba, Sheria, Kanuni na Taratibu, unaposema Katiba imevunjwa ni *allegation*, ni afadhali wangesema wanadai kwamba Katiba imevunjwa, wao wamesema Katiba imevunjwa na ndiyo maana mimi inaniwia vigumu sana kama Mwenyekiti kwa hoja hiyo. *(Makofi)* Pia mimi kama mwanasheria, masuala mazito kama haya tukianza kufanya tafsiri, kujichukulia majukumu ya kufanya tafsiri ya Katiba ya nchi na sheria, mimi nasema hatuko sahihi. Hatulitendei Bunge haki, tunatunga sheria lakini tunajua mipaka yetu, ukishatunga sheria kazi ya kutafsiri sheria na Katiba ya nchi siyo jukumu letu, sisi tunaweza tu kusaida. *(Makofi)*

Sasa kama Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wanaona hali ndiyo hiyo, ushauri wangu ni afadhali taratibu za kisheria zikafuatwa. Turuhusu shughuli ya hoja iliyo mbele yetu ziendelee kama zilivyowasilishwa, na wao wakipenda kushiriki washiriki maana ndiyo kazi iliyowaleta hapa Bungeni, yale mengine yataendelea kushughulikiwa kama wakiona kuna hoja za msingi za kufuatwa. Mimi sikuombwa nitoe mwongozo lakini kwa uzito wa wasilisho hilo nimeona niseme hayo niliyosema. *(Makofi)*

Tuna orodha ya wachangiaji hapa maana hoja hii sasa iko kwenu muiamue, lakini kabla ya kufika kwenye uamuzi wa mwisho, lazima tupate maoni na ushauri kutoka kwa Wabunge. Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(10), wakati wa kujadili makadirio ya Wizara, muda wa Wabunge kuchangia utatolewa kulingana na uwiano wa idadi ya Wabunge kutoka katika kila chama.

Sasa mimi hapa kama Mwenyekiti nazingatia orodha ambayo imeletwa mezani, ikitekeleza matakwa au sharti hilo la Kanuni ya 99, uwiano wa vyama vyetu. Kwa hiyo, msione kwamba nitakuwa nasoma, mkasema mbona anasoma wengi sana wa chama kimoja na wengine wawili au mmoja, hizo ndizo Kanuni.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa, mchangiaji wetu wa kwanza jioni hii ni Mheshimiwa Dkt. Diodorus Buberwa Kamala.

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hotuba muhimu iliyowasilishwa leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kutoa pongezi zangu za dhati kwa kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu

na Serikali kwa ujumla kwa kutekeleza kwa ufundi na ustadi mkubwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote ni mashahidi, yako mambo mengi ya kuthibitisha hilo, mambo mawili yanathibitisha jinsi Ilani inavyotekelezwa vizuri, Serikali imeweza kuongeza mapato kutoka bilioni 870 Novemba, 2015 hadi trilioni 1.3 kwa mwezi ilipofika Machi, 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali imeweza kuanza kutekeleza mkakati wa elimu bure hata kabla ya bajeti mpya ya 2016/17 haijawekwa, hiyo imewezekana tu kwa kubana matumizi, kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima, yakaelekezwa kwenye utekelezaji wa elimu bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa tunalojifunza baada ya kuanza kutekeleza elimu bure ni kwamba ukiangalia shule ya awali pamoja na darasa la kwanza uandikishaji wa wanafunzi wameongezeka zaidi ya asilimia 100. Kwa maneno mengine, wako Watanzania wengi walioshindwa kuanza shule ya awali, walioshindwa kuanza darasa la kwanza, kwa sababu ya gharama zisizokuwa na tija ambazo wazazi walikuwa wanalazimishwa kwamba lazima zilipwe hivyo kuna watoto walioshindwa kuendelea na shule, sasa baada ya kuanza kutekeleza elimu bure tunaona vijana wakiongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba wako wengi tuliowapoteza. Ni matarajio yangu katika Wizara inayohusika itakuja na mpango wa kuonesha ni jinsi gani wale tuliowapoteza Watanzania wengi tu ni kwa jinsi gani tutaweza kuwapa elimu ya msingi kwa sababu wao tayari wameshaikosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa ziara aliyofanya katika Jimbo langu la Nkenge, na pia kuweza kutembelea Wilaya ya Misenyi, kwa kweli niseme amekuwa Waziri Mkuu wa kwanza kutembelea kata ya Kakunyu katika Wilaya ya Misenyi, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika ziara ile alitoa maelekeza mbalimbali ambayo yatasaidia kumaliza mgogoro kati ya wakulima, wafugaji wazawa, na wawekezaji mbalimbali waliopewa *blocks* katika Ranchi ya Misenyi. Matarajio yangu ni kwamba maelekezo hayo yataweza kutusaidia kuondoa mgogoro uliodumu kwa zaidi ya miaka 15 na ningependa kuchukua nafasi hii kushauri baadhi ya mambo yakizingatiwa yatatusaidia kumaliza mgogoro huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo lazima lizingatiwe ni dhana na maneno ya watu ambao wamekuwa wakisema vijiji vilivyo ndani ya Kata Kakunyu, Kilimilile, Nsunga na Mtukula viliingilia maeneo ya Ranchi za Mabale pamoja na Misenyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji hivi vilikuwepo kabla ya Ranchi mbili za Mabale na Misenyi hazijaanzishwa. Kwa hiyo, wale wanaosema vijiji viliingilia maeneo ya ranchi kuanzia leo naomba waseme kwamba ni Ranchi za Mabale na Misenyi zilizoingilia maeneo ya vijiji kwa sababu vijiji vilikuwepo na vilishasajiliwa na vinatambulika Kiserikali na vina hati. Kwa kuwa vijiji ndivyo vilitangulia kuwepo kabla ya ranchi ni makosa na dharau kwa wananchi wa Misenyi kusema wameingilia ranchi wakati wao walikuwepo hata kabla ya ranchi haijakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nashauri lizingatiwe Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea kule na kutoa maelekezo, tunatarajia kwamba Mawaziri watayafanyia kazi na bado wanaendelea kuyafanyia kazi. Kabla hawajamaliza kuyafanyia kazi, wananchi wameshaanza kubugudhiwa, tarehe 17 mwezi uliopita na tarehe 18 mwezi huu, baadhi ya wananchi wamenyang'anywa majembe ili wasiendeleo na kilimo. Kufanya hivyo ni kuchelewesha kutekeleza sera ya Hapa Kazi tu! pia ni kutoheshimu maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo lazima lizingatiwe ili tupate ufumbuzi wa kudumu ni lazima Waziri wa Mifugo ashirikiane na Waziri wa Ardh, ashirikiane na Waziri wa Ulinzi na Waziri wa TAMISEMI; nina uhakika hawa wote wakishirikiana kwa pamoja na siyo kila mmoja anakwenda kwa wakati wake na kufanya yanayomhusu eneo lake, tutaweza kupata ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme na nisisitize kwamba kuna umuhimu ukiangalia mpango wa pili wa maendeleo wa miaka mitano ambao tunalenga kuutekeleza unabainisha kwamba tunahitaji trilioni 107 kuweza kuutekeleza, na kati ya hizo Serikali itatoa trilioni 59 na zilizobaki zitatolewa na *private sector*, hivyo, ukiangalia Mpango wa Pili tunaopanga kuutekeleza, sehemu kubwa ya fedha zitatokana na *private sector*. Sasa ili *private sector* waweze kufanya kazi lazima tuongeze nguvu za kujenga mazingira wezeshi kama ambavyo imebainishwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira wezeshi ni muhimu kwa sababu ndiyo yatawezesha *private sector* kuweza kuchangia vizuri katika utekelezaji wa

Mpango wetu. Nitaeleza mambo matatu muhimu kama mfano wa mambo muhimu ambayo yakifanywa na ambayo hayahitaji fedha za kigeni kuyafanya, lakini ukiyafanya unaweza kusaidia kuharakisha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kwa mfano, hivi sasa hapa Tanzania viwanda vinavyozalisha simenti vikitaka kuuza simenti yake ndani ya Afrika Mashariki vinalazimika kutafuta kibali kutoka kwa Mkemia Mkuu kabla hawajauza, lazima watoe asilimia 2.5 ya thamani ya simenti wanayouza. Ukifanya hivyo unakwamisha viwanda bila sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wananchi wa Mkoa wa Kagera wanapotumia sukari na wengine wa Kanda ya Ziwa na Watanzania wengine kila kilo ya sukari inakatwa kodi ya reli. Sasa mtu unajiuliza, kuna uhusiano gani kati ya sukari na kodi ya reli? Utaratibu huu unaongeza gharama ambazo hazina tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunaambiwa waliopo kwenye kilimo cha alizeti kama wataanzishiwa utaratibu wa kupata mbegu mpya wataweza kuongeza ajira kutoka milioni moja ya Watanzania wanaopata ajira hivi sasa hadi Watanzania milioni kumi, lakini ili kupata mbegu mpya waliopo kwenye sekta ya alizeti kwa Tanzania unahitaji miaka saba ili kuweza kupata kibali cha kupata hiyo mbegu mpya, wakati Uganda wanahitaji miezi sita tu ya kuweza kupata hiyo mbegu mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba naunga mkono hoja na naomba nimalizie kwa kuisitiza kwamba ili tuweze kujenga Tanzania yenye viwanda, lazima tuhakikishe tunaunga mkono zoezi la *Export Processing Zones* na tutafanya hivyo kwa kutenga maeneo na kuhakikisha maeneo ya wawekezaji yanapatikana siyo ya kutafutwa. Vilevile kule Nkenge kuna mpango mkubwa wa kujenga uwanja wa Kimataifa wa Mkajunguti natarajia kwenye bajeti hii zitatengwa fedha za kulipa fidia kama tulivyoahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kupitia Wizara ya Viwanda tunataka kuanzisha *Export Processing Zone* ya Kimataifa ili uwanja wa kimataifa wa Mkajunguti usiwe uwanja tu usiyokuwa na cha kusafirisha, vilevile tuwe na *Export Processing Zone*. Tukifanya hayo tunaweza kupiga hatua na kwenda kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho tuondoe utitiri wa ukiritimba katika kuratibu masuala mbalimbali. Kwa mfano, mwekezaji yeyote akitaka kuwekeza Tanzania lazima kabla hajaanza kufanya hivyo aende TBS kutafuta

kibali, lazima aende TFDA kutafuta kibali cha kitu kile kile, akitoka huko lazima aende kwa Mkemia Mkuu wa Serikali. Sasa ukiangalia yote haya yanaongeza ukiritimba usio kuwa wa lazima na kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyosema Tanzania ni ya 139 sasa ili tuweze kuboresha mazingira ya wawekezaji, lazima hatua za makusudi zichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Dokta. Anayefuata ni Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, akifuatiwa na Mheshimiwa Omary Ahmad Badwel.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunifanya kuwa mchangiaji wa pili kwa hotuba hii iliyotukuka ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ambayo imebeba maudhui ya Wizara zote, imesheheni mipango na mikakati madhubuti ambayo kama itatekelezwa hivi ambavyo imewekwa, kwa hakika itatutoa Watanzania hapa tulipo leo na kutufikisha kwenye maisha ya uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba hii nzuri, pia niwapongeze sana Wenyeviti wa Kamati zote mbili, ambao pia wameleta hotuba yao mbele ya Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika tu kwamba kwa bahati mbaya nilitarajia nipate mawazo mbadala, lakini yameshindikana, hata hivi nadhani tutakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikubaliane na mipango pamoja na mikakati yote ambayo hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imebeba. Maeneo ambayo nilipeda nitoe ushauri na niombe Ofisi ya Waziri Mkuu kuifanyia kazi, katika kipindi hiki cha mwaka 2016/2017, moja ni Kitengo cha Maafa.

Katika hiki Kitengo cha Maafa kwanza nimpongeze sana Mkurugenzi wa Kitengo hiki kwa kazi yake nzuri anayoifanya mpaka sasa, licha ya changamoto alizonazo zinazoendana na ukosefu wa nyenzo za kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupitia makabrasha ya kitengo hiki, nilibaini kwamba pamoja na nia nzuri ya kitengo hiki kukabiliana na maafa, pamoja na jitihada nyingi zilizofanyika kuwajengea uwezo wanaofanyia kazi

katika kitengo hiki, bado kitengo hiki hakijawa na nguvu ya kutosha kuweza kukabiliana na changamoto za maafa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe jitihada za makusudi zifanyike kuhakikisha kwamba kitengo hiki, pamoja na kujengewa uwezo wa kinadharia ambao kwa sasa wameendelea kujengewe kupitia miradi mbalimbali ingefaa pia kitengo hiki sasa kiwe na vituo maalumu vyenye nyenzo maalumu za kuweza kukabiliana na maafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi ni kwamba wakati Dodoma na Kondoa wanalia kwelea kwelea *responsiveness* ya kitengo kinachohusu maafa ilikuwa ndogo sana, huu ni ushahidi kwamba bado tuna changamoto kubwa kwenye eneo hili, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie kuhakikisha kwamba tunafanyia kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nilipenda nichangie ni eneo la elimu. Wakati nachangia jana nilimueleza Mheshimiwa Spika kuhusu hali ya Jimbo langu la Madaba. Jimbo letu la Madaba ni Jimbo changa lina takribani miezi michache sana na Halmashauri ya Wilaya nayo ina miezi michache tu. Lakini upande wa elimu kama ilivyo katika maeneo mengine tuna changamoto nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao walimu zaidi ya 412 ndani ya Wilaya ya Songea, walimu hao Wilaya ya Songea inahusisha pia Halmashauri ya Wilaya ya Madaba, walimu hawajapandishwa madaraja kwa muda mrefu pamoja na kwamba wana hizo sifa. Nimeomba Chama cha Walimu kiniwasilishie nyaraka mbalimbali ambazo nitaziwakilisha katika Ofisi ya Waziri Mkuu ili mtusaidie kutanzua tatizo hili kwa sababu ni kikwazo kikubwa cha maendeleo ya elimu katika Halmashauri yetu na Wilaya ya Songea kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ambalo ningependa nitoe mchango wa kina ni eneo la soko la mazao ya mahindi. Kama unavyojua Mkoa wa Ruvuma ni ghala la Taifa la chakula. Mkoa huu kwa miaka mingi umeendelea kuzalisha chakula cha kuwalisha Watanzania, katika Mkoa huu Halmashauri Wilaya ya Madaba, Jimbo la Madaba lina wakulima ambao wanazalisha sana mahindi ambayo yanachangia sana kwenye chakula cha Taifa letu. Kwa bahati mbaya mfumo wa manunuzi wa haya mahindi bado siyo rafiki kwa wananchi wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa bado tunategemea kituo kimoja cha Madaba, yapo maghala katika kila Kata yanajengwa kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kupitia mradi wa *BRN*. Maghala haya mpaka

sasa hayajakamilika, na ujenzi wake umesimama kwa muda mrefuwakandarasi bado wanalalamika hawajalipwa.

Naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu, wakati tunaendelea na mchakato huu tuhakikishe kwamba ule mchakato ambao umesimama katika vijiji vyote vya Halmashauri ya Wilaya Madaba ya kujenga na kuimarisha maghala ukamilike kwa sababu wananchi wa Jimbo la Madaba wataanza kuvuna mwezi ujao na watahitaji kuhifadhi mazao yao. kama ambavyo ulisema mwenyewe Mheshimiwa Waziri Mkuu ulipotembelea Mkoa wa Ruvuma, ulishauri kwamba NFRA wanunue mahindi katika vituo vilivyoko vijijini ili kuwaondolea Wananchi adha ya kusafirisha mazao haya kuyapeleka katika vituo maalum vya mjini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri yetu ya Madaba pia inachangamoto kubwa sana ya maji. Mji wa Madaba pekee na Kijiji cha Mkongotema ndiyo wenye maji yanayotiririka, lakini wingi wa mabomba hauwiani na idadi ya wananchi waliopo. Ipo miradi iliyofadhiliwa na *World Bank*, miradi hii imetekelezwa katika vijiji vitatu vya Mkongotema, Lilondo na Maweso. Kwa bahati mbaya miradi ya Maweso na Lilondo imesimama kwa muda mrefu sana, kwa vyovyote vile jitihada zilizofanyika mpaka sasa kubwa na niishukuru sana Wizara husika kwa kutufikisha pale ambapo tumefika. Ninaomba sana tunapoendelea na mchakato huu zoezi hilo pia la kukamilisha hii miradi ya maji katika maeneo yaliyobaki liendelee, lakini pia niombe sana Mji wa Madaba una kilio sana cha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kumshukuru sana Waziri wa Afya Mheshimiwa Umy Mwalimu, pamoja na Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo ambao wamekuja ndani ya Jimbo langu na kushirikiana na wananchi kutatua kero zinazowakabili kwenye eneo la afya na eneo la umeme. Hivi ninavyokuambia Mheshimiwa Sospeter Muhongo yupo kwenye mchakato wa kukamilisha umeme wa maeneo ya Mji wa Madaba na Mungu bariki Disemba tutakuwa na umeme, ninaniomba sana zoezi hili liendelee, wananchi wa Madaba wanatambua sana juhudi za Mheshimiwa Sospeter Muhongo, lakini pia wanatambua sana jitihada za Waziri wa Afya, Mheshimiwa Umy Mwalimu za kuhakikisha kwamba Madaba tunapata Hospitali ya Wilaya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho na la muhimu sana ni kwamba tulipokuwa tunaelekea uchaguzi wa mwaka 2015 vipo vijiji vingi vilivyozaliwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba kama ambavyo vilizaliwa katika maeneo mengine ya Songea Vijijini. Vijiji hivi bado havijapata usajili wa kuduma na kama vimepata havija...

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Tunakushukuru sana Mheshimiwa, anayefuata kama nilivyosema mapema ni Mheshimiwa Omary Ahmad Badwel.

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuwa miongoni mwa Wabunge watakao changia katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini kwa kuwa ndio mara yangu ya kwanza katika awamu yangu hii ya pili ya kuwa Mbunge wa Bahi kusimama hapa katika Bunge lako Tukufu naomba nichukue nafasi hii pia kuwashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Bahi, kwa kweli kwa kuniamini na kunichagua tena kuwa Mbunge wao na mimi ninawaahidi mbele yako, imani ile ile waliyokuwa nayo katika kipindi cha miaka mitano iliyopita nitaendelea kupambana nihakikishe mwaka 2020 imani yao inakuwa bado ipo hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuchaguliwa kuwa Waziri Mkuu wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mawaziri wote ambao Mheshimiwa Rais amewachagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajadili leo hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kupitisha bajeti yake katika mwaka wa fedha unaokuja. Nimemsikiliza kwa makini sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na maeneo mbalimbali ya maendeleo ya nchi yetu ambayo ameyagusa hususan amegusa katika uboreshaji na kuleta mapinduzi ya kilimo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni muhimu na nadhani wote tunatambua namna ambavyo kwamba sehemu kubwa ya wananchi katika nchi yetu ya Tanzania wanategemea kilimo. Zipo juhudi mbalimbali ambazo zimefanywa na Serikali zimewatoa walikuma walipokuwa wakilima kwa jembe la mkono kwa sehemu kubwa sasa wanalima kwa zana mbalimbali ambazo wanazitumia na wameongeza uzalishaji. Katika hili nataka nichukue nafasi kumpongeza sana Mheshimiwa Mwigulu, ameanza vizuri na mimi nataka nimtie moyo katika kazi yake ambayo amefanya, sisi tumekuwa tukimfuatilia, kama alikuwa nalala masaa kumi, sasa apunguze alale masaa matano kwa sababu

kazi hii ni kubwa ya kupambana kuhakikisha kwamba wakulima wetu wanapata mabadiliko makubwa ya kimapinduzi na waweze kuvuna kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ambayo yanapata mvua nyingi wachukue hatua ya kuwaendeleza lakini yapo maeneo kama Dodoma ambapo pia hayapati mvua za kutosha na tunahitaji sana kilimo cha umwagiliaji. Katika Wilaya yangu ya Bahi sehemu ya umwagiliaji ni sehemu muhimu kwa sababu ni Wilaya ya ukame lakini tumeanza, miradi ile ni ya muda mrefu imechakaa nilikuwa naomba Wizara ipitie ione namna ambavyo itaboredha na kufufua miradi mbalimbali ya kilimo cha umwagiliaji katika Wilaya ya Bahi ili kuwapunguzia wananchi adha ya kuomba chakula kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nisisitize na niseme wakati tunaendelea kuwahamasisha wananchi kulima na kufanya juhudi mbalimbali za kuhakikisha kwamba kilimo kinachukua nafasi kubwa katika nchi yetu lazima tuangalie na mambo mbalimbali ambayo yanaweza yakawakuta wakulima hasa wakati wanandelea na zoezi la kulima. Kwa mfano majanga mbalimbali, nilikuwa najaribu kuangalia pamoja na juhudi mbalimbali Serikali bado yapo maeneo inapaswa kujipanga upya. Kwa mfano, unapo himiza wakulima kulima wanakumbwa na majanga mbalimbali, wanakumbwa na ndege waharibifu wa mazao, wanakumbwa na wadudu, wanakumbwa na magonjwa lazima sasa pia tuwe na dhama ambazo zitaweza kupambana na mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wananchi wa Bahi wamekumbwa na ndege waharibifu, Mheshimiwa Mwigulu amehangaika sana lakini Tanzania nzima hatuna hata ndege moja yaani ni jambo la ajabu kabisa! Kwamba hakuna hata ndege moja katika nchi yetu ambayo inaweza kumwagilia dawa wakati kuna wadudu au kuna magonjwa au kuna ndege wamevamia mashamba. Tukipata matatizo kama haya tunakwenda kukodi ndege Nairobi, tunakwenda kukodi ndege nchi jirani, hivi maafa haya yakija kwa pamoja nchi zote hizi za Afrika Mashariki Tanzania tutakimbilia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anajibu hoja hii atuambie katika Bajeti ijayo wahakikishe kwamba wanatenga fedha za kununua ndege kwa ajili ya dharura ya mambo mbalimbali yanayowakumba wakulima. Kwa kweli, hii ni aibu na ni jambo la hatari kwa sababu wakulima wamefanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue nafasi nimshukuru sana Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye kitengo chake cha maafa wakati zoezi linaendelea na Mheshimiwa Mwigulu anahangaika wale ndege

wameshindikana alituma watu wa maafa kupitia Brigedia Msuya kwenda kuona namna ambavyo ndege wanashambulia na wenyewe wamejiaonea lakini hakuna kitu cha kufanya. Ndege imekodiwa, imekuja mpaka Dodoma haijafanya kazi unaambiwa ndege haina dawa ya kumwagilia. Sasa hata gharama ambazo ndege hiyo imekodiwa kuja kutoka Nairobi mpaka hapa halafu inafika hapa Tanzania haiwezi kufanya kazi iliyokusudiwa inasema hakuna dawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tujue hivi katika awamu ijayo wanafanya nini kuhakikisha kwamba hata kama bado wanakodi ndege lakini dawa ipo na maandalizi mengine yamefanyika vizuri.

Nakushukuru sana Mheshimiwa Jenista pia kuagiza sasa waende wakafanye tathmini katika vijiji vyangu vya Bahi ambavyo vimeathirika, vijiji 15 wananchi wale wamerudi kabisa nyumbani mashamba yameliwa ndege wamewashinda kwa hiyo nakushukuru sana na ni matumaini yangu kwamba tathmini hiyo itafanyika mapema kwa sababu wale wananchi chakula walishamaliza toka mwaka uliopita walikuwa wanatarajiwa wavune sasa wapate hicho chakula hawana chakula, siyo kwamba mnakwenda kuwafidia lakini waende wakasaidiwe na Serikali kuhakikisha kwamba wanarudisha maisha yao ya kawaida kupitia janga hili la ndege ambalo wamelipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa habari ya umeme tumetoka REA two tunakwenda REA three. Lakini mtakumbuka bahati nzuri baadhi ya Wabunge tuliokuwa hapa, mimi ni miongoni mwa Wabunge waliolalamika sana katika awamu iliyopita kusahuliwa kwa habari ya umeme katika vijiji vyake. Mimi nadhani ndiyo Wilaya pekee katika nchi nzima, ambayo wakati tunahangaika habari ya umeme ndiyo haikupata umeme hata kijiji kimoja cha REA. Hili halikuwa jambo nzuri ilikuwa ni uonevu kwa Wilaya ya Bahi, wakati Kondo wanaipa vijiji 56, Mpwapwa vijiji 40, Kongwa vijiji 30, Mkoa huu huu Bahi hauipi hata kijiji kimoja. Namshukuru sana Mheshimiwa Simbachawene baada ya kuona malalamiko yangu hapa yeye akiwa Waziri akafanya kila jitihada ambayo inatakiwa nikapatiwa vijiji vitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vijiji ilikuwa ni kama zima moto ya uchaguzi, kweli wale Wataalamu walikwenda, mkandarasi alipewa ile kazi mpaka ilipofika mwezi wa kumi wakati tunapiga kura vile vijiji vimesimama vyote, hakuna hata mashimo yamechimbwa, nguzo zimewekwa leo tunahesabu miezi minane, mradi ule umesimama.

Mheshimiwa Waziri Mkuu nilikuwa naingoja hii siku ya leo ili nije hapa kwako, kwa sababu mimi nimeenda kushukuru vijiji, sijaenda kushukuru hivyo vijiji

vitano nimefanya hivyo kwa maksudi. Sijaenda kushukuru kwa sababu nataka yule uliyemwambia au Serikali iliyomwambia afute vile vijiji vitano tuende naye tukashukuru naye pamoja ili kama tutazomewa azomewe yeye na mimi, kwa sababu kwa kufanya hivi kwa kweli ni kutokuwatendea haki watu wa Bahi mmewanyima vijiji kabisa asilimia mia moja, halafu mmewapa vijiji vitano wameanza kazi ya kuchimba mashimo na kuchomeka nguzo mmekwenda kufuta hivyo vijiji vitano!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kwa kweli siyo sawa mimi naomba maelezo Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwa nini vijiji vimefutwa na lini vijiji hivi vitarudishwa kabla ya REA III, naambiwa sasa vimepelekwa kwenye REA III kitu ambacho siyo sawa. Nataka virudi kwenye REA II wakati inamalizika mwezi wa saba kwa kweli na hivi vijiji viwe vimewaka umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la maji; kama nilivyosema Mkoa wa Dodoma ni kame na sisi kama Wilaya ya Bahi tuna shida kubwa sana ya maji, tumehangaika sana, Bahi ni Makao Makuu, ni Wilaya mpya na mji mpya ambao sasa ilikuwa kijiji tume- *promote* kile kijiji kimekuwa Mji uhamiaji umekuwa mkubwa ofisi za Serikali zote zimeamia pale.....

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mwongozo wa Mwenyekiti.

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, watu mbalimbali wamehamia pale kwa hiyo panahitaji maji. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana nisisitize Mheshimiwa Waziri Mkuu Mji huu wa Bahi utizamwe kwa jicho la umakini.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Badwel naomba uketi.

Waheshimiwa Wabunge, sikumsikia huyo aliyekuwa anaomba Mwongozo kwa sababu Kanuni zipo wazi unaomba mwongozo tu wakati ambapo hakuna Mbunge anayeongea, sasa ulipaswa tu uje kwa taarifa nitakubali au kuhusu utaratibu maana tupo hapa kufuata Kanuni, endelea. *(Makofi)*

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mzungumzaji ambaye anachangia kwa sasa naona yeye bado amekariri kwamba Waziri Mkuu anashughulika na mambo ya maji, nishati, ndiyo yale ambayo Kiongozi wa Upinzani amesema hapa. Waziri Mkuu alichotelele leo na alichozungumza hakina mambo ya maji, nishati na mambo mengine hayo

yapo kwenye TAMISEMI anatupotezea muda badala ya ku-discuss kinachohusika analalamika mambo ya nishati, maji hayo hayapo kwa Waziri Mkuu sasa hivi, ndiyo maana tumesema watoe miongozo ya uendeshaji wa Wizara sasa hivi, ndiyo maana watu wanachanganyikiwa hapa Bungeni hawaelewi wafanye nini...

MBUNGE FULANI: Soma hotuba wewe!

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naombeni tuwe na utulivu tuvumiliane kwanza. Pili, Mheshimiwa Badwel unaikubali taarifa.

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, siikubali taarifa nadhani hajui cheo cha Waziri Mkuu ni nani.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiye Mkuu wa Mawaziri wote, kwa hiyo, hata ninapomueleza hapa atatoa maelekezo kwa Wizara husika kufanya kazi ambayo mimi naisema hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasa ukizingatia nafasi zetu hapa ni ndogo, unapopata fursa kama hii ni vizuri kuwasemea wananchi. Inawezekana nimechangia hapa nisipate fursa ya kuchangia mahali pengine na mimi ni Mbunge kama yeye na Jimbo na yeye ana Jimbo aniache nifanye kazi walionileta wananchi wa Bahi. Simuingilii kwenye Jimbo lake kama hana cha kusema arudi nyumbani kwake Jimboni akafanyae kazi za Jimbo kule asikae hapa Bungeni lakini sisi tunayo mambo ya kusema nitaendelea kuyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza habari ya maji Mheshimiwa Waziri Mkuu, Bahi hakuna maji najua unanisikiliza na kwa kauli hii ya Mbunge ambaye hataki wewe uambiwe juu ya maji, utapeleka maji Bahi ili wananchi wajue kazi niliyoifanya hapa ilikuwa na tija na sikuja kufanya mchezo hapa. *(Makofi)*

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Hawakuoni *brother!*

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ilikuwa ni habari ya sheria mbalimbali. Wizara yako Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiyo inasimamia Tume ya Kurekebisha Sheria, zipo sheria nyingi sana zimepitwa na wakati, ni vizuri Serikali ikatafuta utaratibu mzuri wa kuziangalia sheria hizi mbalimbali ili ziweze kufanyiwa marekebisho ziweze kutoa tija iliyokusudiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunapitia kwenye Kamati zetu hususan Kamati ya Katiba na Sheria, tumeona namna ambavyo Tume ya Sheria inapitia sheria moja kwa miaka mitatu, inafanya uchunguzi wa mapitio ya sheria moja kwa miaka mitatu! Mimi nadhani huu ni muda mrefu sana, unatenga fedha mwaka huu milioni 800 kuipa Tume ya Kurekebisha Sheria kuangalia sheria tatu tofauti, mwakani haijamaliza unatenga tena milioni 800, mwaka unaofuata milioni 800, utakuta zaidi ya bilioni mbili zinatumiwa lakini yale makusudio ya kurekebisha ile sheria bado hayajafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani mkae muangalie namna nzuri ambapo itaweza kufanya hii Tume ya kurekebisha sheria nyingi kwa wakati mmoja ili ziweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia unasimamia Tume ya Haki za Binadamu. Hii Tume ya Haki za Binadamu imesahauliwa kabisa na Serikali. Ukiangalia katika bajeti ya mwaka huu, Tume hii imepewa pesa ya pango tu kwamba pale wanapokaa waweze kulipia ofisi, sidhani kama hiyo ndiyo kazi ya Tume ya Haki za Binadamu. Tume ya Haki za Binadamu ina kazi nyingi, kama Serikali ipo *serious* kuhakikisha kwamba haki za wananchi zinapatikana waiangalie hii Tume ya Haki za Binadamu, waipe fedha za kutosha ili iweze kufanya ufuatiliaji mbalimbali wa mambo yanayohusu haki za binadamu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nizungumzie habari ya fedha milioni 50 ambazo tunatarajia kwenda kuzipata katika vijiji vyetu, tunaomba kwa kweli utaratibu uandaliwe vizuri na pengine sisi Wabunge tushirikishwe kuletewa utaratibu huo ili tuweze kujua fedha hizi zinakwenda kugawiwa vipi na zitumikeje katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakumbuka yalikuwepo mabilioni ya Kikwete yalikuja hivi tu kwa matamko, lakini baadaye fedha zile zilitoweka hatukujua zimekwenda wapi, tunatamani sana kuona fedha hizi safari hii zinakwenda kila kijiji zinawekewa utaratibu mzuri na Wabunge ambao tunakaa kule tunajua vikundi vyetu tunajua wananchi wetu uchumi wao, tushirikishwe vizuri ili na sisi Wabunge tuweze kutoa ushauri kusaidia yale madhumuni ya milioni hamsini kupelekwa katika kila kijiji yaweze kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante tunakushukuru, tunaendelea na mchangiaji wetu anayefuata ni Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi.

MWONGOZO WA SPIKA

MWENYEKITI: Mwongozo!

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kwa kauli ambayo aliitoa Mheshimiwa Esther Matiko kwamba hotuba ya Waziri Mkuu haijzungumzia maji, naomba nimpe taarifa kwamba kitabu chenye hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 56 umezungumzia maji.

MBUNGE FULANI: Aah, huo ni Mwongozo ama maelezo?

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naomba atambue kwamba suala hilo ambalo alikuwa anazungumzia Mheshimiwa Badwel, Waziri Mkuu alilizungumzia. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naelewa mna nia njema, lakini mniachie mimi niongoze shughuli za Bunge.

Tunaendelea nimemtaja Mheshimiwa Mbilinyi haya anayefuata Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, naenda upande wa Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Vedasto Ngombale, Mheshimiwa Yussuf Kaiza Makame, haya tunaendelea Mheshimiwa Raphael Japhary Michael.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia, kwa sababu hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni imeonesha jinsi ambavyo Bunge hili limenyimwa haki, demokrasia na uwezo wa kujiendesha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa nakuomba uchangie, kama yale mengine...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima zote nadhani mlinuelewa nilichosema mimi nataka tujielekeze kwenye hoja iliyo mbele yetu hayo makando kando yenu nawaomba sana tuitendee haki hoja iliyo mbele yetu, Mheshimiwa Raphael twende kazini.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mojawapo ya jambo ambalo limejaa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu ni demokrasia, utawala bora na mambo

mengine yanayofanana na hayo, na kwa sababu hotuba ya Kambi ya Upinzani Bungeni imeonesha jinsi ambavyo demokrasia haitekelezwi na hata wale watu walioandaliwa kuwawakilisha wananchi kusimamia sheria na Katiba ya nchi hii, ninaona udhia sana kuwa sehemu ya watu watakao kuwa wameshindwa kusimamia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninajisikia vibaya sana kama nitakuwa ni miongoni mwa watu wanaobariki Bunge hili kudhibitiwa na Serikali badala ya kuidhibiti na kuisimamia Serikali. (Makofi)

Kwa hiyo, kwa heshima na taadhima naomba huo uwe mchango wangu kwa siku ya leo ili nisiweze kuongeza maneno mabaya, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Tunakushukuru.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Ndiyo mawazo ya Jimbo lake hayo!

MWENYEKITI: *Order please, ahsanteni.*

Tunaendelea wachangiaji wetu wanaofuata sasa hivi ni Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi akifuatwa na Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mjimwa.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha afya na nguvu kuweza kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza basi niwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Lushoto. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kushukuru hotuba hii ambayo imejaa maudhui mema, niendeleo kumshukuru Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri. Andiko linasema nimrudishie nini Bwana kwa wema wake alionitendea, kwani hotuba ya Waziri Mkuu imekuna wengi na inastahili kupongezwa hata Mwenyezi Mungu naamini ameibariki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waislamu tunasema; *maa yashkuru-annasa laa yashkuru-Allah* (usiposhukuru watu basi hata Mwenyezi Mungu hutamshukuru). Basi nishukuru hotuba hii na pia niwashukuru Watanzania wote kwa kumchagua Rais wetu John Pombe Magufuli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja nijikite katika kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Hakuna asiyefahamu kwamba Wilaya ya Lushoto ni Wilaya ya kilimo cha matunda na mboga mboga. Wilaya ile na wakulima wanalima kwa zana ambazo ni dhaifu mno, wanalima kwa mbolea ya samadi yaani kinyesi ng'ombe. Wakulima wanapovuna mazao yao huwa wanapata taabu sana, wanunuzi wakati wa mvua barabara hazipitiki na inapelekea mazao yale yanauzwa bei rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika suala zima la ukusanyaji wa mazao wananchi wa Lushoto wanapata taabu sana. Mimi kama Mbunge wao ambaye wamenituma niwawakilishe kwao, kwani wakati wa kura za maoni walisema tunakutuma wewe mnyonge mwenzetu, mkulima mwenzetu ukatuwakilishe, basi na mimi ninawaahidi kutowaangusha na ndiyo maana mkulima mimi, mnyonge mimi nimesamama mbele ya Bunge hili Tukufu kwa ajili ya wananchi wa Lushoto hususani wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hotuba ya Waziri Mkuu iangalie wakulima wangu wa Lushoto hususan katika suala zima la pembejeo, suala zima la masoko, suala zima la kujenga maghala na kujenga mabwawa kwa ajili ya kilimo cha kisasa cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la maji. Lushoto imezungukwa na vyanzo vingi vya maji, lakini miundombinu ya maji hakuna katika Jimbo zima la Lushoto. Ukianzia Kata ya Ngwelo, Gare, Mlola, Ubili, Makanya, Kwemashai, Mbwei, Ngulwi, Malibwi, Kilole, Kwekanga na Lushoto Mjini. Nakuomba katika bajeti hii basi uwafikirie watu wa Lushoto hususan katika suala zima la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la afya, tunashukuru tuna Hospitali ya Wilaya ya Lushoto, lakini hospitali ile ina changamoto. Hospitali ya Lushoto hususani wodi ya akina mama wajawazito, ile wodi ni ndogo inastahili kuongezwa. Sambamba na hilo katika Kata za Ngwero, Gare, Magamba, Ubili, Kilole na Kwemashai tunahitaji kujengewa vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la miundombinu, Lushoto wenyewe tunaita Lushoto ya wazungu, kwani Wazungu Wajerumani walikuwa wanaishi maeneo yale, miundombinu ya barabara imejengwa tangu kipindi cha mkoloni. Kwa hiyo, niombe Serikali ituangali katika vipaumbele vya barabara, hususan barabara ya kutoka Lushoto kupitia Soni hadi Mombo. Barabara hii ni nyembamba na mvua zikinyesha huwa kuna mawe yanaporomoka yanazuia barabara. Hata juzi kati tarehe 17 zaidi ya siku tatu magari yalilala pale mpaka hata maiti zinatoka Dar es Salaam, Tanga na

sehemu zingine basi zilishindwa kupita pale kwa sababu ya mawe yaliyoshuka pale na makalvati kuziba, maji yanatiririka katikati ya barabara ilichukua takribani ya siku tatu, naomba katika bajeti yako hii basi waifikirie barabara ya Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo kuna barabara ya kutoka Mlalo kupitia Ngwelo, Mlola hadi Makanya kwenda kwa Mheshimiwa January, Mlingano kwa Mheshimiwa Majimarefu, Mashewa, barabara hii tunaomba sasa ipandishwe hadhi iwe ya Wakala wa Barabara TANROAD. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya kutoka Dochi kupitia Ngulwi hadi Mombo, kwa kuwa barabara hii ya Lushoto - Soni - Mombo, mara nyingi mvua zinaponyesha barabara ile mawe yanashuka yanaziba barabara ningeishauri Serikali iwe na barabara mbadala ya kutoka Dochi - Ngulwi hadi Mombo ijengwe kwa kiwango cha lami na iweze kupandishwa daraja ili iweze kuwa barabara mbadala kwa ajili ya matatizo yanapotokea na *breakdown* zinapotokea katika barabara ya Soni - Mombo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hawa ndugu zangu, vijana wenzangu siyo vijana wa Lushoto tu ni Tanzania nzima, vijana wanaojihusisha na bodaboda. Vijana hawa inapaswa walindwe maana bodaboda ni ajira kama ajira nyingine. Bodaboda hawa naomba kama kuna uwezekano watengewe fungu katika bajeti hii kwa ajili ya kukidhi mahitaji yao kwani katika vipaumbele vinavyotoa ajira ni watu wa bodaboda. Wamepata ajira kwa kuwa watu hawa wana watoto, wanao wake zao na wanawasomesha watoto na bodaboda ndiyo kipato chao, ndiyo ajira yao, ninaomba askari wasiwanyanyase vijana wanaojishughulisha na bodaboda, siyo kwa Lushoto tu ni Tanzania tuwalinde vijana wetu wa bodaboda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la umeme. Nimshukuru Waziri Muhongo, alituma timu yake wakazunguka katika Wilaya nzima ya Lushoto siyo Jimbo la Lushoto tu, Wilaya nzima ya Lushoto alituma timu yake ikazunguka na kubaini maeneo ambayo hayana umeme na kuyaandika, kuyahakikisha kwamba ameyachukua *then* atayafanyia kazi. Kwa hiyo nampongeza sana Profesa Muhongo, Mungu akulinde na akuzidishie umri! *(Makofi)*

Kuna suala zima la michezo. Lushoto kuna vipaji vingi sana, kuna vijana wengi sana ni wanamichezo wazuri na hata timu za Simba na Yanga zinakuja Lushoto kwa ajili ya kufanya mazoezi. Kwa hiyo, niombe sasa, nimuombe Waziri wangu, mpendwa wangu Mheshimiwa Nape Nnauye katika bajeti hii aifikirie Lushoto kimichezo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Mheshimiwa Mgimwa.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia kusimama leo hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayofanya ya kizalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. John Pombe Magufuli anafanya kazi nzuri ya kusimamia uwajibikaji na uadilifu katika Serikali yetu. Pamoja na kazi nzuri bado anaendelea kutumbua majipu ndiyo maana leo hii wenzetu wa upinzani wameamua kuweka mpira kwapani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waswahili wanasema mwenye wivu ajinyonge, tutaendelea kumpongeza Dkt. John Pombe Magufuli na tutaendelea kumuunga mkono kwa kazi anayoifanya katika nchi hii. Kwa namna ya kipekee naomba nimpungeze sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na kwa kazi nzuri anayoifanya kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mufindi Kaskazini kwa kunirudisha tena katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitaanza kwa kujielekeza katika ukuaji wa uchumi. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema mwaka 2015 uchumi ulikua kwa asilimia 7.1, mwaka 2014 uchumi ulikua kwa asilimia 7. Ni kweli uchumi unakua, lakini ninaomba Serikali inapozungumzia suala la ukuaji uchumi lazima waangalie na hali halisi ya maisha ya Mtanzania. Ukuaji wa uchumi unatakiwa uende sambamba na huduma za jamii kama afya, elimu pamoja na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vipaumbele ambavyo amevizungumzia Mheshimiwa Waziri Mkuu vya ukuaji wa uchumi amezungumzia suala la kilimo. Jana katika hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti alisema asilimia 79 ya Watanzania wameajiriwa katika eneo la kilimo, lakini ukuaji katika eneo hili unakua kwa asilimia 3.4 ambao ni ukuaji mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Waziri Mkuu amesema wakulima ni asilimia 66.3 ya Watanzania wote ambao wako kwenye eneo hili. Serikali ni kweli imeona kwamba, zaidi ya asilimia 79 ya Watanzania wameajiriwa katika sekta hii ya kilimo, lakini bado Serikali haijaamua kuwekeza kwenye eneo hili, katika eneo hili hakuna Mbunge ambaye haguswi. Tunaiomba Serikali iangalie kwa macho yote katika eneo hili haswa katika mfuko wa pembejeo, ule mfuko wa pembejeo umewekewa hela ndogo sana kulinganisha na pesa ambazo zinatakiwa ziwepo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutawekeza vizuri katika eneo hili la kilimo nina hakika kabisa hata eneo ambalo tumekusudia kwenda kwenye Mpango wa Pili wa viwanda tutakwenda vizuri, kwa sababu Mheshimiwa Mwigulu pamoja na Waziri wa Viwanda ni watoto pacha, kama tutafanya vizuri kwenye kilimo *automatically* tutafanya vizuri kwenye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba sana, kwenye eneo la pembejeo Serikali iongeze mfuko wa pembejeo ikilinganishwa na ilivyo sasa, kwa sababu unawagusa Watanzania karibu wote, aidha inagusa wananchi wa Chama cha Upinzani na wa Chama Tawala, kwa hiyo tunaiomba Serikali iwekeze sana kwenye eneo hili. Lakini la msingi zaidi tunatakiwa tuhakikishe zile pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati, zikiendelea kuchelewa zitaendelea kuwapa matatizo wakulima wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, eneo la kilimo ni eneo *very sensitive*, Serikali iliamua kuanzisha Benki ya Kilimo, benki hii ya kilimo ilianza miaka mitatu iliyopita, na tulikubaliana kwamba, benki hii ianze kwa mtaji wa shilingi bilioni 100, lakini jambo la kusikitisha mpaka leo benki hii ya kilimo imepewa shilingi bilioni 60 wanashindwa kumudu na wanashindwa kuwasaidia wakulima.

Hivyo, tunaomba benki hii iongezewe mtaji na kama tulivyokubaliana kila mwaka benki hii ya kilimo iendelee kupata mtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi bilioni 60 hazitoshi! Tunaomba benki hii isiwepo Dar es Salam tu, iende hadi kwenye *site* ambako wakulima wapo. Itakuwa bora kama benki hii ya kilimo itakuwepo kwenye mkoa haswa ya kilimo na iwafikie wananchi, utaratibu wa kupata mikopo uwekwe uwe wazi na wananchi wajue ni haki yao kupata mikopo ya riba nafuu. Tukifanya vizuri kwenye eneo hili kama nilivyosema awamu ya pili ya mpango tutakwenda tukiwa kifua mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ninalotaka kuchangia kidogo ni kuhusu mfumuko wa bei. Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia sana mfumuko wa bei na jana Waziri wa fedha alizungumzia mfumuko wa bei. Lakini Waziri wa Fedha jana alizungumza jambo moja kwamba, tukidhibiti eneo la mafuta tutakuwa kwenye hali nzuri ya kuzui mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kabisa mfumuko wa bei unasababishwa na mambo makubwa mawili, la kwanza *Cost Push Inflation* na la pili *Demand Pull Inflation*. Tunapozungumzia *Cost Push Inflation* ni kweli kwenye eneo la mafuta tunaweza tukawa kwenye eneo hili, lakini hatuwezi kuzungumzia eneo la mafuta peke yake bila kuzungumzia umeme, kama tuta- *control* bei ya umeme itakuwa iko chini na umeme utapatikana kwa wakati, *automatically* utapunguza *cost of production*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuishii kwenye jambo hilo tu, vilevile nilitaka tuzungumzie suala la *infrastructure* kwa maana miundombinu kama tuna uhakika na miundombinu mizuri *automatically* tutakuwa tumefanya vizuri. Kwa namna ya kipekee naomba nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali kwenye suala la *Demand Pull Inflation* Serikali iko vizuri na Watanzania tumekuwa tuna chakula kingi na hatuagizi nje ya nchi. Kwa hiyo katika jambo hili tuko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo huwa tunalipigia sana kelele hapa suala la *dollarization* lakini Serikali imekuwa siyo sikivu haisikii kwenye jambo hili. Tunaomba hawa watu ambao wanaendeleza utaratibu wa *dollarization* kwa njia moja au nyingine ina-*affect* uchumi wa nchi hii, thamani ya shilingi *automatically* inapoteza mwelekeo kutokana na *dollarization*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekisoma kitabu cha Waziri Mkuu, nimeona haikuzungumzia kabisa suala la uvuvi. Tunatakiwa tuwekeze kwenye eneo la uvuvi, eneo la uvuvi ni eneo muhimu ambalo tunawekeza mara moja na baada ya kuwekeza nina hakika tutakuwa tume-*create* ajira za kutosha, vijana wengi wanaweza kujijiri katika eneo hili na tukapata mtaji mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatakiwa tuwe waangalifu na tunatakiwa tuwe waangalifu na tuwekeze hasa kwenye bahari kuu ili kusudi tuweze kupata mitaji mikubwa. Kuna baadhi ya nchi hapa duniani kama Sychelles zinaishi kwa uvuvi na sisi hatuna sababu ya kutokupata mapato makubwa kwenye eneo la uvuvi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ninayotaka kuzungumzia ni kuhusu suala la maji. Maji ni muhimu sana kwa maisha ya Mtanzania na kwa

masikitiko makubwa katika Jimbo langu ambalo lina Kata 11 maji ni tatizo, sina hata Kata moja ninayoweza kuzungumzia suala la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wetu ile senti 50 ambayo imeingizwa kwenye tozo ya mafuta ingeongezwa ikawa shilingi 100 badala ya shilingi 50 kusudi tuweze kupata maji katika Majimbo mengi na katika maeneo mengi. Tunaiomba Serikali inapoleta bajeti kwenye eneo la maji tuongeze hatuna sababu ya kutochangia kwenye eneo la mafuta badala ya shilingi 50 tuweke shilingi 100 ili mfuko wa maji uendelee kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la miundombinu. Ili tuone uchumi unakua vizuri ni vema tukahakikisha miundombinu yetu ni ya uhakika. Katika eneo langu lina matatizo katika barabara ya Mapanda, Usokami, Ihalimba na Kinyanambo, barabara ya Mtili, Ifwagi, Mdabulo na Ihanu. Tumewaandikia wenzetu wa TAMISEMI kwa vile hivi sasa barabara zile hazipitiki, tumewaandikia kwenye mfuko wa *emergency* watusaidie katika eneo hili. Wakitusaidia nina uhakika kabisa tunafanya vizuri katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu eneo la nishati. Tunazungumzia sana sasa hivi nishati ya gesi, tumesahau habari ya makaa ya mawe. Makaa ya mawe ni muhimu sana, ukiangalia wenzetu wa *South Africa* asilimia 57 ya umeme unatokana na makaa ya mawe. Sisi hatuna sababu ya kutokuwekeza kwenye makaa ya mawe, tulitakiwa tujenge *transmission line* kutoka Makambako kwenda Songea mpaka Mbinga ambayo gharama yake ilikuwa shilingi bilioni 60 na wenzetu wa *SIDA* walishakubali kutusaidia kwenye eneo hili. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba Serikali inasuasua kwenye eneo hili! Kuna uwezekano wa ku-*produce* megawati 120 kwenye kilowati 210.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipofanya hivyo kwenye eneo hili tutakuwa tunawaonea watu wanaotoka kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunakushukuru, tunaendelea anayefuata ni Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, atafuatiwa na Mheshimiwa Kaboyoka.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nishukuru kupata fursa hii ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niseme ninaunga Mkono hoja hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa asilimia 100. Sababu ziko wazi, imesheheni karibu pande zote, mikakati yote, kutokana na utendaji wa kazi

tunaouona kwa sasa wa Mheshimiwa Rais na Mawaziri wake hatuna mashaka, tusonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie upande wa hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa nane mpaka wa 10 katika eneo la siasa. Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maagizo kwenye Tume ya Uchaguzi kubaini sababu zilizopelekea wapiga kura milioni saba kutokupiga kura. Idadi hiyo ni kubwa sana, lazima na sisi tuweze kueleza baadhi ya sababu ambazo zinaweza kuwa kwa namna moja au nyingine zimechangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu ni umbali wa vituo vya kupigia kura. Watu walikuwa wanatembea kilometa 20 mpaka 10 kufuata kituo cha kupigia kura, sasa ni watu wachache ambao wanaweza wakamudu hali hiyo, lakini zipo sababu zingine za baadhi ya wananchi kukata tamaa zikiwemo sababu zifuatazo:-

Kwanza, wananchi kukata tamaa kutokana na baadhi ya Viongozi kutotenda haki, kuwa na upendeleo na ubinafsi uliokithiri. Hiyo ni sababu mojawapo inayowafanya wananchi wakate tamaa na ninaomba nieleze sababu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hatujaenda kwenye uchaguzi wa mwaka 2015, Tume ya Uchaguzi ilitoa vigezo vinavyoweza kuwezesha Jimbo likagawanyika. Sisi wote tunajua, vigezo tunavijua lakini cha ajabu unakuja kuona majimbo ambayo hayakufikia vigezo hivyo yaliweza kugawanywa na kuacha majimbo ambayo vigezo vimezidi hata vigezo vilivyowekwa. Unashindwa kupata majibu, wananchi wanakata tamaa, wananchi wanaelewa, wananchi wanafuatilia sana vyombo vya habari na wanachanganua na wanaona wakati mwingine kama Serikali ina upendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wanakuwa wameomba mara kadhaa, wameomba Wilaya, wameomba Halmashauri, wameomba Jimbo hawajapata na ninao ushahidi wa kutosha, katika Wilaya yangu Jimbo la Kwela Halmashauri ya Wilaya imeomba Wilaya, imeomba Jimbo, imeomba Halmashauri haijapata wakati ina vigezo vilivyopitiliza. Hii inatokana na viongozi kutokutembelea maeneo yote, hii ni moja ya sababu muhimu sana ambayo inakatisha wananchi tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine ni kuchelewa kwa utatuzi wa Migogoro ya ardhi. Kwanza napaswa nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ardhi aliyepo sasa hivi, kwa kweli lazima tumpongeze anafanya kazi kubwa sana,

tena yenye moyo na kujitoa muhanga, mimi nampongeza sana. Lakini ningeomba ajielekeze katika maeneo sugu ambayo yamelalamikiwa kwa muda mrefu kutoa ufumbuzi na utatuzi wa mara moja ili kutokukatisha wananchi tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumza hivi ninaongelea suala la shamba la Malonje ambalo limekuwa ni sugu sana na kwenye uchaguzi limetupa shida sana, hasa mimi Mbunge ndiye nimepata kazi kubwa kana kwamba mimi ndiye niliyebeba mzigo huo. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri uliangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni baadhi ya maeneo kutofikiwa na viongozi wa Kitaifa. Tangu tumepata Uhuru sasa hivi tuna Rais wa Awamu ya Tano, lakini yapo maeneo hawajawahi kumuona Rais hata wa Awamu ya Kwanza, ya Pili na Awamu ya Tatu, wanamuona tu kwenye luninga, sababu za msingi hazipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine kiongozi anaenda wanasema hakupitiki barabara ni mbaya nani atengeneze? Huko ni kutenga wananchi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba viongozi mnaotumbua majipu muangalie hayo ni majipu, kama Kiongozi anakuelekeza mahali pa kwenda kuzuri huko anaficha nini? Ni majipu nayo vilevile tunaomba tabia hiyo isiwepo tena, tunaimani na Serikali hii tabia hiyo itajifuta yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kubaki nyuma kimaendeleo, kukosa huduma muhimu. Kwa mfano, nitoe mfano kwa mambo mawili, barabara na umeme. Wilaya ya Sumbawanga Vijijini pamoja na kuwa kubwa mno, ina kata zaidi ya 28, vijiji 115 hakuna hata kijiji kimoja ambacho kina umeme, na wananchi wanasikia maeneo mengine kata mbili zina umeme na hata Kata jirani zina umeme, unadhani wananchi wanatafsiri kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri nyepesi ya wananchi wanadhani labda Mbunge wao hana uwezo, hasemi! kitu ambacho kila wakati tunazungumza. Kwa hiyo, ningeomba Serikali ijaribu kuweka uwiano isiwe na upendeleo, iweke uwiano kwa sababu nchi hii ni yetu sote. Iweke uwiano siyo kukimbilia upande mmoja, huko ni kuumiza wananchi bila sababu, niliona na lenyewe hilo nilizungumzie. *(Makofi)*

Suala lingine ni miundombinu ya barabara. Katika Jimbo langu ni mibovu mno, kwanza jiografia yenyewe ya Jimbo imekaa hovyoy, miundombinu ni mibaya, hata viongozi wanaokuja, mfano Dada yangu Paresso alikuja wakati

wa uchaguzi, Katika vitu alivyovitumia ni uchakavu wa miundombinu katika Jimbo langu, aliuliza hii ni Tanzania au ni Tanganyika? Nikamwambia Tanzania. Tulipata taabu kweli, hebu jamani jaribuni kuangalia maeneo haya, zipo barabara zaidi ya 10 hazipitiki. Sina sababu za kuzitaja kwa sababu naona muda hautoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ninapenda kulizungumzia ni kuhusu kilimo. Katika Hotuba ya Waziri Mkuu upande wa akiba ya chakula, inaonesha kwamba wametenga kununua tani 100,000 hicho kiwango ni kidogo mno, na sijui vigezo gani mnavitumia? Sijajua vigezo gani mnavitumia hivi tani 100,000 mnapanga zinaweza kuwasaidia Watanzania kama mvua hazitapatinaka miaka miwili, mitatu? Hizo tani 100,000 zinaweza zikasaidia? Na bado miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji bado hatujafikia kiwango kizuri.

Kwa hiyo, mazoea ambayo tumekuwa nayo ya neema ambayo tunayo Tanzania tunadhani miaka yote tutakuwa tunapata mvua mfululizo ndiyo sababu ya kutenga kiwango kidogo ,tani 100,000 ni kiwango kidogo mno kwa Nchi ya Tanzania. Kwa hiyo, ningeshauri kiwango hiki kiongezwe ni kidogo sana.

MBUNGE FULANI: Hiyo ni Rukwa peke yake!

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Hiyo ni Rukwa peke yake kama anavyozungumza Mheshimiwa aliyepo nyuma yangu, naomba kiwango hicho kiongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni upande wa afya, tunalo tatizo la upungufu wa wataalamu, waganga, tunalo tatizo la ukosefu wa kumalizia zahanati ambazo zimeanza kujengwa na wananchi na vituo vya afya, madaktari hakuna, ukosefu wa magari ya kubeba wagonjwa.

Mfano, tatizo la Kituo cha Afya cha Milepa, maombi yamekuja huu ni mwaka wa tatu na kutokana na kuchelewa tumepoteza karibu akina mama wajawazito 10 kwa mwaka jana tu, nimetoa taarifa mara kadhaa, nimerudia kuomba mara kadhaa. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu mambo mengine kama haya uyachukulie ni mambo muhimu, yanatutia doa kwa Serikali yetu nzuri hii ya sasa. Naomba uyabebe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni upande wa elimu. Tunalo tatizo la upungufu wa walimu wa sayansi upande wa shule za msingi hata upande wa shule za sekondari.

Tumejenga shule nyingi za sekondari za kata, tunaomba tupate Walimu wa Sayansi na wapo walimu ambao wamepata mafunzo wamemaliza wanazagaa mitaani hatujui wataajiriwa lini? Tunaomba wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anakuja kutoa ufafanuzi atueleze wataajiriwa lini walimu wapya wa sayansi na kwa kiwango gani kinachoweza kukidhi hali tuliyonayo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni ukosefu wa hosteli hasa hosteli za wasichana. Shule za Kata zina tatizo kubwa la kukosa hosteli za wasichana, jambo ambalo linarudisha maendeleo nyuma la vijana wetu wa kike, sote tunafahamu watoto wa kike wana vikwazo vingi, kutembea kilometa 5 anapambana na vikwazo vingi, wakati mwingine tunaweza tukalaumu kumbe waharibifu ni sisi wenyewe tusioangalia matatizo kama haya. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikatilia umuhimu wa kujenga hizi hosteli kwa shule zetu za kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchukua fursa hii kuishukuru Serikali kwa haya ambayo wameandika humu, tunasubiri utekelezaji na vilevile kwa haya niliyoyasema ningepomba ufafanuzi hasa kuitenga Wilaya ya Sumbawanga kutoipa Jimbo au Wilaya au Halmashauri wakati inavigezo lukuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti naunga mkono hoja

MWENYEKITI: Nakushukuru sana kwa mchango wako, tunaendelea Mheshimiwa Kaboyoka.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii maana nimeona mara nyingi hata nikileta maombi ya kuchangia sichaguliwi, lakini leo umenichagua ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kusema kwamba, kutokana na tamko la Kiongozi wetu wa Kambi ya Upinzani kuhusu uvunjaji wa Katiba ambao unawanyima wananchi wetu kufuatilia haya yanayotendeka hapa Bungeni ningepomba nisubiri mpaka tupate ufumbuzi wa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MBUNGE FULANI: Kwa nini uliomba?

MWENYEKITI: Tunaendelea, anayefuata kwenye orodha yetu ni Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy!

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi jioni ya leo.

Waheshimiwa ndugu zangu Wabunge, ukiona mtu kapigika ujue amekwisha. Ndugu zangu wameshaona, wameshafanya utafiti huko nje, hali zao ni mbaya, *speed* ya Magufuli inawatisha, walipania mwaka huu ndiyo waingie Ikulu, Ikulu ndiyo hawataiona tena kwa *speed* ya Magufuli. Sasa hawa jamaa ni wa kuonea huruma tu wameshapigika vibaya, hawajiwezi...

MBUNGE FULANI: Achangie, kwanza wewe una kadi mbili.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Magufuli anasifiwa dunia nzima. Kwa ushahidi Nigeria nimesikia Nigeria wanamsifu, Kenya wanamsifu, Uarabuni wanamsifu, Ulaya wanamsifu, hapa wanakaa wanampiga vijembe!

MBUNGE FULANI: Wewe una kadi ya CHADEMA wewe..

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo Katiba amevunja Katiba gani? Katiba kuwasaidia mafisadi kutuibia pesa? Mimi nilizungumza hapa Bungeni, mafisadi wauwawe mapema na makaburi yao yawekwe minyororo, nilimwambia Mheshimiwa Magufuli...

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Umesimama umekaa?

MHE. ALLY K. MOHAMED: Kwanza hawa jamaa hakuna haja ya Kuwapeleka Mahakamani. Haiwezekani mtu ana nyumba 70 bado unampeleka mahakamani, alipata wapi? Wewe tuchukue watu wa vijweni, nenda pale *Nyerere Square* wako watu wanahangaika pale. Wako tayari kufungwa miaka miwili miwili wapewe milioni 100 wako tayari, itakuwa fisadi unamfunga miezi sita au unampa kifagio anafagia Sinza akitoka anakula mabilioni ya shilingi ya hela? Haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wameshaona wamepigika, *speed* ya Magufuli inawatisha, hawana chao, iliyobaki jiungeni na CCM mapema.(*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Lugumi ya nani?

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kugusia habari ya mapato ya Serikali, mapato ya Serikali yanavyopotea katika nchi hii.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Ninyi tulieni mmeshakwisha, *speed* ya Magufuli inawatisha, hamna leo, hamna lolote, mnajiona mmefanya utafiti huko nje hamuungwi mkono na wananchi wote. Mlituambia hapa hapa Bungeni kwamba tukapimwe akili zetu kama tunamuunga Mheshimiwa Lowassa!

Je, ninyi mlipimwa akili zenu wakati mnamuunga Lowassa? Mlifanya utafiti, mliandika na vitabu, mkapita nchi nzima kumwambia Lowassa ni fisadi, je, mmepokeaje huyo fisadi mwenzenu? Sasa mmegeuka ninyi ndiyo mmekuwa mafisadi, CCM imekuwa safi, tulieni. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Achangie hotuba.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Wateja wangu wa bangi hao!

MBUNGE FULANI: Wewe wa kike au wa kiume mbona sikuelewi?

MHE. ALLY K. MOHAMED: Magufuli *speed* anayokwenda nayo ni hiyo hiyo hamna kupunguza, hamna kupunguza aendeleo zaidi ya mara mbili au mara tatu, hamna chenu. Tumepewa wajibu wa kuiongoza Serikali kwa miaka mitano na mmeona *speed* inavyokwenda mkajua mwaka 2020 hamtapata kura, hamkutegemea *speed* hiyo. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Hakuna, mbona ume-panic brother?

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia vinasaba. EWURA waliingia mkataba vinasaba na shirika moja bila kupitia tenda, huyo jamaa anajichukulia kila mwezi shilingi bilioni 9.8, tulieni ninyi vimeshawauma hivi hampati kitu!

MBUNGE FULANI: Huyo Lowassa au nani?

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mtakalia mnapiga kelele na 2020 mtapungua kwa *speed* ya Magufuli. Hamkutegemea!

MBUNGE FULANI: Wewe una akili, una matope?

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vinasaba anavyotumia EWURA kuweka kwenye Mafuta. Vinasaba vinagharimu shilingi 12.50. Vinasaba vyenyewe gharama yake ni shilingi 5.25 na mwenye vinasaba

huyo mwenye hiyo kampuni anapata shilingi 7. Kwa hiyo anakusanya kila lita kwa mwezi jumla anapata shilingi bilioni 14 amekaa tu bila sababu yoyote!

MBUNGE FULANI: Serikali ya nani?

MHE. ALLY K. MOHAMED: Ndugu zangu wakati anaingia Mkataba Waziri Mkuu alikwa ni Mheshimiwa Lowassa ambaye mmemnadi nchi nzima, na hii kampuni ya vinasaba ni Lowassa ana ushirika ndani yake, vinasaba vya Lowassa. Ni kampuni ya Lowassa na ndiyo alituingiza mkenge, ni Lowassa alipokuwa Waziri Mkuu.

MBUNGE FULANI: Miaka yote mlikuwa wapi?

MBUNGE FULANI: Lowassa hayupo si mumfute?

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Lowassa anyongwe.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Hili fisadi, anachukua Lowassa kila mwezi shilingi bilioni 14 hii kampuni yake, sasa ndiyo nawaambia mkakae mkachunguze huko. Mafisadi wakubwa. Mnaniharibia hata kuchangia kwangu. Mmemnadi ninyi nchi nzima, juzi ndugu yangu Mheshimiwa Khatib hapa anasema mwaka 2020 mtamleta yule yule Mheshimiwa Lowassa.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Keissy ukae, Kuhusu Utaratibu, Kanuni Mheshimiwa

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu, ingekuwa vema anayezungumza akalindwa amalize hotuba yake, kama wao hawazungumzi wakae kimya kama walivyooombwa, wasimvuruge Mheshimiwa Keissy aendelee kutiririka. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Keissy endelea bwana.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Serikali ilipiga marufuku kuagiza sukari nje. Ninachowaomba, wapige marufuku kuagiza mchele kutoka nje. Kuna mchele kutoka India, kutoka Thailand katika nchi yetu hii wakati mchele wetu uko mwingi, tuokoe hela za kigeni kama tunavyofanya mambo ya sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kuagiza mchele nchi za nje wakati tuna mchele umerundikana Kyela, Tunduma, Sumbawanga. Kwa hiyo upigwe marufuku mchele kuingizwa kama ilivyopigwa marufuku sukari ili kuokoa wakulima wetu.

Kuhusu usafiri mwambao wa Ziwa Tanganyika, Serikali ya Awamu ya Nne ilituahidi meli mbili, ninashangaa hata Awamu ya Tano hata meli hakuna ni kukarabati MV Liemba tu! Sasa inakuwa ni matatizo, hakuna cha kutengeneza meli mbili, hata hiyo moja nimeona kuna ukarabati MV Liemba. MV Liemba ina umri wa miaka 112, hatukatai kukarabati MV Liemba, ikarabatiwe, lakini tunahitaji na meli mpya.

Kuhusu suala la uvuvi, wavuvi wetu katika Ziwa Tanganyika wako duni sana. Tunaomba wafikiriwe ili na wao waweze. Zambia ina asilimia sita ya maji ya Ziwa Tanganyika lakini Zambia ndiyo inakuwa muuzaji mkubwa wa samaki na dagaa, ina asilimia sita ya maji lakini ndiyo muuzaji mkubwa wa dagaa na samaki za Ziwa Tanganyika, wakati sisi tuna asilimia 38 ya Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Idara ya maji, nimezungumza sana habari ya idara ya maji ni majipu na Namanyere. Siyo lazima kumngoja Rais au Waziri Mkuu nimezungumza mara kwa mara hapa. Wanaiba, wameandika gari hewa Dar es salaam na Namanyere na mabomba hewa hakuna kilichopelekwa, kila mara nazungumza hapa, ni hewa tupu hakuna kitu kinachofanyika!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Namanyere wananchi wana taabu ya maji miaka na miaka, wananidanganya hapa eti watanipa bilioni tatu, hamna cha bilioni moja, wala 500 milioni. Kwa hiyo, naomba bajeti ya safari hii, mradi wa maji na Namanyere ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mafisadi hukumu yao haitoshi kuwapeleka tu mahakamani. Haiwezekani mtu anakamatwa na nyumba 70 au 40, Serikali inachukua muda kumpeleka mahakamani na anapata dhamana.

Kwanza naiomba Serikali zile nyumba zinyang'anywe, kama alikuwa polisi, nyumba ziende Polisi, kama alikuwa mtu wa TRA (*Tanzania Revenue Authority*) ili wafanyakazi wa TRA wakodishe zile nyumba. Haiwezekani wewe mtu umefanya kazi yako inajulikana mshahara wako ni mdogo leo unanunua nyumba 40 au 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapato na matumizi ya Bunge, Wabunge wengi nilizungumza hata mara ya kwanza hapa, wanasafiri kama wakimbizi wa Burundi. Wanapishana *airport* kama Wakimbizi, Magufuli amedhibiti hii wanaanza kumpiga vita, ndugu zangu kwa vipi? Mpaka timu za mpira zinakwenda kwa ndege Rwanda, hamna lolote!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba apige marufuku timu zote za Bunge kwenda nje ya nchi. Safari za hovy hovy marufuku, Wabunge tuishi hapa tufanye kazi majimboni kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari za nini kwenda nje? Hakuna cha kutoa safari kwa Wabunge, Wabunge tukae hapa hapa tufanye kazi kwenye Majimbo kwa wananchi waliotuchagua. Kwenda nje iwe marufuku na mimi ninamuunga mkono Mheshimiwa Magufuli azuie safari zote za Wabunge za michezo hovy hovy kwenda nje, Wabunge wakakae majimboni kwao baada ya Bunge kutekeleza majukumu yao Majimboni. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru, tunaendelea. Anayefuata ni Mheshimiwa Desderius John Mipata atafuatia Mheshimiwa Sixtus Mapunda.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa pongezi kubwa sana kwa spidi na kasi nzuri sana ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano. Naunga mkono juhudi zote anazozifanya na kasi hii inatakiwa iungwe mkono na viongozi wote na wananchi wote kwa ujumla. Anatibu majipu, anatibu matatizo ambayo yamekuwa sugu katika jamii na kwa namna hii, natabiri kwamba, nchi yetu sasa hivi italetwa mapinduzi makubwa sana kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipitie hotuba ya Waziri Mkuu kuwasilisha ombi la Mji Mdogo wa Namanyere kuomba kuwa Mamlaka ya Mji wa Namanyere. Wilaya ya Nkasi iko pembezoni na mara zote mmekuwa mkitutolea mfano kwamba tuko pembezoni na maendeleo yetu yako chini. Namna ambayo mnaweza kutusaidia na kutuimarisha ni kutusogezea maeneo ya kiutawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Namanyere una zaidi ya watu 135,000, eneo la kilometa za mraba zaidi ya 16,000, ina bajeti zaidi ya shilingi milioni 359, ina Makao Makuu ya Tarafa, Makao Makuu ya Wilaya, Polisi, Sekondari saba, Chuo cha St. Bakhita kinachokusanya watu karibu 1,000 na ina Hospitali ya Wilaya. Kwa msingi huo, tunakidhi vigezo vingi vya kuwa Halmashauri ya Mji.

Tunajua mkitupa Halmashauri ya Mji mtakuwa mmetusukuma na kutusaidia katika matatizo mengi yanayotukabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupitia nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, niwasilishe ombi rasmi na lishughulikiwe na maombi tumeshapeleka mezani. Tuna Kata 10 tayari na Madiwani tumeshafanya uchaguzi. Kwa hiyo, kwa sasa tuna uwezo kabisa wa kuwa Halmashauri. Hilo ni ombi la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni sekta ya kilimo. Mimi wapiga kura wangu wengi ni wakulima. Miaka mitano yote niko Bungeni lakini sijaona mabadiliko makubwa katika sekta hii. Tumekuwa tunazungumza tunagusagusa na matatizo sugu hayajawahi kushughulikiwa inavyotakiwa. Kwa mfano, suala la utawanyaji wa pembejeo sijaliona kama limekuwa likienda vizuri na nimekuwa nikichangia hapa kila mwaka mabadiliko sijawahi kuyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu wanapelekewa pembejeo muda sio muafaka, wananchi wetu wanaoitwa walengwa pembejeo za ruzuku hawapati. Namwomba mtumbua majipu aelekeze nguvu zake eneo hili la pembejeo za wakulima wanyonge. Haki yao haifiki inavyostahili, haifiki hata kidogo. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Ruzuku ya mifugo.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Nashangaa hata ruzuku ya mifugo haifiki inavyotakiwa, wavuvi hawapati ruzuku yoyote, hii sekta yote ni kilimo kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kuwaombea wakulima ruzuku ipatikane kwa wakati. Pia mtafute mwenendo mzuri, mbuni mbinu nzuri kama mnavyobuni za kukamata hawa mafisadi, mnavyokamata wauza madawa ya kulevya sasa hivi, hii Serikali ina mbinu ambazo hata hatukuzitegemea kuwepo, ni kama kitu kimekuja ambacho hatukukitarajia, naomba muelekeze nguvu hiyo kwenye kilimo ili mboreshe kilimo. Kilimo kinatuajiri Watanzania 75%, kilimo kinatuchangia hela nyingi za kigeni, kilimo kinaleta utulivu na amani ya nchi kwa kuwepo kwa usalama wa chakula, kwa hiyo, kina kila umuhimu. Sisi Mkoa wa Rukwa ni wakulima na maeneo yote ambayo yanalima wasaidiwe kuangalia kwamba vigezo kama hivi vinazingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya ya kilimo yanahitaji kupata miundombinu ya usafiri. Barabara zinazoelekezwa katika maeneo ya kilimo

bado ni mbovu. Barabara ya kutoka Sumbawanga kwenda Mpanda inayojengwa kwa kiwango cha lami imekuwa ikicheleweshwa tu.

MBUNGE FULANI: Kabisa!

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Miaka saba tuko hapa Bungeni hatuioni hiyo barabara inakwisha kwa nini? Tukitembea sehemu nyingine nchini tunakuta kuna wakandarasi wenye nguvu na miradi inakwenda kwa speed zinazotakiwa, kwa nini kwetu kwa sababu ya upembazoni? Naomba mliangalie, Sumbawanga, Rukwa, Mpanda kote huku barabara haziendi vizuri kwa sababu ya upembazoni wake, lakini sasa ni awamu nyingine mtazame wanyonge. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni maji. Matatizo ya maji katika Jimbo langu na vijijini kwa ujumla ni kubwa sana mliangalie kwa umakini. Nikitolea mfano katika Jimbo langu kuna mradi wa kutoka Kate kupeleka maji Isale ambayo yangeweza kusaidia vijiji karibu saba vya Ntemba, Ntuchi, Isale katika mtiririko mzima wa njia hiyo ya maji. Naomba mradi huu pamoja na miradi mingine iliyoko King'ombe ambayo haijakamilika, tumepeleka zaidi ya shilingi milioni 500 amesema Mzee Keissy hapa kwamba kuna pesa zinatumiwa visivyo, zaidi ya shilingi milioni 500 lakini huoni maji hata kidogo yanatoka. Nafikiri muangalie yapo majipu kweli kweli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mradi wa maji Vijiji vya Nkundi na Kalundi bado haujakamilika, upo mradi Kijiji cha Chala bado haujakamilika, Kijiji changu cha Kasu hakuna mradi wa kutosha wa maji kakamavu kama tunavyoweza kuona katika sehemu nyingine. Kijiji cha Wampembe, Kijiji cha Namansi bado kote huko kuna matatizo ya maji naomba mtusaidie kupitia bajeti hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia bajeti hii naomba pia suala la mtandao wa mawasiliano. Nashukuru Serikali kwa kazi nzuri iliyofanyika katika Kata ya Ninde na ya Wampembe. Bado kuna dosari ndogo ndogo ili kukamilisha kazi hiyo, lakini Kata ya Kala ambayo ina tatizo kubwa zaidi bado kuna nini? Bahati nzuri Waziri ni yule yule ambaye alikuwepo. Sasa nakwambia katika bajeti yako siwezi kupitisha kama huwezi kupeleka au kunipa majibu mazuri ya kupeleka mtandao Kala. Sehemu zingine hizi umejitahidi vya kutosha lakini nataka kujua Kala kwa nini? Pembezoni kila siku tunakuwa wa mwisho, kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni suala la umeme. Mwambao mwa Ziwa Tanganyika katika Vijiji vya Kata ya Wampembe, Ninde na Kala hazijafikiriwa kabisa katika suala zima la umeme. Katika Jimbo langu la Nkasi Kusini maeneo kama vile Vijiji vya Kate, Katani, Nkomolo II, Kisura na Malongwe

tulikwishasema kwamba sasa hivi wangeweza kupata umeme, lakini mpaka sasa navyosema umeme haujawashwa. Wanapelekwa Wakandarasi goigoi hawafanyi kazi inavyotakiwa. Naomba muwabadilishe mlete wenye nguvu ili waweze kuleta matarajio ya wananchi haraka. Kilimo hakiwezi kwenda vizuri kama hata umeme wenyewe unasuasua namna hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mradi wa kupeleka umeme mkubwa katika mikoa ya pembezoni ikiwa ni pamoja na Rukwa, Kigoma na Katavi kutoka kwenye *grid* ya Taifa. Naomba isiishie maelezo tu ambayo tunayasikia hapa kwamba utafiti unaendelea. Tunataka tuone angalau katika bajeti hii umeme mkubwa ufike Sumbawanga ili mazao na mahindi yaliyopo ya wakulima wale yaweze kuchakatwa vizuri, ili samaki ambao wako mwambao mwa Ziwa Tanganyika minofu yake iweze kuchakatwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunakuwa watumwa wa watu wa Zambia, minofu yetu inapelekwa Zambia, halafu inasafirishwa Afrika Kusini kwa sababu tu hatuna umeme wa kutosha. Wavuvi wetu kule wanakuwa maskini wakati hawastahili kuwa maskini kwa kweli wanacheleweshwa kwa nini? Naomba umeme safari hii ufike Kirando, Wampembe, Ninde, Namansi kwani itakuwa ni ukombozi mkubwa sana wa wananchi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni barabara za Halmashauri. Zipo barabara ambazo nilikuwa nasaidiwa sana na Mheshimiwa Rais ambaye alikuwa Waziri. Barabara ya Kitosi – Wampembe, barabara ya Ninde, barabara ya kutoka Kasu - Katani - Nyula, barabara hizi Halmashauri haiziwezi. Tunaomba msaada zaidi kwa sababu sasa hivi karibu zitafunga, bila juhudi za ziada kutoka Serikalini tutaabika. Naomba ni maeneo ya wakulima wengi na tunatakiwa kuhakikisha kwamba barabara zinapitika. Hii ni pamoja na barabara kutoka Milundikwa - Kisula pamoja na Malongwe. Ni barabara sumbufu na zinasumbua sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa sababu muda unaniruhusu ni suala la zahanati. Tumesema kila kijiji kipate zahanati, lakini zipo zahanati ambazo zilishajengwa hazijafunguliwa bado kuna nini? Ipo Zahanati ya Nkomolo II na Msilihofu bado hazijafunguliwa rasmi ili ziweze kuwekwa kwenye utaratibu wa kuletewa dawa hizo zinazoweza kupatikana kwa njia ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tuangalie sana Hospitali ya Wilaya ya Namanyere. Hospitali ya Namanyere ni *DDH*, iko chini ya Kanisa la *Roman Catholic*. Utaratibu wa huduma umezorota kupita kiasi. Naomba Serikali itimize wajibu wake kwa hospitali hii lakini na wale wanaohusika juu ya uchunguzi na uangalizi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako ndiyo huo, tunakushukuru sana. Mheshimiwa Mapunda!

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii ya leo. Awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza Waziri Mkuu kwa jinsi alivyoitoa hotuba yake kwa umahiri na ufundi mkubwa, iliyogusa kila sekta. Hakika hotuba hii ime-reflect katika maana ya utendaji, hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Rais siku analizindua Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri Mkuu imegusa mambo mengi ambayo kama hayo yote tutakwenda kuyafanyia kazi kama alivyoyawasilisha hapa, nina uhakika ndani ya miaka michache nchi yetu itakuwa katika kiwango cha hali ya juu sana cha maendeleo. Niwaombe Mawaziri wote, kadiri Waziri Mkuu alivyoeleza kwenye hizo sekta, tuziongezee nguvu ili maendeleo kwa Watanzania yapatikane kwa haraka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya mambo yote mazuri ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameyaeleza, kuna maeneo machache naomba nijikite ili kuiomba Serikali iongeze nguvu sana ili tuweze kuendelea kwa wakati.

Jambo la kwanza ameeleza nishati ya umeme. Umeme ni jambo muhimu sana kwenye maendeleo ya Taifa lolote lile. Tuko kwenye mfumo wa gesi na aina nyingine zote za umeme ambazo zimewekwa katika programu ya mwaka 2016/2017. Niwaombe sana mtusaidie na sisi watu wa Songea katika maana ya Mkoa wa Ruvuma kama mlivyoeleza kuweka mfumo mpya wa umeme wa gridi ya Taifa kilowatt 220 kutoka Makambako Songea na nina imani hautaishia Songea utafika Mbinga utakwenda mpaka Nyasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni suala la viwanda. Suala la viwanda ni zito na ni kubwa sana na ni moja kati ya sera ya Awamu hii ya Tano. Kama tutawekeza kwenye viwanda hasa vile viwanda ambavyo vilisinzia na vingine vilikufa au vingine vinafanya kazi chini ya kiwango, nina uhakika ajira itapatikana kwa vijana na maendeleo makubwa yatapatikana kwa nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule Mbinga tuna kiwanda cha kahawa. Niiombe Serikali ikitazame kile Kiwanda cha Kahawa Mbinga na kiende hatua ya pili sasa kuweka kiwanda kingine cha *Instant Coffee* ili kahawa ile

ikishakobolewa siyo lazima tuipeleke Brazil, India au Ujerumani, tutengeneze pale pale kahawa na sasa tuwe na kahawa *made from Mbinga*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka niliongelee ni suala la afya. Kati ya changamoto ambazo zinatukabili kule Mbinga ni Hospitali yetu ya Wilaya. Hospitali yetu ya Wilaya ilianzishwa kama kituo cha afya. Kwa bahati nzuri maendeleo ya Mji wa Mbinga yakapelekea kuwa na Wilaya ya Mbinga ambayo baadaye ikazaa Wilaya ya Nyasa. Hata hivyo, hizi wilaya zote mbili, Wilaya ya Mbinga na Nyasa zinategemea Hospitali ya Wilaya ya Mbinga, Hospitali ya Mbuyula ambayo kwa sasa inahudumia Halmashauri nne za Nyasa, Mbinga Vijijini, Mbinga Mjini na sehemu ya Halmashauri ya Songea Vijijini. Niombe sana Serikali iwekeze kwenye ile hospitali ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ninayoomba Serikali iongeze nguvu ni kwenye huduma ya maji safi na salama. Ule mji unakua kwa kasi sana lakini mpaka sasa hatuna mradi mkubwa wa maji wa kuweza kuwasaidia wananchi wa Mbinga wanaoongezeka siku mpaka siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipongeza hotuba nzuri sana ya Waziri Mkuu, nimepata muda kidogo kuisoma hotuba ya Kambi ya Upinzani. Hii hotuba ya Waziri Mkuu ina *page 82*, imegusa kila maeneo, hii iliyowasilishwa na Mheshimiwa Freeman Mbowe ina *vi-page* kama tisa vile, *font* ni kubwa sana na *double space*, haiwezi hata kidogo ikajibu hoja ya *page 82*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiondoa hayo, ameiwasilisha hoja hii na amepotosha watu hapa kana kwamba watu hawasomi au hawafikiri. Nimwombe Mheshimiwa Mbowe akasome mambo yafuatayo. Kwanza, akaisome vizuri Katiba aielewe, akishaelewa vizuri akasome Sheria ya Bajeti, halafu vile vile akasome na *Appropriation Act* ya mwaka 2015. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoongelea kutengeneza bajeti lazima uweke sheria itakayosimamia utekelezaji wa bajeti ile na sheria hiyo inaitwa *Appropriation Act*. Kwa muktadha wa shughuli yetu ya leo ile *Appropriation Act* ilikuwa ya mwaka 2015 ambayo ina *section* sita au kwa lugha nyingine ina vifungu sita. Katika vile vifungu sita kuna kifungu cha 6 kinasema mamlaka ya Serikali kubadilisha matumizi kadiri itakavyoona inafaa kwa maslahi ya Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Mbowe alinukuu vipengele vya Katiba sasa mimi nimuambie Katiba ni sheria mama, inatafsiriwa kwenye sheria na ukitoka kwenye sheria ukafika kwenye bajeti utekelezaji wa

bajeti unakwenda kwenye *Appropriation Act*. Sasa mimi nampeleka kwenye *Appropriation Act* ya mwaka 2015, kifungu cha sita (6) kinachosema, *power of the Minister to reallocate certain appropriated moneys*. Imeeleza kifungu cha kwanza (1) mpaka cha tano (5) ila kwa faida ya kikao hiki mimi nakisoma vizuri kifungu kile cha tano (5), kinasema hivi, nanukuu:-

“The Minister may, by certificate under this hand, reallocate any sums arising from savings in the Consolidated Fund to any of the purposes specified in the second, third and fourth columns respectively of the Schedule to this Act, and where this occurs, the provisions of section 3 and 4 shall take effect as if the total sum granted out of the Consolidated Fund and the amounts appropriated for the purpose specified in such certificate were raised by the amount or amounts specified in the certificate”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa anachotuambia hapa ni nini? Anachotaka kutukoroga hapa ni nini? (Makofi)

MBUNGE FULANI: Mweleze.

MBUNGE FULANI: Tupe raha.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbowe aliongea kwa Kiingereza, mimi najua alikuwa na maana ya kupotosha watu wasielewe Kiingereza. Kwa Kiswahili kisichokuwa rasmi, Waziri ana mamlaka kwenye hii Sheria ya Bajeti tuliyoipitisha kwa maslahi ya nchi anaweza akaondoa kifungu kimoja *under certificate* kwa matumizi mengine yenye muktadha ule ule unaofanana kwa maendeleo ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuchukua pesa ambayo ilibaki kwenye matumizi *from July, August, September, October* ambapo Bunge halikuwepo tukaenda kununua madawati kwa mujibu wa sheria aliyetunga yeye mwenyewe na alikuwa amekaa pale, leo anajidai kasahau, huku kujisahaulisha kunatokana na nini? Niwaombeni, watu kama hawa tuwaangalie vizuri wenye ndimi mbilimbili, huku unauma huku unapulizia...

MBUNGE FULANI: Wateja wangu.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Unafikiri sisi wote hapa ni matutusa? Humu hakuna zero, watu tunafikiri kwa kutumia vichwa, hatufikiri kwa kutumia matumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunakushukuru kwa ufafanuzi wako mzuri. Tunaendelea, anayefuata kwenye orodha yetu hapa ni Mheshimiwa Omary Mgumba.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana nami kupata fursa hii ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza, kabla ya yote naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, maana yake nisije nikatiririka mpaka nikajisahau kama ule upande wa pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ya bajeti ambayo inagusa, inakidhi na inajibu changamoto nyingi za Watanzania mpaka imewaogopesha upande wa pili kwa sababu watachangia nini wakati Waziri Mkuu amemaliza kila kitu na ukija kuchanganya na utendaji wa Rais Dkt. John Pombe Magufuli amewamaliza kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu hawa wamekuwa kigeugeu sana. Tuwaambie kabisa CCM imejaa viongozi wa kila aina. Awamu ya Nne hawa hawa walikuwa wanalalamika Serikali haichukui maamuzi, ikichukua maamuzi inachelewa, tukawaambia sasa tunaleta Rais ambaye anachukua maamuzi haraka. Sasa wameanza kulalamika, wanalalamika nini, ni kwa sababu ameshawapiga Dokta John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza bajeti ya Waziri Mkuu kwa hali halisi, kuna Mbunge mmoja huku huwa anasema kwamba maneno yanadanganya lakini hesabu hazidanganyi. Nataka nimpeleke huko huko kwenye hesabu, hii bajeti imemaliza kila kitu, ukurasa wa mwisho kabisa kwenye fedha pale zilizopitishwa kwa sababu Waziri Mkuu ameonesha kwamba anaenda kutokana na maneno wanayozungumza Serikali ya Awamu ya Tano na vitendo vinaelekea vitakuwa hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende tu kwenye fedha alizoomba tuzipitishwe ni Sh. 236,759,874,706 wakati mwaka 2015/2016 fedha zilizopitishwa zilikuwa ni shilingi milioni 391.966 kwa kukaribisha, ni punguzo zaidi la asilimia 40 maana yake ni jinsi Serikali ilivyojipanga kubana matumizi na kuleta bajeti halisi ambayo inalingana na uwezo wa nchi yetu. Pia data hizo hizo, katika OC, mwaka 2015/2016 ilikuwa shilingi bilioni 349.288 mwaka huu OC imepunguzwa mpaka imekuwa shilingi bilioni 71.564, ni punguzo la asilimia zaidi ya 79.5, kujibana kwenye matumizi ya hovyoy. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupunguza pesa hizo katika bajeti halisi ameenda kuziongezea kwenye masuala ya maendeleo. Suala la maendeleo mwaka 2015/2016 ilikuwa ni shilingi bilioni 42.6 lakini bajeti ya Waziri Mkuu hii aliyoileta hapa ni shilingi bilioni 165.196, ni sawa na ongezeko la asilimia 122.5. Ndiyo maana nimesema naunga mkono hoja siyo kishabiki kwa uhalisia na namba halisi alizoleta Waziri Mkuu. Inaonesha ni jinsi gani bajeti hii inavyoenda kuwakomboa Watanzania walio wengi ambao kama anavyosema Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwamba waliteseka muda mrefu sasa nao ni zamu ya kuteseka upande wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema upande wa pili unaona wanavyolalamika ni baada ya hii kasi ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ya kutumbua majipu na hasa baada ya jipu kumfikia mkwe wao. Baada ya mkwe kuwekwa ndani ndiyo hawa wapambe wanaanza kulalamika na kujihami wanaona huu moto unakuja. Niwatoe shaka tu kwamba aliyekuwa msafi ataendelea kuwa msafi, wale wachafu mkono wa sheria utaendelea kuwafikia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya *facts* hizo, naomba nishauri Serikali katika mambo yafuatayo:-

Kwanza suala la ajira, naiomba Serikali izingatie sana katika kuweka mipango thabiti kwa ajili ya SME kwa maana ya wafanyabiashara wadogo na wa kati na hasa ukizingatia nchi yetu watu wengi wamejiajiri kwenye kilimo na kilimo ndiyo kinatoa ajira nyingi kwa maana ya kilimo na wafanyabiashara wa kilimo na watu wa namna hiyo. Kuna mambo mengine ambayo yako kisheria kwa mfano mfumo stakabadhi ghalani upo kisheria lakini ni mfumo ambao unawatoa SME na wafanyabiashara wadogo kushiriki katika biashara ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali itafute namna yoyote inavyowezekana ku-*accommodate* kundi hili kubwa la SMEs jinsi ya kushiriki katika mfumo huo ili kuweza kukabiliana na tatizo kubwa la ajira na ukizingatia Serikalini ajira hamna hata huko sekta binafsi siyo nyingi kiasi hicho kama tunavyofikiria, nyingi tunategemea watu wajishughulishie katika ujasiriamali, mambo ya biashara na mambo mengine. Ndiyo maana Mheshimiwa Waziri Mkuu utaona hata kule anasema changamoto mojawapo ni urejeshaji wa mikopo kwa sababu vijana wanakwenda kujiajiri lakini wanakosa hizo fursa za kujiajiri kwa sababu fursa zimekuwa chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukiwatengenezea vizuri namna ya kuwasaidia kwa ajili ya kushiriki katika ujasiriamali hata urejeshaji wa mikopo

tutakuwa tumetatua tatizo hilo. Hata hizi fedha ambazo Serikali kwa nia nzuri inataka kuzi-allocate kwa ajili ya kukopeshana kwenye kila kijiji shilingi milioni 50, lakini lazima tuwatafutie kazi za kufanya la sivyo utawapa shilingi milioni 50 kama kazi hakuna watu watakula. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kuishauri Serikali kwenye suala la maji hasa kwenye Bwawa la Kidunda. Bwawa la Kidunda nimeanza kulisikia hata shule sijaanza lakini mchakato wake umekuwa mrefu ukihusisha mambo ya mazingira na kadhalika. Tangu miaka 80 wazee wengine wananiambia tangu miaka ya 70 Kidunda inazungumziwa lakini sasa hivi Serikali imefika mahali pazuri naomba utekelezaji wake uende haraka sana. Kwa kumaliza utekelezaji wa mradi huu Jiji la Dar es Saalam ambalo linategemewa kiuchumi na Tanzania zaidi ya asilimia 70 utaweza kupata maji ya uhakika na viwanda vitaweza kwenda, lakini na sisi huku Morogoro tutaweza kuneemeka na fursa zinazokuja na Bwawa la Kidunda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kuishauri Serikali kuhusiana na migororo ya ardhi. Serikali imekuja na mpango mzuri wa majaribio katika Wilaya za Mvomero, Ulanga na Kilombero, naipongeza sana. Naomba katika mpango huu kwa sababu sasa hivi Morogoro ndiyo tunaongoza kwa migogoro ya ardhi na sababu kubwa ni kwamba ndiyo ardhi ambayo ina rutuba lakini kuna mashamba pori mengi na pia tuko karibu na soko kubwa la nyama kwa maana ya Dar es Salaam na kwenda nje, lazima mtu apitie Morogoro kwenda ku-export.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nia nzuri ile ya majaribio kwa Wilaya tatu tu ningeomba ingefanyika kwa Mkoa mzima wa Morogoro ili kuondoa hili tatizo, ukiwabana huku wanahamia upande wa pili. Mtamaliza huku watatoka upande wa pili wataenda kule kwa sababu ilishatokea katika ile Operesheni Tokomeza walianza Kilombero wote wakaja kwetu Morogoro Vijijini, operesheni ilivyokwisha wakarudi upande ule ule. Ni vizuri jambo hili lingefanyika kwa mkoa mzima ili kuwadhibiti vizuri hasa wale wavamizi waliokuja bila utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka pia kushauri katika suala la afya. Wilaya ya Morogoro ni kongwe lakini mpaka leo haina Hospitali ya Wilaya. Wilaya hii ina Halmashauri mbili, Manispaa na Morogoro Vijijini lakini mpaka leo hii hatuna Hospitali ya Wilaya. Naomba katika mpango huu ingeingizwa pia na Hospitali ya Wilaya ili tuondoe adha ya watu wa Halmashauri hasa wa Morogoro Vijijini ambao wanatembea zaidi ya umbali wa kilometa 180 kufuata huduma hiyo katika Hospitali ya Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nataka niishauri Serikali katika suala la uhifadhi wa mazingira na utunzaji wa vyanzo vya maji. Wote tunakubaliana miongoni mwa vyanzo vya maji katika nchi yetu vipo katika milima ya Uluguru kwa maana ya kule Kinole na Tegetero mpaka Mgeta, lakini utunzaji wa vyanzo hivyo inaachiwa Halmashauri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako ndiyo huo umekwisha. Tunakushukuru kwa mchango wako mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawaita wachangiaji wetu wanaofuata nitoe tangazo. Kuna mwenzetu kasahau simu yake ya mkononi nadhani kwenye row ya Mheshimiwa Faida Bakar. Asihangaikie sana tutawapa wahudumu wa ndani ya ukumbi huu wataipeleka pale kwa walenzi wetu pale waisajili halafu ataichukulia huko.

MBUNGE FULANI: Ya Mbowe. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Tunaendelea, anayefuata ni Mheshimiwa Leonidas Tububert Gama atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Suleiman Nkamia.

MHE. LEONIDAS T. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kumpongeza sana Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri sana aliyoianza ambayo imetupa matumaini Watanzania wote ya kuona kwamba sasa tunakwenda kule tunakokuhitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maelezo yake mazuri sana. Sisi sote tuna imani mno na yeye binafsi na tuna imani sana na timu yake ya Mawaziri ambao nashukuru wote wanakwenda kwa kasi ile aliyooanza nayo Mheshimiwa Rais. Tunaomba basi Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ulivyoanza uendeleo hivyo kuhakikisha unasimamia yale yote ambayo umewasilisha katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, nina maeneo machache ya kushauri. Eneo la kwanza, naomba nishauri juu ya wastaafu. Kwenye Majimbo yetu tuna wastaafu wengi sana. Mimi kuanzia nilipochaguliwa kuwa Mbunge moja kati ya watu wengi sana waliokuja kwa malalamiko mbalimbali ni wale ambao wamestaafu kutoka maeneo mbalimbali kwenye taasisi za umma na binafsi. Imeonekana dhahiri kwamba wastaafu wengi wanachelewa kupata malipo

yao au wengine wanalipwa malipo kwa kupunjwa au wengine hawapati kabisa malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ifanye zoezi la makusudi la kuwatambua wastaafu wote na jinsi walivyoshughulikiwa na taasisi zao ili tuweze kuona namna ya kupunguza na kuiondoa kero hii na matatizo ya wastaafu. Wastaafu hawa wamefanya kazi kubwa sana ya kutumikia nchi hii, kwa hiyo, wanapoteseka maana yake hatuwatendei haki. Ni imani yangu tukifanya zoezi la kuwatambua wote na maeneo ambayo wamestaafu na kile wanachokidai itakuwa rahisi zaidi kutoa maelekezo na miongozo ili kuhakikisha wastaafu wote wanapata haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Ilani yetu ya Uchaguzi ya CCM ilivyosema, tunao wastaafu kutoka kwenye taasisi mbalimbali za umma, lakini vile vile tunao wazee ambao hawakuwa watumishi katika maeneo mbalimbali, nafikiri sasa ni muda muafaka wa Serikali kujenga utaratibu wa namna ya kuwalipa pensheni wazee wote, kwa wale ambao walikuwa watumishi wa umma na wale ambao wamezeeka wakiwa wanafanya kazi za kujenga nchi yetu hasa kwenye eneo la kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu kwamba wazee hawa waliokuwa wanafanya kazi kwenye taasisi za umma na wale waliokuwa wanafanya kazi za kujenga nchi kwa kutumia sekta binafsi, wote wamesaidia sana kuichangia nchi hii kufika hapa tulipofika. Kwa hiyo, kama ilivyosema Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ni vizuri ukatayarishwa utaratibu ili pensheni iwe kwa wazee wote waliostaafu kwenye mashirika ya umma na wale waliostaafu kwenye shughuli binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia maeneo mengi ya wastaafu ni zile taasisi au Mifuko ya Jamii ndiyo wengi wanatoka huko. Ukienda kwenye historia ya Mifuko ya Jamii unakuta tuna Mifuko ya amii mingi sana kiasi kwamba hata watumishi wamekuwa wanayumba, wengine hawajui waende Mfuko gani, wengine wanakwenda kwenye Mifuko kwa sababu ya kushawishiwa bila kujua vizuri Mifuko hiyo na kuna utitiri wa Mifuko ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri hebu tuangalie uwezekano wa kuwa na Mifuko ya Jamii michache ambayo inaweza kuwafanya wafanyakazi na vikundi mbalimbali vikajiunga na Mifuko michache na tukaweza kuisimamia vizuri zaidi. Nashauri tuwe na Mifuko ya Jamii katika sekta kama nne hivi. Tunaweza kuwa na Mfuko wa Jamii kwa ajili kuhudumia sekta binafsi, tunaweza kuwa na Mfuko wa Jamii kuhudumia sekta ya umma, tunaweza kuwa na Mfuko

wa Jamii kuhudumia sekta ya afya na tunaweza kuwa na Mfuko wa Jamii kwa ajili ya kuhudumia sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ifanye kazi ya ziada ili kutoa elimu ya kuhakikisha kwamba watu wote wanaelewa na wanajiunga na Mifuko hii ya Jamii kwa maana ya watu katika makundi yao. Kuna akinamama lishe au mama ntilie, bodaboda, wafanyabiashara ndogondogo, wakijiunga na Mifuko hii itasaidia sana kuweza kujiwekea akiba ya uhakika wa maisha yao baada ya kufikia umri wa utu uzima. Tunajua tatizo la ajira lilivyo pamoja na juhudi zinazofanywa na Serikali bado vikundi vya wajasiriamali ni sehemu moja muhimu sana ya ajira binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba tuna Baraza la Taifa la Uwezesaji, Baraza hili lingeweza kabisa kuona namna gani tunaweza kuwezesha vikundi hivi vya akinamama wajasiriamali, vijana wajasiriamali na bodaboda, tuone namna gani Mfuko huu au Baraza hili linaweza kujikita katika suala hili kuona namna gani tunawasaidia ili kuondoka kwenye umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kuwa na maamuzi thabiti. Hivi sasa wote tunajua vijana wa bodaboda au vijana kwa ujumla. Kulikuwa na kundi kubwa sana ambalo lilikuwa halina mwelekeo. Katika Bunge hilihili kipindi kilichopita tumeruhusu kuanzisha usafiri wa bodaboda. Usafiri wa bodaboda ndiyo msaada mkubwa sana kwa shughuli mbalimbali za kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na watu wa bodaboda kusaidia sana kupunguza kundi kubwa la wazururaji lakini mpaka sasa haiieleweki, hivi tuna tatizo la kutokuwataka bodaboda? Maana kila ukisikia habari unasikia Dar-es-Salaam wamekamatwa, pikipiki 100 zimekamatwa, Songea wamekamatwa wako Polisi, mahali fulani wamekamatwa. Kwa nini hatufiki mahali tukaweka utaratibu mzuri wa kuyashughulikia matatizo katika uendeshaji wa bodaboda badala ya kuwanyanyasa hawa vijana bila kujua sababu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hofu kubwa sana kwamba kama tutaendelea kuwanyanyasa hawa vijana, tunakamata pikipiki zao zinakaa Polisi, maana yake tutatengeneza kundi lingine ambalo litakuwa kundi kubwa tusiloweza kulimudu wakiingia mitaani kwa nia mbaya. Kwa hiyo, nashauri Serikali hii ijipange vizuri kuona namna gani tunashughulikia kundi hili na makundi mengine ili yaweze kujitegemea na vijana waweze kuendesha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nataka nishauri. Tuna mahusiano mazuri sana kati ya Tanzania na nchi nyingine. Sote tunajua kwamba tuna mahusiano mazuri na jirani zetu wa Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, Zambia, Msumbiji, Kongo na kadhalika. Hata hivyo, naona mwelekeo wa Serikali umebana sana Kaskazini, upande wa Kusini kasi siyo nzuri sana. Sisi tutakumbuka mahusiano yetu mazuri yalivyo kati ya sisi na ndugu zetu wa Msumbiji. Tuna mahusiano mazuri sana ya kihistoria lakini tumewasahau ndugu zetu wa Msumbiji kwa maana ya kufungua mpaka kati ya Tanzania na Msumbiji kupitia Kijiji kile cha Mkenda kule Songea.

Mheshimiwa Spika, kama tutafungua mahusiano yale tutaimarisha sana mahusiano ya kibiashara kati ya Tanzania na wenzetu wa Msumbiji kwa upande wa Mkoa wa Ruvuma, lakini vilevile wananchi wetu wataweza wakafanya kazi nzuri ya biashara kati ya sisi na Msumbiji na hivyo kuinua kipato cha wananchi. Kwa hiyo, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu ione namna gani inafanya utaratibu wa kufungua mpaka ambao upo na kuna barabara ambayo ipo lakini haishughulikiwi. Barabara ile ikishughulikiwa inaweza kutusaidia sana katika shughuli nzima za kuongeza na kupanua uchumi wa wafanyabiashara wa eneo lile la Songea na Mkoa wa Ruvuma kwa jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na mengine lakini naona muda wangu hauniruhusu, basi nichukue nafasi hii niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. Niitakie Serikali yangu ya Awamu ya Tano utekelezaji mzuri wa Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunakushukuru. Tunaendelea na Mheshimiwa Juma Nkamia atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala*, kwa kutujalia afya njema leo. Nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais na kumpongeza kwa kazi nzuri anayoifanya, amefanya kazi nzuri sana kwa muda mfupi sana na naomba aendelee na moto huohuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri unayoifanya na Waheshimiwa Mawaziri wote. Kwa kweli sasa tunaamini kabisa kwamba Serikali iko kazini. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Spika na Katibu wake Dkt. Kashillilah pamoja na Naibu Spika kwa kufanikisha Bunge kuwa na *studio* yake. Duniani hakuna ambapo Bunge linaoneshwa toka asubuhi mpaka jioni na vyombo vya habari, jambo hili ni zuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilishangaa kusikia mtu anasema matangazo kutooneshwa ni kuvunja demokrasia. Hao waliotuletea hiyo demokrasia wenyewe hawaoneshi Bunge toka asubuhi mpaka jioni. Sisi tumechaguliwa na wananchi baada ya kwenda kuwaona na kuwaomba kura, siamini kama tulikaa kwenye televisheni na kuwaambia wananchi tuchagueni, turudi huko tukawatumikie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa niipongeze sana Timu ya Yanga Afrika wamefanya vizuri sana. Mimi ni mwanachama wa Simba na-*declare interest* lakini katika mechi yao ya juzi kule Cairo walicheza mpira mzuri sana, walikuwa wanawakilisha Tanzania. Naomba nimpongeze sana Rais wa Yanga Bwana Yussuf Manji kwa kazi nzuri ya kusajili wachezaji wazuri. Huwezi kuwa na wachezaji wabovu halafu unalalamika tunafungwa...

MBUNGE FULANI: Kama Simba.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Kama hali ilivyo. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimpongeze sana Bwana Manji kwa kazi nzuri aliyofanya na aendelee kuisaidia Yanga Afrika. Naamini katika mchezo wao na Angola wanaweza kupita. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye hoja zangu chache, kwanza nianze na suala la kilimo. Sisi Wilaya ya Chemba tuna mgogoro kidogo, si mgogoro *in such*, bali ni tamaa za watu wachache na wenzetu wa Kiteto. Tunaishi vizuri sana na watu wa Kiteto lakini wapo baadhi ya watu wanatuvuruga sana. Ni wazi kwamba Tanzania unaweza kwenda mahali popote bila kubaguliwa ili mradi tu ufuata sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, wakulima wetu wa Wilaya ya Chemba wanaokwenda Kiteto wengi wamefukuzwa na juzi juzi wakati mimi na Mheshimiwa Ndugai, bahati mbaya hana nafasi ya kusema humu, Mkuu wa Wilaya ya Kiteto kule akasema mimi na Mheshimiwa Ndugai tutamkoma kwa sababu tunatetea haki za wapiga kura wetu. Mheshimiwa Waziri Mkuu hebu liangalie jambo hili vizuri ili wananchi hawa waweze kuishi kwa amani, walime na waweze kufanya kazi zao bila tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kushauri ni suala la mfumo wetu wa uendeshaji wa Serikali. Tulipokuja kwenye ule mfumo wa *D-by-D* nashauri turudi tukaangalie upya tena. Huu ugatuaji wa madaraka umefanya baadhi ya mambo hayaendi vizuri kwangu mimi ninavyoona, kwenye elimu na afya ndiko kwenye matatizo makubwa. Leo Waziri wa Elimu hana mamlaka na shule ya kata, Waziri wa Afya akienda Hospitali ya Wilaya hana mamlaka nayo na Waziri wa Habari akienda kule Sumbawanga akawaambia wawe na Maafisa Habari kila Halmashauri hana mamlaka nayo. Kwa hiyo, naomba jambo hili tuliangalie vizuri kwa kufanya marekebisho kidogo ili tupunguze kidogo nguvu ya TAMISEMI iende kwenye Wizara nyingine kazi ziweze kwenda haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kushauri kidogo kuhusu usafiri Dar-es-Salaam. Njia ya kupunguza tatizo la msongamano ni pamoja na Serikali kuhamia Dodoma. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Aah wewe.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Wewe unaweza kusema aah wewe kwa sababu inawezekana fikra zako zinaishia hapa karibu, huoni mbali. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la msongamano wa magari Dar-es-Salaam na hata huu utaratibu wa *DART* tunaoanza nao siyo suluhisho. Hakuna miji mikubwa duniani kwa watu waliojipanga vizuri hata London, hakuna foleni kubwa pale mjini kwa sababu wametengeneza utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuhamia Dodoma imeshindikana basi tuanzishe utaratibu kwamba mtu anayetoka Gongo la Mboto akifika *Airport* kutengenezwe *parking* mahali aache gari aingie kwenye *public transport*. Vivyo hivyo kwa njia ya kutoka Bagamoyo, Mbagala, Tabata, tutapunguza tatizo la msongamano wa magari pale Dar-es-Salaam. Naamini jambo hili likifanyika litakuwa limetusaidia kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hata mfumo wa mabasi ule ambao mmeutengeneza pale Dar-es-Salaam, njia za mabasi zile ziko katikati. Unapotengeneza *bus lane* katikati pale halafu ni njia moja basi likiharibika katikati pale ya nyuma yatakwenda wapi kwa sababu iko *line* moja tu! Hebu angalieni vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kushauri kidogo, amezungumza hapa Mheshimiwa Kessy kwamba wafute hata michezo watu

wasiende nje, hapana, mimi napingana naye kidogo. Kwa mfano, Timu ya Bunge kwenda kucheza kwenye michezo ile ya EALA ndiyo ushirikiano wenyewe wa Afrika Mashariki. Nimwombe Mheshimiwa Keissy aje tufanye mazoezi akifanya vizuri na aende kwenye timu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Malocha amezungumzia suala la watu wengi kutopiga kura katika uchaguzi uliopita. Mimi nikupe tu mfano, Wilaya ya Chemba kijiografia ndiyo wilaya kubwa kuliko wilaya nyingine katika Mkoa wa Dodoma, kutoka Kata moja ya Mpendo mpaka kufika Makao Makuu ya Tarafa ni kilometa 64, kutoka mpakani na Kiteto mpaka kufika mpakani na Singida kilometa 275. Nilishangaa kuna wilaya nyingine zilikuwa na Kata nane (8) ama 12 zimegawanywa yakawa majimbo mawili, hata hiyo *population* yake siyo hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Mheshimiwa Malocha, tazameni namna gani baadhi ya Wilaya kama Chemba igawanywe yawe majimbo mawili, tuna kata 26, eneo lake ni kubwa kweli. Kuna wilaya sitaki kuzitaja, lilikuwa na Mbunge mmoja sasa hivi kuna majimbo matatu, ndani ya Tanzania Bara, hebu tuliangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa nataka kushauri kwenye suala la maji, tuongeze nguvu kwenye mabwawa. Sisi tumehangaika na mradi wa maji wa Ntomoko kule, sasa hivi mradi ule hauwezi kufika vijiji vyote 17, tuangalie utaratibu mwingine lakini tuongeze nguvu kwenye kujenga mabwawa. Mfano, Bwawa la Farkwa pale, Mlongia na Itolo pale katikati likitengenezwa bwawa wananchi hawa wataondokana na matatizo yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana wewe binafsi na nirudie kusema Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli chapa kazi. Wenzetu sasa ndiyo basi tena kwa sababu hata mgonjwa akiwa mahtuti unajua huyu kesho sijui kama atafika. Sasa baada ya kuisoma namba hata namba sasa hivi kuisoma inakuwa ni shida. Wakati mwingine tulieni, binadamu mzuri hapigi kelele hovyoy. Utalalamika sana, kuonekana kwenye TV si hoja, kwani unatafuta mchumba? Wewe unataka uonekane kwenye TV unatafuta mchumba? Unataka wakuone ili iweje, nenda Jimboni! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa anakuja mtu mzima analalamika hapa ndani ya Bunge, TV hazionekani, wewe unataka ya nini?

MBUNGE FULANI: Kwanza hakuna umeme.

MBUNGE FULANI: Mbona zamani hazikuwepo.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Ndiyo, mbona zamani hazikuwepo TV hizi ulikuwa wapi wewe? Unakuja humu ndani mtu mzima kabisa, tunakuheshimu sana, unasema TV hizi, sasa hivi watu hawaonekani, waonekane ili iweje, nenda kafanye kazi. Mimi nawashangaa tu, kumbe watu walikuwa hawafanyi kazi wanategemea TV, tuonekane hapa ili iweje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia, naomba kazi hiyo iendelee. Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Katibu wa Bunge kwa kazi nzuri mliyofanya. Sisi wengine ndiyo tulioanzisha mawazo hayo, yamefanya kazi vizuri hongereni sana. Hawa wanaosubiri televisheni waende. Kwa nini usiende kuomba kazi ya utangazaji kama unataka kuonekana kwenye televisheni? Nenda, nafasi zipo tu, TV ziko nyingi tu utaonekana, utapaka poda usoni, tutakuona. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Na *profession* ni ma-DJ hao! *(Makofi)*

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunakushukuru. Wanaofuata ni Mheshimiwa Leah Komanya na Mheshimiwa Amina Saleh Mollel kwa mpangilio huo.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu jioni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ni mara yangu ya kwanza kuchangia, naomba niwashukuru akinamama wa Mkoa wa Simiyu walioniwezesha kuingia katika Bunge hili. Pia, naomba niwashukuru wananchi wote wa Mkoa wa Simiyu waliokichagua Chama cha Mapinduzi nafasi ya Ubunge kwa asilimia mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa namna inavyofanya kazi ya kutumbua majipu. Wananchi wa Simiyu wana imani na Serikali na wanaiunga mkono. Hii imejidhirisha katika ziara ya Waziri Mkuu aliyoifanya mapema mwezi wa Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo naomba niombe yafuatayo katika bajeti ya mwaka huu. Mkoa wa Simiyu ni mpya una changamoto nyingi na changamoto moja ni ukosefu wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Wananchi

wanalazimika kusafiri umbali wa kilomita zaidi ya 100 wakifuata huduma hiyo Mkoa wa Shinyanga ama Mwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali katika bajeti yake ya mwaka 2015/2016, ilitoa fedha kidogo kwa ajili ya uanzishaji wa jengo la mapokezi. Naomba katika bajeti hii pia Serikali itenge fedha za kutosha ziweze kujenga hospitali hiyo na iweze kukamilika na kuanza kutumika. Hospitali hii itasaidia kuondokana na tatizo la mama wajawazito wanapopata dharura za kujifungua kusafiri zaidi ya kilometa 100 na hali barabara zetu zikiwa na ubovu hasa katika kipindi cha mvua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kuharakisha maendeleo katika uchumi wa viwanda pamoja na maandalizi mengine ni vyema Serikali ikaona haja sasa ya kuandaa mafundi mchundo wa kutosha ambao watahitajika kwa wingi katika viwanda vyetu. Mafundi hao wanaandaliwa na VETA zilizopo katika wilaya na mikoa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa masikitiko yangu, Mkoa wa Simiyu hauna Chuo cha VETA hata kimoja katika wilaya ama mkoa kwa ujumla. Naomba Serikali kupitia bajeti hii iweze kuuona Mkoa wa Simiyu ili hata vijana wetu waweze kupata mafunzo ya ufundi stadi ambayo pia yatawasaidia kujijari wenyewe. Pia chuo hicho kitaweza kusaidia kutoa ushindani katika kazi ambazo sasa halmashauri zinapaswa kutenga 30% ya kazi za zabuni kwa ajili ya vijana wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naiomba Serikali katika kufanya uchaguzi wa wanafunzi wanaoenda kidato cha tano kuwepo pia na uchaguzi wa wanafunzi watakaokwenda katika vyuo vya VETA. Hii itasaidia kuwepo na uhakika na wanafunzi katika vyuo vya VETA, pia itasaidia kuondoa ile dhana kwamba wanaoenda VETA ni wale waliofeli kuendelea na kidato cha tano. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichangie upande wa nishati ya umeme. Ni dhamira ya Serikali kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika unaokidhi mahitaji na wenye gharama nafuu ili kusukuma mapinduzi ya viwanda kwa kasi zaidi. Wilaya ya Meatu iko nyuma sana katika usambazaji wa umeme wa vijijini wa REA ukilinganisha na maeneo mengine. Wilaya ya Meatu ina vijiji 109 na Majimbo mawili, lakini ni asilimia 19 tu ya vijiji vilivyopata umeme. Niiombe Serikali yangu sikivu iangalie kwa jicho moja Wilaya ya Meatu iweze kusambaziwa umeme huo wa REA. Umeme huo utawasaidia wanafunzi wetu tunaowaandaa kuweza kujisomea vizuri na kuepukana na vibatari wanavyotumia. Umeme pia utawasaidia wananchi wetu waweze kununua

mashine za kukamua alizeti na kuweza kujipatia kipato na kujikwamua kutoka katika umaskini tulionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichangie kuhusu upatikanaji wa maji salama. Natambua Serikali katika Mpango huu wa Miaka Mitano imepanga kuleta maji kutoka Ziwa Viktoria kwa kupitia Wilaya ya Busega, Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu lakini maji haya yata-cover vijiji vilivyo ndani ya umbali wa kilomita 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Simiyu una changamoto ya upatikanaji wa maji. Kuna ukanda ambao unahitaji mabwawa kama vile ukanda wa Meatu. Tunaomba Serikali kwa maeneo ambayo hayatafikiwa na Mradi wa Maji toka Ziwa Victoria, ichimbe mabwawa zaidi katika Wilaya ya Meatu kuliko visima vya maji ambavyo vinakauka wakati wa kiangazi. Hata maji hayo yakipatikana huwa ni ya chumvi. Kanda zingine kama za Itilima, Kisesa, Bariadi, Busega, Maswa Serikali iendelee kuchimba visima virefu kwa ajili ya upatikanaji wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono sana hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Namwita sasa Mheshimiwa Amina Saleh Mollél, atafuatiwa na Mheshimiwa Kasheku Musukuma.

MHE. AMINA S. MOLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu kuhusu mapitio na mwelekeo wa Serikali na Makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Ofisi yako wewe mwenyewe, kwa maana ya Ofisi ya Spika, kwa jitihada zake za kuhakikisha kwamba masuala ya watu wenye ulemavu yanafanyiwa kazi. Pia pongezi za kipekee kabisa zimwendee Mheshimiwa Waziri Mkuu ambapo amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba haki za watu wenye ulemavu zinatimizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Rais amefungua milango na kuthamini haki za watu wenye ulemavu kwa kuona kwamba kuwa na ulemavu siyo kulemaa na ndiyo maana leo hii katika Idara mbalimbali watu wenye ulemavu wamepewa nafasi kuonesha uwezo wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimpe pongezi za dhati kabisa kwa kuhakikisha kwamba Wizara yetu inahamishiwa Ofisi ya Waziri Mkuu. Hiki kilikuwa ni kilio cha watu wenye ulemavu kwa muda mrefu. Kana kwamba hiyo haitoshi ni furaha iliyoje kuwa na Naibu Waziri katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri Mkuu imejitosheleza. Ni hotuba ambayo imegusa maeneo yote. Sisi watu wenye ulemavu tunaona ni fahari kubwa kwa sababu masuala yetu mengi yamezungumzwa na yameguswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, naomba tu nishauri mambo machache ambayo naamini kabisa kwa jitihada zilizoanza kutekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tano mambo haya yatafanyiwa kazi hasa katika suala la elimu. Naomba nitoe mapendekezo yangu kwa Serikali hasa kipindi hiki ambapo Mheshimiwa Rais ametoa kipaumbele cha elimu na kuhakikisha kwamba watoto wa Kitanzania wanasoma bure, ni jambo muhimu sana kuhakikisha kwamba sasa ni wakati wa kuboresha miundombinu ili watoto wenye ulemavu waweze kupata elimu pasipo vikwazo vyovyote. Pia ni wakati muafaka sasa kuboresha vyo vyetu ili kuhakikisha kwamba navyo mazingira yanakuwa rafiki kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mambo mengi yameorodheshwa humu na kwa kuwa matarajio yetu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni pande zote mbili kugusia mambo haya ya watu wenye ulemavu ambayo siku zilizopita yalikuwa nyuma sana, lakini sasa tumeona yanapewa kipaumbele. Tulitarajia Kambi ya Upinzani pamoja na vyama vingine vyote ambavyo vinawakilishwa hapa Bungeni vingekuwa mstari wa mbele kuunga mkono hotuba hii kwa kushauri ili kuboresha kwa namna moja au nyingine na kuhakikisha masuala ya watu wenye ulemavu yanasonga mbele na kuendana na kasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya hapa kazi tu. Ni jambo la kuhuzunisha hasa tukizingatia kwamba tunapokuja hapa Bungeni tunategemea kupata mambo yenye msingi, matokeo yake upande wa pili unatoa vitu ambavyo haviendani na wakati uliopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vyombo vya habari kurusha moja kwa moja matangazo ya Bunge ndiyo hoja yao hivi sasa. Tunapozungumzia suala zima la habari, habari zinapatikana wakati wowote na katika matukio yoyote muhimu. Hatujaona vyombo vya habari kama vimekatazwa kurusha habari na matangazo yanaendelea kutolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinacholiliwa hapa ni kule kurushwa habari moja kwa moja. Hata ukiangalia katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hakuna sehemu ambayo imezuia kurusha matangazo ya Bunge na matangazo haya yanaendelea kurushwa. Hata kama hayajarushwa moja kwa moja lakini si yanaendelea kurushwa kwa wakati mwingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri ni wakati muafaka wa kujiuliza ni kwa nini wenzetu wanalilia matangazo haya kurushwa moja kwa moja. Pengine ni kutokana na ajenda zao kwa hivi sasa zimeweza kufanyiwa kazi kwa kiasi kikubwa na Serikali ya Awamu ya Tano na kujikuta hivi sasa hawana la kusema. Ndiyo maana hata wakati mwingine wanaona kwamba ni bora wafanye yale ambayo yamefanyika na tumeshuhudia leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale masuala ya ufisadi waliyokuwa wakiyapigia kelele hivi sasa mafisadi wanashughulikiwa. Wamekuja hapa na kuzungumzia kuhusiana na matumizi ya fedha ambazo hizi fedha Waziri mwenye mamlaka husika sheria inamruhusu. Ni kwa vipi sheria inamruhusu, hivi hata nyumbani baba anapotoa fedha na zikabaki zikatumika kwenye matumizi mengine kuna ubaya? Katika sheria hii ambayo tumewasikia leo wakizungumzia ya *Appropriation Act* ya mwaka 2016 iko wazi kuhusiana na Waziri kutoa Fedha na kwenda kutumika sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tumeona Sherehe za Uhuru fedha zile zimetumika kutengeneza barabara ya Mwenge, kuna ubaya gani? Vile vile tumeona fedha za Muungano zitatumika kufanyia ukarabati barabara ya kwenda uwanja wa ndege kule Mwanza. Katika hili Serikali inapoamua kutekeleza mambo muhimu ambayo yataleta unafuu kwa wananchi hivi tatizo liko wapi? Ajenda yao hapa ni nini? Tumeona jitihada za Rais katika kutumbua majipu. Nafikiri kwa upande mwingine hata hawa pia ni majipu ambayo yanapaswa kutumbuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine wanapozungumzia utawala bora hapa Tanzania ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekuwa ikilivalia njuga suala hili na utawala bora upo, upo kwa maana gani? Hebu tuangalie hata katika vyama vyetu. Katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeshuhudia kabisa kwamba kila kipindi cha miaka mitano uchaguzi upo, miaka kumi uchaguzi upo na hata Rais anayekuwa Mwenyekiti katika chama husika anapomaliza muda wake unafanyika uchaguzi. Hata hivyo, tangu upinzani umeanza hapa nchini hebu tuangalie hawa Wenyeviti kwa muda wote wamekuwa Wenyeviti wa vyama hivyo na wao ndiyo wa kwanza kuzungumzia demokrasia, lakini ndiyo wavunjaji wa demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunapozungumzia Upinzani kwa chama cha CUF, tangu kimeanza Maalim Seif ndiye Mwenyekiti, hivi hakuna wengine ambao wana sifa za kuwa Wenyeviti? *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Sahihisha ni Katibu.

MHE. AMINA S. MOLEL: Kuwa Katibu Mkuu, amekuwa Katibu Mkuu kwa muda wote kwani hakuna wengine wenye sifa?

WABUNGE FULANI: Hawana.

MHE. AMINA S. MOLEL: Sasa mnazungumzia demokrasia ipi?

MBUNGE FULANI: Si udikteta huo.

MHE. AMINA S. MOLEL: Ni demokrasia ipi mnayoizungumzia wakati ninyi ndiyo wa kwanza kuivunja hiyo demokrasia? *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Huoni Hamad Rashid imem-cost.

MHE. AMINA S. MOLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, linapokuja suala la uongozi wakati mwingine Mwenyezi Mungu ndiye anayeteua viongozi...

MBUNGE FULANI: Ameen.

MHE. AMINA S. MOLEL: Siyo kila mtu tu atakuwa kiongozi, siyo kila mtu tu atakuwa Rais, miaka yote hujawa Rais basi achia ngazi wapishe wengine. Mnafurahisha sana, mlisusa uchaguzi, uchaguzi umefanyika wa haki, halali kabisa mmewaumiza wengine ambao hivi sasa wanalia ambao kwa namna moja au nyingine wangeweza kuendeleza Taifa hili, lakini leo hii mmewazuia. Kwa maana hiyo ninyi ndiyo wa kwanza kuvunja demokrasia kwa sababu hamuitimizi hiyo demokrasia. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Kweli.

MHE. AMINA S. MOLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe tu Rais wetu na tuzidi kumpa moyo, aendelee kufanya kazi, aendelee kuyatumbua majipu, Watanzania wanayaona. Wanaona jitihada za Rais, wanaona jitihada za Mawaziri wetu, kazi kubwa wanayoifanya na hicho ndicho tunachokihitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine wanasema kelele za chura hazimzui ng'ombe kunywa maji. Naomba kuwatia moyo muendele kufanya kazi, kazi inaonekana na wananchi wanaifurahia, kila siku umaarufu wao unazidi kushuka. Tunapoelekea sasa mwaka 2020 ni dhahiri kabisa hizi row ambazo hivi sasa mmeongezeka zitapungua kwa sababu matarajio makubwa ya wananchi ni kufanyia kazi matatizo yao, lakini hivi sasa mmekwenda kinyume kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja, naomba kuwapa moyo Mawaziri wetu, naomba kumpa moyo Waziri Mkuu, naomba kumpa moyo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tunamwomba aendele kufanya kazi kwa mwendo huo huo. Kauli mbiu ya hapa kazi tu iendele isirudi nyuma, tunachotaka sisi ni maendeleo. Wananchi kwa muda mrefu walikuwa na kero nyingi hivi sasa basi hizo kero ziweze kufanyiwa kazi, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niwe mchangiaji katika mjadala unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hotuba yake nzuri iliyosheheni matatizo ya Watanzania ambayo tumekuwa tukilia kwa siku nyingi. Tunakutia moyo tunasema endelea na moyo huo, Watanzania wanaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya ya kutumbua majipu na Watanzania wanaona. Napenda kumshauri kama atapata taarifa hizi aangalie hata kwenye Vyama vya Upinzani na kwenyewe kuna majipu ambayo yanatakiwa yatumbuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Bunge la Kumi na Moja Mheshimiwa Lusinde alichangia hapa akasema Chama cha Upinzani kikishindwa zaidi ya mara tatu kinageuka kuwa chama cha kigaidi. Nakubaliana na Mheshimiwa Lusinde kwamba hawa ndugu zetu wanakoelekea sasa ni kutengeneza ugaidi kwenye nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu sina hakika kama mawazo aliyoyasoma Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ni ya Wabunge wote. Kama ni ya Wabunge wote, Wabunge wote wa Kambi ya

Upinzani mtakubaliana na mimi ile hoja yangu ya bhangi tuitafutie muda tujadili. Niliwaambia humu kuna wateja, sababu ya kuwabanabana wanavuta bila kipimo, wanakuja humu wana stata zimezidi kipimo. Sina hakika kama haya mawazo ni ya watu wote ama ni ya mtu mmoja aliyevuta bila kipimo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unaona hata hali halisi ya Kambi ya Upinzani ilivyokaa, ndugu zangu watu wa Upinzani, hebu tumieni akili zenu mlizotumia kuwaomba watu kura kule mkaletwa humu ndani. Mnadanganywa mnatoka kwenye mada, mtu anasimama hapa anasema eti kwa sababu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani amesema bado anafikiria naomba kuchangia hiyo ndiyo hoja yangu, hayo ndiyo yamekutoa kwenye Jimbo kukuleta humu Bungeni? Watu wako wana njaa, wana shida ya maji, umeme, madawati, Mawaziri hawa hapa wewe unazungumza suala la Kiongozi wa Upinzani, ana nini humu ndani? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tukubaliane na hii hali kwamba yale maneno ya Mheshimiwa Lusinde yanaenda yanatimia. Ukiangalia hata Wapinzani waliobaki humu ndani sasa hivi ni wale waliokosa tu nafasi, ni wana CCM walioingilia dirisha la pili, wanajiandaa kurudi humu ndani. Tukubaliane na hii hali, hawa wenzetu hawana hoja, walikuja na hoja ya CUF ya Zanzibar wamepigwa bao. *(Makofi)*

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Wewe kaa chini. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walikuja na hoja ya Zanzibar, hoja ya Zanzibar tumewashinda...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma keti. Haya taarifa.

MBUNGE FULANI: Kaa chini.

TAARIFA

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Wewe uwe na heshima, aliyepewa nafasi na Mheshimiwa Mwenyekiti ni mimi, tumekaa muda mrefu sisi tunavumilia tuko makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa cha msingi na kubwa kuliko yote, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa mzungumzaji kwa kutumia Kanuni ya 64(f) na (g), aisome vizuri sana, naomba nimwambie maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, katika mambo ambayo hayakubaliki na yasiyo ruhusiwa Bungeni, kwa taarifa yako ni hatamsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine na hatatumia lugha ya kuudhi inayodhalilisha watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Mheshimiwa Mbunge ajielekeze katika shughuli zake kwa sababu hata sisi wachache tuliobakia hapa ni ukomavu wetu wenyewe tunasikiliza, ni *tolerance*, ni ngozi ngumu lakini hatujawahi kuwa CCM na hatutakuwa CCM. Lazima uwe na lugha nzuri ya kuzungumza ambayo ni lugha ya staha ya Bunge, lugha ya adabu itakayoheshimu watu wengine na siyo kama sisi hatuna lugha ya kusema humu ndani, lazima tuheshimiane, kuna lugha ya adabu Bungeni na kila mtu anamheshimu mwenzake vizuri sana. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Anachangia huyo.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ni vyema uelekeze...

MBUNGE FULANI: Usichangie toa taarifa.

MWENYEKITI: Usichangie.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, uwaelekeze kama Kiti wawe makini na hizo shughuli waeleze vizuri sana.

MBUNGE FULANI: Muda.

MBUNGE FULANI: Anachangia muda.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

MBUNGE FULANI: Wewe kaa chini.

MWENYEKITI: Naona Mheshimiwa alitafuta tu njia ya kuingia. *(Makofi)*

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamaliza nilipewa taarifa.

MWENYEKITI: Kanuni ya 64 inahusu masuala ya utaratibu, inataja yale ambayo huwezi kuyataja, Mheshimiwa kaingilia kwenye taarifa. Naendelea kuwasihi Waheshimiwa Wabunge, kila siku tunajifunza, lazima tuendeleo kusimamia Kanuni zetu. Ukiona mwenzako anakiuka Kanuni hata kama Spika au Kiti hakijagundua hilo ni wajibu wako kutumia utaratibu na ndiyo maana Kanuni zinasema utaje na Kanuni ipi. Wewe pale ulipaswa tu useme kuhusu utaratibu, Kanuni ya 64 tungeenda vizuri tu. Kwa vile umelisema, mimi narudia tu hayo kwamba tukizingatia Kanuni hizi shughuli za humu ndani zinakuwa nyepesi tu tena za kiungwana.

Naendelea, muda ambao umebaki bado unaruhusu wachangiaji wengine. Mheshimiwa malizia muda wako.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na namshukuru mkomavu wa kisiasa ambaye pia anajua kuzisoma Kanuni vizuri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuwasifu baadhi ya viongozi wa upinzani, Waheshimiwa Wabunge kama Mheshimiwa Profesa J, unaonesha uvumilivu wa hali ya juu. Wewe kwa sababu ni kioo cha jamii ningepomba uachane na mawazo ya kufundishwa ukipata nafasi changia, wasanii wanakutegemea humu ndani, usitegemee mawazo ya kuambiwa na wenzio hawa wazoefu hutarudi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye hoja yangu ya msingi. Nataka kuchangia baadhi ya mambo ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameandika humu ndani kuhusiana na matatizo yaliyoko kwenye Majimbo yetu. Kwanza ni kuhusiana na suala la TV. Naipongeza Serikali na uongozi wa Bunge, Jimbo langu halina umeme, tulikuwa tunatumia generator kuangalia Bunge na toka mmezua Bunge vijana sasa wanashinda mashambani. Endeeleni na mpango huu na ikiwezekana vipindi vya Bunge vioneshwe hata saa sita wakati wa kupumzika ili hata usiku kuwe na kazi zingine za kufanya wakati ambao watu wana nafasi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niishauri Serikali, kumekuwa na kasi ya kutumbua majipu watendaji wa Serikali, tunaipongeza sana Serikali, lakini hatutumbui vyanzo vinavyosababisha wafanyakazi wetu wa Serikali wanakuwa wezi. Nataka kutoa mfano, kuna mkandarasi anaitwa JASCO ambaye amesababisha Mkuu wa Mkoa wa Bariadi akasimamishwa na Mkurugenzi na Mhandisi wakafukuzwa lakini yeye akaachwa palepale kwa kuiba shilingi bilioni 19. Sasa amehamia Geita ana mkataba wa shilingi bilioni tano kwa kilometa tatu, ana mkataba wa shilingi bilioni sita kwa kilometa mbili, ana mkataba wa

shilingi bilioni kumi na nne kwa kilometa thelathini na nane na bado anafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri watu kama hawa kwenye kasi ya wakati wa Waziri Magufuli alikuwa anazifuta hizi kampuni. Tutamaliza watumishi wetu kuwaacha wafanyabiashara wenye uwezo wanawashawishi watendaji wetu kwa pesa, wanawapa mikataba ambayo ni mibovu. Tunawajua kabisa wamefanya hayo Bariadi leo amehamia Geita na tunawaacha wanaendelea kufanya kazi. Je, tunasubiri tena kwenda kufukuza Mkuu wa Mkoa na Wakurugenzi? Kwa hiyo, nashauri kwamba tuchukue hatua kabla mambo hayajawa mabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza kipindi kilichopita kuhusiana na suala la ulinzi kwenye Jimbo langu. Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba utuonee huruma. Ukiangalia kwenye taarifa Jimbo langu nadhani sasa hivi Tanzania ndiyo tunaongoza kwa kukatwa mapanga. Nilisema kila mwezi wastani wa watu wanne wanakatwa mapanga. Leo tunavyozungumza nurse kavamiwa hospitali kakatwa mapanga. Kwa mwezi wanakatwa mapanga siyo chini ya watu wane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo kwa wananchi wa Jimbo langu, kutoka kilipo kituo kikuu cha Polisi Geita ambako kuna usafiri ni zaidi ya kilometa hamsini. Unapopiga simu Geita gari kufika kwenye eneo la tukio inachukua zaidi ya saa moja kulingana na hali ya miundombinu. Pengine kuna njia gani mtufundishe na sisi ambao ni Wabunge wageni tuweze kuwaona Mawaziri mtupe Kanda Maalum. Wakati Rorya watu walikuwa wanaibiwa ng'ombe mkatoa Kanda Maalum na gari, sasa kwetu binadamu wanauawa wanne kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza humu Mheshimiwa Masauni akasema mwezi mmoja tuangalie tunapata magari sijaona mpaka leo. Mheshimiwa Waziri Mkuu labda mnataka mpaka msikie na Mbunge amekatwa mikono ndiyo mlete helikopta? Naomba mlipe kipaumbele Jimbo langu kwani kwa hali ilivyo sasa tunahitaji kupata gari kwa dharura ambalo litafanya doria kukamata wakata mapanga, pengine wahame basi hata warudi Mikoa ya Kusini huko na ninyi muweze kupambana nao huko. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapiga kelele sana kuhusu suala la maeneo ya kuchimba Geita. Nimeona humu amesema ameongeza ruzuku, Mheshimiwa Waziri Mkuu imekuwa ni porojo. Ndugu yangu Mheshimiwa Kalemmani nataka nikwambie uliahidi mara ya tatu juzi akiwepo Waziri Mkuu kwamba tarehe 16 utaachia *magwangala* hujaachia. Sasa nakusubiri ukivuka feri labda upae na

helikopta hutapita pale Geita, tutakusubiri, tutahakikisha tunakupeleka kwenye *magwangala* wewe ukawe ni mmoja wa waathirika kama wale vijana wanaopigwa mabomu bila sababu kwa kusikiliza kauli yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Kitu kizuri huwa hakina mjadala na ndiyo maana umeona wenzetu wale wamekimbia. Hotuba ya Waziri Mkuu inajitosheleza tunachotakiwa sisi ni kuisimamia na tuko tayari kuisimamia na ndiyo maana hata Wapinzani wanakwambia wanakwenda kujipanga. Hakuna cha kujipanga, hiyo ni dalili ya kukwambia Mzee uko safi, endelea na spidi hiyo hiyo na ikiwezekana geukia na upinzani utumbue majipu maana hata kwao kuna ufiada mkubwa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka, Mheshimiwa Sabodo walionesha kwenye TV, aliwasaidia shilingi milioni mia mbili na kiwanja Mwenge, mkasema mnajenga Chuo cha Viongozi wa Vyama vya Upinzani, kiko wapi hata tofali hazipo na hela ziko wapi? Kwa hiyo, tuangalie hata kwenye Vyama vya Upinzani. Kama mnataka kuiga siasa ya kweli ya kuwasaidia Watanzania, hii ndiyo mlukuwa mnaililia miaka yote kasi ya *jet*, nendeni mkajifunze kwa Magufuli na kwa Waziri Mkuu na timu nzima ya Mawaziri, sasa hivi tuko vizuri, mjiandae 2020 kurudi CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Vulu hayupo, haya Mheshimiwa Augustine Holle Vuma.

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nishukuru kwa kunipa nafasi hii angalau niweze kuchangia kidogo kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niungane na wenzangu kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, lakini pia na Waziri Mkuu pamoja na Baraza lake la Mawaziri kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea nayo na kasi ya hapa kazi tu ambayo sifa zake zimetamalaki Tanzania nzima lakini pia na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nilishukuru sana kuona kwamba barabara ya Kidahwe - Nyakanazi imewekwa kwenye kipaumbele, Malagalasi *hydropower* ipo na Kiwanda cha Sukari - Kigoma *Sugar* nacho pia kimepewa kipaumbele. Najua haya yatakuwa ni chachu ya maendeleo katika Mkoa wetu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala la umeme wa REA. Naomba Waziri mwenye dhamana husika, Mzee wangu Mheshimiwa Profesa Muhongo, lakini pia Naibu Waziri wake, suala la umeme wa REA katika Jimbo langu la Kasulu Vijijini bado utekelezaji wake siyo mzuri, ni wa kusuasua. Nashukuru sana Naibu Waziri alifika Jimboni kwangu pale tukaweka mikakati mizuri lakini napenda kumkumbusha tu kwamba, bado utekelezaji siyo mzuri na aweze kusukuma kuhakikisha kwamba umeme wa REA unafika kwenye Jimbo langu la Kasulu Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa mapato, nipende kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa namna ambavyo imeendelea kuongeza kukusanya mapato kila mwezi. Napenda kuwakumbusha kwamba mpakani kule bado zipo fedha zinapotea. Jimbo langu limepakana na nchi ya Burundi, kule wako watu ambao bado wanaingia pasipo kutozwa ushuru *formally*. Pia fedha zingine zinaishia kwa wajanja wachache ambao ni Maafisa. Kwa hiyo, ni bora sasa, Wizara husika ikaenda kuweka pale utaratibu wa namna ya kukusanya fedha zile ambazo zitakuja kusaidia Halmashauri yetu lakini pia na nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimdokeze Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Mzee wangu Mheshimiwa Simbachawene kwamba pale Kasulu bado kuna majipu, nakuomba sana utue mahali pale. Ripoti ya CAG mwaka jana ilionyesha upotevu wa shilingi bilioni 5.9, lakini mpaka leo hakuna kitu ambacho kimefanyika kushughulikia watu ambao walihusika na upotevu ule. Watumishi walikuwepo lakini pia na viongozi wa halmashauri walikuwepo. Kwa hiyo, ni vyema Mheshimiwa ukatua pale kwa ajili ya kushughulikia watu hawa ili fedha zile ziweze kuja kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo. Mheshimiwa Mwigulu, wananchi wanakusubiri sana Jimbo la Kasulu Vijijini uende ukamalize tatizo au mgogoro wa pori la Kagerankanda. Wananchi kwa muda mrefu sana hawana maeneo ya kutosha kwa ajili ya kilimo kwa sababu tu ya uwepo wa hifadhi ya pori la Kagerankanda ambalo kimsingi ukiangalia uhitaji wake sio mkubwa. Nadhani mipaka ile ilichorwa zamani wakati ambapo uhitaji wa ardhi haukuwa mkubwa. Kwa sasa kimsingi hatuwezi kuendelea kufuga miti ile ilhali watu wanakufa na njaa. Kwa hiyo, nikusihi sana Mheshimiwa Waziri uweze kufika pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Bunge lililopita Mheshimiwa Waziri ulisema kwamba, Wabunge tuje hapa tuseme ni lini tunahitaji mbolea za ruzuku ziweze kufika Jimboni kwetu. Naomba niseme kwamba Jimbo la Kasulu Vijijini tunahitaji tupokee mbolea ya ruzuku mwezi wa nane kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nipende kusisitiza tu kwamba, Watanzania wa Jimbo la Kasulu Vijijini wanayo imani kubwa sana na Serikali ya Awamu ya Tano na wana imani kubwa sana na kasi ambayo inakwenda nayo. Niwatie nguvu sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, hizi mbwembwe ambazo unaziona hapa, watu kugomea kuchangia na kususia vikao vya Bunge, hizi sarakasi tu wanajaribu kupanda kichuguu wakati mvua imenyeshwa, ni suala la kisikitisha sana. Nadhani hata Watanzania wanashuhudia nini kinatokea. Watu ambao waliwachagua kwa ajili ya kuja kimsingi kuwasilisha matatizo yao na kuyashughulikia wakisia vikao mahsusi ambavyo vingenda kutatua matatizo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niwashauri ndugu zangu Wapinzani lakini pia na uongozi wa Bunge hebu tumshauri Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni akae chini atafakari aone kama nafasi ya kuwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni bado inamfaa, ajipime vizuri. Kwa sababu ukiangalia namna ambavyo anaendesha kambi hii ni kinyume kabisa na matarajio ya Watanzania ambao wanahitaji maendeleo kwa nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wa Upinzani napenda kuwashauri kitu kimoja, nimesikia wakiitwa majina mengi sana ambayo mengine siyo mazuri kuyataja, lakini suala la kuja kujipanga kugomea mipango madhubuti ya kwenda kutatua matatizo ya wananchi, kujipanga kuchafua Serikali ambayo inakwenda kwa kasi ya ajabu, kujipanga kukwamisha maendeleo kwa namna yoyote siyo tabia ya kibinadamu ni tabia ya kinyama kabisa ambayo inafaa kulaaniwa na watu wote wanaopenda maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua wako watu ambao wakati mwingine wanalazimishwa kufikiria kinyume na vile ambavyo wanaamini kwa sababu tu labda kiongozi amesema, wanalazimika kufuata vile ambavyo wameelekezwa. Tabia hii wako wanyama ambao kiongozi akitangulia bila kujua anaelekea wapi, anaelekea shimoni, anaelekea mtoni au kiongozi wa wanyama wale anaelekea kwenye miiba, anaelekea kuliwa na mamba, wao huunga mkono na kumfuata nyuma, wanyama hawa wanaitwa nyumbu. *(Makofi)*

KUHUSU UTARATIBU

MWENYEKITI: Kuhusu utaratibu.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Kanuni?

MHE. MARWA R. CHACHA: Nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(1)...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Augustine keti.

MWENYEKITI: Endelea.

MHE. MARWA R. CHACHA: Inayosema: "Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno "kuhusu utaratibu", ambapo Mbunge yeyote ambaye wakati huo atakuwa anasema, atanyamaza na kukaa chini."

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko sasa kwenye Kanuni ya 64(1)(b) ambayo inasema, naomba niisome: "Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge, hatazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muongeeji ambaye anaendelea anachokiongea hakiko kwenye mjadala. Kwa hiyo, namtaka ajielekeze kwenye mjadala, sisi siyo nyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Anajihisi huyo.

MWENYEKITI: Umenipeleka kwenye Kanuni sahihi kuhusu utaratibu, umeisoma vizuri sihitaji kuirejea, ni kweli inasema tutaongelea hoja iliyo mbele ya Bunge. Hata hivyo, hoja hii ni pana, ina sura ya kisiasa, ina masuala ya uchumi na yote hayo. Haiwezekani tukawa kidogo tuna mawazo ambayo yanatufinya. Tunajenga nchi yetu, tunaimarisha Bunge letu, tunataka mjadala ambao utakuwa na tija wenye afya kwa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa endelea umalize.

MBUNGE FULANI: Kwa kuitwa nyumbu?

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tu sana na nisingependa muongeeji anifanye nikaenda mbali zaidi kwa sababu kama ni kuminya demokrasia wao ni vinara na hayo yamejidhihirisha wazi, hata kupitia kwenye Kamati za LAAC na PAC ambapo wajumbe wako wa Upinzani na wa CCM lakini...

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Tulia bwana wewe. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Naruhusu kwa sababu ni Kanuni, kuhusu utaratibu ni suala zito linaenda kwenye Kanuni, niambie Kanuni ipi.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(1) lakini natumia Kanuni ya 64(1)(a) ambayo inasema Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji anajaribu kupotosha Bunge lako Tukufu lakini pia na ambao wanaweza wakabahatika kupata taarifa hii. Hakuna Mbunge wa Upinzani ambaye huwa analazimishwa kufikiri. Taarifa ambayo imesomwa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni ni taarifa ambayo tumejadili kwenye kikao cha pamoja na tukakubaliana aisome kwenye Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, Kiongozi wa Upinzani ana namna ambayo anaweza kupatikana. Sasa anachosema kwamba ajipime, utaratibu tulishamaliza, ni jukumu letu sisi kama Upinzani kama ambavyo hatusemi Waziri Mkuu hafai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hizi taarifa za uongo ambazo anajaribu kuzitoa azirekebishe ziweze kusomeka sawasawa. Tuna uwezo wa kufikiri sawasawa na tumeamua hivyo na hayo ndiyo maoni yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwasilishe. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa. Kanuni ya 64(1)(a) ambayo umeitumia ungeimarisha zaidi sasa kwa sababu ni suala la ukweli, wewe unatuhumu hajasema ukweli, ungesoma pamoja sasa na Kanuni ya 63 ili umtake huyo Mbunge ambaye anatoa hayo maelezo ambayo wewe unaamini sio ya kweli ayathibitisha, hivyo ndiyo ingekuwa imekwenda vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema mapema, ningependa Kanuni hizi zituongoze yale makatazo ya lugha za uchokozi, za maudhi na kadhalika tuachane nazo, tutumie lugha za Kibunge. Unaweza ukafikisha ujumbe wako bila kutukana watu. Nataka hilo tuliweke wazi na ndiyo maana Mabunge haya yanaheshimika sana kwa sababu ya Kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge kwa sababu hukulikamilisha lote hilo, ushauri na uamuzi wangu kwa leo, hebu tumalize mjadala wa leo vizuri, tusifikishane kwenye kuonyeshana hizi Kanuni ambapo ungesoma vizuri ingelazimu tufanye hivyo. Tunaendelea, malizia Mheshimiwa. *(Makofi)*

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nina imani muda wangu umeulinda vizuri maana wanajaribu kunitoa kwenye mstari ili nisiseme kile ambacho nataka kukisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme tu kwamba hapa ni Bungeni na kila mtu kaja kwa kura ambazo amepewa na wananchi na kila mtu anao uhuru wa kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikumbushe tu jambo moja kwamba wako watu ambao wakati mwingine wanajaribu kukuondoa kwenye kile ambacho unahitaji kuzungumza, labda niachane nayo hayo. Tuko hapa mbali na kuzungumza namna ya kuleta maendeleo ya kiuchumi ya nchi yetu lakini pia lazima tuweke sawa ili kuhakikisha kwamba tunalinda misingi ya demokrasia na kuikuza vizuri na hatimaye nchi yetu iwe katika nafasi nzuri sana katika nyanja ya demokrasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi nimeyazungumza hapa lakini itoshe kusema kwamba naunga mkono hoja vizuri kwa asilimia 100 na Serikali ya Awamu ya Tano iendelee kuchapa kazi vizuri na wana CHADEMA wakubali wajumbe wa PAC na LAAC watoke CUF bila kinyongo chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru, tunaendelea. Mchangiaji wetu anayefuata ni Mheshimiwa Flatei Gregory Massay.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kabla sijasahau na muda haujakwisha nipongeze hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kweli imelenga kila mahali na kwa mimi mwenyewe nimekosheka kwa maana ya kwamba imegusa maeneo mengi sana. Pia nimpogee sana Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwanza kwa kasi aliyoanza nayo na pia kwa kazi anayofanya, kwa kweli maarufu sana kwa kutumbua majipu. Sisi wanyonge na maeneo ambayo kimsingi tulikuwa tumesahaulika sasa tunaanza kupata ahueni ya kupata maisha bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze Mawaziri ambao wamekuja kwenye Jimbo letu la Mbulu ambalo lilisahaulika kwa muda mrefu sana. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Lukuvi, Waziri wa Ardhi kwa kusaidia kutatua matatizo au mgogoro wa ardhi ulioko katika Bonde la Yaeda Chini kule eneo la Wahadzabe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Ummy Mwalimu pamoja na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kwa kuja kuisaidia Hospitali ya Haydom ili iweze kupandishwa kuwa Hospitali ya Kanda ambapo inaweza kuhudumia Mikoa yetu ya Arusha, Manyara, Singida, Simiyu na Meatu. Pamoja na pongezi hizi kwa kweli niwapongeze Mawaziri wote wanaofanya kazi na kwenye kasi hii ya hapa kazi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwa kweli naomba nizungumzie kwenye sekta ya miundombinu. Tunayo barabara moja kubwa sana kule Nyumbani ya Mbulu - Karatu- Haydom – Singida - Mbuyu wa Mjerumani – Mbulu - Dareda-Dongobesh. Barabara hii ni muhimu sana kwa ajili ya mawasiliano ya Wilaya ya Mbulu Vijijini ili kukutana na Hanang na Katesh. Barabara hii inahitajika sana kwa wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini, Mbulu Mjini, Katesh, Babati, Mkalama na kwenye Majimbo ya Singida ili kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Hospitali ya Haydom kwa sasa ni ya rufaa na ina wataalam wa kutosha barabara hii inahitajika sana ili iweze kufikiwa na watu wetu wa maeneo haya niliyoyazungumzia wapate tiba. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alinjibu kwenye swali langu nililouliza Bungeni Na.76, kwenye Bunge la Februari kwamba, ataweka kwenye Mpango ili barabara ile itengenezwe kwa kiwango cha lami, naomba kwa kweli azingatie hili ili wananchi wa Mbulu Vijijini na maeneo niliyoyataja waweze kupata mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo jambo moja la kushauri Serikali. Kuna taasisi mbili za RITA na NIDA. Ili kubana matumizi, nadhani taasisi hizi mbili zinafanya kazi moja, kwa sababu RITA inasajili vizazi na vifo na NIDA hali kadhalika inafanya kazi hiyohiyo. Ni vyema basi ili kupunguza matumizi ikafanywa kuwa taasisi moja katika hali ya kubana matumizi ili Serikali ipeleke pesa kwenye maeneo mengine kwa ajili ya maendeleo. Huu ni ushauri wangu kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie suala la umeme. Suala la umeme ni jambo ambalo limezungumziwa sana na Wabunge wengi. Nimuombe Mheshimiwa Waziri, Mbulu tangu kumekucha yaani imezaliwa 1905 sawa na Nairobi lakini kwa masikitiko yetu Mbulu umeme umepatikana

mwanzoni mwa miaka ya 90 kwenye Kata moja ya Haydom lakini mpaka leo haujasogea kijiji hata kimoja. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri kwenye REA III tafadhali angalia sana Mbulu ili mtusaidie Mbulu tuondokane na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata leo hii ukiwaambia wananchi wa Mbulu waangalie TV wataonea wapi, umeme katika kata 18, kata tatu tu ndiyo zina umeme. Kama Mheshimiwa Joseph Musukuma alivyosema, leo hii hata nikiiongea hapa hawawezi kuniona labda wawashe jenereta. Naamini katika mpango wa Serikali na kasi hii, umeme utafika kwenye Vijiji vyetu vya Endadubu, Masieda, Endanyawish, Endanaichan na maeneo mengi ambayo kwa kweli hata nikiyasema leo naona kabisa napoteza wakati lakini nina hakika Mheshimiwa Waziri ananisikia na nimeshampelekea orodha ya Vijiji vya Mbulu ambavyo havijapata umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie suala la mawasiliano. Kama unavyojua mawasiliano yanahitajika sana kwa ajili ya kuwasiliana na wananchi wetu. Sisi kule ni wakulima wa vitunguu swaumu ambavyo vinakwenda hata nje ya nchi kama vile Uarabuni na maeneo mengine mengi. Kule kwetu wamekuja watu kutoka Zanzibar kwa sababu biashara hii inauzika lakini tuna shida ya mitandao ya simu maeneo ya Tumati, Dongobesh, Maretadu na maeneo mengi hasa ya Masieda basi tungeomba Mheshimiwa Waziri aone maeneo haya hasa Kata ya Tumati kutupatia minara michache ili walau tuweze kuwasiliana na watu wetu. Mimi kama Mbunge wa Mbulu Vijijini nikitaka kuwasiliana na wananchi wangu kutoka hapa siwezi mpaka nifike *manually* niweze kuzungumza na watu wangu kule. Kwa hiyo, naomba sana Waziri wetu wa Ujenzi na Mawasiliano alione hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo la kushauri kuhusiana na suala la michezo. Mimi ni mwanamichezo, napenda ku-*declare interest*. Mbulu ni Wilaya ambayo ilikuwa inatoa wanamichezo wengi sana hasa maarufu ambao wamevunja historia na kuweka rekodi katika *Olympic* hasa kwa michezo ya riadha. Ndugu Filbert Bayi anatoka Mbulu, Gidamis Shahanga anatoka Mbulu, John Bura anatoka Mbulu, hawa wote wameweka rekodi ya dunia. Kwa hiyo, nishauri hivi vyama vya michezo viangalie wapi hasa historia ilipo ili viisaidie Tanzania iweze kujulikana Kimataifa kama ulivyokuwa miaka ya 70. Hii inawezekana kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nape ni rafiki yangu sana najua ananisikiliza katika hili. Kambi nyingi zimewekwa mijini, *nature* ya Mbulu inafanya vijana wengi waweze kujiingiza katika michezo na waweze hakika kuzinyemelea hizo medali, sasa hivi Tanzania ni vigumu sana kushinda katika jumuiya yoyote

hata Olympic kwa sababu tu michezo mingi imewekwa mijini, mtukumbuke na kule. Wananchi na vijana wa Mbulu wamenituma niwaeleze hili ili muweke kambi kule, historia ya akina Filbert Bayi haijavunjwa mpaka leo, rekodi yake ya dunia iko pale. Ni vema tutafute na kuinua vipaji vya kina Filbert Bayi na wengine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba nzuri sana ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimpongeze rafiki yangu msanii mwenzangu Profesa Jay na wenzake ambao wamebaki humu. Kwa kweli huu unaonekana ni uzalendo wa kutosha. Nawapongeza na Wapinzani wengine ambao wamebaki hapa. Sina sababu ya kusema sana kuhusu upinzani lakini najua dozi wamepata na wanaelewa nini maana ya kubaki na kuendelea kuzungumza, kusikiliza na kuchangia hoja hii.

Naomba tuwe na kitu kimoja tu kinachoitwa uzalendo. Uzalendo hauwezi kuonekana katika vyama vyetu, unaonekana katika mtu kufanya jambo. Ndiyo maana nimekupongeza Profesa Jay kwa sababu najua tulipotoka, tulikuwa tunaimba mimi na wewe unakumbuka (*huku akiimba madawa bangi ni saa utajiri kuuchuma mashangingi*) mambo kama haya, leo tupo Bungeni. Kaka usitoke hapa, ukitoka mwanangu kule watakuchimbia mbali na mimi Fletei si unajua mwana sarakasi sitoki hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumkumbusha tu kwamba na yeye aangalie, kwa nini nasema haya? Leo hii tunatakiwa kufanya kitu kinachoitwa maendeleo katika Majimbo yetu, leo hii TV kule haionekani ni vizuri tukashauriana humu ndani, tukitoka hapa nenda Jimboni watakuangalia. Muombe Waziri hapa akifika kule atakusaidia umeme utakwenda na maji yatakwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwenye maji. Jimbo langu la Mbulu Vijijini tuna miradi mitatu ya maji ambayo imefadhiliwa na Benki ya Dunia. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Maji nadhani ananisikia, miradi ile ya World Bank imesimama, naomba basi tusaidie iongezee pesa ili miradi ile iweze kutekelezeka wananchi wa Haydom, Bashay na maeneo ya Masieda na Dongobesh waweze kupata maji ili yale maji tuyatumie katika kilimo na kilimo kiweze kuwapatia wananchi wetu faida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda wangu nao umeanza kusogea sana. Mwisho, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu Majaliwa, ni Waziri wa kwanza kwa miaka 10 iliyopita amefika Jimboni kwangu akiwa Naibu Waziri, hakuwahi kutokea Waziri mwingine mpaka awamu hii imekwisha. Nakushukuru sana umefika kule na sasa basi nawashukuru Mawaziri ambao

wanategemea kufika na wengine wameniahidi kufika katika Jimbo la Mbulu. Ni kweli barabara yetu haipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi mimi na Mheshimiwa Jitu tulisukumwa na wananchi baada ya mvua kunyesha. Walipojua tunakuja Bungeni wakasema basi tuwatoe hawa kwenye matope ili wafike Bungeni, tulitumia saa tano kutoka kule kuwahi hapa Bungeni kutokana na jinsi miundombinu ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuendelea sana lakini kubwa zaidi nataka kuonesha tu umuhimu wa kuiona na kurudi Mbulu na Wilaya ile ni kongwe. Haya maeneo matatu niliyoyasema naomba mtusaidie sana Serikali. Kwa nini nasema haya ni kwa sababu naona uchungu. Mimi ni mjukuu nimekuja huku, alikuja Sarwatt, Marmo na Akunaay sasa kumbuka mimi ni mjukuu nimekuja kuwaambieni Mbulu muiangalie kwa jicho la pekee sana. Mbulu ni Wilaya mama imezaa Hanang kwa Mama Nagu, imezaa Babati kwa mtu anayeitwa Jitu, imezaa Babati Mjini kwa mtu anayeitwa Pauline Gekul na imezaa Karatu kwa mtu anayeitwa Willy. Jamani, sasa leo wote hao wana lami wana kila kitu, wana umeme, Mbulu kata tatu, mtuonee huruma jamani, hatuna hata kipande cha kilometa moja cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kabisa kwa asilimia mia moja, naunga mkono hoja hii ili Serikali ifike Mbulu ikanifanyie haya. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunakushukuru sana Mheshimiwa Massay. Kwa muda tuliobaki nao tunaweza kuchukua Waheshimiwa Wabunge wawili, nao ni Mheshimiwa jirani yako hapo Jitu Soni, Mbunge wetu wa Manyara Vijijini. Nasema wawili kwa sababu asubuhi tumetengua Kanuni tunaenda mpaka saa mbili. Wa pili atakuwa Mheshimiwa Issa Mangungu kama yupo. Haya tunaendelea, Mheshimiwa Jitu Soni.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake nzima kwa kazi na juhudi kubwa wanayofanya kuleta maendeleo ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchagua timu nzuri, timu ya hapa ni kazi tu, wametuonesha kwa vitendo kasi yao mpaka wengine tunafikiria tunafanyaje na sisi twende na kasi hiyo. Wenzetu wameanza kufikiria na imebidi watoke hapa ndani waende wakajipange huko nje ili na wao waweze kwenda na kasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze katika maeneo machache. Serikali imedhamiria kuleta maendeleo kwa kasi kubwa. Zile sekta ambazo imeahidi kwamba zitafanyiwa kazi, moja ni sekta ya kilimo tujikite vizuri, bajeti ya kilimo ambayo tutakuja kupitisha hapa wote tuiangalie vizuri iweze kufikia katika lile lengo tulilojiwekea la *Maputo Declaration* la asilimia kumi. Asilimia kubwa ya wananchi wetu ndiyo wapo huko vijijini na tukitenga bajeti kubwa kwenye sekta hii ya kilimo mambo mengi yatawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Wabunge wote tuunge mkono hoja ya kuongeza fedha ya kutosha katika mambo ya *research and development*. Bila utafiti hatutaweza kwenda mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *na-declare interest*, nipo kwenye Kamati ya Bajeti, katika hoja za awali tumeona fedha zilizotengwa upande wa utafiti ni ndogo sana, ni vizuri tujipange. Bila utafiti wetu wa ndani ya nchi iwe kwenye kilimo, mifugo, afya au jambo lolote hatutaweza kusonga mbele. Naomba Serikali kwa upande wa utafiti tuwekeze fedha ya kutosha ili tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia upande wa pili ni kwenye masuala ya mazingira. Tumbaki kusemea tu mambo ya mazingira kama jambo la kawaida, tunalisema linapita, hakuna mpango thabiti. Ni lazima Mfuko huu wa Mazingira tuufanyie kazi. Mfuko upo kisheria ni vizuri tuhakikishe kwamba unapatiwa vyanzo vya uhakika vya mapato ili tuweze kwenda kuboresha mazingira yetu. Hali hii ambayo tunakwenda nayo kwa sasa hivi kutokana na tabia nchi ni vizuri tuwekeze pia kwenye masuala ya mazingira la sivyo sisi kila siku tutakuwa watu wa kuangalia Mfuko wa Maafa kujazia badala ya kuangalia kutibu. Bora kinga kuliko tiba na namna ya kuinga ni kuwekeza kwenye masuala ya mazingira. Kwa hiyo, naomba tujitahidi sana kuwekeza katika masuala yanayohusu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu zaidi niishauri Serikali juu ya *coordination* baina ya Wizara moja na nyingine. Mwanzo ni mzuri lakini bado jitihada kubwa inatakiwa baina ya Wizara moja na nyingine *coordination* ile iwepo zaidi. Wasiwe kama wanashindana, wote mnakwenda kujenga nyumba moja, msishindanie fito. Kwa hiyo, mjitahidi *coordination* baina ya Wizara mbalimbali iwe ya uhakika na iwe lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi naomba katika Mkoa wa Manyara, wilaya zote masuala ya miundombinu yawekewe mikakati. Hii Mifuko yote ambayo tumeiunda tuhakikishe kwamba zile fedha mahali ambapo tumelenga ziweze kwenda. Mimi nishukuru kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu

umepunguziwa kazi ya TAMISEMI sasa imepelekwa Ofisi ya Rais. Utakuwa na muda wa kutosha na ni muafaka sasa kuhakikisha unasimamia Wizara nyingine zote na kufanya kazi ya kutembea katika wilaya na mikoa yetu kuhakikisha kwamba kazi inakwenda vizuri, uratibu wako sasa utakuwa wa uhakika zaidi. Badala ya kuwa mezani na ofisini sasa utaweza kutembea na kutoa maamuzi wakati unafanya ziara zako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu naomba Wabunge wote tuunge mkono suala la nishati na maji na hapo hapo tukiunganisha na suala la Mfuko wa Mazingira na utafiti. Bei ya mafuta iliposhuka duniani, leo bei ya mafuta ya jumla kwa *diesel* ni Sh.1,500. Napendekeza tuipandishe bei mpaka ifike Sh.1,700 ili ile Sh.200 inayopatikana iende kwenye Mfuko wa Maji, Umeme Vijijini pamoja na Mazingira na utafiti ili ile fedha iweze kupeleka nishati, maji na masuala ya mazingira na utafiti kwa haraka zaidi. Baada ya bei kuteremka hakuna Mtanzania aliyenufaika, hakuna nauli iliyoshuka, hakuna bidhaa yoyote iliyoshuka isipokuwa wafanyabiashara wachache wameendelea kupata ile faida kubwa na ile faida hata kodi yake hawalipi kwamba Serikali inapata kodi kutokana na suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wizara ya Fedha pamoja na Mawaziri wa Maji, Mazingira, Nishati na Elimu waangalie Wizara zao zinapokuja kuleta bajeti basi fedha hizo zitumike kuongeza Mfuko wa Mazingira, Mfuko wa Maji na Mfuko huo wa Nishati na utafiti ili kasi ya maendeleo iweze kwenda huko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bado ni muumini wa maendeleo vijijini zaidi kwa sababu huko vijijini ukiboresha huduma mbalimbali, iwe ya maji, elimu, afya basi wananchi hawatakuwa na hamu ya kuhamia mijini na pia huku mijini tayari kuna maendeleo makubwa. Kwa hiyo, Serikali ijikite zaidi kupeleka maendeleo katika sehemu mbalimbali huko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nimshukuru Mheshimiwa Lukuvi, nimshukuru Mheshimiwa Mwigulu na Waziri wa Maliasili, Wilaya ya Babati ina matatizo makubwa sana ya ardhi. Tatizo hilo likiisha basi Wilaya ya Babati na Mkoa wa Manyara unaweza kuwa moja katika mikoa ya mfano ambapo maendeleo yatakuwa kwa kasi sehemu kubwa. Tunaomba mjitahidi, tunaomba ushirikiano wenu ili tuweze kumaliza migogoro hii ambayo imedumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niendeleo kuisitiza kwamba kuna haja kubwa sasa, wenzangu pia walichangia kuhusu suala la kuunganisha utawala kuanzia juu kwenda chini, hii *D by D*, kwa sasa *chain* ile kuna mahali inakatika.

Ni vizuri tujaribu kuangalia upya sera namna ya kuunganisha hiyo *chain* ili maendeleo yakipangwa kuanzia ngazi ya chini kuja huku juu basi yaweze kwenda kwa kasi tunayoitarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niendeleo kushukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Jitu Soni kwa ushauri wako na mchango wako mzuri. Tunaendelea na mchangiaji wetu Mheshimiwa Issa Mangungu.

MHE. ISSA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kupata nafasi hii kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo kusimama hapa nikiwa Mbunge wa Jimbo la Mbagala. Pili, nimpongeze na niwapongeze wote ambao wameshinda katika Uchaguzi Mkuu huu akiwemo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama Samia Suluh Hassan, Mawaziri na Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchangia moja kwa moja hotuba ya Waziri Mkuu katika eneo la ajira. Jimbo langu la Mbagala lina viwanda ambavyo vinachangia pato la Taifa, vinachangia kodi lakini kumekuwa na malalamiko na manung'uniko mengi ya wafanyakazi katika viwanda hivyo. Waajiri wamekuwa wananyanyasa wafanyakazi, wanawatumikisha zaidi ya miaka sita mpaka miaka nane hawawapi mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru tangu Serikali ya Awamu ya Tano ilivyoingia nimekuwa nikilifuatilia jambo hili na namshukuru sana Mheshimiwa Mavunde amenipa ushirikiano mkubwa maana Wilaya yetu ilikuwa hata Afisa Kazi hakuna lakini ameniahidi na amekuwa akimpa maelekezo Afisa Kazi yule ili kuweza kuja kutatua matatizo haya. Kwa hiyo, naomba muendeleo kutusaidia maana wananchi wetu wanapata tabu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili katika eneo hili, katika Jimbo langu kuna viwanda lakini wawekezaji wale wameleta wafanyakazi wenye asili ya kigeni. Watu wale wanafanya kazi ambazo zingeweza kufanywa na mwananchi wa kawaida lakini wanaachwa wanaishi kwenye ma-godown mle, hakuna Afisa Uhamiaji anayekwenda kukagua vibali vyao, hakuna Afisa Kazi, wananyanyasa Watanzania kumekuwa na matatizo ambayo yangeweza kuepukika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana eneo letu la viwanda Mbagala mfanye ukaguzi wa uhakika na wa umakini. Zile kazi ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania wa kawaida wazifanye na hao wageni watafutiwe maeneo mengine ya kuweza kufanya kazi. Japokuwa tunataka teknolojia na maendeleo lakini nchi yetu isiwe jalala la kufanya watu waje tu kufanya kazi ambazo hata Watanzania wa kawaida wanaweza kuzifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo nije vilevile kwenye ajira za Walimu. Katika suala hili la ajira za Walimu kuna malalamiko mengi. Malalamiko haya yanatokana na kutopandishwa vyeo kwa muda mrefu na wanapandishwa vyeo lakini hawalipwi stahiki zao. Leo asubuhi limeulizwa swali na Mheshimiwa Naibu Waziri amelijibu, imefika mahali Walimu wamefanya kazi ya kusahihisha mitihani hawajapewa malipo yao. Yametoka maelekezo mikoa ilete, imeleta mikoa tisa kwa mujibu wa Mheshimiwa Waziri lakini hao waliochelewesha kuleta hawakutumbuliwa majipu na wameongezewa muda mpaka Jumatatu kama nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya Walimu yako mengi, matatizo ya Walimu yako mengi na kero za Walimu ziko nyingi. Mheshimiwa Waziri Mkuu wewe ulikuwa Mwalimu unajua changamoto zinazowakabili Walimu nchi hii, jitahidi kuhakikisha Walimu wanapata stahiki zao kwa wakati, wale wanaostahili kupandishwa vyeo wapandishwe vyeo kwa wakati na vile vile malipo yao yafanyike kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile niipongeze Serikali hii, leo tuna Waziri anayeshughulikia ulemavu. Napenda kuipongeza Serikali kwa sababu hapo nyuma ilikuwa inaonekana walemavu ni kama watu walioshindwa maisha, wasiokuwa na mwelekeo, walikuwa wanatengwa lakini baada ya kuteuliwa tu Mheshimiwa Possi amefanya ziara kuangalia vyo vya walemavu, amezunguka kuangalia changamoto na matatizo ya walemavu, nampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana waendeleo kuimarisha kambi zile za walemavu mfano kule Nunge Kigamboni na Mbagala eneo la Chamazi kuna kambi ya Muhimbili. Kambi ile ilikuwa inawaweka wale walemavu wa matatizo ya akili na mambo mengine, lakini sasa hivi haina huduma zozote, eneo lake limeanza kuvamiwa na matokeo yake inakuwa ni maficho ya wahalifu. Ningeomba sana Mheshimiwa Possi na hili alitazame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kuchangia ni kwenye elimu, Jimbo langu ni jipya ambalo lina wakazi zaidi ya watu laki nane. Baada ya kuanzishwa elimu bure kuna mfumuko mkubwa wa wanafunzi. Nitatolea mfano Shule ya Msingi Mbande iliyoko Kata ya Chamazi tuna wanafunzi wa darasa la kwanza 1,375; Shule ya Msingi Majimatitu nina wanafunzi elfu moja na mia mbili kadhaa. Juhudi zimekuwa zikifanywa na Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya lakini tunaomba Ofisi ya Waziri Mkuu itutazame kwa jicho la huruma sana. Jimbo la Mbagala limeelemewa na idadi kubwa ya wanafunzi na halmashauri ile uwezo wake ni mdogo. Kwa hiyo, naomba sana ndugu zangu Ofisi ya Waziri Mkuu mtuangelie kwa jicho la huruma kwa kutuongezea ruzuku, ushauri na ufundi na kwa jinsi mtakavyoweza kutusaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoke hapo niende kwenye suala la maji. Nimesikia programu nyingi sana za maji lakini hakuna hata moja iliyogusa Jimbo la Mbagala na Wilaya ya Temeke. Ukisikia programu Ruvu Juu inakwenda Kimara, Changanyikeni na maeneo mengine. Kulikuwa na mradi wa Kiperu, Mkuranga na mradi wa Kimbiji, huu sasa ni mwaka wa nane haujatekelezwa na hatujapata maji hayo yanayotoka katika vyanzo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukisema hapa kuna Mto Rufiji unao uwezo wa kuchangia upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo mengi ambayo mradi huu wa maji unaweza ukapita kama ukiwekewa msisitizo. Mfano ukitoa maji Mto Rufiji yatapita Ikwiriri, Kibiti, Bungu, Jaribu, Njopeka, Kimanzichana, Mkuranga yenyewe, Vikindu, Kongowe, Mbagala, Temeke na maeneo mengine ya Jiji la Dar es Salaam. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wa Maji hebu angalia jinsi gani unavyoweza ukaanza mchakato wa kutuletea maji kupitia Mto Rufiji na vile vile mradi huo wa Kiperu, Kimbiji nao utekelezwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba Mbagala sasa hivi ina wakazi karibu laki nane, maji ni ya kisima. Mbagala ina viwanda, maji ni ya visima, je, mnatuweka katika kundi gani? Maana walioko pembezoni ya nchi wanasema wamesahauliwa, jamani Mbagala iko Dar es Salaam, tumekosa nini kule hatuna maji safi na salama? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie kwenye suala la ulinzi na usalama. Mbagala sasa hivi imekuwa wilaya lakini Kituo cha Polisi kinachotumika kama wilaya hata *Police Post* haistahili lakini Askari wetu kule sasa hivi wanatafuta bodaboda kwenye mitaa na mitutu ya bunduki, usiku wamelala, uhalifu unafanyika sana usiku hakuna misako, hakuna doria.

MBUNGE FULANI: Wanaitwa Tigo.

MHE. ISSA A. MANGUNGU: Siku hizi Tigo wamekuwa kazi yao kukamata pikipiki mpaka mitaani zamani walianzia jijini katikati kule sasa wamekuja kwenye maeneo yetu ya mitaa. Kama kuna matatizo na maelekezo wapeni madereva wajielewe na waelewe, kama kuna elimu wapeni, wapewe leseni wafuate utaratibu, hawajakataa kufuata utaratibu lakini haya yamekuwa ni manyanyaso na kero kubwa. Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu hili nalo ulitazame na utoe maelekezo mahsusi juu ya madereva wa bodaboda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastaafu nao jamani wamelalamika sana nchi hii. Kila tukija kwenye Bunge kuna kero za wastaafu, hebu tumalize na hili nalo ni jipu, walipwe stahiki zao. Juzi Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza vizuri, kuna mchakato wa kuwaongezea zile pesa zao laki moja kutoka elfu hamsini lakini hata hiyo elfu hamsini maeneo mengine hazifiki, hebu angalieni jinsi gani ya kuwasaidia wastaafu hawa. Wapo wastaafu ambao wamestaafu jeshini, Walimu na watumishi wengine katika kada mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie mradi wa REA. Jimbo langu la Mbagala katika Kata ya Tuangoma, Chamazi na maeneo mengine yalipata mradi huu, nguzo sasa zimelala barabarani mwaka, miezi sita, waya hakuna, hakuna Mkandarasi, Wizara imekaa kimya na tunategemea Julai tunaanza mradi mpya, *phase III*, hebu hii *phase II* basi muisimamie maeneo yetu yapate umeme. Sambamba na hilo kuna *low voltage*. Mbagala ikifika saa 12 huwezi kuwasha *fridge*, kupiga pasi na kusikiliza redio na TV, umeme ni mdogo. Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini hebu tuangalie Mbagala kwa huruma, tuweze kupata umeme wa kutosha na wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba niseme jambo moja. Hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu huna pa kuikosoa, imejielekeza katika kila eneo. Kwa hiyo, ninachoomba ni usimamizi ili yale ambayo tumeyakusudia yaweze kutekelezeka. Pili, wengi wanasema, Upinzani wanasema hivi, mimi sitaki kuwasema Upinzani, tulishasema toka kwenye kampeni tumejipanga na wataisoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Majaliwa ametokea tangu Mwalimu, ametokea kwenye utumishi sasa ni Waziri Mkuu utamdanganya nini kwenye utumishi wa umma? Siyo hilo tu, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mavunde alikuwa Mwenyekiti wa Vijana anawajua vijana na anajua mazingira ambayo anatakiwa ayatumikie, leo utasema nini na utamkosoa nini? Mheshimiwa Dkt. Possi ameshakuwa Mwalimu UDOM na maeneo mengine nje ya nchi

amefundisha, leo ni Waziri anayeshughulikia walemavu utamdanganya nini, utamkosoa wapi? Mama Jenista Mhagama ninyi wenyewe mnamfhamu na mnamjua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme kwamba, tukijipanga vizuri siyo watasusia tu, watakuja kutaka ushauri kwetu na tunawakaribisha na tutawasikiliza ili tuweze kulipeleka mbele gurudumu la maendeleo ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, juzi amefungua Daraja la Kigamboni, lakini pale pale baada ya kufungua daraja lile ameona kutakuwa na changamoto ya foleni. Kwa hiyo, amesema kabisa zijengwe njia sita kutoka Rangi Tatu mpaka Gerezani. Niombe sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ahadi ile ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa pale isimamiwe kwa haraka ili kupunguza kero ya foleni kutoka Mbagala kuingia katikati ya mji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kuna barabara inayotoka Charambe kwenda Chamazi mpaka Msongola. Barabara ile iliwahi kuleta kashfa katika Serikali ya Awamu ya Pili na baadhi ya Mawaziri wa Awamu ya Tatu wakaenda Mahakamani, lakini mpaka leo haina marekebisho hasa kipande cha kutoka Kwa Mbiku mpaka Mbande haipitiki kabisa. Naomba sana Waziri wa Ujenzi katika majumuisho yake atujibu hili, imekuwa ni kero na ni tatizo kubwa. Ile barabara haina vituo vya basi, haifanyiwi matengenezo na imekuwa ni mahandaki matupu. Naomba sana Mheshimiwa Waziri ututazame kwa jicho la huruma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nipongeze sana Chama chama Mapinduzi kwa Ilani nzuri inayotekelezeka na inayoeleweka. Huwa wanasema Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi mnaahidi hamtekelezi, wameahidi Daraja la Kigamboni juzi tumefungua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, labda uelewa wangu mdogo. Mheshimiwa Rais alifuta Sherehe za Uhuru akasema pesa hizi ziende kutengeneza barabara ile ya Mwenge. Leo watu wanasema anatomia pesa vibaya, pesa zile hazijaidhinishwa, kwani jamani Wapinzani wamekuwa CAG wa nchi hii? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Bunge limetoa pesa kwa ajili ya utengenezaji wa madawati, ooh *allocation* ya ile pesa imeidhinishwa na nani, CAG atasema, kama kuna *misallocation* atasema jamani mlíchofanya siyo. Leo wameanza wao kukosoa, si kwamba wanakosoa wanaona sasa hivi foleni hakuna kabisa

barabara ya Mwenge kwenda katikati ya mji, kwa hiyo, hawana cha kusema na kama hawana cha kusema tutatafuta mengine ya kusema na tutawapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni demokrasia na utawala bora. Wanajua leo sisi tuna Awamu ya Tano ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, tumetoka tangu Awamu ya Kwanza ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, wao wana awamu ngapi hata ya uongozi wa kwenye chama? Kwa hiyo, chama chetu kina demokrasia na tunakubali kukosolewa, tunajikosoa, tunasonga mbele na tutaendelea kusonga mbele Watanzania wanatuamini na wanakiheshimu Chama cha Mapinduzi kimekuwa chama cha mfano wa kuigwa Barani Afrika na dunia kwa ujumla. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nichukue fursa hii kuunga mkono hoja na niwapongeze sana Mawaziri kwa ushirikiano wanaotupa, hakuna matabaka, wamekuwa wasikivu na tutaendelea kuwaomba Mungu mfanye kazi zenu ili nchi yetu isonge mbele. Matatizo na changamoto zipo, naamini kwa Serikali hii ilivyojipanga tutayatatua na tutakwenda tunapopahitaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ahsante sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Tunakushukuru sana kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema huyo ndiye alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa jioni ya leo. Niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote mliopata nafasi ya kuchangia kwa michango yenu mizuri. Hoja hii bado ina siku mbili mbele yetu, ila kwa kesho hatuna shughuli hiyo. Shughuli hiyo tutaianza Jumatatu ili mpate fursa nzuri ya kuitafakari, kuisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuzisoma taarifa za Kamati hizo mbili za kisekta, lakini pia pamoja na haya mliyoyasikia. Serikali ipo, watatoa maelekezo mazuri tu zaidi ya haya aliyoyatoa Mheshimiwa Mapunda.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nadhirisha shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu, Tarehe 25 Aprili, 2016, saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.00 Usiku Bunge liliahirishwa Hadi Siku ya
Jumatatu, Tarehe 25 Aprili, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*